# HISTORIA FUPI YA IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA

## UTANGULIZI

Katika hatua za awali za uanzishwaji wake kanisa la Waadventista Wa sabato halikuwa na muundo maalum wa huduma za vijana.

Pamoja na ukweli kwamba vijana walikuwepo na walifanya kazi kubwa, kama vile James White alieanza kuhubiri akiwa na umri wa miaka 21, Ellen White ambaye alipata njozi yake ya kwanza akiwa na umri wa miaka 17, na John Loughborough aliyeanza kuhubiri akiwa na umri wa miaka 17, hawakuwa na muongozo wowote wa Idara ya huduma za vijana, bali walifanya kama walivyofanya watu wengine tu. Waliamua wenyewe kwa msukumo wa Roho Mtakatifu ndani yao kushirikisha ukweli walio upata kutoka katika Neno la Mungu.

E. G. White, 7T. P 64; anasema * In His master Plan "the Lord has appointed the Youth to be His helping hand".

Katika mpango wake mkuu "Bwana aliwachagua Vijana kuwa Mkono wake wa msaada". Kanisa lilivyoendelea kukua mpango huu wa Mungu ulifunuliwa kwa watu wake na Idara ya huduma za vijana ikaanza.

## HISTORIA FUPI YA IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA KANISANI

Katika uhalisi wake, uanzishwaji wa Idara ya huduma za vijana hauwezi ukaelezwa vizuri bila kuwataja hawa Vijana wawili:- Harry Fenner Umri wa miaka 17, na Luther Warren umri wa miaka 14 ambao katika mwaka 1879 walipiga magoti chini ya mti katika maeneo ya nyumbani mwao huko Hezelton Michgan wakimuomba Mungu jinsi wawezavyo kuwaleta vijana wenzao kwa Kristo. Kama matokeo ya maombi yao, vijana hawa wawili walianzisha umoja wa vijana tisa kwa ajili ya shughuli hiyo. Umoja huu waliouanzisha ulijulikana kwa jina la Missionery Volunteer (M.V.)

Mwaka 1891 umoja kama huu wa Hezelton, ulianzishwa huko Antigo Wisconsin. Hawa walikuwa na wanachama 30 chini ya uongozi wa Meade MacGuide. Mwaka 1892, Mama Ellen White alihimiza na kutia moyo vyama vya vijana vilivyoanzisha akisema hakika ni mpango wa Mungu kuunganisha nguvu za vijana ili kuharakisha marejeo ya Kristo.

Mwaka 1901 kanisa la Waadventista Wa sabato katika Konferensi yake kuu ulimwenguni lilipokea chama hiki na kuchukua hatua za awali za kuanzisha Idara ya huduma za vijana. Kijana Luther Warren ndiye aliyekuwa mwenyekiti wa kamati hiyo. Kwa mara ya kwanza huduma za vijana zikaanza rasmi katika Kanisa la Waadventista Wa sabato zikiendeshwa chini ya Idara ya shule ya sabato.

Mwaka 1907 katika kikao cha shule ya Sabato huko Mount Vernon, Ohio, jina la Seventh day, Adventist Young People's society of Missionary Volunteers" lilipendekezwa kuwa jina la Idara mpya ya huduma za vijana General Conference.

Katika miaka hii , ndio MV ilipoanzisha huduma za vijana wadogo JMV Junior Missionary Volunteer.

**Wavumbuzi**
Chama cha wavumbuzi kilianza shughuli zake rasmi mwaka 1939. Huu ndio mwaka General Conference iliidhinisha wazo la madarasa ya wavumbuzi ya Nyuki wa shughuli, Mwali wa jua, Mjenzi na mkono wa msaada.

**Watafutanjia**
Mwaka 1950 Junior Missionary Volunteer ilijulikana kwa jina la Path Finder Club- chama cha watafuta njia ambayo hadi leo kimeenea ulimwengu mzima.

**CONGRESS RALLIES NA CAMPOREES.**

1928-congress huko ulaya ilikusanya vijana 3,000.

1947- vijana 12,000 walihudhuria congress, huko NAD san Francisco.

1951- Vijana 6,000 toka nchi 25 walihudhuria congress huko Paris Ufaransa.

Leo hii congress, rallies na camporees zinafanyika karibu ulimwengu mzima.
1999- vijana 22,000 waliohudhuria Pathfinder camporee kubwa na ya ajabu huko Oshkosh Wisconsin, U.S.A.

Mwaka 2008 camporee ya ECD ilifanyika huko Mwanza SNC. Vijana zaidi ya 4000 walihudhuria

- Mwaka 1978 ndipo jina " idara ya vijana" lilitumika badala ya missionary Volunteer ambalo kwa nchi nyingi lilipingwa kwa sababu za kisiasa (ndipo nchi nyingi walikuwa wanapigania uhuru wao toka kwa wakoloni).

- Katika miaka ya 1980s idara ya vijana ilijulikana kama AYO
- Miaka ya 1990s jina lililojulikana kumaanisha idara ya vijana lilikuwa AYS.
- Miakaya 2000 jina linalotumika ni AY. Japokuwa wengine hulitumia wakimaanisha vijana wakubwa, ndilo jina la idara.- Adventist Youth.

- Chama cha Mabalozi pia kilianzishwa mwaka 2001 ili kuwasaidia vijana walio kati ya umri wa miaka 16 na 21 walio na changamoto kubwa sana za maisha.

- Hadi sasa Idara yetu ya vijana inaundwa na vyama vinne ambavyo ni.

    1. Adventurer (Wavumbuzi) Miaka 6 – 9
    2. Pathfinder (Wataftanjia) Miaka 10 – 15
    3. Ambassador (Mabalozi) Miaka 16 – 21
    4. AY. (Vijana wakubwa) Miaka 22 – 35 + +

**HITIMISHO**:
Tuungane na Mungu katika mpango wake mkuu, kuiendeleza Idara ya vijana ili kutimiza makusudi yake – kuhubiri habari njema ulimwenguni kote na kuharakisha kurudi kwa Yesu mara ya pili.

**IDARA YA VIJANA TANZANIA UNION**

**FANI ZA UONGOZI WA KIKRISTO**

Kiongozi ni mtu wa namna gani?

- Mtu anayeanzisha mipango na kuifanya endelevu
- Ni mtu anayejihusisha na watu. Huwasikiliza watu kwa makini. Hujali hisia za wngine.
- Ni mtu anayekaribisha mawazo ya wengine,na kuyafanyia kazi.
- Ni mtu anayewaletea watu wake kilicho bora.
- Ni mtu rahisi kufanya kazi naye.
- Ni mtu anayeangalia hali inavyoenda; na kutafuta ufumbuzi.
- Ni mtu anayekiri pale anapokosea na kuchukua hatua kusahihisha makosa yake.
- Ni mtu mwenye mbinu, msimamo; asiyekimbia , wala kulalamikia matatizo.
- Ni mtu anayehimiza mchango wa kila mmoja katikakufanikisha malengo.
- Ni mtu anayeleta muafaka kunapokuwa na kuhitilafiana.
- Ni mtu anayewahimiza wengine kujitahidi; huku yeye mwenyewe akiwa mfano.

**MISINGI YA MUHIMU YA UONGOZI**

a) **Kupanga:** Kiongozi huangalia mbele na kuweke malengo. Kupanga hujibu maswali mapema yafuatayo: Nini kifanyike, Kwanini kifanyike hivyo, kitafanyika wapi, lini kitafanyika, Nani atafanya nini, Kitafanyikaje.
b) **Kuwasilisha mipango**: Kiongozi huandaa raslimazote na zinazohitajika, na hasa raslimali watu ili kuifanya kazi ifanikiwe. Kila mwanachama anapaswa kujua aina ya kazi anayotakiwa kuifanya katika chama.
c) **Kuhamasisha:** Kuhamasisha huwaleta watu katika vitendo
d) **Kusimamia:** Usimamizi mzuri huleta ufanisi katka kazi.
e) **Kutathmini.** Ni muhimu kupima mafanikio kila robo ili kujua kama yapo au la. Hilo litawapa mbinu za kuboresha mipango yenu zaidi.

**MTAZAMO WA BIBLIA WA UONGOZI**

- **UTUMISHI :** Kutoa huduma, Kuitegemeza kazi, Kuwezesha**.**
  **Mrk 10:45; Lk 24-27; Math 20:26-27; Yoh 13:12-17**
- **UCHUNGAJI** : Kutunza, kutia moyo, na kuelekeza.
  - Bwana ndiye mchungaji wangu. (Zab 23:)
  - Yeu- Mimi ndimi mchungaji mwema (Yoh 10: 11)
  - Petro aliagizwa kuchunga (Yoh 21:15-17)
  - Petro anaagiza- Lichungeni kundi lililo kwenu…(1Pet 5:2-5)
- **UWAKILI**: Dhamana, wajibu, na majukumu.
  - Kama msimamizi (Lk 12:42-43)
  - Aliyependelewa na mwenye wajibu.
  - Mtu wa kutumainiwa. (1kor 4:1)

- Kama mwelekezaji. (2Tim1:14)
- Kama mrithishaji wa maarifa (2Tim 2:2)

**KIONGOZI KAMA MTUMISHI (**Kutoa huduma, Kuitegemeza kazi, Kuwezesha)

- Yesu ni mfano halisi wa utumishi. (Luka 22:27)
- Alionyesha mfano halisi usiku ule alipowatawadha wanafunzi wake miguu (Yoh 13: 1-17 )
- Tabia mojawapo ya kiongozi wa kikristo ni kuonyesha mfano.
- Paulo aliwaelekeza waumini wake kufuata mfano wake. (1 Kor 11:1)
- Njia mojawapo yenye nguvu katika kufundisha tabia ni kuonyesha mfano.

Uongozi wa utumishi unatofautiana sana na uongozi wa madaraka ambao walimwengu wanautumia. Angalia tofauti zake katika jedwali lifuatalo.

| Uongozi wa utawala | Uongozi wa utumishi |
|---|---|
| Mawasiliano ni ya maagizo kutoka juu kwenda chini. | Mawasiliano ni kati ya kiongozi na wale anaowaongoza. Kiongozi hutoa mawazo yake na yuko tayari kusikiliza mawazo ya wale anaowaongoza. |
| Huongoza kwamaagizo na amri. | Huongoza kwa mvuto, kusikiliza na kushawishi. |
| Hutumia mwavuli wa uongozi kama kinga | Hutumia nafasi yake binafsi uongozi. |
| Watu hufanya kazi kwasababu wameagizwa kufanya hivyo | Watu wamejitoa. Wanafanya kazi kwasababu wanapenda. |
| Watu hufanya kazi li kumridhisha kiongozi wao | Watu hufanya kazi kwa bila kujali muda na kwa nguvu moja. |
| Watu hukata tama a haraka | Watu hupata mori wa kufanya kazi. |


- Kiongozi Mtumishi huwawezesha wengine akitambua kuwa kesho hatakuwepo, hivyo kazi itaendelea kupitia kwa wale aliowaandaa. Njia za kuwawezesha wengine ni pamoja na;
  - Kugawa madaraka.
  - Kuwashirikisha katika kufanya maamuzi
  - Kupanga mikakati.
  - Kuona njozi
- Kiongozi Mtumishi huwawezesha wengine kwa njia zifuatazo:
  - Kwa njia ya yeye kuwa mfano.
  - Kuwaelekeza.
  - Kuwatunza
  - Kuwaamini.
  - Kuitambua kazi yao
  - Kuwatia moyo
- Idara ya vijana inahitaji kiongozi mtumishi.
- Kiongozi atakayeongoza na kutoa huduma ya utumishi kama alivyofanya Yesu.
- Kuongoza kwa maneno na kwa mfano.

- Tafakari mafungu yafuatayo:
    - Luka 22:26-28.
    - Marko 10:45
    - Mathayo 20:26-27.


**KULINGANISHA KATI YA MTUMISHI NA KIONGOZI MTUMISHI**

| MTUMISHI | KIONGOZI MTUMISHI |
|---|---|
| Huonyesha roho ya unyenyekevu | • Anatambua ya kwamba ameitwa kutumika (Math 20:23)<br>• Anatambua uthamani wake katika mahusiano yake na Mungu (Ebr 11:26)<br>• Hana makuu bali anajali wengine (Rum 12:3-8; Efe 4:32)<br>• Anahisi wito wa kweli moyoni kuliko nafsi yake (Mdo 20:24) |
| Hutoa huduma yake kwa manufaa ya mtu binafsi. | • Anauthamani wenye nguvu katika kuwahudumia wengine. (Rum 12:5-8)<br>• Njozi zake huzielekeza katika huduma (Rum 1: 9-10) |
| Hujenga kuliko kubomoa | • Hushughulikia ukuaji wakiroho na kutoa huduma kwa wengine. (Efe 4:12-16)<br>• Huhamasisha kuliko kuelekeza. (Yoh 13:1-5; 1kor11:1; 1Pet2:21)<br>• Wanaoongozwa huwa imara, huwa na hekima, na uwezo. |

**PIRAMIDI YA UONGOZI WA UTAWALA**




**PIRAMIDI YA UONGOZI WA UTUMISHI**




- Uongozi wa utawala una mfumo mmoja wa maagizo unaoanzia juu kuelekea chini.
- Mipango na maamuzi hufanywa na viongozi wachache na kuiwasilisha ngazi za chini kwa utekelezaji .

- Uongozi wa utumishi huruhusu mawasiliano kufanyika katikapande zote; wanaoongoza na wanaoongozwa.
- Kuna uhusiano wa hali ya juu kati ya wanaoongoza na wanoongozwa.
- Kama kiongozi mtumishi, jiulize kuwa ninawahudumiaje watu wangu? , Ninawatumikiaje?
- Namna unavyowahudumia watu; nao watafanya hivyo kwa wengine.
- Kila unalolifanya kama kiongozi mtumishi linabaki kuwa mfano kwa wale unaowaongoza.
- Kiongozi mtumishi huhakikisha kwamba mahitaji makuu ya watu wake yanafikiwa
- Kiongozi mtumishi:
    - Husikiliza kwanza ili ajua namna ya kusaidia.
    - Huona mbele mambo ambayo wengine hawayaoni.
    - Huongoza kwa ushawishi badala ya kulazimisha.
    - Huwawezesha wale anaowaongoza kwa kuwapa fursa za kutumika.

**TABIA ZA KIONGOZI MTUMISHI**

**Zifuatazo ni tabia za kiongozi mtumishi.**

- **Msikilizaji.**
    - Kusikiliza hukuleta karibu na wale unaowaongoza.
    - Kusiliziliza hukusaidia kumwelewa kwa kina yule unayemhudumia
    - Kusikiliza humjengea imani yule unayezungumza naye kwamba unamjali.
    - Kusikiliza hukusaidia kujua namna ya kumsaidia Yule unayeongea naye.
- **Ushilikeli**
    - Hii ni tabia ya kulichukua tatizo la mwenzako na kulifanya lako. Kwa lugha nyingine ni kuvaa kiatu cha mwenzako.
    - Kiongozi mtumishi huzichukua changamoto za wale anaowaongoza kana kwamba ni zake, na kuzitafutia ufumbuzi**.**
- **Kuponya.**
    - Watu wengi wamekata tamaa na wamepitia maumivu mengi yanayotokana na msongo wa mawazo. Wanahitaji ushauri nasaha.
    - Matatizo mengi ya vijana yanahitaji tiba ya akili. Kiongozi mtumishi ni Yule anayewapatia vijana njia mbalimbali za kujitegemea.
- **Ushawishi**
    - Kiongozi mtumishi ni yule anayeongoza kwa nguvu ya ushawishi kuliko kutumia mamlaka ya uongozi katika kufanya maamuzi.
    - Kiongozi mtumishi huleta mipango yake na kuifafanua ili iweze kuungwa mkono au kusahihishwa na wale anaowaongoza.
- **Kujitoa kwa huduma**
    - **Kiongozi mtumishi ni wakili aliyejitoa kuhudumia mahitaji ya wale anaowaongoza.**
    - **Kiongozi mtumishi ni mtu aliyetayari kutumika wakati wowote huduma yake inapohitajika.**
- **Kujitoa kwajili ya kuendeleza wengine**.

- Kiongozi mtumishi anatambua kuwa wale anaowaongoza wana talanta na karama anazopasa kuziendelea katika muda wake wa uongozi.
- Kiongozi mtumishi hutumia muda wake wa uongozi kuandaa wengine kuwa viongozi.

Kiongozi mtumishi:

1. Ni mnyenyekevu. (Math 10:24; 2Tim 2:25)
2. Ni mchapa kazi. (Math 24:45-47, Luka17: 7-8)
3. Ana uwezo wa kufundisha. (2Tim 2:24)
4. Ni mvumilivu. (2Tim 4:2)
5. Ni mtii. (Efe 6: 5-6; Tito 2:9)
6. Amejitoa wakfu. (2Sam 15:21)
7. Ni mlinzi (Luka 12:35-36)
8. Ni mwaminifu. (1Sam 22:14)
9. Amejazwa na uwezo wa Roho Mtakatifu. (Mdo 2: 16-18)

**KIONGOZI KAMA MCHUNGAJI ( Kujali, Kuwatia watu moyo, kutoa mwongozo)**

Mara nyingi tunapomfikieia kiongozi kama mchungaji, mawazo yetu huelekea moja kwa moja katika Zab 23:1-6

**“Bwana ndiye mchungaji wangu…”**

- Huleta hisia za usalama.
- Hutuhakikishia kuwa Mungu anatujali.
- Huonyesha kuwa Mungu anahusika na utawala wa maisha yetu.
- Huonyesha kuwa Mungu ndiye usukani wa maisha yetu.

Sifa moja ya mchungaji ni kwamba yeye huishi na kondoo. Hushiriki ugumu wote na hatari  zote zinazomkabili kondoo.

**TABIA ZA MCHUNGAJI KIONGOZI**

1. **Mchungaji kiongozi huwatambua kondoo wake anaowachunga.**
    - Huwamtambua kila kondoo kwa jina lake , na yeye mwenyewe binafsi huwaita kondoo wote kwa majina. (Yoh 10:3-14,27)
    - Mchungaji kiongozi huwajua watu wake.
    - Anazijua changamoto zao. Anajua mahali walipo dhaifu na mahali walipo na nguvu.
    - Anajua ni wakati gani wanahitaji chakula na ni wakati gani wanahitaji maji.

- Wanazijua njozi za kiongozi wao; na wameshiriki kuziboresha ili zifae katika utekelezaji.

2. **Mchungaji kiongozi ni mtu anayepatikana wakati wote**.
    - Mchungaji siku zote yuko na kondoo wake; na anapatikana kila anapohitajika. (Luka 22:27)
    - Mchungaji kiongozi anapaswa kupatikana na pia awe mtu wa kufikika.
3. **Mchungaji kiongozi huongoza kutokea mbele.(Yoh 10:3-4)**
    - Mchungaji kiongozi hutangulia mbele ya wale anaowaongoza ili kuwaelekeza kwenye majani mabichi na mahali palipo na maji ya utulivu.
4. **Mchungaji kiongozi ni jasiri**
    - Mchungaji kiongozi huwalinda kondoo wake na wakati mwingine yuko tayari hata kuutoa uhai wake kwaajili ya kondoo. (Yoh 10:10-18)
    - Daudi alithibitisha ujasiri aliokuwa nao mbele ya Sauli. (1Sam 17:34-37)
    - Mchungaji kiongozi anapaswa kuwatetea wale anaowaongoza pale anapogundua kuwa wananyanyaswa na hawatendewi haki wanayostahili kupewa.
5. **Mchungaji kiongozi huonyesha na huelekeza**.
    - Kando ya kuwalinda wale anaowaongoza, mchungaji kiongozi huonyesha uwezo wa kuwatawala ili wasitangetange ovyo wasije wakavamiwa na kuraluliwa na adui.
    - Ni lazima awe namsimamo wa kutoyumbishwa na wachahe wasiopenda kujiweka chini ya uongozi wake.
    - Ingawaje mchungaji kiongozi anapaswa kuwa kuonyesha uwezo wake wa kuongoza, hapaswi kuonyesha ile roho ya kuwaburuza.
    - Anapaswa afuate mfano wa Mungu kama mchungaji, kwa jinsi ulivyoelezwa katika Biblia.
        - Atawakusanya wana-kondoo mikononi mwake. (Isa 40:11)
        - Atawafunga waliovunjika. (Eze 34:16)
        - Atawaongoza katika maji ya utulivu. (Zab 23)
6. Mchungaji kiongozi huwajibika na kondoo waliopotea.
    - Katika mfano wa kondoo aliyepote, Yesu aliongea juu ya mchungaji aliyeacha kondoo tisini na kenda na kwenda kutafuta kondoo mmoja aliyepotea. (Luka 15:4-6; Math 18:12-14)
    - Kiongozi Mkristo asiye na moyo wa kichungaji anaweza kusema, “Hao wachache waliopotea ninini?” “Au hao wachahe walioacha ukristo ni kitu gani?”
    - Kwanini nipoteze muda wangu wa thamani kujaribu kuwarudisha zizini?
    - Lakini Tesu alichangamana na watoza ushuru, makahaba, wenye dhambi na alikuwa rafiki kwa wote. (Math 11:19)
    - Moyo wake wa uchungaji ulikusudia kumfikia kila mmoja.
    - Ndivyo inavyopaswa kuwa kwa kiongozi mchungaji; kuwa na roho ya kuwafikia wote waliopotea.

Jipe changamoto wewe mwenyewe kujiuliza maswali yafuatayo.

- **Mchungaji huwajua kondoo wake na kuwaita kwa majina**.
    - Ni kwa kiasi gani ninawafahamu kwa majina wale ninaowaongoza?
    - Ninazijua changamoto zinazowakabili hao ninaowaongoza?
- Kondoo huitambua sauti ya mchungaji wake.
    - Je, nimekuwa mtu wa kupatikana kwa wale ninaowaongoza au ninajali tu maisha yangu?
    - Niko tayari kiasi gani kuwashirikisha wengine katika madaraka?
    - Je, mimi niko kama Yesu aliyechagua kuwa na wanafunzi 12?

I. **KIONGOZI KAMA WAKILI**: Dhamana, wajibu, na majukumu

- Mtu anayeitwa wakili amepewa dhamana. Katika mfano wa talanta tunaambiwa kwamba yule mtu aliweka kwao mali zake (Math 25:14)
- Uwakili hudhihirisha kupewa dhamana; na kila aliyepewa dhamana anatakiwa aonyeshe uaminifu.(1kor 4:1)
- Paulo anajiona mwenyewe kuwa amepewa dhamana, na hivyo ameaminiwa uwakili, (Ikor 9:17)
- Ukijua kuwa umeaminiwa, ni lazima ni lazima udhihirishe kwa wale waliokupa dhamana kwamba unaweza.

II. UWAKILI NI KUPEWA MAJUKUMU (Luka 12:42-43)

- Kazi ya kiongozi wakili ni kuhakikisha kuwa mahitaji ya watu yanakidhiwa.
- Kiongozi wakili anapaswa kujua nini cha kufanya na matarajio ya watu wake ninini.
- Watu hawapangi kushindwa, ila wanashindwa kupanga,’
- Kushindwa kupanga ni matumizi mabaya ya uwakili’

**III. UWAKILI NI KUTOA HESABU.**

- Wakili hutambua kuwa atawajibika kutoa hesabu kulingana na alivyopokea. (Luka 12:48)
- Viongozi wamepewa kwa kiasi cha kutosha mvuto, uwezo, na raslimali
- Mungu atawahitaji kutoa hesabu ya jinsi walivyotumika kuandaa watu kuokolewa
- Uongozi ni huduma ya uwakili wa raslimali, muda, fursa, talanta, na nguvu kwaajili ya kukamilisha kazi ya utume.
- Viongozi wanatazamiwa kuwa mawakili wazuri wakitumika kuujenga mwili wa Kristo.

**IV. UAMINIFU, UKWELI NA UWAZI**

- Mojawapo ya tabia muhimu kwa kiongozi wakili ni uaminifu, ukweli na uwazi.
- Kiongozi wakili huishi kulingana na miiko ya uongozi. (Mith 22:1)
- Kiongozi wakili ni mwaminifu na husema ukweli.
- Kiongozi wakili ni mwenye haki na hutenda haki.
- Kiongozi wakili hujijali na hujali wengine.

- Uwazi huendana na uaminifu.
- Uwazi ni kinyume cha unafiki.
- Matendo huongea zaidi ya maneno.
- Watu huaminiwa kwasababu tabia zao hufahamika.

**JINSI YA KUJENGA UAMINIFU NA KUTUMAINIWA**.

i. **Timiza ahadi zako.**
- Ikiwa unahitaji watu kujenga matumaini kwako; wanahitaji kuona unatimiza ahadi kwao.
- Kutimiza ahadi ni pamoja na kufanya kile ambacho ulisema utafanya.
- Zishughulikie ahadi kwa bidii.

ii. **Uwe mu wazi na mkweli**.
- Usijaribu kuficha udhaifu wako .
- Wakiufahamu watakudharau
- Watu wakishagundua kuwa kuna dalili za kukosekana kwa uaminifu katika upongozi wako; watapata nafasi ya kutilia mashaka kwa kila unachofanya.
- Ukikubali makosa na udhaifu wako, watu watakuheshimu na kukusaidia.

iii. **Onyesha msimamo wa tabia isiyobadilika**.
- Chagua kusimama katika tabia ya maadili mema siku zote.
- Wafanye wale unaowaongoza kutambua la yako na ndiyo yako.

iv. **Jenga mtazamo wa huduma ya unyenyekevu**
- Tumewekwa duniani si kwaajili ya kutumikiwa bali kwaajili ya kutumika.
- Watu hawatakuamini ikiwa watagundua kuwa umetawaliwa na roho ya ubinafsi
- Roho ya huduma ya unyenyekevu ni udhihirisho wa tabia halisi ya uwakili wa Kikristo.

**VITABU VYA REJEA.**


- Leaders for today hope for tomorrow by Anthony A. D’Souza (Uk.18-59)
- Leadership by A. D’Souza (Uk 11-20)

**KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO TANZANIA UNION**

**IDARA YA HUDUMA ZA VIJANA**

**STADI ZA MAISHA**

- **Maana ya Stadi za Maisha:**

Ni mbinu ,ujuzi, au uwezo wa kuwa na tabia chanya ambayo humsaidia kijana kupambana na changamoto za maisha ya kila siku zinazoweza kumsababishia asifikie malengo yake.

**FAIDA ZA STADI ZA MAISHA**

I. Zinamsaidia kijana kujitambua, na hivyo kuishi kwa uangalifu.
II. Zinamwongezea kijana uaminifu kwa Mungu wake na hivyo kumfanya ajisalimishe maisha yote kwake.
III. Zinamfanya kijana kuheshimika katika jamii.
IV. Zinamsaidia kijana kufikia malengo aliyojiwekea katika maisha yake.
V. **Zinamfanya kijana kuwa mtu wa kutegemewa katika jamii.**
VI. **Zinaondoa magonjwa yasiyo ya lazima na kuongeza siku za kuishi.**

- **Stadi za maisha zimegawanyika katika makundi matatu.**
  1. Stadi za kujifahamu
  2. Stadi za kufikiri
  3. Stadi za mahusiano
- **Ndani ya Stadi za kujifahamu kuna Stadi tatu ambazo ni;**
  1. Kujitambua
  2. Kuhimili mihemko
  3. Kuhimili misongo
- **Ndani ya Stadi za kufikiri kuna Stadi nne ambazo ni;**
  1. Fikra bunifu
  2. Fikra yakinifu
  3. Uthubutu
  4. Kufanya maamuzi sahihi
- **Ndani ya Stadi za mahusiano kuna Stadi tatu ambazo ni;**
  1. Mahusiano.
  2. Ushilikeli
  3. Mawasiliano
- **Hivyo kwa ujumla wake, Stadi za Maisha ziko kumi kama ifuatavyo;**
  1. Stadi za kujifahamu
  2. Stadi za kuhimili mihemko
  3. Stadi za kumili misongo
  4. Stadi za fikra bunifu
  5. Stadi za fikra yakinifu

6. Stadi za uthubutu
7. Stadi za kufanya maamuzi sahihi
8. Stadi za mahusiano
9. Stadi za ushilikeli
10. Stadi za Mawasiliano

**A: STADI ZA KUJIFAHAMU: (Luka 15: 11-19)**

Vijana wengi wamejikuta wakitumbukia katika maovu kwasababu ya kutojifahamu. Masawali yafuatayo ni ya muhimu katika kumwongoza kijana kujitambua.

- Mimi ni nani?
- Kwanini nilizaliwa duniani.?
- Wajibu wangu ni upi katika jamii?

Kuyajibu maswali haya, kutamwongoza kijana kujitambua. Hebu tujaribu kuyajibu kama ifuatavyo.

- **Mimi ni nani? (Mwa 1: 26, Zab 139:14)**
  **Jibu:** Mimi ni mwanadamu niliyeumbwa kwa mfano wa sura ya Mungu .
  Nimepewa uwezo wa kutawala na kuvitiisha viumbe vyote.
  Nimeumbwa kwa jinsi ya ajabu na ya kutisha.
  Hakuna mwingine aliye kama mimi katika dunia yote.
  Hivyo **mimi ni wa pekee**, na **wewe pia ni wa pekee (Isa 49: 1)**
- **Kwanini nilizaliwa duniani? (Mwa 12:2, 2kor 3: 3, 2: 15)**
  **Jibu:** Nilizaliwa dunuani ili niwe mbaraka kwa wengine.
  Nilizaliwa ili niwe barua ya Yesu kwa wengine
  Nilizaliwa ili niwe manukato ya Yesu kwa wengine
- **Wajibu wangu ni upi katika jamii? (Yer 1: 4-10, Eze 3:17-19)**
  **Jibu:** Kuwa chombo cha kupitishia wokovu kwa watu wengine.
  Kuuonya ulimwengu juu ya hatari inayokuja ikiwa watu hawatatoa maisha yao kwa Yesu
- **Nikishajifahamu nitahakikisha kuwa nazingatia maagizo ya 1Tim 4:12 ambayo ni:**
  1. Kuhakikisha kwamba ujana wangu haudharauliwi na mtu yeyote
  2. Kuhakikisha kwamba ujana wangu unakuwa **kielelezo** katika mambo matano yafuatayo
     1) Usemi
     2) Mwenendo
     3) Upendo
     4) Imani
     5) Usafi
- ❖ **Kumbuka, mambo haya hufanywa na mtu anayejifahamu.**

**B: KUHIMILI MIHEMKO**

**Maana ya mihemko**: Ni hisia zinazomsukuma binadamu kufanya jambo fulani. Hisia hizo zaweza kuchochewa na:

- Hasira
- Wivu
- Furaha
- Majonzi/huzuni
- Tamaa ya mwili
- Upweke n.k

Kila binadamu aliyezaliwa na kuwa na akili timamu anayo mihemko. Mihemko hii haijali umri wala rangi. Haijalishi kuwa umeoa au umeolewa. Kuwa na mihemko siyo dhambi maana Mungu ameiweka kwa makusudi maalumu ya kumsaidia binadamu kuchukua hatua fulani ya maendeleo katika maisha yake. Hili litategemea jinsi unavyotawala mihemko uliyo nayo mwilini.

Mihemko hii imegawanyika katika makundi mawili.

1. Mihemko chanya
2. Mihemko hasi.

Mihemko chanya imetawaliwa na hisia zinazomsukuma binadamu kufanya shuguli za maendeleo na ukomavu kuelekea utu uzima; mfano kuoa/kuolewa, kusoma, kujenga, kunua gari, kusomesha watoto, n.k.

Mihemko hasi imetawaliwa na misukumo ya hisia zinazomsukuma binadamu kufanya uharibifu; kama vile, kuua, kujinyonga, kufanya ngono kinyume na mpango wa Mungu, kubaka, n.k

**Jinsi gani unaweza kuwa na mihemko chanya?**

i. Sikiliza ushauri kutoka kwa watu wenye uzoefu wa maisha (Mith 12:15, 13:10, 19:20;Ay 12:12)
ii. Jifunze siri za mafanikio kwa wale waliofanikiwa katika maisha.
iii. Uwe na moyo wa kujaribu jambo fulani unaloamini kuwa litakuletea maendeleo au faida.
iv. Uwe kijana mwenye njozi na kuishi kwa malengo.

**Jinsi gani unaweza kuepuka mihemko hasi?**

i. Kuomba / kufunga/kusoma neno la Mungu
ii. Kujua jinsi ya kuutawala mwili wako (1The 4:4-5)
iii. Epuka kufanya jambo lolote unapogundua kuwa umepatwa na hisia za hasira. (Mith 16:32, Mh 7: 9)
iv. Fanya kwa bidii mazoezi ya viungo.

v. Uwe na ratiba inayoeleweka
vi. Epuka kukaa katika maeneo yenye vishawishi vibaya ; kwa mfano katika kumbi za starehe. (Mith 21: 17)
vii. Uwe mlinzi wa milango yako ya fahamu. (Mith 4:23,19:19)
viii. Jihadhari na mashinikizo rika. (Mith 1:10)
ix. Chagua program zinazo jenga, unapoangalia TV au Internet.
x. Chagua vitabu na magazeti ya kusoma.
xi. Chagua marafiki wenye hekima.
xii. Jishughulishe na kazi za kanisa, mfano kuimba, kuhubiri, kuwa katika chama/idara

- ❖ Muhemko unaosumbua na kuangusha vijana wengi hata walio ndani ya kanisa, ni muhemko unaosukumwa na tamaa ya mwili (Yak 2:14-15)
- ❖ Mwili una tabia gani? Rum 8: 7-8.
- ❖ Una tabia ya kutotii sheria za Mungu.
- ❖ Unatamani vile vinavyoonekana hata kama vinapingana na neno la Mungu
- ❖ Umetawaliwa na hisia za kufanya ngono.
- ❖ Umejaa kiburi, kujiona na kujisifu.
- ❖ Umejaa wivu na kutopenda maendeleo ya wengine.
- ❖ Umejaa uongo na masengenyo
- ❖ Umejaa dharau na matukano

Paulo anasemaje? (Rum 8: 8). Hivyo ndivyo virusi vinavyofisha .

Je, ninani anayesababisha mihemko ya tamaa ya ngono?. (Math 4:8.)

Shetani hukuonyesha fahari yote ya dunia ili kukuangusha katika dhambi.

**MAMBO YANAYOCHOCHEA HISIA ZA MIHEMKO YA NGONO**

**1.** Kuangalia picha za watu walio uchi (Ponography). Picha hizi hupatikana katika baadhi ya magazeti, vitabu, majarida, runinga, tovuti, n.k

**2.** Kuangalia picha za watu wanaofanya ngono katika maeneo yaliyotajwa katika namba moja

3. Kupiga chabo (Kuangalia mtu halisi akiwa uchi au watu halisi wakifanya ngono)

4. Kutembelea majumba ya starehe kama vile bar, kumbi za dansi, kasino, fukwe za maziwa, au za bahari nyakati za usiku au siku za sikukuu

**BAADHI YA WAHANGA WA MIHEMKO YA NGONO KATIKA BIBLIA**

- Amnoni. 2 Sam 13:1…
- Daudi 2 Sam 11:1…
- Samson Waam 14: 1…

**Ushauri wa neno la Mungu**

- Fanya agano na macho yako (Ay 31:1)
- Yakimbie mazingira hatarishi. (1kor 6:18,Mwa 39:12)
- Uwe na uthubutu wa kusema **HAPANA! (**Mith 1:10)
- Epuka kuamsha hisia za ngono ( Wimbo ulo bora 3:5 )

**3 . Kuhimili Misongo. (Stress)**

**Misongo ni hali inayompata mtu anapokabiliwa na changamoto zaidi ya moja zinazomhitaji afanye maamuzi sahihi bila kuathirika kiakili; kijamii , kiroho, kimwili na kisaikolojia.**

**Kisa cha Malkia Vashti) (Esta 1:10-11) ni mfano halisi wa msongo. Changamoto zilizokuwa zinamkabili Malkia Vashti ni hizi zifuatazo:**

- Kukubali kuonyesha uzuri wa maumbile yake mbele ya umati wa watu
- Kukataa.

**Zifuatazo ni faida ambazo angezipata kama angekubali kuonyesha uzuri wa maumbile yake mbele ya watu.**

1. Angefurahisha umati wa watu na kukifanya kilele cha sherehe kufana.
2. Angeleta sifa na heshima kwa mfalme.
3. Upendo na mahusiano kati yake na mfalme vingeongezeka**.**
4. Umaarufu wake ungeongezeka.
5. Huenda angeongezewa madaraka.

**Zifuatazo ni hasara ambazo alizipata kama matokeo ya kukataa kuonyesha uzuri wa maumbile yake mbele ya watu (Esta 1:12)**

1. Alipoteza taji lake la umalkia.
2. Alidharauliwa na watu wote hasa wanawake wenzake.
3. Kwa kuonyesha maumbile yake, angeweza hata kubakwa na watu wanapomtazama anapopita mbele yao
4. Angehatarisha maisha yake hata pengine kupigwa au kuuawa.
5. Angesondwa vidole na kila mtu na kufanywa duni.

**Jambo hili lilimletea msongo maishani. Alielewa kukataa kutamgharimu.**

**MAMBO MBALIMBALI YANAYOSABABISHA MSONGO**

1. Kulazimishwa na wenye madaraka/mamlaka ili ufanye jambo lilio kinyume na imani yako. Wenye mamalaka hawa wanaweza kuwa wazazi, walezi, walimu/wakufunzi, kiongozi wa kazi (Boss) n.k

2. Upweke unaotokana na kuachwa na mchumba, kukosa marafiki wa karibu, kufiwa na mtu unayemtegemea, kufeli masomo, mzazi kukataliwa na mtoto wake, n.k (Ayubu 2:9)
3. Kufukuzwa /kuachishwa kazi iliyokuwa inakupatia kipato cha kuishi, kuibiwa mali ambazo ulikuwa unazitegemea katika kuendesha maisha yako.
4. Kukosa kazi/ajira ingawaje elimu ya kukuwezesha kufanya kazi unayo.
5. Ugumu wa maisha. Kila unalojaribu kulifanya maishani halikupi mafanikio unayoyatarajia.
6. Magonjwa yanayokufanya uwe dhaifu muda wote.
7. Kupata taarifa mbaya za kushtusha.
8. Kukosa uaminifu katika ndoa.

**MADHARA YANAYOTOKANA NA MSONGO**

**1.** Kukosa usingizi.
**2.** Kupata vidonda vya tumbo
**3.** Kupata mshituko (Stroke)
4. Kuchanganyikiwa
5. Kuamua kujiua aidha kwa kunywa sumu, kujirusha toka juu ya ghorofa, kijitupa mtoni, kujinyonga kwa kamba n.k

**DALILI ZA KUMTAMBUA MTU MWENYE MSONGO**

1. Anashikwa na fadhaa. (Hatulii sehemu moja)
2. Anaweza kuamua kulia au kucheka muda wote.
3. Mawazo yake huwa mbali na matendo yake. Kwa mfano, mara nyingi anakosa uangalifu anapovuka barabara.
4. Anapoteza mwelekeo wa kufanya shughuli zake za kawaida. Mfano anaweza kuduwaa au kukujibu jibu ambalo hukutegemea.
5. Hapendi kusemeshwa au kuulizwa maswali yanayohitaji majibu ya haraka.
6. Anamuona kila mmoja ni adui yake.
7. Anapoteza hamu ya mambo ya kiroho
8. Anapoteza hata hamu ya kula
9. Anaweza kuamua kukimbia na kuelekea kusikojulikana.
10. Anatamka maneno yanayoashiria kuwa haoni faida ya kuishi duniani.

**NAMNA YA KUKABILI MSONGO**

1. Mtegemee Mungu (Mith 3:5-6) kwa maombi na kusoma neno lake.
2. Pata ushauri kutoka kwa watu wenye hekima. (Mith15:22)
3. Uwe mvumilivu na mwenye subira kwasababu wewe si wa kwanza kupata tatizo hili. (Gal 5:19)

4. Jishughulishe na kazi za kanisa. Mfano kuimba, kushiriki shughuli za vijana, shughuli za akina mama nk. Hiyo ni dawa ya kuodoa misongo.
5. Epuka kukaa kivivu. Muda wote uwe na kitu cha kufanya.
6. Fikiria kabla ya kutenda.

**4. FIKRA BUNIFU**

Huu ni ujuzi unaotumika katika kujinasua unapogundua kuwa umezungukwa na mazingira hatarishi hasa yale ambayo yanaashiria kukusababisha utende dhambi.

**MIFANO YA MAZINGIRA HATARISHI**

- Kupelekwa na marafiki wanaokunywa pombe katika baa/kilabuni/kwenye holi za muziki wa kidunia/kwenye matamasha/sherehe za kidunia, n.k. Mahali ambapo huwezi kuomba wala kusoma neno la Mungu wala kushuhudia,
- Kutembea jinsia mbili tofauti katika maeneo ya upweke kama vile ufuoni mwa bahari/ziwa/ au eneo lolote lisilokuwa na watu mfano mlimani, kwenye magofu,n.k
- Kukaa pamoja, jinsia mbili tofauti nyakati za usiku au sehemu za giza
- Kumtembelea rafiki yako wa kiume/wa kike sehemu aliyopanga au anayoishi peke yake.
- Watu wa jinsia mbili tofauti kuhamishia makao yao kwa muda katika hoteli kwa lengo la kuliwazana au kupongezana juu ya jambo fulani.
- Kukaribishwa na boss wako katika chakula cha mchana au usiku katika hoteli fulani
- Mtoto wa kike kumpelekea mwalimu/mkufunzi wake zana za kazi nyumbani huku akifuatwa kwa nyuma.
- Mtoto wa kike anayeomba kazi na kuahidiwa na boss wake akutane naye kwanza kwenye baa au hotelini
- Kupewa zawadi nyingi za thamani zisizo na maelezo toshelevu.
- Kuletewa usafiri bure unapokwenda mahali fulani katika shughuli zako.
- Kukubali kupapaswa katika viungo vyako.
- Komba lifti ya gari kwa kila gari linalopita mbele yako.

**WAHANGA WA MAZINGIRA HATARISHI.**

Ni kweli kwamba binadamu wote ni wahanga wa mazingira hatarishi, lakini utafiti unaonyesha kuwa wahanga wakubwa ni wana wa kike. Sababu zake ni hizi zifuatazo:

- Maumbile yao ni dhaifu.

- Ni wepesi kudanganywa kwakuwa wanavutwa na kudanganywa kwa urahisi na vitu vidogovidogo.
- Wengi wa wana wa kike hawana uthubutu wa kukataa wanapojaribiwa kufanya dhambi.

**MFANO WA KIJANA ALIYETUMIA FIKRA BUNIFU KATIKA BIBLIA**

- Yusufu alitumia fikra bunifu alipolazimishwa kufanya mapenzi na mke wa bwana wake (Mwan 39:1-12)
- Ushauri wa neno la Mungu (1kor 6:18). Unapogundua kuwa upo katika mazingira hatarishi  kimbia.

**MBINU ZA FIKRA BUNIFU**

**Unapogundua kuwa umebanwa katika mazingira hatarishi; fanya yafuatayo:**

- Kamata sehemu za siri za mwanaume
- Ingiza vidole machoni.
- Sihi kuahirisha  tendo hadi wakati mwingine muafaka.
- Tumia lugha za kukatisha tamaa, kama vile "Niko katika siku zangu, nisije nikakuambukiza virusi." n.k
- Ng'ata kwa kutumia meno.

6. STADI ZA UTHUBUTU

Maana ua uthubutu:

- Ni kukataa kwa ujasiri jambo ambalo litagharimu maisha yako ya kimwili au ya kiroho.
- Kukataa kwa nguvu zote kufanya jambo ambalo litakuaibisha na kuyadhuru maisha yako na kukufanya uishi maisha ya majuto na hata kutamani kuwa heri usingelizaliwa.

Vijana wengi hasa wa kike huonyesha unyonge wa hali ya juu hasa wanapotakiwa kukanusha jambo ovu ambalo litawaletea madhara katika siku za usoni.

Vijana wenye tabia dhaifu na zenye unyonge mwingi huonekana katika mambo yafuatayo:

- ➢ Huwaachia watu wengine wafanye maamuzi yanayohusiana na masuala ya maisha yao .
- ➢ Hawasimami kidete kutetea haki zao.
- ➢ Wanapokuwa na jambo linalowasumbua, huamua kunyamaza kimya.

- Wakati mwingine huzungumza hoja zao kwa unyonge na aibu nyingi

Kijana aliye na tabia ya uthubutu atafanya yafuatayo:

- Atamweleza mtu kinagaubaga kile anachokitaka bila ya vitisho.
- Atasimamia haki yake bila kuathiri haki ya wengine.
- Atajiheshimu yeye mwenyewe na kuheshimu wengine.
- Atasikiliza na kuzungumza kwa makini.
- Atakuwa huru kueleza hisia zake chanya na hasi.
- Atakuwa na uhakika na anachosema akitumia kwa mfano "Ninafikiri…., Ninahisi…."
- Atazungumza uso kwa uso na kukazia kile anachokisema.

Maeneo yafuatayo yanahitaji uthubutu.

- Mashinikizo kutoka katika makundi rika.
- Kulazimishwa na wazazi/ndugu/walezi kuoa au kuolewa kabla ya umri.
- Kulazimishwa kufanya ngono kabla ya ndoa au nje ya ndoa.
- Kushawishiwa kuikana imani yako kwasababu ya kuoa au kuolewa.
- Kulazimishwa kurithi mke au kurithiwa na ndugu wa karibu wa aliyekuwa mume wake.
- Kushawishiwa kukatisha masomo ili kuoa au kuolewa.

Mbinu mbalimbali hutumika kumyumbisha kijana ili asiwe na uthubutu. Jifunze Jedwali lifuatalo.

| No | MBINU | MFANO |
|---|---|---|
| 1 | Kunyamazisha | • Unaogopa bure<br>• Wewe ni mkubwa sasa wa kufanya mambo haya. |
| 2 | Kujenga hoja | • Kwanini usifanye?<br>• Mbona kila mtu anafanya? |
| 3 | Vitisho | • Fanya ninavyotaka, ama sivyo, kwaheri.<br>• Nitamtamtafuta mwingine atayefanya nitakavyo<br>• Nitakuumiza, ikiwa utaendelea kukataa. |
| 4 | Kuonyesha kuwa hakuna tatizo | • Hakuna kitakachoharibika'<br>• Usihofu, nitachukua tahadhari zote.<br>• Nitashughulikia kila kitu<br>• Nimeandaa mazingira salama kwaajili yako. |
| 5 | Kutoa sababu | • Lakini hata hivyo si tutaoanatu? |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Mara moja tu hutapata mimba<br>• Hata hivyo ninakudai<br>• Sikuachii kwasababu umekua sasa.<br>• Silali wala sili chakula kwaajili yako |
| 6 | Kukutoa nje ya mada | • Una macho mazuri.<br>• Ninakupenda zaidi unapokuwa umekasirika.<br>• Unajua kuwa nakupenda? |

Mbinu za kujinasua zinaweza kuwekwa katika makundi matatu yafuatayo:

| No | MBINU | MAELEZO |
|---|---|---|
| 1 | Kukataa | • Sema hapana waziwazi na kwa uhakika<br>• Hapana, ahsante<br>• Hapana hapana- kwaheri (Ondoka) |
| 2 | Kuchelewesha | • Bado siko tayari<br>• Labda tuzungumze baadaye<br>• Ningependa kupata ushauri kwa wazazi/viongozi wangu wa kiroho kwanza |
| 3 | Kujadiliana | • Badala ya kufanya hivi tungefanya …….<br>• Sitafanya hivyo, pengine tungefanya……….<br>• Unafikiri ni kitu gani kitatufanya sisi wote wawili tufurahi na bila mmoja wetu kudhurika? |

**MIFANO YA UTHUBUTU KATIKA BIBLIA**.

1. Yusufu aliikataa ngono isiyo halali. (Mwa 39:9)
2. Musa alikataa kuitwa mwana wa binti Farao (Ebr11:24)
3. Malkia Vashti alikataa kuonyesha uzuri wake katika ukumbi uliojaa watu. (Ester 2:12)
4. Danieli aliazimu moyoni mwake kutojitia unajisi. (Dan 1:8)
5. Danieli na wenzake walikataa kuabudu sanamu. (Dan 3:16-18)
6. Timayo Batimayo alikataa kunyamazishwa kumwita Yesu. (Mark 10:48)

Ushauri wa neno la Mungu. –Mith1:10

## 7. STADI ZA KUFANYA MAAMUZI SAHIHI

**UTANGULIZI:**

Mojawapo ya mambo magumu yanayomkabili kijana ni namna ya kufanya maamuzi sahihi katika maisha. Maisha ya mwanadamu yametawaliwa na maamuzi anayoyafanya kila siku. Maendeleo mengi tunayoyaona leo, yametokana na maamuzi ya watu yanayofanywa kila siku.

Vilevile maisha yako kijana yanategemea kile unachokiamua leo. Je, unataka kuwa nani miaka kumi ijayo? Anza kuiandaa kesho leo. Kumbuka kuwa maisha ya ujana yanapita bila wewe kujitambua. Uamuzi unaoufanya leo, utakufanya uwe na furaha siku zako za usoni au uwe na huzuni.

**Kisa mkasa:**

Sarah ni mwanafunzi anyesoma katika mojawapo ya vyuo vikuu huko Ghana. Ni mwanafunzi mwenye uwezo darasani. Ni mkristo mzuri anayempenda Yesu. Anapanga kuwa mhandisi mara baada ya kumaliza masomo yake.

Alipokuwa mwaka wa nne wa masomo, wazazi wake walikufa katika ajali ya gari. Sarah alisikika akilia hivi, **"Ni nani atakayenilipia ada ya masomo yangu!, ninani atakayesomesha wadogo zangu! ni nani atakayetunza familia yetu!"**

Shaaban ni boss katika kampuni moja. Amejitoa kuisaidia family ya Sarah iliyoachwa na wazazi wao. Yuko tayari kulipa ada yote ya Sarah kwa masharti ya kufanya mapenzi naye. Shaaban ana wanawake wawili na watoto11. Watoto wake wawili wakubwa wana umri mkubwa kuliko Sarah. Mmoja ameoa na ana mtoto mmoja. Watu mbalimbali, wakiwemo akina mama wa heshima na wakutegemewa, wanamshauri sarah kuolewa na Shaaban; maana ana uwezo kifedha. Sarah anakabiliwa na changamoto kuu mbili.

1. Je, niendelee na masomo yangu au nirudi kutunza wadogo zangu?
2. Je, nikubali kutimiza matakwa ya Shaaban ili nipate ada ya masomo na famalia yetu ipate msaada kutunzwa?

Ni uamuzi gani Sarah anapaswa kuuchukua bila kuathirika kimwili, kiakili, kijamii na kisaikolojia?

**HATUA ZA KUFUATA KATIKA KUFANYA MAAMUZI SAHIHI**

- **<u>Tambua tatizo</u>: (Mwa 39:9**), tatizo hapa halikuwa ngono. Yusufu alitambua kuwa kufanya ngono isiyo halali atakuwa amevunja uhusiano wake na Mungu. Ni lazima kijana ujiulize kuwa, jambo hili nikilifanya litaendelea kudumisha uhusiano wangu na Mungu?
- **<u>Fikiria matokeo yauamuzi unaotaka kuufanya</u>: (Josh 24:15),** Daudi hakufikiria matokeo ya uamuzi alioufanya. Matokeo yake ilimgharimu. (2 Sam 11:1…).Kuna aina mbili za matokeo. Matokeo chanya na matokeo hasi. Unapolinganisha matokeo, ukagundua

kuwa matokeo hasi ni mengi kuliko matokeo chanya, ni bora uahirishe jambo hilo. Tutumie kisa mkasa cha Sarah.

| No | Matokeo chanya | Matokeo hasi |
|---|---|---|
| 1 | Atapata ada ya shule | Atakuwa amekwenda kinyume na Mungu. |
| 2 | Atafikia malengo yake ya kuwa mhandisi | Anaweza kupata mimba |
| 3 | Atakuwa mtu wa maana na mwenye kuheshimiwa katika jamii. | Anaweza kupata UKIMWI |
| 4 | Maisha yake yataboreshwa maana atapata mshahara, atanunua gari, samani za nyumbani, n.k | Anaweza kudhuriwa na wake za Shaaban |
| | | Anaweza asifikie malengo yake |
| | | Anaweza asipate hata ada ya shule baada ya Shaaban kutimiza tamaa zake |
| | | Hata pata heshima kwa wake za Shaaban |
| | | Hatapata heshima kwa watoto wa Shaaban |
| | | Anaweza kuuawa au kupigwa na watoto wa Shaaban |

- <u>**Tumia Te3**</u> **(Tatizo, Tatuzi, Tokeo) katika kufanya maamuzi sahihi.**

**Tutumie mfano wa kisa mkasa cha Sarah**

| Tatizo | Tatuzi | Tokeo |
|---|---|---|
| Kuvunja uhusiano na Mungu | Kuwa na msimamo wa neno la Mungu | Uhisiano wake na Mungu utaimarishwa<br>Imani yake itaimarishwa.<br>Mungu atampatia mlango mwingine wa kutokea |
| Kuingilia ndoa isiyo yake | Kuepuka mahusiano ya mapenzi na mume wa watu | Heshima yake kwa familia ya Shaaban itaendelea kuonekana |
| Kuliaibisha kanisa | Kuwa na msimamo wa neno la Mungu | Heshima ya kanisa itaendela kuimarika |

- <u>**Je, imani yako inakufundisha nini?**</u> **(**Ebr 11:1)
- <u>**Pata ushauri kwa watu wenye hekima.**</u> (2Ny 20:20, Mith 11:14)
- <u>**Tegemea uongozi wa Roho wa Mungu**</u>. (Rum 8:14)

**8. STADI ZA MAHUSIANO**

**Maana ya mahusiano:**

**MBINU ZA UWEZESHAJI KATIKA KUFUNDISHA MITAALA YA IDARA YA VIJANA**

**UTANGULIZI:**

- Binadamu ana njia mbalimbali za kuingizia maarifa akilini.
- Anatumia milango mitano/sita ya fahamu, ambayo ni kuona, kusikia, kunusa,kugusa, kuonja na kuhisi.
- Watafiti wa masuala ya binadamu wanasema, binadamu hukumbuka 30% kwa kusikia, hukumbuka 50% kwa kusikia na kuona, hukumbuka 80% kwa kusikia, kuona na kutenda.
- Kadiri unavyoshirikisha milango mingi ya fahamu, ndivyo unavyopanua wigo wa kumfanya kijana kuelewa zaidi.
- Unapoandaa mada, jiulize maswali yafuatayo "Nifanye nini ili vijana wasikie, waone, washike, wanuse, n.k
- Kwa ujumla kinachohitajika hapa ni **ubunifu**
- Kila binadamu ana kiwango fulani cha maarifa. Hili halijalishi umri wala maeneo anayoishi.
- Anachotakiwa kusaidiwa ni kumwongezea maarifa kutoka kwa kile anachoelewa, kuelekea kwa kile asichokifahamu.
- Hivyo unaposimama kutoa maarifa, usiwe kama **Imamu** ukidhani wale wanaokusikiliza ni **Mamuma**
- Hatua ya kwanza unayopaswa kuchukua ni kupima kiwango chao cha uelewa kwa kutumia dhana ya **ushirikishwaji (Participatory method)**
- Hii ina maanisha kwamba, katika dhana hii ya ushirikishwaji hakuna mwalimu wala mwanafunzi ila kuna mwezeshaji na wawezeshwaji.
- Mwezeshaji anaposimama, anafanya kazi ya kuwajengea uwezo **(Capacity building)**
- Hivyo mwezeshaji asipuuze wazo la kila mwezeshwaji, maana laweza kuwa na ukweil kiasi fulani, ila likahitaji maboresho kiasi zaidi.
- Katika dhana hii ya ushirikishwaji, wanenaji wakuu ni wawezeshwaji.Watie moyo wawezeshwaji wa jinsia ya kike kutoa mawazo yao.
- Elekeza majadiliano yao kwenye mada husika.

**MATAYARISHO YA AWALI**

Mwezeshaji mzuri ni lazima aandae mazingira ya kujifunzia kabla wawezeshwaji kufika.

- Andaa mazingira mazuri ya kujifunzia. Chumba lazima kiwe safi, vipaza sauti, generator ya akiba, hewa ya kutosha, utulivu wa kutosha, n.k
- Wapange wawezeshwaji katika mfumo wa duara na sio mfumo wa darasa..
- Wape nafasi wajitambulisha ili wafahamiane, huku wakitaja majina yao, makanisa wanayotoka, na kazi zao kanisani.
- Wape nafasi ya kutengeneza sheria za mkutano.
- Wape nafasi wataje hofu au wasiwasi walio nao, na matarajio yao.

- Hakikisha kwamba unazijibu hofu au wasiwasi walio nao ili kuwafanya wawe na amani wanapoendelea kujifunza
- Wafahamishe  taratibu zao za ukaaji katika hiyo semina, ukiwaeleza bayana ninini watarajie kupata katika semina hiyo. (Mfano, mahali pa kulala, chakula, vitini, n.k)
- Wape nafasi watunge sheria za semina au mafunzo.
- Itambulishe mada na waruhusu kuijadili.
- Waweza kuwagawa katika vikundi il kwenda kujadili mada zingine na kuleta mrejesho.
- Hitimisha mada kwa kukazia sehemu muhimu.

**MAMBO MUHIMU YAMPASAYO MWEZESHAJI KUYAKUMBUKA** .

- Wakaribishe wana semina
- Toa sauti ya kusikika.
- Watazame wana wawezeshwaji.
- Waite kwa majina.
- Washirikishe wawezeshwaji katika kuchangia mada.(Kwa kuwauliza maswali,, kujibu maswali, kuchangamsha darasa kwa wimbo au mpasho, kuwagawa katika vikundi, n.k
- Tawala darasa.
- Usitawaliwe na notice
- Jali muda wa kuanza na muda wa kumaliza.
- Wape motisha wale waliofanya vizuri.
- Badilisha mazingira ya kujifunzia
- Wasomee utaratibu utakaofuata baada ya shughuli za siku hiyo kwisha.
- Unaweza kutoa karatasi ili kuwapa nafasi ya kuandika maoni yao bila kuandika majina yao.

**MATAYARISHO YA AWALI YA MWEZESHAJI**

**Kabla hujasimama mbele ya watu, fanya matayarisho yafuatayo.**

- Jiandae kiroho. Ingia katika huduma ya maombi. Jiombee nafsi yako. Waombee wale unaokusudia kuwapatia maarifa mapya.
- Ingia katika kusoma neno la Mungu. Jilishe chakula cha kiroho. Soma Roho ya Unabii. Jishibishe wewe kwanza.
- Andaa vitendea kazi, ambavyo ni vitabu, miongozo, zana za kuwezesha, n.k
- Jiandae kimwili. Hii ni pamoja na kuwa msafi, kuvaa vizuri,kuwa mchangamfu na mwenye tabasamu wakati wote.
- Kumbuka mwonekano wako wa nje una mvuto wa kwanza kuliko hata kile unachokwenda kuwezesha.
- Andaa mazingira ya kujifunzia. Pata funguo za jengo mapema, hakikisha eneo ni safi, andaa mpangilio wa ukaaji ndani.
- Fika mapema kabla ya wengine wote ili uhakikishe kuwa, kila kitu kiko mahali pake.

- Kumbuka, hawa ni wateja wetu. Kila jambo tunalolifanya, laweza kuwafanya wabaki nasi au watuache.

**SAIKOLOJIA YA KUJIFUNZA.**

- Mtu hujifunza akiwa tayari.
- Mtu hujifunza ikiwa kile anachofundishwa ndilo hitaji lake.
- Mtu hujifunza ikiwa kile kinachofundishwa kina mvuto kwake.
- Mtu huwa tayari kujifunza ikiwa ana mahusiano mazuri na mwezeshaji wake.
- Mtu huwa tayari kujifunza ikiwa anapata maarifa mapya.
- Mtu huwa tayari kujifunza ikiwa anashirikishwa.

**UTUMIAJI WA MITAALA**

**A:ELEWA KILICHOMO NDANI YA MTAALA**

Idara ya vijana ni taaluma. Hakuna namna ya kuwa mwezeshaji mzuri kama huna mitaala ya idara au hujaipitia mitaala ya idara ya vijana na kuielewa elimu iliyomo ndani ya mitaala hiyo. Mwinjilisti mzuri anayefaulu kuuza vitabu vyake, ni yule ambaye anaelewa ujumbe uliomo katika vitabu hivyo, japo kwa muhtasari tu. Huwezi kuwa mwezeshaji mzuri ikiwa huelewi hata kilichoandikwa ndani ya mitaala hiyo.

Hivyo, ni wajibu wa mwezeshaji kwanza kuelewa kilichomo katika mtaala anaokusudia kuufundisha.

**B:CHAMBUA TAALUMA ILIYOMO KATIKA MTAALA**

Si kila kilichomo katika mtaala kinafaa kufundishwa katika mazingira ya kanisa lako.Taaluma nyingine inafaa kufundishwa katika mazingira ya mijini,au hata katika nchi za nje.Chambua taaluma inayofaa kufundishwa katika mazingira yako.

**C: UWEKE MTAALA KATIKA LUGHA RAHISI.**

Hakikisha kuwa, taaluma iliyomo ndani yake unaiweka katika lugha inayolingana na uelewa wa waelimishwaji, bila kupoteza maana iliyokusudiwa na watunzi wa mtaala. Hili litakufanya uwe na daftari lako mwenyewe unalotumia kutengeneza notisi zako.

**D: TUMIA VITABU VYA ZIADA**

Vitabu vya ziada ni vile ambavyo havimo katika mitaala yetu, lakini vina taaluma iliyomo katika mitaala yetu. Mada zilizomo katika vitabu vya ziada huenda zikawa na ufafanuzi mzuri kuliko ule uliomo katika mitaala yetu.

**E: TENGENEZA ANDALIO LA SOMO KABLA YA KUWEZESHA**

Andalio la somo ni mpango ulioratibishwa, unaoonyesha wakati muafaka wa kufundisha mada fulani, muda utaotumika, na mbinu utakazotumia kufikisha ujumbe kwa hadhira iliyokusudiwa. Vifuatavyo ni vipengele muhimu vinavyopaswa kuonekana katika kuandaa andalio la somo

- Tarehe
- Mahali
- Mada kuu
- Mada ndogo
- Muda
- Kazi za mwezeshaji
- Kazi za mwezeshwaji
- Zana
- Maoni/Tathmini

**JEDWALI LA ANDALIO LA SOMO**

| TAREHE | MAHALI | MADA KUU | MADA NDOGO | MUDA | KAZI ZA MWEZESHAJI | KAZI ZA MWEZESHWAJI | MAONI/TATH |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **12.1.2011** | **BURKA** | **VITAMBULISHO VYA UANACHAMA** | Nembo za chama | Dk 40 | • Kueleza maana ya nembo za chama na umuhimu wake<br>• Kuuliza maswali<br>• Kujibu maswali | Kumsikiliza mwezeshaji, kujibu maswali, kuuliza maswali, | Somo lilifundi kama lilivyopa |
| 19.1.2011 | -do- | -do- | Sare ya chama | -do- | • Maana ya sare ya chama na umuhimu wake,<br>• Aina ya sare za chama,<br>• Ukamilifu wa sare ya chama.<br>• Uvaaji wa sare ya chama<br>• Kanuni za uvaaji wa sare ya chama | -do- | Halikufundish kwasababu si kulikuwa na m Litafundishwa tarehe 26.1.2 |

**SANAA YA UWEZESHAJI**

Uwezeshaji ni sanaa ya muhimu kwa mwezeshaji kuwa nayo. Unaweza ukawa na andalio zuri la somo, lakini ukashindwa kuwasilisha maarifa yaliyokusudiwa kwa kukosa sanaa ya uwezeshaji. Mambo yafuatayo ni ya muhimu unapohitaji kuwezesha.

i. Uwe na notisi za kufundishia.
ii. Hakikisha wawezeshwaji wamekaa katika mkao wa kuwezeshwa.
iii. Wasalimie wawezeshwaji.
iv. Tambulisha mada unayokusudia kuwezesha.Yaweza kuwa imeandikwa ubaoni, au katika karatasi au imerushwa kwa projector kwenye kitambaa cheupe au kwenye screen.
v. Anza na kisa mkasa, au wimbo, au onesho (Role play), au igizo (Drama) au hadithi ili kuvuta hamu na usikivu. (Apetizer). Hakikisha kuwa hicho ulichochagua kuanza nacho kinaendana na mada unanyokusudia kuiwezesha. Kumbuka ni kitu kinachoamsha

usikivu. Ni lazima kiwe kitu chenye nguvu ya mvuto kwa wasililizaji. Kinafananishwa na ndege inayokusudia kupaa.

vi. Waulize wawezeshwaji maswali yafuatayo: Je, umeona nini? Au umesikia nini?Je, hiki kitu ulichokiona au hiki kisa ulichokisikia kinaweza kutokea katika maisha ya kila siku?, Je, unaweza kutoa mfano mmojawapo halisi unaoufahamu unaofanana na kisa hiki?

vii. Kumbushia mada itakayozungumziwa. (Mfano-kama unavyoona pale ubaoni, au katika karatasi iliyo mbele yako, mada tutakayozungumzia leo inahusu jinsi na ujinsia.)

**viii.** Waulize maswali yanayohusiana na mada hiyo. Au waweza kuwagawa katika vikundi na kila kikundi ukipatie swali la kujadili. Mfano, tutagawanyika katika vikundi vya majadiliano vitano. Kundi namba moja watajadili nini maana ya **jinsi**. Kundi la pili watajadili nini maana ya **ujinsia,** kundi la tatu watajadili swali lisemalo, mtoto alipozaliwa, mama alijuaje kuwa amepata mtoto wa kike au wa kiume?, kundi namba nne, jaza majina viungo vinavyokosekana katika picha hii. Kundi namba tano liorodheshe kanuni za usafi katika viungo vya uzazi. Kila kundi watachagua mwenyekiti na katibu wake.

**ix.** Ikiwa uliwagawa katika makundi, wape nafasi ya ktoa mrejesho.

**x.** Ongezea pale panapopungua au boresha pale palipo hafifu.

**xi.** Wape maarifa mapya.

**xii.** Hitimisha mada kwa kutoa ufupisho wa mada.

**xiii.** Kazia mambo ya msingi katika mada yako.

**xiv.** Waeleze kile kitakachoendelea kesho.

**xv.** Wakumbushe kutoa maoni yao katika karatasi iliyoko ukutani.

**SHUGHULI ZINAZOFANYIKA KATIKA VIKUNDI**

1. Majadiliano katika vikundi, yataongozwa na kusimamiwa na kiongozi wa kikundi aliyechaguliwa na wana kikundi.
2. Katibu ambaye pia huchaguliwa na wana kikundi, ataandika majibu yote yaliyotolewa na wana kikundi
3. Katika kuleta mrejesho, mwenyekiti wa kikundi atasimama na kuwatambulisha wawezeshwaji jina lake, jina la kikundi chake, idadi ya wana kikundi na mada waliyopewa kuijadili.
4. Ndipo atamkaribisha katibu wake kuwasilisha majibu ya mada waliyopewa.
5. Mwenyekiti ataruhusu nyongeza toka kwa wana kikundi
6. Mwenyekiti ataruhusu maswali au nyongeza kutoka kwa wawezeshwaji.
7. Ikiwa kuna uwezekano, hayo majibu yabandikwe ukutani kwajili ya wale wanaoandika notisi zao.

**MAMBO YAKUZINGATIA KATIKA VIKUNDI**

I. Majadiliano katika vikundi ni ya siri. Mifano mbalimbali inaweza kutolewa kwa kugusa maeneo fulani au hata majina ya watu kwa nia ya kujifunza. Hayo yote hubaki kuwa siri ya wana kikundi.

II. Mawazo ya kila mtu yanapaswa kuheshimiwa.

III. Ongea kwa kifupi ili kuwapa nafasi wengine wapate kuongea.

IV. Jali muda wa kuanza na muda wa kumaliza.

V. Shirikisha jinsia zote katika majadiliano.

**MBINU ZA UWEZESHAJI**

Ili kujenga maarifa na stadi, zinazohitajika na vijana, ni vizuri uwezeshaji uwe wa kuchangamsha na kuwapatia vijana vigezo vya kukumbuka baada ya mafunzo. Njia bora ya kufanikisha haya ni kutumia mbinu shirikishi. Washiriki wenyewe wanafanya vitendo mbalimbali na kisha kujadili matokeo yanayojitokeza . Ni muhimu kwa mwezeshaji kuwa na upeo wa kuongoza vitendo hivi vya majadiliano yake. Mara nyingi matayarisho ya kila zoezi au kitendo huwa ni pamoja na kutayarisha maswali ya kuongoza majadiliano. Mfano wa maswali kama haya ni:

- Je, umeona nini kilichofanyika hapa?
- Ulijisikiaje au ulijihisi vipi wakati zoezi hili lilipofanyika?
- Zoezi hili linatufundisha nini"
- Je, ungelikwa wewe ungelifanya jambo gani la tofauti?
- Unafikiri nini kingefanyika kuboresha jambo hili?

**Baadhi ya mbinu shirikishi ni hizi zifuatazo**:

- ✓ **Majadiliano:** Yanaweza kufanyika kwa pamoja ama kwa vikundi. Washiriki hujadiliana kuhusu mada waliyopewa. Mbinu hii ni muhimu kwasababu watu huchangia na kushirikisha mawazo na uzoefu wao kwa njia ya mazungumzo. Mara nyingi majadiliano ya vikundi hutoa nafasi kwa washiriki wenye aibu ambao wasingezungumza mahali kwenye watu wengi Ni vema kama mwezeshaji akitoa vidokezo vya nmajadiliano mwanzoni mwa zoezi na kufunga majadiliano mwishoni kwa kutoa mwelekeo ulio sawa.
- ✓ **Maigizo dhima:** (Role plays) Haya ni maigizo mafupi ambayo washiriki hujifanya kuwa watu fulani au huchukua majukumu fulani ili kuonyesha mambo yanayojitokeza katika hali fulani. Ni wajibu wa mwezeshaji kuwapa waigizaji hali inayotakiwa kwenye igizo dhima. Pia ni wajibu wa mwezeshaji kutayarisha maswali yatakayoongoza majadiliano.
- ✓ **Visa mkasa:** Hizi ni hadithi fupi zilizotungwa au za kweli zinazoeleza matukio au matatizo fulani. Washiriki hujadili hadithi hizi kwa kufuatisha mwongozo wa vidokezo walivyopewa.Siyo lazima mwezeshaji atayarishe visa mkasa kila vinapohitajika . Wakati mwingine anaweza kuwaomba washirkiki watoe visa mkasa vinavyotokana na uzoefu wao.
- ✓ **Picha za uchokozi;** Mwezeshaji anaweza kutayarisha picha inayohusika na mada na kuwaonyesha washiriki. Kisha awaulize washiriki kile walichoona kwenye picha hizo. Njia hii huibua mjadala ambao mwezeshaji aweza kuuongoza ili kufikia tamati fulani.
- ✓ **Bungua bongo**: Mwezeshaji hutoa tatizo, huuliza swali au hutoa mada yoyote inayohusiana na somo fulani. Kisha washiriki hutoa mawazo yao bila kuingiliwa. Kila wazo linalotolewa liandikwe bila kufanyiwa marekebisho au uhariri wowote. Mwisho wa zoezi, washiriki wakiongozwa na mwezeshaji huchambua mawazo yote yaliyotolewa nakuyapanga kulingana na jinsi yanavyohusiana na mada husika. Kisha wote hujadili na kufikia mwafaka.
- ✓ **Michezo:** Michezo kama ile ya kuunganisha maumbo n.k inaweza kutumika ili kuimarisha maarifa na stadi.
- ✓ **Sinema/picha za video:** Ziko picha nyingi ambazo zina maudhui yanayowahusu vijana katika ulimwengu wa leo. Ni vema picha hizi zikaonyeshwa na kisha zijadilliwe

## KOZI YA MSINGI KWA VIONGOZI WA WAVUMBUZI

**Falsafa ya program za Wavumbuzi**

Program za Wavumbuzi zimeanzishwa ili kuwasaidia wazazi katika wajibu wao mkuu kama walimu wa msingi na wahubiri. Program hizi zimelenga kukuza uhusiano wa mtoto na mzazi na maendeleo ya mtoto kiroho, kimwili, kiakili na kijamii. Kupitia maendeleo ya mtoto kanisa, kaya na shule vinaweza kufanya pamoja na wazazi kuendeleza ukomavu wa mtoto mwenye furaha.

Rasilimali kubwa ya kanisa ni watoto wetu, hivyo tunakabiliwa na changamoto ya kutoa huduma kwao tangia umri wao wa awali. Tunataka mazoea sahihi, mafikara, tabia, mielekeo mizuri viendelezwe. Mwenye hekima aliandika:- Mlee mtoto katika njia impasayo, naye hataicha hata atakapokuwa mzee. Mith 22:6

**Historia ya Huduma za Wavumbuzi**:- (Advetenture Club Manual p. xiii)

Ili kusaidia watoto kujifunza zaidi Biblia, afya, na asili, na hivyo kuendeleza ujuzi watu wake, General Conference katik mwaka 1939 iliidhinisha wazo la madarasa ya Wavumbuzi ya Nyuki wa Shughuli, Mwali wa jua, Mjenzi, na Mkono wa Msaada.

Katika mwaka 1972 Conference ya Washington ilianzisha chama kwa ajili ya watoto kilichoitwa “Beavers” chini ya maelekezo ya Carolee Riegel. 1980 Conference nyingi zilikuwa zimesha anzisha vyama kwa ajili ya watoto. 1988 – Divisheni ya Amerika kaskazini Idara ya huduma za kanisa ilialika zile Conference zilizohamasika, na wataalamu wa watoto kujifunza na kutathimini wazo la chama Wavumbuzi. Walikutana mwaka 1989 kuhakiki mitaala ya wavumbuzi, kuunda/kuanzisha tuzo za wavumbuzi, na kuandika miongozo kwa ajili ya Muundo wa chama cha Wavumbuzi.
Ile kamati ilihusisha viongozi wa shule ya sabato ya watoto, viongozi wa Elimu, na mabingwa wa kaya na familia.

**KUWAELEWA WAVUMBUZI**

- Mvumbuzi ni mtoto ambaye yuko kati darasa la kwanza na la nne na kwa mujibu wa umri ni kati ya miaka 6 na 9.
- Kila mvumbuzi ni mtu wa pekee/maalumu. Zipo tabia ambazo ni za umri wa wavumbuzi peke yao:

| Tabia za Wavumbuzi (kama vile anajieleza mwenyewe) | “Mwitikio” Namna ya kufanya |
|---|---|
| **Kimwili**<br>- Nina nguvu<br><br>- Ninakua | <br>- Tafadhali usinitake mimi kukaa tu kwa muda wote nataka Kufanya vitu.<br>- Nifanye nikue vizuri kwa kucheza michezo na shughuli za Ubunifu. |
| **Kiakili**<br>- Najifunza kwa kutenda.<br>- Ni mdadisi kwa kila kitu<br><br>- Naelewa ninachoweza kuona na kugusa<br>- Ninakariri kwa urahisi<br>- Napenda mambo mbalimbali | <br>- Usiniambie tu vitu, niache nijaribu na kuwa mzoefu navyo.<br>- Natakakujua kuhusu ulimwengu wangu niambie njia nzuri (ya kuweza kuuelewa)<br>- Nionyeshe njia nzuri ya kutumia kumbukumbu zangu nzuri kwa kusudi zuri/jema.<br>- Napenda hadithi na kuvumbua mambo<br>- Tumia aina nyingi za hadithi, nyimbo, michezo, na Shughuli. |
| **Kijamii**<br>- Najifunza elimu ya jamii<br><br>- Ninajitegemea binafsi zaidi<br><br>- Ninahitaji mafanikio na msaada toka kwako | <br>- Nipe muda wa kutosha wa kuhusiana na wengine katika makundi rika<br>- Niruhusu nivumbue na kufanya mambo mwenyewe pale inapowezekana.<br>- Nisaidie kuona vitu ninavyoweza kufanya vizuri, na nifanye nielewe kuwa unanijali. |

| | |
|---|---|
| - Nasisimka kwa urahisi (I am easily over excited)<br><br>- Ni mshirika (I am very social | - Nahitaji muundo na uongozi kudhibiti hisia zangu na mihemko ya ghafla.<br><br>- Napenda kucheza na kuzungumza na marafiki zangu. |
| **Kiroho:**<br>- Nahusika katika kubainisha kati ya mema na mabaya<br><br>- Ninahamasika kwa fursa zangu binafsi<br><br>- Ninatafuta maarifa ya kibiblia. | - Nisaidie kuelewa yaliyo mema na kwanini kanuni (rules) ni muhimu.<br><br>- Niongoze kufanya maamuzi yaliyojengwa katika upendo na mvuto kwa wengine<br><br>- Niko tayari kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi naweza kuomba na kufanya maamuzi yaliyojengwa juu ya Biblia. |

**UONGOZI**

Sheria na Ahadi za Wavumbuzi

**Ahadi**

Kwa kuwa Yesu ananipenda, nitafanya vyema kila wakati.

**Sheria:**

1. Kuwa mtii
2. Kuwa safi
3. Kuwa mkweli
4. Kuwa mwema
5. Kuwa na heshima
6. Kuwa Msikivu
7. Kuwa tayari kutoa msaada
8. Kuwa na furaha
9. Kuwafikiria wengine
10. Kuwa na kicho mbele za Mungu

**Ahadi:** Watoto waelekezwe kuutambua upendo wa Yesu kwao ili nao wampende. Kutambua vile Yesu anavyokupenda husaidia kujitoa kumtumikia.

**Sheria:**

1. Kuwa mtii - Utii kwa wazazi na utii kwa Mungu
2. Kuwa safi - Usafi wa kimwili na usafi kiroho (mf. Kufua nguo, kuoga, kupiga mswaki, kusafisha mazingira nk. Na kiroho:- kusoma neno la Mungu na maombi na kufanya yale yaliyo mapenzi ya Mungu.
3. Kuwa mkweli -Ndiyo yako iwe ndiyo na hapana iwe hapana. Kuepuka udanganyifu wa namna zote
4. Kuwa mwema -Wema unajulikana kutokana na zile huduma za mtu kwa wengine zaidi ya kusema tu. Mf. Wema wako kwa mwenye kiu ni kumpa maji na sio umwambia maji ni mazuri kwa kukata kiu.
5. Kuwa na heshima -Amri ya tano kati ya zile kumi inazungumzia jambo hili, Baba na Mama huwakilisha watu wote. Kuheshimu baba na mama kutaongoza katika kumheshimu Mungu.
6. kuwa msikivu -Kutulia na kusikiliza mashauri na mafundisho ya wazazi, walimu na viongozi wengine.
7. Kutoa msaada -Kusaidia wahitaji ni kujiwekea akiba kwa Mungu mbinguni

8. Kuwa na furaha -Ni kinyume cha huzuni. Huboresha afya na kuongeza siku za kuishi

9. Kuwafikiria wengine -Kuepuka ubinafsi

10. Kuwa na kicho - Kutetemeka, kuwa na hofu vinavyosababishwa na kuutambua ukuu wa Mungu sio kutetemeka na hofu kama za aliyekutana na Nyoka au simba.

**MUUNDO**

Jedwali la Muundo wa Chama cha Wavumbuzi kanisa la kiulimwengu.

1. Kanisa mahalia- Linaongozwa na uchaguzi wa maofisa na wakuu wa maidara. Mkurugenzi wa chama cha Wavumbuzi huchaguliwa kila mwaka au kila baada ya miaka miwili.

2. Conference/Field – Hufanywa na makanisa mahalia ya eneo Fulani lililopangwa na inawajibika kwa makanisa yote na kazi ya uinjilisti. Mkurugenzi wa Conference/Field wa Wavumbuzi huchaguliwa kila baada ya miaka mitano (5)


3. Union – Hufanywa na Conference mbalimbali katika himaya iliyoamrishwa. Uongozi kila baada ya miaka mitano (5)

4. Division – Huundwa na Union mbalimbali katika eneo maalumu lililotengwa.


5. General Conference – Hufanywa na Division zote zilizopo duniani – Mkurugenzi huchaguliwa kila baada ya miaka mitano (5)

6. Viongozi wa ngazi hizo ni
    1. Conference/Filed ………………………
    2. T. U Pr. Joseph Dizombe
    3. DV. Magulilo Mwakalonge
    4. GC. Gilbert R. Cangy

Jedwali la Muundo wa Wavumbuzi katika kanisa dogo mahalia



**KANISA KUBWA**




**Club Uniform (Sare za Chama)**
Sare hufanya chama kuwa halisi na mwonekano mzuri inakuwa utambulisho na huwakilisha viwango vizuri. Moja ya njia ya kuweka viwango na kuwainua wanachama na kuwafanya kuwa na mvuto ni sare. Inashauriwa kila mwanachama wa wavumbuzi awe na sare.

**Sare hizo ni kama ifuatavyo**:-

1. Suruali/Sketi Bluu nyeusi
2. Shati/Blauzi Nyeupe
3. Mkanda Bluu nyeusi
4. Skafu Orange
5. Viatu Vyeusi
6. Soksi Nyeupe

**Itavaliwa wapi?**
Sare ya Wavumbuzi itavaliwa tu katika matukio yafuatayo:-

1. Kwenye mikutano ya kawaida ya wavumbuzi
2. Kwenye program maalumu mf. Siku ya Wavumbuzi, kupokea wanachama wapya (induction), kuhitimishwa (investiture) nk.
3. Kwenye mikusanyiko mingine ya hadhara ambapo wavumbuzi wanatumika kama wahudumu, wakaribishaji, watoa huduma ya kwanza Guards of honor, color of honor n.k

**TUZO ZA WAVUMBUZI**
Tuzo za Wavumbuzi ni ujuzi au Elimu inayotolewa kwa Wavumbuzi ili kupanua ufahamu wao katika mambo mbali mbali. Kiongozi au mwalimu wa Tuzo za Wavumbuzi anatakiwa awe mbunifu ili kufanya tuzo hizi kuwa na manufaa kwa watoto. Atie moyo kila mtoto kufanya vizuri. Mwalimu lazima azifahamu vizuni na namna ya kuzifundisha.

**Baadhi ya Tuzo hizo ni:-**

1. Artist - Uchoraji
2. Astronomer - Unajimu
3. Basket maker - (Kutengeneza vikapu)
4. Bible 1 - Kujifunza Biblia I

5. Bible II - Kujifunza Biblia II
6. Computer skills -Ujuzi wa computer
7. Environmentalist -Utunzaji wa mazingira
8. Friend of animals -Rafiki wa Wanyama
9. Friend of nature -Rafiki wa asili
10. Road safety -Usalama barabarani
11. Trees -Miti
12. Cyclist -Uendeshaji wa Baskeli
13. Fitness fun -Mazoezi
14. Friend of Jesus -Rafiki wa Yesu
15. Gardener -Bustani
16. Swimming fun -(Kuogelea
17. Temperance -(Kiasi)

Hizi ni baadhi tu kati ya nyingi zipatazo karibu hamsini (50).

**Program za Chama cha Wavumbuzi**

Luka 2:52. Naye Yesu akazidi kuendelea katika hekima na Kimo, akimpendeza Mungu na Wanadamu.

Fungu hili linabeba mambo makuu manne ambayo program za Wavumbuzi ni lazima ziya zingatie.

1. Kimo - Kimwili
2. Hekima - Kiakili
3. Kumpendeza Mungu - Kiroho
4. Kuwapendeza Wanadamu - Kijamii

Kwa sababu Wavumbuzi wako katika hatua za ukuaji, program zao lazima zilenge kuwakuza vijana hawa kimwili na kiakili pia. Mazoezi, Michezo, Maswali ya ufahamu, Ziara za majifunzo, Nyimbo, na Michezo ya Biblia ni vya muhimu sana katika ukuaji huo.

Wafundishe maadili mema wewe mwenyewe ukiwa kielelezo. Panga siku za kujumuika na wazazi wao.

**ELIMU YA KUJIEPUSHA NA UKIMWI**

Watoto wa Umri huu wa 6-9 (Kando ya wale wachache ambao huenda waliathirika wakati wa kuzaliwa na wazazi walio na Ukimwi) hawajaambukizwa bado. Kwa sababu hiyo, ni muda muafaka kuwafundisha athali za Ukimwi na jinsi wawezavyo kuepuka maambukizi hayo. Tumia miongozo iliyokubaliwa na Kanisa kuwafundisha Wavumbuzi.

# KOZI YA MSINGI KWA WATAFUTANJIA

## Sehemu ya I: Historia, Falsafa na Lengo la Chama cha Watafuta njia

1. Falsafa na Lengo la Chama cha Watafutanjia

***Falsafa***

WOKOVU na MAFUNZO ya Vijana ni moja ya Utume muhimu wa kanisa la Waadventist wa Sabato

**Kwa nini**

Kwasababu ya:

- Mithali 22:6 – Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.
- Kuvunjika kwa Mfumo wa Jamii
- Kuvunjika kwa Mfumo wa Familia
- Wtoto wa Kiadventist katika Shule zisizo za Kiadventista.

**Pathfinder song**

Oh! We are the Pathfinder strong,
the servants of God are we.
Faithful as we march along,
in truth and purity.
A message to tell to the world,
a truth that will set us free.
King Jesus the Savior's coming back,
for you and me.

**Lengo la Watafutanjia**

Ujumbe wa Marejeo uhubiriwe Ulimwenguni mwote katika kizazi hiki.

**Motto Wa Watafutanjia**

Kwa maana Upendo wa Kristo watubidisha.

**Ahadi Ya Watafutanjia**

Kwa Neema ya Mungu,
Nitakuwa Mpole, Mwaminifu na Safi,
Nitazishika Sheria za Watafutanjia,
Nitakuwa Mtumishi wa Mungu na Rafiki wa Wanadamu.

**Sheria Za Watafutanjia**

Sheria za Watafutanjia ni kwaajili yangu kwa:

1. Kushika somo la Asubuhi na Kuomba.
2. Kufanya bidii katika Mambo yote.
3. Kutunza mwili wangu.

4. Kuwa na Moyo safi.
5. Kuwa na adabu na utii.
6. Kuhesimu Nyumba ya Mungu.
7. Kufurahi daima.
8. Kufanya kazi ya Mungu.

***<u>Lengo</u>***

1. Wasaidie Watafutanjia kuelewa kuwa kanisa linwapenda, linwajali na linawathamini na linwahitaji katika program zake zote za Kanisa.
2. Waonyeshe Watafutanjia kile ambacho Mungu amewaandalia.
3. Wafundishe Watafutanjia huduma ya Utume.
4. Fanya kwaajili ya wokovu wa kila Mtafutanjia.
5. Kuza kwa kila Mtafutanjia hali ya kufurahia na kuthamini viumbe vya asili na kujali mazingira.
6. Wafundishe ujuzi ambao utawajengea maisha yenye maana na kuwaletea faida.
7. Watie moyo kutunza afya zao.
8. Toa nafasi kwaajili ya kukuza vipawa vya uongozi.
9. Kuza Elimu sawia ya Kimwili, Kiakili, Kroho, Kijamii na Maisha kiroho.

**2. Historia ya Chama cha Watafutanjia**

**Mwanzo wa JMV – (Junior Missionary Volunteers)**

- Mwaka 1907 – hatua za awali za kiofisi zilifanywa kuanzisha utendaji wa vijana wadogo huko Mount Vernon, Ohio nchini Marekani.
- Mwaka 1911 – klabu za Wavulana zilianzishwa katika Takoma Park, Maryland Marekani (clab hizo ziliitwa Takoma Indians. Mission Scouts, Woodland Clan na Pals)
- Baada ya vita ya kwanza ya Dunia viongozi wa Vijana wa Kanisa la Kiadventista walianzisha mtazamo mpya wa kufundisha Vijana. Masomo kama Masimulizi, Hiking, Michezo, Sanaa, Moto wa Kambi na Ufundi/Kazi za Mikono. Mambo hayo yalifundishwa katika Conference nzima.
- Mwaka 1919 – A. W. Spalding, alianzisha Missionary Scouts Organization huko Madson, Tenesee kwa Vijana wake na Marafiki zao. Huyu ndugu ndiye aliyeanzisha Ahadi na Sheria ambazo baadaye zilikuja kutumika katika Junior Missionary Volunteers (JMV)
- Mwaka 1920 – Harriett Holt alichaguliwa kama Katibu mdogo wa JMV katika General Conference. Lengo likiwa kuhamasisha program hii ya vijana wadogo kila mahali.
- 1921 – JMV ndipo ilipoanzishwa rasmi.

**Chama cha Watafutanjia (Pathfinder Club)**

Neno "Pathfinder" kwa mara ya kwanza lilitumika katika program za JMV na Walei wawili huko Santa Ana, California mapema miaka ya 1930. Hiki kilikuwa na chama cha Wavulana kilicho endesha program ambazo zinafanana sana na tufanyazo leo. Mwaka 1940 – Conference nyingi katika Amerika ya Kaskazini waliendesha program za Pathfinder. Katika Pacific Northwest - L. A. Sknar alikuwa katibu wa MV wa Union. Chama kilijulikana kama Trailblazers (Waonyesha njia kwa kutumia alama). Mwaka 1946 – J. H. Hankock, kama katibu wa MV katika Conference ya South Eastern California aliendesha kambi la Watafutanjia (Pathfinder Camp) lilijulikana kama JMV Pathfinder Camp. J. H. Hankock ndiye aliyefanya

mambo yafuatayo; Mwaka 1946 – alibuni Nembo ya Dunia ya Watafutanjia, Mwaka 1948 – Bendera ya Watafutanjia ilibuniwa na Mwaka 1952 – Wimbo wa Watafutanjia ulitungwa.

Mipango hii ya Watafutanjia ilianza kusambaa kila mahali katika Conference mbali mbali, na mwaka 1947 General Conference kupitia Idara ya MV iliwaomba Pacific Union kuandaa program za Watafutanjia ili kuifanyia majaribio. Union hii walifanya hivyo na Mwaka 1950 – General Conference ndipo ilipo anzisha rasmi Chama cha Watafutanjia katika Ulimwengu mzima, Mwaka 1973 – kulikuwa na Vyama 200 na wanachama 10,000.

Mapema miaka ya sitini, vyama vya Watafutanjia vilianzishwa katika maeneo mbali mbali ya Divisheni ya Trans – Africa, lakini vyama vipatavyo 30 tu ndivyo vilivyokuwa vimeanzishwa hadi kufikia mwaka 1970 Inashauriwa kuwa katika kanisa lolote ambapo vijana wadogo wapo na wanaanzia idadi ya watoto sita, Chama cha Watafutanjia kianzishwe.

## Sehemu ya II: Kuwaelewa Watafutanjia

1. **Ukuaji na Maendeleo ya tabia za Watafuta njia**
   **Tabia za Ujana**
   - Akili isiyotulia (Restlessness)
   - Wanapenda kuchunguza vitu (Curiosity)
   - Wepesi wa kuamini (Credulity)
   - Ubunifu wa wazi (Vivid Imagination)
   - Wana silika ya kuigiza (Dramatic Instinct)
   - Hutenda kivikundi (Group Life)
   - Wanapenda kufanana (Uniformity)
   - Wenye kudhamiria (Conscience)
   - Wanaujuzi (Mastery)
   - Uzoefu mpya (New Experience)
   - Usalama (Security)

**Maendeleo ya tabia za Watafutanjia**

**a. Kabla ya Ujana = (Miaka 9-12)**

<u>Tabia zao Kiakili</u>
- Hujifunza kwa haraka na kuwa na uwezo mkubwa wa kukariri.
- Huwa makini, na hamu ya Kuchunguza na Kujifunza.
- Hupendelea hadithi na Vitabu vizuri; wanapenda kusoma.
- Wanapenda kukusanya vitu na kujifunza.
- Wanapenda kujifunza vitu vingi. Hwaishii kuwa na ujuzi mmoja.

<u>Tabia zao Kimwili</u>
- Nikipindi ambacho wanakuwa na Afya kuliko wakati wowote.
- Mwili na Akili huwa na uwiano mzuri kkiutendaji.
- Nikipindi ambacho huwa hawana utulivu hadi jambo lake litimie.
- Huwa na kelele nyingi na shughuli zisizo na ukomo.

<u>Tabia zao Kijamii</u>
- Hupenda kutenda kwa usiri na Kuvumbua.
- Hujifunza kimakundi, lakini huacha nafasi ya kufanya kibinafsi.

- Ni umri wa Ugunduzu na Ubunifu.
- Hupenda ibada na niwepesi wa kuamini.
- Uhusiana na jinsia nyingine huwa ni mdogo sana.

Tabia za Kiroho

- Wako makini na mambo ya kiroho na kazi za kanisa.
- Ni muda mzuri kufanya maamuzi ya kubatizwa. (12)
- Hupenda shughuli za kushuhudia na Tuzo mbalimbali.
- Niwepesi wa kuamini. Hivyo umri huu mzuri sana kuwafundisha mambo ya msingi ya dini.

**b. Sehemu ya Awali ya Ujana = (Miaka 13 -15)**

Tabia za Kiakili

- Mchangamfu lakini mwenye ndoto za mchana.
- Wavulana = mambo ya kiufundi, Wasicha = hupendelea shughuli za nyumbani.

Tabia za Kimwili

- Afya zao huwa nzuri
- Ukuaji wa hara wa miili yao na hupenda kula chakula kingi.
- Hakuna uwiano katika ukuaji wao, misuli hushindwa kwenda sambamba na mifupa kiukuaji.
- Mabadiliko ya haraka ya kimaumbile: via vya uzazi hukua, homoni mpya humbadili tabia yake.
- Kati ya miaka 12 – 14 Wasichana huonekana kuwa na kimo kirefu kuliko Wavulana, lakini katika ya miaka 15 na 16 Wavulana huwazidi Wasichana urefu kiasi cha nchi 2"

Tabia za Kijamii

- Niwatiifu kwa makundi rika. Huogopa kutenda kinyume na Kundi Lake. Huhitaji jambo analolitenda litambuliwe na wenzake.
- Hutaka uhuru binafsi anapotaka kufanya mambo yake binafsi. Hapendi kuingiliwa.
- Huanza shauku ya kutafuta pesa; wakatifulani wengine huacha shule.
- Hali zao (mood) hubadilika badilika: Shughuli na Uzembe, Ukarimu na Uchuyo, Kujiamini na Woga. n.k.
- a. Kujichagulia aina Fulani ya chakula na kukataa kingine; kile kinachopendwa hutumika zaidi.
  b. Hupenda ukakamavu, pamoja na tabia ya kufanya kupita kiasi.
  c. Uchangamfu usio na msingi. Wasichana huwa na tabia ya kucheka cheka ovyo.
- Jinsia moja huvutwa na jinsia nyingine. [Huu ni umri hatari sana kwa mambo ya ngono na majaribu ya kijamii]. Shughuli za kimakundi zinatakiwa ziangaliwe na kusimamiwa kwa uangalifu wa hali ya juu sana.

Tabia za Kiroho

- Hamu ya mambo kiroho hupungua. Kijana huvutwa zaidi na mtazamo wa Kundi Lake.
- Wakiwa na umri wa miaka 13 kundi la pili la vijana wengi huamua kubatizwa.
- Uchaguzi wa kazi ya maisha huamuliwa katika kipindi hiki.
- Hali ya kuonyesha hisia zao katika mambo ya imani na kujitoa huwa ni kidoga sana.
- Maranyingi uzoefu huhitilafiana na dhamira.

**c. Umri wa Kati wa Ujana = (16 - 17)**

Tabia za Kiakili

- Huuliza maswali kwa kila kitu na hutaka kuthibitisha kabla ya kukubaliana na kitu chochote.
- Huheshimu sana "utaalamu" na huamini kuwa kitu kilichosemwa mtu maarufu na msomi kuwa kweli.
- Mawazo yao huanza sasa kupangika vizuri na huanza kuweka mipango inayoeleweka wanayotaka kuitekeleza.

Tabia za Kimwili

- Hisia za ngono huongezeka, nguvu za kimsukumo huwa kubwa.
- Urefu na uziti huwa asilimia 85 ya ut uzima.
- Misuli yao hukua na hupenda na hupenda program za mazoezi ya viungo.

Tabia za Kijamii

- Hupenda kundi la watu wenye mawazo yanayofanana (cliques), na kushirikiana na marafiki wa kundi hilo.
- Mkosoaji, na mara nyingi mkali wa wazi anapoeleza mawazo ya watu wengine.
- Wako makini sana, na maranyingi huongozwa na mawazo wazi na kile ambacho kundi lake wanakiunga mkono nayeye hukubaliana nacho.

Tabia za Kiroho

- Mambo ya kiroho huenda juu au hushuka chini kulingana na kundi alilomo au ikiwa program zinazoendeshwa zinamvutia.
- Ikiwa kijana huyu hakuwa amepewa msingi mzuri, huu sasa huwa niwakati mgumu sana wa kurekebisha tabia yake.

**2 Kanuni za Msingi za nidhamu katika Chama cha Watafutanjia**

- Toa mazingira ya uchangamfu ambayo motto aweza kuwa huru.
- Sisitiza Maelekezo badala ya Makatazo
- Tumia njia ya kujenga zaidi na siyo kubomoa.
- Usionyeshe hali ya vitisho bali ya upendo.
- Sisitiza moyo wa kujiamini na kufanya vema kila wakati.
- Muonyeshe kuwa Mungu yupo japo haonekani.

- Mfundishe mototo kufanya jambo sahihi, kwa wakati sahihi, na katika njia sahihi na kwasababu sahihi.
- Wewe uwe kiongozi mfano itapunguza matatizo watoto na wazazi watakuamini. Hii ni hatua kubwa ya kutatua matatizo katika chama cha Watafutanjia.

## Sehemu ya III: Uongozi wa Chama

1. **Sifa za Kiongozi Mkristo anayefanya kazi na Watafutanjia.**
    - Ishi maisha yanayo mwakilisha Kristo.
    - Waoneshe upendo wa thati Watafutanjia (wavulana na Wasichana)
    - Uwe mwenye msimamo mzuri na Shauku ya kuwa kielelezo.
    - Uwe mdhibiti wa mihemko yao. (Be master of his or her emotions)
    - Furahia mazingira ya nje (Enjoy the out-of-doors)
    - Fahamu tabia za Vijana hao wadogo (junior youth)
    - Uwe na Ujuzi mbali mbali.
    - Jua namna ya kuandaa mipango.
    - Kuza tabia ya kushirikiana na viongozi wenzako vizuri.
    - Uwe kiongozi mwenye mwonekano wa kutegemewa.
    - Uwe mchangamfu.
    - Uwe mbunifu.
    - Uwe tayari kupokea ushauri.

2. **Aina Tano za Uongozi (Five Styles of Leadership)**
    a. Uongozi wa Kiimla (Authoritative) – maagizo zaidi
    b. Uongozi kisiasa (Political) – huuza mawazo
    c. Uongozi wa kutathmini (Evaluative) – hujaribisha mambo
    d. Uongozi wa kushirikisha (Participative) – huomba ushauri
    e. Uongozi wa kuachilia (Laissez-faire) – huyumbia upande wenye nguvu

3. **Majukumu ya Uongozi: (Leadership Roles and Functions)**

**<u>Majukumu ya Kujenga (Building Functions)</u>**
Kiongozi ni mtiaji moyo (Encourager)
Kiongozi ni muonyesha hisia (Feeling Expresser)
Kiongozi hupatanisha pande mbili zisizoelewana (Harmonizer)
Kiongozi huridhia (Compromiser)
Kiongozi ni Mlinzi wa lango (Gate-Keeper)
Kiongozi ni mtoa viwango (Standard-Setter)
Kiongozi ni huuangalia muafaka kwa jambo Fulani (Consensus-Tester)
Kiongozi ni mfuasi(Follower)
Kiongozi ni msikilizaji (Listener)

**<u>Majukumu ya kiutendaji (Task Functions)</u>**
Kiongozi ni muanzisha jambo (Initiator)
Kiongozi ni Mtafuta habari (Information Seeker)
Kiongozi ni mtoa Taarifa (Information Giver)
Kiongozi ni mtafuta Mawazo (Opinion-Seeker)

Kiongozi ni mtoa Mawazo (Opinion-Giver)
Kiongozi hufafanua na kuliweka jambo wazi (Clarifier)
Kiongozi ni mchanganuaji (Elaborator)
Kiongozi hutoa muhtasari au ufupisho (Summarizer)

## Sehemu ya IV: Muundo wa Chama:

1. Mkurugenzi wa Watafutanjia General Conference
2. Mkurugenzi wa Watafutanjia Divisheni
3. Mkurugenzi wa Watafutanjia Union
4. Mkurugenzi wa Watafutanjia Conference
5. Mratibu wa Watafutanjia (Area Coordinator)
6. Baraza la Kanisa
7. Mkurugenzi wa Watafutanjia Kanisa mahalia
8. Kamati ya Chama cha Watafutanjia
9. Pathfinder Staff Meeting

**Mkurugenzi msaidizi (ME)**
Mlezi (Counselor)
Kamanda wa Kikosi
Mwandishi wa Kikosi
Wanachama

**Mkurugenzi msaidizi (KE)**
Mlezi (Counselor)
Kamanda wa Kikosi
Mwandishi wa Kikosi
Wanachama

**Support Staff**
Katibu
Mhazini
Waalimu wa nishani
Waalimu wa madarasa
Kiongozi wa Kwata

**1. Kamati mbali mbali (Committees and Staff)**

**A. Kamati ya Uratibishaji:**

Mahali palipo na Klabu za Junior na Teen zinazo jitegemea chini ya usimamizi wa Mkurugenzi kiongozi (Administrative Director.),
Mkurugenzi Kiongozi (Administrative Director) - Mwenyekiti
Wakurugenzi wa Klabu za (Junior and Teen)
Wakurugenzi wasaidizi wa Klabu za (Junior and Teen)

* Kamati ya uratibishaji inaundwa na wafuatao, Mkurugenzi kiongozi, wakurugenzi wa Klabu za Junior na Teen, wakurugenzi wasaidizi wa junior na teen, Mchungaji, Katibu, Mhazini, na Chaplain. Mkurugenzi Kiongozi ndiye Mwenyekiti na anahusika kwa mikutano yote ya kuunganisha shughuli za Watafutanjia.

**B. Kamati kuu ya Watafutanjia:**

Mkurugenzi wa Chama (mwenyekiti)
Wakurugenzi wasaidizi

Katibu
Mhazini
Chaplain
Mchungaji (ex officio)
Mlezi wa Vijana/Mzee (ex officio)
Mkurugenzi kiongozi (ex officio)

* Hii kamati kuu inaundwa na Mkurugenzi wa Chama, Wakurugenzi wasaidizi, Mchungaji, Katibu, Mhazini, na Chaplain. Mwenyekiti wa kamati hii atakuwa mkurugenzi wa Chama, kamati hii itahusika na shughuli zote za Watafutanjia.

**C. Kamati ya Watendaji wa Watafutanjia (Pathfinder Staff Committee):**

Wajumbe wa Kamati kuu wote, pamoja na
Walezi (Counsellors)
Walezi wasaidizi (Junior Counselors)
Waalimu wa Madarasa
Waalimu wa fani mbali mbali (Instructors)
Viongozi wa vikosi waweza kukaribishwa katika Kamati hii

* Kamati hii inaundwa na Kamati kuu, pamoja na Counselors, Junior Counselors and Instructors. Viongozi wa vikosi waweza kukaribishwa katika Kamati hii

**a. Hatua za kuanzisha Chama cha Watafutanjia Kanisani:**

1. Shauriana Mkurugenzi wa Conference
2. Kutana na Mchungaji na Mkurugenzi wa Conference.
3. Peleka hiyo mipango kwenye baraza la Kanisam ili kuubariki mpango wa kuanzisha Chama cha Watafutanjia. Wafanye wajumbe wa baraza waelewe Falsafa, Lengo, na Mkusudi ya Chama cha Watafutanjia.
4. Baraza linalofuata la kanisa (au Kibaraza cha uchaguzi) akiwepo Mkurugenzi wa Conferece au Area coordinator aweza kushirikishwa wakati wa kuchagua Mkurugenzi na Wasaidizi wake.
5. Kanisa lijulishwe wakati wa Ibada ya siku ya Sabato kuhusiana na uanzishwaji wa Chama cha Watafutanjia, Malengo yake na Program kwa ujumla.
6. Maofisa wa Chama cha Watafutanjia watachagua wajumbe waliosalia wa Kamati kuu.
7. Kikao cha kwanza cha Kamati kuu ya Watafutanjia kitachagua viongozi walio baki.
8. Maofisa na viongozi wote watahudhuria semina ya Kozi ya Msingi itakayosimamiwa na kiongozi wa Conference.
9. Itisha kikao cha kamati kuu cha Watafutanjia kupanga mipango ya mwaka mzima
10. Peleka mipango yote kwa mkutano wa watu wote wa Watafutanjia
11. Tangaza program majuma sita kabla kufanya ufunguzi
12. Waandikie Familia muhimu wanaopenda kuunga mkono program za Watafutanjia
13. Fanya usajili wa Watafutanjia kwa kutumia fomu maalumu.

14. Counsellors wawatembelee Wazazi wa Watafutanjia ambao wamejiunga na Chama.
15. Sherehe za uzinduzi – Watafutanjia kuruhusiwa kusonga mbele na madarasa.
16. Establishing church and community interest.
17. Kufanya Tathmini.

**b. Majukumu ya Viongozi**

**Mkurugenzi Kiongozi**

- i. Ataratibu shughuli za Vyama vya Juniour na teen.
- ii. Ataviwakilisha Vyama katika baraza la Kanisa.
- iii. Ataendesha vikao vya kila mwezi vya Chama cha Watafuta njia.
- iv. Ataangalia program za kila Chama na kushauri jinsi kitakavyo fanikiwa.
- v. Atajenga uhusiano wenye furaha kati ya Vyama hivyo viwili.
- vi. Ataratibu Mafunzo endelevu kwa viongozi wa Chama.
- vii. Atatuma taarifa ya kila robo kwa Mkurugenzi wa Conference.
- viii. Atakuwa tayari kuziba nafasi ya Mkurugenzi wakati wa dharura.
- ix. Ataleta miongozo toka Conference.

**Mkurugenzi wa Junior/Teen**

- i. Atasimamia shughuli za chama.
- ii. Ataandaa Vikao vya Chama na kuwaita wajumbe.
- iii. Atahakikisha kuwa Chama kinafikia malengo yake.
- iv. Ata andaa mipango ya Mwaka mzima ya Chama.
- v. Atafanya kama Mwenyekiti wa Kamati kuu yaChama.
- vi. Atakuwa mjumbe wa Baraza la Kanisa (ikiwa chama ni kimoja Kanisani)
- vii. Awe mwenye tabia nzuri kama Kiongozi wa Watafuta njia.
- viii. Awe na mawasiliano ya karibu na Mkurugenzi wa Conference na kutuma taafa ya robo

**Mkurugenzi Msaidizi**

- i. Atapokea majukumu atakayopewa na Mkurugenzi, na kushiriki majukumu ya Uongozi.
- ii. Mkurugenzi msadizi wa kiume atahudumia wavulana na yule wa kike atahudumia wasichana.
- iii. Wakati fulani hawa wasaidizi wawili mmoja aweza kuwa Katibu na mwingine Mhazini wa Chama.
- iv. Atashika majukumu ikiwa Mkurugenzi hayupo.
- v. Atamwakilisha Mkurugenzi kwenye baraza la Kanisa ikiwa Mkurugenzi hayupo.

**Counselor**

- i. Atakuwa karibu sana na Watafuta njia, na uwe msikilizaji wa shida zao na kuwa tayari kuwashauri.
- ii. Atawasaidia Watafuta njia katika kikosi chake kushirikiana pamoja.
- iii. Atawasaidia Watafuta njia katika shughuli zao za madarasa na masomo ya nishani.

iv. Ata himiza Watafuta njia kukamilisha matakwa ya Madarasa yao.
v. Atawafundisha Sheria na Ahadi Watafuta njia wapya ambao wamejiunga karibuni ili wazipende na kuzitumia maishani mwao.

**Junior Counsellor**

i. Atakuwa Couselor mafunzoni(akisimamiwa na Counselor)
ii. Anatenda kama msaidizi wa counselor katika kikosi.
iii. Atapokea majukumu atayopewa na counselor
iv. Aweza kuteuliwa na kuwa counselor ikiwa atakuwa amefaulu mafunzo yake kwa muda wa mwaka mmoja chini ya usimamizi wa counselor

**Mwalimu wa Darasa**

i. Atatafuta mafundisho (materials) mapya kwaajili ya Watafuta njia.
ii. Ajue matakwa yote ya nishani zinazo paswa kufundishwa na aweze kuzifundisha kwa mamlaka.
iii. Ajue kufundisha Nishani na mahitaji mengine ya madarasa ya Watafuta njia.
iv. Atatunga maswali na kutoa mitihani na kutoa alama.
v. Atasaini kwenye kadi la Mtafuta njia kwa mahitaji ya darasa na nishani.
vi. Aweza kutenda kama pia counselor.

**Mlezi/Chalain**

i. Atakuwa ni mshauri wa mambo ya kiroho katika Chama.
ii. Ata andaa ratiba ya maombi katika Chama.
iii. Atakuwa mtoa somo wakati wa maombi au kupanga mtu wa kufanya hivyo.
iv. Atamsaidia Instructor kufundisha nishani zile zinazo husika na umisherari.
v. Atasaidia kufundisha matakwa ya Biblia katika madarasa ya Watafuta njia.

**Kamanda wa Kikosi**

i. Aweza kubadilishwa kwa robo, kwa miezi sita au kwa mwaka.
ii. Kiongozi wa kikosi (watu 6-8)
iii. Hubeba bendera (guidon) katika kikosi.
iv. Atatoa taarifa ya mahudhurio (attendance report)
v. Atashika majukumu ya counselor akiwa hayupo.

**Katibu wa Kikosi**

i. Katibu na muweka hazina wa kikosi.
ii. Huchukua majukumu ya Captain akiwa hayupo.
iii. Hukusanya ada za Wanachama.
iv. Hutunza kumbu kumbu za mahudhurio katika kikosi.

**c. Operating Policies**

**a. Sare**

Chama cha Watafutanjia kinyo sare ambayo makusudi yake ni kuleta sera ya chama na kukitambulisha chama. Sare hizi pia zinao utaratibu wake wa uvaaji, na maelezo haya yanafafanua ni aina gani ya sare ya Watafutanjia na taratibu zao za uvaaji wa sare za Chama hiki cha Watafutanjia.

**Namna ya Uvaaji wa Sare**

- Uvaaji wa sare hukifanya chama kionekane kipo na ni halisi.
- Ni mojawapo ya kitambukisho kikuu cha uanachama.
- Kila mwanachama aliyevaa sare; huenakana anaiwakilisha idara ya vijana ya kanisa la Waadventista Wasabato.
- Sare yapaswa kuwa siku zote safi na maridadi. Kuivaa tu katika hali ya kawaida kando ya mikutano ya kanisa na ile ya chama hushusha kiwango na uthamani wake.
- Sare huitwa unifom pale inapowekwa vifaa mbalimbali vya idara ya vijana kama vile pini, nembo, n.k
- Sare ikishawekwa kifaa chochote kinacholiwakilisha kanisa la Waadventista wasabato; kupitia idara ya vijana, basi sare hiyo hugeuka kuwa ni mali ya kanisa.
- Hivyo itavaliwa kwa mujibu wa maekekezo na miongozo ya idara ya vijana ya kanisa la Waadventista Wasabato.
- Inashauriwa kwamba; sare zivaliwe katika matukio yafuatayo:
  - ❖ Katika mikutano yote ya watafutanjia
  - ❖ Katika mikutano ya injili ya chama au ya kanisa ikiwa vijana wamepewa majukumu ya kukaribisha wageni au kuendesha program maalum.
  - ❖ Katika matukio mengine yoyote ya kanisa yanayohusisha vijana.
  - ❖ Wakati vijana wanajishughulisha na shughuli za kushuhudia, au kuisaidia jamii.
  - ❖ Katika huduma ya ibada ya mazishi ya mwanachama aliyefariki ikiwa kutakuwa na hitaji la idara ya vijana kuendesha program hiyo.
  - ❖ Kaika huduma ya ndoa ya mwanachama aliyeomba idara ya vijana ihudumu katika ndoa yake.

**Sare zisivaliwe:**

- ❖ Na mtu yeyote asiye Mwadventista Msabato
- ❖ Na mtu yeyote asiye mwanachama wa chama chochote cha idara ya vijana.
- ❖ Katika shughuli zozote binafsi kama biashara, kilimo, ufugaji, ofisini, n.k
- ❖ Katika huduma za mazishi ambayo idara ya vijana haina program yoyote.
- ❖ Katika huduma ya arusi ambayo idara ya vijana haina program yoyote.
- ❖ Katika matukio yoyote amabayo sare ikivaliwa; hushusha kiwango na uthamani wa idara ya vijana.

**Matumizi ya Sare**

- Sare rasmi katika vyama vya wavumbuzi, watafutanjia, mabalozi na kiongozi Mwadventista zimekwisha ainishwa na makao makuu ya kanisa la Waadventista ulimwenguni.
- Mabadiliko yoyote, maboresho ya rangi na aina ya mshono wowote ni lazima kwanza yapate kibali katika makao makuu ya kanisa la Waadventista Wasabato ulimwenguni kupitia idara yake ya vijana.

**Uvaaji wa vifaa mbalimbali vya Idara ya Vijana (insignias)**

1. **Nembo ya Watafutanjia ya pembe tatu: (Pathfinder triangle)**
   - Hii ni alama inayokiwakilisha chama cha watafutanjia.
   - Ina ukubwa wa inchi 2 (sm 5)

- Huvaliwa mbele ya kofia ya cap/mtumbwi au berrette.
- Nembo ya pembe tatu ya chama cha watafutanjia -inchi 3 (sm 7.5) huvaliwa kwa juu katika bega la kushoto.

2. **Nembo ya ulimwengu ya watafutanjia: (Pathfinder World Emblem)**
   - Nembo hii ina pembe tatu ndani yake; huwakilisha chama cha watafutanjia ulimwenguni cha kanisa la Waadventista Wasabato.
   - Nembo hii huvaliwa juu ya bega la kushoto.
3. **Nembo za madaraka: (Pocket strips)**
   **Area /district director/Co-ordinator**- Nembo hii huvaliwa na mratibu aliyechaguliwa na kanisa kuratibu shughuli za watafutanjia katika ngazi ya mtaa.
   **Club director-** Nembo hii huvaliwa na mkurugenzi wa watafutanjia aliyechaguliwa na kanisa mahalia kuongoza chama hicho katika mwaka huo.
   **Deputy director-** Nembo hii huvaliwa na mkurugenzi msaidizi wa watafutanjia aliyechaguliwa na kanisa mahalia kuongoza watafutanjia katika nafasi hiyo ya uongozi.
   **Instructor:** Nembo hii huvaliwa na mwalimu aliyechaguliwa na kanisa kuwafundisha watafutanjia matakwa ya madarasa au nishani.
   **Counselor:-** Huyu ni mshauri wa watafutanjia aliyechaguliwa na kanisa mahalia
   **Jr. Counselor:** Huyu ni mshauri wa watafutanja wadogo (Miaka 10-12) aliyechaguliwa na kanisa mahalia.
   Huvaliwa na mhusika wa cheo chake- inchi 2 (sm 5) chini ya bega la kulia; ¼ inchi (sm 0.8) juu ya nembo ya pembe tatu ya watafutanjia.
4. **Chevrons za madarasa ya watafutanjia**
   - Hizi huvaliwa juu katika bega la kushoto chini ya nembo ye watafutanjia. Juu kuelekea chini huanzia na chevron ya Mster Guide, Guide (Kiongozi), Voyager (Msafiri), Ranger (Msimamizi), Explorer (Mgunduzi), Companio (Mwenzi), na Friend (Rafiki)
   - Watu wote pamoja na Master Giude watavaa chevron ile tu inayohusiana na darasa lake.
5. **Nyota ya Master Guide (Master Guide Star)**
   - Hii ni nyota iliyofumwa kwa rangi ya dhahabu na huvaliwa juu ya bega la kushoto
   - Mtu aliyepitia madarasa yote kuanzia rafiki hadi kiongozi mkuu; ana ruhusa ya kuvaa ile chevron moja ya Master Guide inayounganisha madarasa yote (Combined Master Guide chevron)
6. **Pini za madarasa ya watafutanjia (Pathfinder pins)**
   - Mtafutanjia anapomaliza darasa; hupewa pini. Pini hiyo huwekwa juu ya mfuko wa kushoto. Pini ya Master Guide huwekwa juu ya pini nyingine zilizopangwa kuanzia kushoto kuelekea kulia.
7. **Pocket strips za madarasa. (Class Pocket Strips**)
   Pocket strip inayowakilisha darasa alilohitimu huwekwa juu ya mfuko wa kushoto
8. **Ribbon/Bar za matakwa ya juu ya madarasa ya watafutanjia**
   - Ribbon hizi huvaliwa na wale waliochukua matakwa ya ziada katika chama cha watafutanjia.
   - Nazo huvaliwa katika mfuko wa kushoto; juu ya mfuniko wa mfuko huo
9. **Beji za Captain (Kapteni) na Scribe (Mwandishi)**
   - Beji za kapteni huvaliwa na viongozi wa vikosi waliochaguliwa na wanachama.

- Beji za Mwandishi huvaliwa na viongozi waliochaguliwa kuwa makatibu wa vikosi.

10. **Mkanda wa watafutanjia wa nishani (Pathfinder Honor Sash)**
    - Mkanda huu huvaliwa kuanzia bega la kulia; kupitia kifuani kuelekea mfuko wa skirt/suruali upande wa kushoto.
    - Mkanda huu hutumika kuweka nishani zote anazofaulu mtafutanjia

**Angalizo:**

- Hakuna vifaa vyovyote vya kijeshi vinavyopaswa kuwekwa katika sare za vyama.
- Maigizo ya silaha zozote za kijeshi kama vile upanga, sime au bunduki, hata kama sio silaha halisi kamwe zisivaliwe katika uniform za vyama vyetu.
- Mishono yoyote ya kijeshi isiyopatana na kanuni zetu isiruhusiwe kushonwa.

**Sare ya Watafutanjia**

| | |
|---|---|
| Shati/blauz | Nyeupe, mikono mifupi, mifuko ya mifuniko, yenye pilot cardet mabegani |
| Suruali/Skirt | Forest green (Jani la mgomba) |
| Kofia | Mtumbwi wenye rangi ya jani la mgomba huku ukiwa na ufito mweupe kuuzunguka mtumbwi au Barrette nyekundu. Nembo ya kofia ya watafutanjia huwekwa mbele ya kofia |
| Scarf | Njano; yenye nembo ya pembe tatu ya watafuta njia. |
| Soksi/Viatu | Soksi nyeupe na viatu vyeusi |
| Mkanda | Jani la mgomba |
| Neck tie | Jani la mgomba |
| Slide | Nyeupe yenye nembo ya pembe tatu ta watafutanjia |

**Sare ya kazi ya Watafutanjia**

| | |
|---|---|
| Shati/blauz | Khaki |
| Suruali/skirt | Jani la mgomba au Khaki |
| Kofia | Cap (yenye nembo pembe tatu ya watafutanjia) |
| Scarf | Njano yenye nembo ya pembe tatu ya watafutanjia |
| Soksi/Viatu | Soksi nyeusi na viatu vyeusi |
| Mkanda | Jani la mgomba |
| Neck tie | Nyeusi au jani la mgomba |
| Slide | Nyeupe yenye nembo ya pembe tatu ta watafutanjia |

**Sare ya Master Guide**

| | |
|---|---|
| Shati/blauz | Nyeupe, mikono mifupi, mifuko ya mifuniko, yenye pilot cardet mabegani |
| Suruali/Skirt | Forest green (Jani la mgomba) |
| Kofia | Mtumbwi wenye rangi ya jani la mgomba huku ukiwa na ufito mweupe kuuzunguka mtumbwi au Barrette nyekundu. Nembo ya kofia ya watafutanjia huwekwa mbele ya kofia |
| Scarf | Njano; yenye nembo ya watafutanjia ya ulimwengu |
| Soksi/Viatu | Soksi nyeupe na viatu vyeusi |
| Mkanda | Jani la mgomba |
| Neck tie | Jani la mgomba |
| Slide | Nyeupe yenye nembo ya ulimwengu ya watafutanjia |

**Sare ya Kazi ya Master Guide**

| | |
|---|---|
| Shati/blauz | Khaki |
| Suruali/skirt | Jani la mgomba au Khaki |
| Kofia | Cap (yenye nembo pembe tatu ya watafutanjia) |
| Scarf | Njano yenye nembo ya watafutanjia ya ulimwengu |
| Soksi/Viatu | Soksi nyeusi na viatu vyeusi |
| Mkanda | Jani la mgomba |
| Neck tie | Nyeusi au jani la mgomba |
| Slide | Nyeupe yenye nembo ya ulimwengu ya watafutanjia |

**Uniform ya mkurugenzi wa watafutanjia**

Mkurugenzi wa watafutanjia ndiye pekee anayeruhusiwa kushona Kaunda suti mikono mirefu au mifupi; huku akitanguliza shati/blauzi nyeupe na kuvaa tai/neck tie rangi ya jani la mgombana kuvaa kamba ya filimbi. Mifuko iwe na mifuniko na mabegani kushonwe pilot cardet. Mwingine anayeruhusiwa kuvaa namna hiyo ni area co-ordinator wa watafutanjia wa mtaa au kanda.

**b. Fedha za kuendesha Chama (Finances)**

i. Ada ya mwaka
ii. Bajeti toka mfuko wa Kanisa.
iii. Sadaka
iv. Ufadhili kutoka kwa washiriki
v. Miradi maalumu
vi. Kuendesha changizo. Andaa taratibu za kuendesha changizo:
   a. Zithibitishwe na Kanisa na zifuate taratibu za nchi.
   b. Ikiwa mtaandaa bidhaa za kuuza ziwe zile zinazo kubaliana na imani yetu.
   c. Ikiwa mtatembelea jamii kuwe na magazeti ya kugawa bure.
   d. Motisha kwa Watafutanjia: zawadi ndogo ndogo, ribbons, tuzo, n.k.
   e. Weka malengo na uyafanyie kazi.
   f. Andaa klabu nzima kwaajili ya kufanya mauzo. Tengeneza taratibu nzuri za kupata faida. Usipuuze mpango wa mtu yeyote

**d. Kutuma taarifa (Reporting)**

Mkurugenzi wa Chama cha Watafutanjia katika Kanisa mahalia atatakiwa kutuma taarifa ya utendaji wa Chama kwa Mkurugenzi wa Conference mara mbili kwa mwaka (March na September)

**e. Uwanachama (Membership)**

- Umri wao: 10 - 15
- Wanapaswa kujaza fomu na kuzirudisha kwa Kamati kuu ya Watafutanjia.
- Baada ya kupokelewa fomu zao sasa wataruhusiwa kuendelea na program.
- Watapaswa kulipa Ada ya uanachama na Bima yao ya Mwaka.
- Wanapaswa kuwa na Sare Daraja A iliyokamilika na kuivaa (na Daraja B pale itakapo hitajika)
- Atahudhuria vipindi vyote kwa uaminifu.
- Lazima ajifunze na kuzishika ahadi na sheria za Watafutanjia.

- Lazima akubaliane kushiriki na kushirikiana katika shughuli zote za Chama kabla ya kujiunga.
- Wazazi wa Watafutanjia lazima washiriki kwa kwa nia yao yote kukiunga mkono chama na kuwahimiza vijana wao kushiriki kwa ukamilifu shughuli zote za chama.
- Wakurugenzi wote waliochaguliwa na wale viongozi ni wajumbe wa Cha kwa mujibu wa nafasi zao.

**e. Bima (Insurance)**

Kwakuwa Watafutnjia wanamikutano ambayo imepangika kwa matukio ya mwaka mzima, hivyo wanapaswa kulipia bima yao ya safari ya mwaka mzima ili kuwawezesha kushiriki mikutano yao bila ya kukwama. Bima italipwa kuanzia April 1 na itaisha mwaka unaofuata march 31.

## Sehemu ya V: Mipango ya Chama na Namna ya Kupanga

1. Mipango ya Mwaka mzima (Yearly Program)
2. Mipango ya juma moja (Weekly Club Meetings)
3. Record Cards and Passports
4. Matukio ya Conference/Mission (Events)
   - Mikutano ya maenesho ya Watafutanjia (Pathfinder Fairs)
   - Camporee za Watafutanjia (Pathfinder Camporees)
5. Uvishaji pini (Investitures)
6. Gwaride la Kanisa (Church Parades)

## Sehemu ya VI: Kufundisha Mtaala WA Watafutanjia

**Teaching preparation**

Soma Mtaala wa Darasa Vizuri.

Chunguza mahitaji ya Watafutanjia katika darasa lako

Andaa Andalio la somo

Somo litafanikiwa vizuri vizuri ikiwa utakuwa:

- ♦ Ni wakati wa kuchangamsha
- ♦ Ni wakati wa Kukubalika na kuelewa
- ♦ Ni wakati wa kutambuliwa na Ubunifu
- ♦ Ni wakati wa kubuni vitu
- ♦ Ni wakati wa mawasiliano mazuri
- ♦ Ni wakati wa kuonyesha wema na haki
- ♦ Ni wakati wa kuwashirikisha
- ♦ Ni wakati wa kumpima mtoto kwa upendo
- ♦ Ni wakati wa kushirikiana

**Jinsi ya kufanya Watafutanjia wafurahie masomo ya Nishani**

- Pawe na tarehe ya kumaliza somo la Nishani – darasa lisiendelee bila mwisho
- Waonyeshe Watafutanjia faida za ile Nishani na jinsi itakavyo wasaidia baadaye
- Waweza weka nyongeza katika Nishani kwa kibali toka kwa Mkurugenzi wa Conference
  - Kamilisha mahitaji yote ya Nishani hiyo
  - Watie moyo Watafutanjia wote waweze kufikia tuzo za Kiongozi Mkuu

- Hakikisha Watafutanjia waliokamilisha nishani zao wanapata vyeti na nishani zao wa sherehe za kuhitimisha. Agiza nishani mapema kabla ya tukio

**1. Understanding Creativity**

**2. Teaching the Pathfinder Curriculum Creatively**

Kuna aina mbili za Ratiba kwaajili ya kufundishia Watafutanjia na kuendesha program zao za kila wiki. Angalia hapo chini modeli **A** na modeli **B** ili uzitumie katika ratiba za kila siku.

**Modeli A**
**(Masaa 3)**

| Dakika | | Shughuli |
|---|---|---|
| 15 | - | Ufunguzi – kupandisha bendera, ombi, ukaguzi wa Vikosi |
| 10 | - | Kwata (Klabu au Kikosi) |
| 15 | - | Mzungumzaji/Idada/Matumizi ya somo la ibada/Maswali ya Biblia |
| 30 | - | Shughuli za Madarasa (shughuli za ndani) |
| 30 | - | Michezo yenye kuongeza ujuzi |
| 30 | - | Shughuli za Madarasa (shughuli za nje) |
| 45 | - | Nishani/ujuzi/ufundi |
| 5 | - | Kufunga – nafasi ya Mkurugenzi (matangazo) na ombi la mwisho |
| 180 | | |

**Modeli B**
**(Masaa 2)**

| Dakika | | Shughuli |
|---|---|---|
| 15 | - | Ufunguzi – kupandisha bendera, ombi, ukaguzi wa Vikosi |
| 10 | - | Kwata (Klabu au Kikosi) |
| 15 | - | Mzungumzaji/Idada/Matumizi ya somo la ibada/Maswali ya Biblia |
| 30 | - | Shughuli za Madarasa (shughuli za ndani) |
| 15 | - | Michezo yenye kuongeza ujuzi |
| 30 | - | Nishani/ujuzi/ufundi |
| 5 | - | Kufunga – nafasi ya Mkurugenzi (matangazo) na ombi la mwisho |
| 120 | | |

**3. Pathfinder Classes**

Madarasa ya Watafutanjia yataendeshwa kila juma kwa majuma yote 20 na kukamilishwa. Waalimu wanapaswa kuwa makini kuhakikisha vipengele vyote vinafundishwa kwa kufuata maelekezo ya mtaala wa darasa husika.

## Sehemu ya VII: Ukambikaji na Elimu ya nje

**1. Philosophy of Camping**

- ❖ Hukuza hali ya na kumjenga tabia nzuri Mtafutanjia
- ❖ Ujuzi wa kambi hutoa nafasi kwa kufanya zoezi la kuishi kama jamii moja, kuwa wa kutegemewa, nidhamu binafsi, na heshima kwa wengine; watajifunza maumbile ya asili, na kuuona ukuu wa Mungu
- ❖ Watafutanjia huyafurahia sana hayo
- ❖ Kuishi katika mazingira ya porini yatawasaidia sana Watafutania kuwa tayari kukabilia na wakati wa taabu utakapo fika
- ❖ Nukuu za Roho ya Unabii zinaunga mkono haya:
  (COL 24 - ), (4T 580 - ), (Ed. 107- ), (Ed. 100-101- ), (DA 70- ) (MYP 380, 381)

**2. Mambo ya Msingi unapoandaa Kambi**

- Kambi liandaliwe kwa lengo maalumu
- Panga usafiri wa kwenda kambini na kurudi
- Hakikisha kuna mahema ya kutosha kwa wanakambi wote
- Njoo na vifaa vifuatavyo shoka, nyundo, Msumeno, bereshi, vyombo vya kutunzia maji, tochi, sindano, wembe, kisu, nk. Kumbuka Biblia, kitabu cha wimbo, Lesoni, daftari na kalamu view nambari moja
- Kisanduku cha huduma ya kwanza
- Ensure adequate camp personnel to staff the camp
- Njoo na chakula cha kutosha kilicho mlo kamili
- Plan meetings around a theme
- Eneo la kambi likaguliwe mapema kabla ya muda wa kambi ili kuona hali ya usalama na mambo mengine muhimu
- Pata kibali cha kutumia hilo eneo ikiwa eneo sio la kwenu
- Hakikisha hali ya usafi inazingatiwa katika eneo la kambi ili pasitokee magonjwa ya mlipuko
- Wajulishe wazazi na Watafutanjia juu ya kambi hilo mapema

**Faida za kukambika**

- ö Kutuleta karibu na Mungu muumba wetu
- ö Kufurahia mazingira ya viumbe vya asili
- ö Kukuza na kujenga moyo wa kujiamini na kujitegemea nje ya mazingira ya nyumbani
- ö Kutoa uwezo wa kuishi katika mazingira yaliyo nje na nyumbani
- ö Kujenga moyo wa kujiamini na uwezo wa kufanya kazi mbali mbali ambazo wengi hawapati nafasi ya kuzifanya wawapo nyumbani
- ö Hutoa nafasi ya kujifunza mambo mapya na uvinjari
- ö Hutoa ujuzi katika kuona na kugundua mambo, masomo mbali mbali ya ukakamavu na kujenga moyo wa kujiamini
- ö Huandaliwa shughuli ambazo Viongopzi na Watafutanjia wote hupata nafasi ya kuzifurahia na kuleta maana katika ibada

**Faida za kiroho za Kukambika**

- ö Kupata uzoefu wa kufuata utaratibu
- ö Kupata muonjo wa ukaribu uliopo kati ya Mungu na maumbile ya asili

- ö Kujifunza Maajabu ya Ukuu wa Mungu
- ö Nguvu ya kuchukuliana na mazingira
- ö Kufurahia kushirikiana
- ö Mguso wa uponyaji mtulivu

**3. Types of Camping**

**4. Mambo ya msingi ya Kambi zuri (Basic Components of Good Camping)**

- Eneo la kukambika linapaswa kuwa lenye vivutio vinavyofanya wanakambi wafurahie kuwa kambini (amenities), kama vile maji, maeneo ya michezo, haiking nk.
- Eneo liwe na maji ya kutosha na lisiharibiwe.
- Pawe na kuni za kutosha kwaajili ya kupikia kuwasha moto wa kambi au moto wa hadithi (choto)
- Vyoo vizuri na vyenye idadi ya kutosha kulingana na wana kambi na jinsia zao.
- Eneo liwe miti ya kivuli ili kuwawezesha watu kujipumzisha wakati wa jua kali.
- Mazingira yafaayo kwa kujenga majiko ya kupikia wengine waweza kuja na gasi za kupikia.

**5. Kujifunza maumbile ya Asili (Nature Study)**

- ö Kuwa katika mazingira ya nje ya kambi kwaweza kuwa ni uzoefu mzuri sana kwa Watafutanjia kunakoweza kuwajenga kiroho na kuwaongezea ujasiri na kujiamini.
- ö Mtafutanjia ambaye ameacha mazingira ya nyumbani na kwenda kuishi huko porini na huyu mtafutanjia atakuwa amepata nafasi ya kuisikia sauti ya Mungu ikizungumza ndani ya moyo wake.
- ö Mazingira hayo ya porini yatamletea mtafutanjia hali ya amani na furaha (peace and tranquility) na huo utakuwa ndio mwanzo wa kumletea furaha ya kuondokana na misongo ya maisha ya kilasiku.
- ö Huu huwa ni wakati mzuri wa kueleza baadhi ya matatizo wanayoweza kuwa nayo watafutanjia na kuwasaidia kutambua kuwa Mungu anao uwezo wa kuwaokoa na matatizo hayo.

## Sehemu ya VIII: Kwata na Sherehe zake (Drill and Ceremonies)

*(Angalia somo la Kwata na Sherehe zake)*

1. Philosophy for Drill Ceremonies
2. Opening and Closing Ceremonies
3. Basic Drill Commands

# JINSI YA KUONGOZA KLABU YA BALOZI (MABALOZI)

MAKAO MAKUU YA KANISA LA WAADVENTISTA WASABATO ULIMWENGUNI
IDARA YA VIJANA
2006

## YALIYOMO


iii . Utangulizi

1. Sehemu 1. Chama (klabu)

5. Sehemu 2: Kuwatambua vijana wakubwa (senior Youth)

9. Sehemu 3: Muundo wa chama

17. Sehemu 4: Mipango na ratiba za chama

29. Sehemu 5: Shughuli (matendo ya chama)

# U T A N G U L I Z I

***Kwa nini daraja jipya?***

Tangu mwanzo wake idara ya vijana ya Waadventista wasabato imekuwa ikiwahudumia vijana katika madaraja matatu ambayo ni chama (klabu) cha wavumbuzi (AC) ambao huanzia umri wa miaka 6-9: chama cha watafuta njia (PFC) ambao huanzia umri wa miaka 10-15 na chama cha vijana wakubwa (AY) ambao huanzia umri wa miaka 16-31+.

Lakini divisheni zimegundua kwamba vijana wadogo wanao timiza masharti ya watafuta njia (PFC) huachwa bila kufika kwenye mambo yaliyokusudiwa kutendwa ili kukidhi mahitaji yao. Hivyo hawataki kutoka katika chama cha watafuta njia na wakati huo huo pia hawajioni wao kuwa wakubwa kiasi cha kushirikiana na vijana wakubwa/watu wazima. Kutokuwepo kwa utaratibu uliowekwa kwa ajili ya kundi au daraja hili baadhi ya divisheni zimekuwa zikiendesha taratibu zao mbalimbali kama vile (Companion) huku ulaya, Medical Brigade katika divisheni za Inter-Amerika na Amerika ya kusini n.k ili kuziba pengo hili.

Katika mkutano wa viongozi wa vijana ulimwenguni wa mwaka 2001 hatua moja na ya muhimu sana iliyochukuliwa ni kuagiza makao makuu ya idara ya vijana kuzalisha na kuendeleza vitu, vifaa na vyombo kwa ajili ya daraja jipya ili kukidhi mahitaji ya vijana, wenye umri wa kuanzia miaka 16-21 katika kanisa la waadventista wasabato. Na leo hii ulichokishikilia mkononi ni matokeo ya hatua hiyo kuchukuliwa.

Tafadhali fahamu kwamba chama cha mabalozi hakikusudii kuchukua nafsi ya AYS badala yake ni kuimarisha chama cha vijana wakubwa (watu wazima) iliyopo sasa katika kanisa letu. Chama hiki kipya kitatoa muundo wa njia zilizopangiliwa kwa umri kuanzia miaka 16-21 ili waweze kushiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kanisa lao kuanzia mahali walipo na hata kwa ulimwengu mzima.

Shukrani nyingi ziende kwa divisheni zote za ulimwengu zilizochangia mambo mbalimbali katika mwongozo huu.

Madaraja ya kiofisi ya idara ya vijana katika kanisa la waadventista wa sabato, itakuwa kama ifutavyo:-

**Daraja la huduma za vijana wadogo**

(Junior Youth Ministry)

| | |
|---|---|
| Chama cha wavumbuzi | Miaka 6-9 |
| Chama cha watafuta njia | Miaka 10-15 |

**Daraja la hudma ya vijana wakubwa**

(Senior Youth Ministry)

| | |
|---|---|
| Chama cha mabalozi | Miaka 16-21 |
| Vijana wakubwa/watu wazima | Miaka 22-31+ |

## S E H E MU 1

***Chama (klabu)***

**UANACHAMA.**
Kijana yeyote mwenye umri wa kuanzia miaka 16 hadi 21 anayechagua kuishi kulingana na kanuni na mwongozo wa kanisa la wadvenista wa sabato.

Kwa ufafanuzi: Idara ya vijana inaielezea idara ya vijana wadogo kama idara inayohusika na vijana wenye umri chini ya miaka 16. (kwa namna nyingine yaweza kuelezwa ni miaka 15 kurudi nyuma). Vijana wakubwa ni wenye umri wa kuanzia miaka 16-19, na watu wazima ni wale wenye umri wa kuanzia miaka 20 - 30+

Chama hiki cha vijana kinatilia mkazo kwanza kwa jamii ya vijana wakubwa (Senior Youth) lakini kundi lenye rika la juu na upeo zadi limeachwa huru kwa sababu katika maeneo mbalimbali kuna vijana ambao katika rika lao la miaka ya 20 ambao wangefurahia na kunufaika na chama hiki.

## ALAMA YA UTAMBULISHO.
## NEMBO YA CHAMA INA VITU VIFUATAVYO;

Kafara ya Yesu imejengwa katika uhusiano na maisha yake. Msalaba hapa duniani ni kielelezo cha kafara yake, na hutupatia tumaini jipya na jema zaidi kwa wakati ujao; vyote ni katika ulimwengu huu kupita dhana ya kuwa kiongozi mtumishi na nchi kufanywa upya wakati wa marejeo yake. Picha ya kitabu kilichofunuliwa ndio msingi wa imani yetu, maarifa na hata mtindo wa maisha tupaswavyo kuishi. Kitabu hicho kimeachwa wazi kuonyesha kwamba ndicho kitabu pekee kinachopaswa kuaminiwa na kuwekwa moyoni kama mwongozo thabiti na mshirika wa karibu kuliko vyote. Pia kitabu hiki kipo kwa ajili ya kushirikisha wale wote ambao wako tayari kukipokea. Mchanganyiko wa rangi ya njano na dhahabu nyekundu ni kielelezo cha pambazuko la uzima wa milele ambao utafuatia baada ya giza tulilonalo kwa muda kwenye dunia hii ya dhambi.

**AZIMIO LA USEMI / MOTO NA KUSUDI LA CHAMA CHA MABALOZI**
Ujumbe wa marejeo kwa ulimwengu wote katika kizazi changu.
Uhusiano wangu na Yesu kristo kwa asili hunitia nguvu za kushiriki na yeyote atakayeipokea injili – yaani habari njema za marejeo yake yaliyo karibu.

Kwa maana upendo wa Kristo watubidisha.
Nalazimishwa na upendo wa Kristo

Navutwa kwake kutipia kielelzo cha maisha yake, alivyo sulubiwa na kuwabwa msalabani, ushindi wa kufufuka kwake na ahadi yake ya dunia mpya kama ilivyokuwa mwanzoni katika uumbaji. Kadri ninavyomkaribia ndipo ninapozidi kutambua mahitaji ya wanadamu wenzangu kwangu.

**KAULI YA UTUME.**
Chama cha mabalozi ni utaratibu wa kanisa la waadvenisa wasabato ambao ulizinduliwa kwa kusudi maalumu la kukabiliana na mahitaji ya kiroho, kijamii na mtindo wa maisha ya vijana wenye umri wa 16-20’s kwa kuwapa changamoto ili wawe na maarifa na hakika ya mambo kwa kila mmoja, katika

kushiriki uhusiano wake binafsi na kristo, kuendeleza mtindo wa maisha unaoafikiana na imani yao na shughuli wanazozipenda na kuwandalia mahali panapofaa au kutosheleza kwa maendeleo mazuri na yenye upendano katika maisha yao yote.

**FALSAFA**

Kanisa la waadventista wasabato limejitolea kwa dhati kwa ufahamu, kuwafundisha, na kuwaandaa vijana wake kwa ajili ya uongozi na utumishi mwema kwa jamii ya wanadamu wote ulimwenguni.

Kwa upya wake na vyama vyote vya awali vilivyoimarishwa na kuwa hai ndani ya idara ya vijana, huenda mambo ambayo sio sahihi kwa chama cha mabalozi yanapaswa kutajwa kwanza. Sio upanuzi wa chama cha watafuta njia au kama wengine wawezavyo kudhania - watafuta njia wakubwa. Hakifuatishi mpangilio wa orodha mambo yaliyokusudiwa kutendwa kama ilivyo kwa watafuta njia wala kwa kuwa na mambo mengine yanayofanana kwa nje. Halitumii alama, ishara na vyombo, njia ila kama klabu maalum, huchagua kwa hiari kushirikishwa katika kupewa kipaumbele au katika aina za madaraja ambayo kwayo pekee alama hizo huhusika moja kwa moja kuwakilisha mahitaji yaliyotolewa.

Pia si chama cha vijana wakubwa AY wala hailazimiki kutimiza kazi ya vijana ya uwakili (AYS) ambayo huwa na utaratibu maalumu kuanzia ijumaa usiku au sabato mchana. Kwa miongo mingi iliyopita (AYS) imekuwa ikielezewa kutokana na kazi yake kama mfumo ambao kwa asili umeelekezwa katika kutoa utaratibu wa programu kwa vijana kanisani siku za sabato na kuhudhuriwa na vijana pamoja na washiriki wakanisa wenye umri mbalimbai lakini wasimamizi au waongozaji wa program wakiwa ni vijana.

Kwa asili chama cha mabalozi kipo kwa ajili ya kutoa utaratibu uliopangiliwa kwa vijana wakubwa, wa miaka 16-21 ambao utawahimiza kuwa wanachama hai katika kanisa lao (mahali walipo na ulimwenguni kote) na hata kwa jamii zao, kwa kuwawezesha kugundua vipaji na ujuzi wa maisha waliyopewa na Mungu.

Shabaha maalumu ya chama yaweza kuthibitishwa na uongozi wa mahali pale kwa kushauriana na vijana wenye nia ya kushiriki kadri wawezavyo bila kuweka ujumbe katika hali ya kutiliwa mashaka.

Shabaha hiyo yawaza kutofautina na kadri utaratibu wa mwaka ulivyotolewa, yaweza kuendelea kwa miaka kadhaa kwa kuzingatia mzunguko wa mafunzo, au yaweza kufanya kazi kwa wakati mmoja kwa ajili ya makundi mbalimbali ya vijana ikikabiliwa na mahitaji yao. Haya ni miongoni mwa yanayoweza kuhusishwa katika mfululizo huo.

**Misingi 7 ya kuendeleza ubalozi**

1. Kuendeleza kipaji cha uongozi kupitia mtaala kama vile kiongozi mkuu na kiongozi wa vijana.
2. Kuendeleza utaratibu wa kuifikia jamii mahali ilipo kupitia huduma na pia kupewa mafunzo ya kuwa hiari na utayari wakati wote kwa kazi.
3. Kukuwa kiroho kupitia njia ya kienyeji au kisasa ya kufanya uinjilisti.
4. Kukua kimaisha kupitia mafunzo mbalimbali ya stadi za maisha.
5. Kukua kimahusiano kupitia mazungumzo ya pamoja na semina za watu ambao hawajaoa.
6. Kukua na kujitambua tabia, mwenendo na utu kupitia mambo na matukio mbalimbali yanayotendeka nje.
7. Kustawi kimaisha kupitia utumiaji wa nishani za juu kama zilivyoonyeshwa katika kitabu cha nishani cha AY.

**MALENGO: / MADHUMUNI**

Malengo ya fuatayo ni lazima yafanikiwe kadri viongozi wa vyama wanavyogundua na kuendeleza mada zilizojengeka katika misingi hiyo saba hapo juu.

1. Kuwawezesha vijana wakubwa kufahamu kwamba Mungu na kanisa lake anawapenda na anawahitaji watumie talanta zao kwa ajili ya kutimiza agizo la injili ya wao kwa wao kama ilivyoelezwa katika Mathayo 28:18-20 na Matendo 1:8. Hii itawawezesha kufanikiwa katika maisha yao kadri wanavyoshiriki imani yao pamoja na wale ambao Mungu anawaleta kwao.
2. Kuwahimiza na kuwasaidia vijana wakubwa ili waweze kugundua talanta zao walizopewa na Mungu na kutumia vipaji na uwezo walionao ili kutimiza kile Mungu anachokitarajia toka kwao.
3. Kuwatia moyo vijana wakubwa ili waonyeshe upendo wao kwa Mungu kwa kuwaunganisha na kuwashirikisha katika huduma mbalimbali za upelekaji injili kwa jamii.
4. Kuwafanya vijana kuona kwamba, kuwa wa kwanza au kushika namba moja katika kuwa balozi ndiyo wokovu pekee wa kila kijana ambaye ni mwanachama.
5. Kuwajengea vijana dhana ya kuthamini, kufahamu kupenda na kufurahia uumbaji wa Mungu katika maisha yao kwa kupitia taratibu nzuri zilizopangiliwa za utafiti na ugunduzi. Kwa kufanya hivyo watauona ushiriki wao na Mungu kuwa kitu cha maana zaidi, kadri wanavyozidi kupata nafasi na uzoefu wa hisia ya maajabu ya Mungu na ibada kama inavyofunuliwa katika siri za kiroho na kuorodheshwa katika Warumi 1:19,20 katika kuona ni kipi cha ukweli na kinachofaa kuabudiwa.
6. Kuwafundisha vijana wakubwa stadi maalunu za masisha na mambo ya kujifurahisha kwao, ambayo vingewajengea malengo na hata nafasi za ajira.
7. Kuwahimiza vijana kujiendeleza na kulinda afya zao toka katika mtindo wa maisha holela ya utumiaji wa madawa ya kulevya kwa nguvu.
8. Kuwapa vijana fursa za kukuza kuonyesha uwezo wao katika uongozi kwa kufanya hivyo watazidi kuwa imara katika maazimio yao na pia kuendelea kuwa na nidhamu na kutumia akili walizo nazo na ufahamu kukabiliana na hatua mbalimbali za mabadiliko ya makundi-rika.
9. Kutoa fursa / nafasi ya kutosha kwa vijana wa jinsia zote katika mambo yote ambayo yatapelekea na kukomaza mahusiano thabiti ya maisha.

## S E H E M U YA 2

*Kuwatambua vijana wakubwa (Seniro Youth)*

**KUWATAMBUA VIJANA WAKUBWA (Senior Youth)**
Kila umri, hatua ya makuzi (ukuaji) kwa vijana wadogo ina mahitaji maalumu ya kisaikolojia yanayohitaji kutimizwa. Vyama vya wavumbuzi na watafuta njia vyote vina mahitaji maalumu kila kimoja kama ilivyoainishwa katika vitabu vyao vya uongozi.

Hii pia kwa vijana wa kati na vijana wakubwa. Vijana wa kati ni umri ambao uaanza miaka 16-17. Vijana wakubwa huanzia umri wa miaka 18, katika baadhi ya nchi, umri huu unachukuliwa kama umri wa mtu mzima kisheria hadi miaka 20 hivi.

Kwa ajili ya chama cha mabalozi na huu waraka, umri wa juu utaishia miaka 24.

**VIJANA WA KATI (MIDDLE ADOLESCENCE)**
Hawa waitwao kama "chipukizi (late bloomers) wote kwa pamoja hupita katika kipindi cha ukuaji kwa kasi wakati wengine, wakipunguza kiwango chao cha ukuaji, mara nyingi huu ni umri ambao mwisho wake kunakuwa hakuna kuongezeka kwa urefu. Katika umri huo kijana anakua na uwezo wa kudadisi (kubaini) na utu wake na huchukua nafasi katika hatua mbalimbali za ukuaji na kuwa na haki zao za utu na kujifanyia thamani. Huwa wanakuwa ni watu wenye kutambua haki zao, hisia, na kujithaminisha.

**Tabia za kimwili.**

1. Jinsia huwa ni kichocheo cha wao kukabiliana nacho.
2. Urefu na uzito hufikia asilimia 85% ya uzito wa mtu mzima
3. Kunakuwa na kujenga kwa misuli na umbo la mwili, hivyo mazoezi ya kuuweka mwili katika hali nzuri yanakuwa ni muhimu kwa wengine.

**Tabia za kiakili**

1. Hupenda kuuliza kila kitu na kuhitaji uthibitisho wa kila kitu kabla ya kukipopkea/kukubali.
2. Mara nyingi wanaheshimu kinachoonekana kama ufadhili wa kimasomo (Scholarship) na mara nyingi wanategemea katika kupokea majibu yanayotolewa na watu muhimu au maarufu (maoni ya waigizaji na wanamuziki wanaopendelea huwa na uzito zaidi).
3. Mitazamo yao hujengwa katika hali sahihi na hupanga namna ya kufikia malengo na mipango hiyo.

**Tabia za kijamii**

1. Hupenda vikundi na kuhitaji kuwa na marafiki zao wakiwazunguka kwa karibu.
2. Hupenda kutoa mawazo yao kwa wengine au wakati mwingine kuwakosoa kwa ukali.
3. Huwa ni wepesi katika kuongozwa mara kwa mara na mitazamo au maoni ya watu wengi na kile ambacho vikundi vya vijana wenzao huona kuwa ndio tabia njema.
4. Huanza tabia ya kutafuta pesa, kitu ambacho huwasababisha wengine kuacha au kufukuzwa shule.

**Tabia za kiroho.**

1. kutokana na uchaguzi wa kundi la rika lao, vijana hao huweza kuimarika katika nia ya mambo ya kiroho na maadili au kupoteza kabisa nia ya mwamko katika mambo ya kiroho na maadili.
2. Kinachokuwa hakijashughulikiwa ka bidii katika kuwajengea msingi wa fikra za mambo ya kiroho na maadili hadi kufikia kipindi hiki, huwa vigumu sana kukifanikisha.
3. Huanza hatua za kujitambua ukaribu wao katika mambo ya dini na nafasi ya Mungu katika maisha yao.
4. Makusudio ni katika kufahamu nini maana ya maisha.

**VIJANA WAKUBWA (Later Adolescence)**

Hiki ni kipindi cha ukuaji wa utaratibu wa mwili ambapo hata wale chipukizi wakubwa huwafikia waliotangulia kwa umri na hata kuwapita. Tabia na utu wao hufanana, tabia ya kupenda makundi huanza kuonekana. Makundi hayo si ya kujitenga kijinsia bali makundi yenye mchanyiko wa jinsia zote kama vile klabu, chama, shirika, makundi ya kikanisa, au kikazi yaani mahusiano yaliyoelekea zaidi katika masuala ya michezo, nk.

Pamoja na mashaka yanayokuwepo kuhusiana na dini, yamekuwa yakizingatiwa na ndipo msingi halisi wa imani ulipo, au kunakuwepo na kutupiliwa mbali kwa dini kama hadithi za kitoto za mambo ya kale yenye mambo yasiyo na ukweli, kitu ambacho hupelekea wao kutokuamini, mambo yajayo. Mivuto ya jinsia hujionyesha kupitia mapenzi na ndoa ambazo husababisha ujengaji wa nyumba (familia) au katika mahusiano tofauti tofauti ya dhati au ya majaribio ya ndoa na viapo kuwekwa kando (kutofuatwa) kwa miaka kadhaa. Miradi ya huduma itakuwa na mafanikio zaidi itakapoelekezwa kwenye ujuzi uliokwisha anzishwa na unaendelea.

**HAIBA (UTU) DHIDI YA TABIA**

Ingawa Biblia husema kwamba "Ishi ulimwenguni lakini usiwe mtu wa ulimwengu" ni vigumu sana kama siyo kutowezekana kabisa kuakisi walau kwa kiasi fulani cha mazingira tunamoishi. Mfano wa ngano na magugu ni sahihi kabisa, na tunaiona tafsiri hii katika baadhi ya maeneo yaliyo muhimu kwetu kuyatazama ili tusije tukajikuta sisi wenyewe (na vijana wetu) katika hali sawa na ile iliyotolewa mifano katika Biblia, wanawali waliokuwa wakimngojea Bwana harusi. Eneo moja linalohitaji umakini wetu ni lile la hali ya tamaduni na tabia.

Katika kupitia maandishi hivi yaliyoandikwa miaka zaidi ya 200 iliyopita ambayo yanahusika na mafanikio, inavutia kuelewa mwelekeo kwa uwazi. Kwa miaka 150 ya mwanzo mafanikio yanatafsiriwa kulingana na ubora huo kama tabia njema, unyenyekevu, uaminifu, kiasi, ujasiri, haki, uvumilivu, ukarimu, unyofu, ukawaida na kanuni ya thamani. Kwa maneno mengine mafanikio yalitafsiriwa kwa matendo mema. Hata hivyo miaka 50 iliyopita kumekuwa na badiliko la wazi kutoka kwenye maadili yanayolenga tabia hadi kwenye maadili yanayolenga utu. Maadili ya kiutu yameelekezwa zaidi katika taswira au mwonekano kwa jamii. Mtazamo sahihi kifikira na hata njia nzuri za udanganyifu. Kwa maneno mengine mabadiliko yamefanyika kutoka kwenye mambo ya kitabia kwenda kwenye mambo ya kiutu. (Tom Osborne: Solid Ground). Mabadiliko haya yamechangia hata kuinua mmomonyoko wa maadili hadi kufikia vijana kutokuwa na kitu chochote cha kuegemea, hakuna dira inayowaelekeza katika mwelekeo sahihi. Siku hizi watu huamini kwamba maisha binafsi hayaendani na mafanikio na uongozi. Ubora wa maadili ya mtu hauna uzito katika msukumo wa mtu kwenye mafanikio. Nukuu inayofahamika vizuri kutoka kwenye kitabu "Education Comes to mind; Hitaji kuu la ulimwengu ni hitaji la watu –watu ambao hawatanunuliwa au kuuzwa, watu ambao katika mioyo yao ya ndani ni wakweli na waaminifu, watu ambao hawaogopi kuitaja

dhambi kwa jina lake halisi, watu ambao dhamira zao huwatuma kufanya wajibu wao iwapasavyo siku zote, watu ambao wataitetea haki na kweli hata kama mbingu zishuke, ("Ed. Uk.57") katika ulimwengu wa leo dhana hii huonekana ya kizamani hata kwa baadhi ya viongozi wa vijana.

Huenda ndiyo ikawa sababu ya nukuu huanza kwa kusema "Hitaji kuu la ulimwengu….." zaidi kama maandishi katika ukuta wa Babeli tunapaswa kujiuliza kama viongozi jukumu letu ni nini? Je, lile la kuwapa vijana kile wanachohitaji ni lile la kuwashauri vijana kwa kuwaonyesha kile Yesu anachokihitaji –mlango mwembamba, njia nyembamba.

**NIDHAMU**

Rika linalohusishwa katika kundi hili bado linawajumuisha wale ambao wanafikiriwa kuwa na umri wa chini katika baadhi ya maeneo pamoja na wale wanao chukuliwa kama watu wazima na hivyo wanawajibika kabisa kwa matendo yao wenyewe. Matumaini ni kwamba wote watafanyakazi kwa kuzingatia nidhamu binafsi kile ambacho mara kwa mara huchukuliwa nidhamu ya ndani. Hivyo haiwezi kuwa hivyo wakati wote. Yawezakana kukawepo na watu wenye umri wa miaka 16 ambao hujidhania kuwa na miaka 25 na kutakuwa na kijana fulani ambaye anaweza kutohiari kuishi hadi kufikia kiwango cha utu uzima utakavyokuwa. Kwa hiyo ni kwa namna gani kiongozi ataweka kanuni za kuongoza ambazo zitaheshimiwa kwenda kwa urahisi bila kukosolewa na washiriki wa kanisa mahalia?

Hapo ndipo ufunguo wa kanuni bora na unyoofu kwa wakati huo huo. Tabia lazima zitarajiwe wakati wote wa kufuatisha maadili kwa kiwango cha juu cha kanisa na kutokuwa na kichocheo kwa uongozi wa kanisa wa mahali hapo kuvunja chama.

Hii lazima liwekwe wazi kabla ya uanachama mwanzoni mwa mambo yanayo kusudiwa kwa mwaka na vilevile kabla ya safari ndogo yoyote, kuanzia safari ndogo ndogo za utafiti wakati wa mchana hadi kwenye safari kubwa katika mikutano mikubwa ya vijana au upigaji kambi wa nje. Hii huwa kanuni ya kwanza katika kuzitawala tabia sio orodha ndefu ya mambo yanayotakiwa kutendwa na yale yasiyotakiwa kufanywa. Tabia inapokuwa hivyo, ambayo itatoa picha mbaya katika kikundi cha kanisa lenyewe, mtu anapaswa kuangilia suala hilo kwa makini kwa utulivu na upole, suluhisho linalopatikana ambalo litaanza katika kutubu badiliko la tabia hadi kuwarudisha watu katika miji yao. Ni rahisi halina hata usumbufu kila mtu anapaswa achukuliwe kama ndiye anawajibika kwa matendo yake ambayo maishani ndiyo yatathibitisha maamuzi rahisi na thabiti. Hayo ndiyo maisha katika ulimwengu wa utu uzima.

# S E H E M U 3
*Muundo*

**MUUNDO**
**KUUNDA KLABU YA BALOZI**

1. **Shauriana na mkurugenzi wa vijana wa conference.**
   Mkurugenzi wa vijana wa field/conference au misheni anahusika na klabu zote za vijana katika eneo alilopangiwa. Mtu yeyote ndani ya kanisa mahali anapoona kunahitaji la kuanzisha klabu/chama chochote cha vijana, ni lazima ashauriane na apate msaada wa mkurugenzi wa vijana kabla ya kufanya mpango wowote. Sababu ya kufanya hivyo iko wazi ni kujua na kutambua miongozo mbalimbali inayopatikana, pia ushawishi wa mkurugenzi wa vijana utawezesha mipango mingine kufanikiwa.

2. **Onana na mzee wa kanisa/ Mchungaji**
   Mkurugenzi wa vijana field/conference anaweza kuhuhudhuria kikao hicho ama kutuma wawakilishi wa vijana wa kanda/mkoa. Wawakilishi hawa watahudhuria kama wawezeshaji na wahamasishaji waliotayari kuuelezea mpango wakuanzishwa kwa klabu ya balozi na kujibu maswali wakuonyesha namna ambayo mpango huu utaboresha huduma ya mchungaji/mzee wa kanisa kwa vijana ndani ya kanisa.

3. **Wasilisha pendekezo kwenye baraza la kanisa**
   Ikiwezekana, mkurugenzi wa vijana wa conference/field ahudhurie baraza hilo na awasilishe pendekezo kwa baraza la kanisa. Ni muhimu kwa baraza la kanisa kuidhinisha kuanzishwa kwa klabu hii. Baraza la kanisa lapaswa lijulishwe kikamilifu kuhusu malengo, mahitaji ya fedha, bajeti na majukumu ya klabu ya balozi katika utume wa kanisa.

   Baraza la kanisa lazima linapewe karatasi zenye maelezo na ufafanuzi wa mambo mbalimbali ya klabu ya balozi vilevile, baraza nalo litoe habari muhimu zinazohitajika. Habari zinazohitajika ni pamoja na:- majina ya wanaklabu/ wanachama watarajiwa pamoja na anuani zao. Pia majina ya watu ambao wanaweza kuombwa kusaidia jukumu la uongozi wa klabu.

   Baraza la kanisa pia lichague mkurugenzi wa klabu ili ashike uongozi kuanzia hatua hii na kuendelea. Mkurugenzi anaweza kuwa mtu yule aliyeanzisha mpango/jambo hili. Ama mtu mwingine, na kumwacha yule mtu aliye anzisha wazo awe mshauri au mwanachama wa heshima kwa kadri atakavyo chagua yeye.

4. **Lijulishe kanisa.**
   Kutakuwa na mafanikio mazuri ukijulisha kanisa wakati wa ibadi siku ya sabato, ama kupitia kijarida cha habari cha kanisa. Ni muhimu kila mshiriki apate habari sahihi kuhusu klabu ya balozi na mipango yake. Mtu mahiri aliyebobea anayefahamu vyema habari za klabu ya Balozi, apewe nafasi siku ya sabato ili alieleweshe kanisa kuhusu hitaji la kuwa na klabu hii, ma wito ulitolewa kwa wale wanopenda kujiunga ama kusaidia klabu.

5. **Itisha mkutano maalumu siku ya sabato mchana**
   Karibisha vijana wote wakubwa wanaopenda kujiunga wahudhurie kwenye kipindi cha kujulisha dhana ya jumla na kupokea mapendekezo ya vipaumbele vya makusudi ya mpango. (watu wengine wamegundua kwamba mkutano huu unakuwa na mafanikio makubwa ukifanyika siku ya Jumapili mchana). Mkutano huu pia unaweza kutumika kama kikao cha kupanga mambo mbalimbali kwa kuwa ni jambo jema kupata maoni mengi kwa kadri inavyowezekana toka kwa wanachama wapya.

6. **Chagua kamati ndogo ya utendaji**
   Ukubwa wa kamati hii hutofautiana kutegemea na wanachama watarajiwa. Katika makanisa madogo yenye kama nusu dazeni ya vijana wenye umri unaostahili, wote wanaweza kushiriki kwenye jukumu la uongozi. Kwenye makanisa makubwa, idadi ya wana kamati inaweza kuwa 6 hadi 12, lakini isizidi kiwango hicho, kwa sababu kadri kamati inayokuwa kubwa ndivyo inavyokuwa vigumu kufanya maamuzi na kufanikisha mambo, kurahisisha utendaji ni vizuri kuwa na kamati ndogo ndogo kwa ajili ya kushughulikia mambo mbalimbali.

7. **Kubuni mpango**
   Kamati ya utendaji itakutana mara kwa mara kuandaa mpango halisi na mapendekezo ya kundi husika. Mikutano hii itafanyika ndani ya kipindi (muda) usiozidi wiki mbili toka sabato ambapo mpango huu ulitangazwa kwa mara ya kwanza (kipengele cha 5) ili kwamba vijana wasipoteze mori/ari yao ya kujiunga na klabu. Tukio la kwanza katika utekelezaji wa mpango litangawe na litekelezwe ndani ya kipindi kisichozidi wiki moja tangu mchakato wa kubuni mpango ulipokamilika.

8. **Undikashaji wa wanachama.**
   Kama sehemu ya tukio la kwanza, kuwepo na unadikaji wa wanachama(washiriki) wa klabu, uwasilishaji wa mipango ya mwaka, kutangaza vipengele vya mpango, kuchagua sare na mambo mengine yenye mvuto kwa klabu.

**KUDUMISHA KLABU/CHAMA**

Ari au moyo kupenda klabu ni jambo muhimu sana ambalo huamua mafanikio klabu/kundi lolote. Ni mkusanyiko wa vitu mbalimbali muhimu. Viongozi wote na wenyeviti wa vikundi watahitaji kufanya kazi pamoja kwa ukaribu katika kukuza hali moja na ushiriano, na kudumisha mvuto na usongo wa kushiriki mambo mbalimbali ya klabu. Viongozi ni lazima wakumbuke kuwa klabu ya Balozi siyo klabu ya watafuta njia wakubwa. Klabu hii inashughulika na mahitaji ya kisaikolijia na kihisia ya makundi tofauti kimaudhui na kifani (Mtindo) na zenye kufuata mapendekezo ya wanaoshiriki (wanachama). Mtindo ulio na kanuni nyingi na utaratibu maalumu uwekwe akiba kwa ajili ya vijana wanaochagua mafunzo ya uongozi wa watafuta njia.

**Viongozi wa klabu watatakiwa mara kwa mara kuupitia upya mpango (program) wakizingatia mambo yafuatayo akilini;**

1. **Makusudi ya kiroho**
   Viongozi wa klabu ya Balozi na wale wa kamati ndogo ndogo wanatakiwa kuhakikisha kwamba klabu inaendeshwa kwa misingi ya kiroho. Kanuni za kiroho nishani ndizo ziwe dira. Kumwakilisha Kristo katika namna sahihi ndicho kiwe kipaumbele, kutumika kikamilifu mchungaji wa mtaa ama wazee wa kanisa. Hakikisha kuwepo na muda wa kutosha wa kukuza moyo wa kujitoa kwa Mungu na kufanya kila linalowezekana kufanya muda huu uwe wa maana kubwa.

2. **Mahudhurio.**
   Wakati mara nyingi watu hulenga kuwa na mahudhurio asilimia 100. Asili ya klabu hii na programu zake hazihitaji mahudhuri ya 100% wapo ambao watachagua kutokushiriki katika kipengele fulani cha programu kwa sababu tu haigusi mahitaji yao halisi, hata hivyo wale ambao mahitaji yao yameguswa, wataona ni faida kuhudhuria na kushiriki. Pia ni lazima kuzingatia ukweli kwamba, katika umri huu vijana wana majukumu ya kazi na shule ambayo yatakwamisha kuwa na mahudhurio ya asilimia 100 kwa matukio yote yanayopangwa. Programu zinazofanyika kwa kuzingatia maoni ya wanachama wengi zitahakikisha ushiriki wa vijana wengi.

3. **Kuwasiliana na mtu mmoja mmoja.**
   Hakuna kitu chenye kuleta mafanikio makubwa kama kitendo cha kiongozi kufanya mawasiliano binafsi na mwanachama mwenye tatizo la kushindwa kuhudhuria mara kwa mara.

4. **Vikao vya viongozi**
   Vikao hivi visifanywe katika hali ya usiri, bali vitangazwe hadharani na kukaribisha watu wengine wasio viongozi kuhudhuria ikiwa watapenda na kutoa maoni yao. Hili litasaida pia kuwapata viongozi wa kushika nafasi mbalimbali pale inapohitajika.

5. **Kuwakaribisha wanachama**
   Inawezekana kuoneka kuwa siyo muhimu kuwakaribisha wanachama. Lakini kila mtu aliyehudhuria ni vyema ajisikie kuwa anakaribishwa, ukaribisho utatia moyo watu kujiunga na utayeyusha mioyo ya wale waliokuja na lengo la kukosoa.

6. **Kuandaa programu yenye ulingalifu**
   Ni jambo jepesi kutoka nje ya mipaka katika klabu kama hii. Hili hutokea kwa sababu viongozi wanaweza kupendelea kufanya jambo fulani na kuacha jingine, ama kwa sababu mwenyekiti wa kamati moja ndogo ni mbunifu kuliko wengine, ama kwa sababu jambo fulani linaburudisha kuliko jingine, ama kwa sababu viongozi wanaogopa kufanya jambo ambalo litasababisha kukosolewa kwingi na sababu zingine. Mara kwa mara tathimini mambo yanayotakiwa kuingia kwenye programu, na hakikisha kuwa unajumuisha mambo mengi kwa kadiri inavyowezekana.

7. **Mahali pakukutanikia**
   Hakikisha kuwa mahali pa kukutanikia palipo chaguliwa panaendana na tukio ama shughuli iliyopangwa na paendane na hali ya hewa, viti vya kutosha, jukwa la kutosha na miongozo ya kazi mbalimbali lazima vizingatiwe.

**SARE**

Hakuna sare rasmi inayotambulika kiulimwengu ambayo imetumika kama utambulisho wa klabu. conference ama klabu husika inawezekana kupendekeza sare ambayo itajumuisha Sharti (imependekezwa rangi ya light blue) pamoja na nembo inayovaliwa juu ya mfuko wa kushoto.

Skafu, slide na pini ya master guide au kiongozi wa vijana vinaweza kuvaliwa pamoja na sare hii ikiwa mvaaji amehitimu madarasa hayo. Skafu ya klabu ya rangi ya blue iliyokoza (Dark blue) na iliyo na nembo ya klabu, inaweza kuvaliwa na wanachama wote ikiwa kiongozi wa vijana wa Division ama union atakuwa ameagiza hivyo.

Nembo za klabu zenye kuwakilisha vyama vilivyoundwa katika eneo fulani mfano mkoa/jimbo ambavyo ni vyama mbadala vya klabu ya balozi zinaweza kuvaliwa sambamba na nembo ya klabu ya Balozi. Skafu za chama cha watafuta njia na wavumbuzi, zisivaliwe pamoja na sare ya klabu ya balozi.

Katika nchi nyingi kuvaa sare zinazofanana na za jeshi ni kosa, ili kulinda heshima ya chama (klabu) mavazi ya namna hiyo yasivaliwe. Vazi lolote ama kitu chochote kinachoweza kuifanya serikali kukifananisha chama/klabu na jeshi kisivaliwe. Vitu hivyo ni kama vile vitabu vya jeshi na vitu vyenye kufanana na silaha za kijeshi.

Mkanda unaofanana rangi na suruali ya ugoro, unaweza kuvaliwa kwa makusudi ya kupachika pini na tuzo, sare ya siku ya sabato inayopendekezwa ni shati/blauzi ya "light blue" suruali ya ugoro na tai ya rangi moja.

**BIMA**

TAHADHARI: Hakikisha kuwa shughuli zote ama matukio yote ya chama/klabu yamelipiwa bima kwa mujibu wa sera za bima za kanisa dhidi ya ajali na bahati mbaya. Pia hakikisha kuwa kanuni zote za kiusalama zimefuatwa kulingana na tukio husika.

FOMU ZA KUJIUNGA/UANACHAMA

Angalia kiambatanisho namba 1.

BENDERA.

Bendera itakayotumiwa na chama/Klabu ya balozi itakuwa ni ile inayotumiwa na AY ikiwa chama kitapenda kinaweza kutumia "Guidon za dark blue na light blue" zenye nembo ya balozi iliyobandikwa kati ya rangi hizo mbili.

**FEDHA**

Kadri ya chama kinavyo kua/panuka na shughuli kuongezeka, fedha itakuwa ni tatizo, wakati vijana wengine wanaweza kuwa na vyanzo binafsi vya mapato, wengine pia watakuwa hawana, mahudhurio yatapungua na kusababisha kukata tamaa na kupunguza ushirikiano. Mengi ya mahitaji madogo madogo yanaweza kutatuliwa kwa kutumia pesa za michango ya wanachama kwa kadri na hitaji yatakavyo jitokeza. Muda si mrefu kuchangisha pesa ili kutunisha mfuko itakuwa jambo la lazima. Kuna maeneo mengi ya kuchangisha fedha kwa vyama vya aina hii. Baadhi ya mbinu hizo ni nyepesi lakini zenye mafanikio kidogo, na nyingine ni ngumu lakini zenye matokeo mazuri. Vyanzo vizuri vya pesa ni vile vinavyo jumuisha wale wenye mapenzi na chama, yaani wanaokipenda chama: wanachama wa klabu, ndugu za wanachanna, na washiriki wa kanisa kwa ujumla. Lakini kumbuka kwamba kundi hili huchangia kwa kiasi kikubwa gharama za uendeshaji wa kanisa kuendelea kuwaongezea mzigo kutupunguza matoleo kanisani.

Vile vyanzo vya pesa vinavyoonekana kuwa ni vigumu kufikiwa bali vyenye rasilimali nyingi ni wale watu matajiri, wafanyabiashara, serilaki za mitaa na jamii yote kwa ujumla, kwa kadri chama/klabu kinavyozidi kujishughulisha na miradi ya huduma kwa jamii kitapata heshima na umaarufu hivyo ufadhili na michango itapatikana kwa urahisi. Heshima na umaarufu utapatikana kwa kujitangaza kwa njia ya vipeperushi/vijarida vilivyoandaliwa kwa ustadi mkubwa na kwa kushiriki waziwazi katika huduma mbali mbali za jamii. Njia nyingine ni kuendesha mafunzo ya bure ya ufundi stadi ambayo yako wazi kwa jamii yote. Siku hizi kuna vyama/klabu vinavyojitegemea kabisa kifedha kwa kutumia njia hizi.

**SERA YA HARAMBEE/KUCHANGISHA FEDHA.**
Hapa ziko kanuni za jumla za kukuwezesha kujua kama harambee iliyopangwa inakidhi viwango vilivyowekwa na kanisa.

1. Je, changizo limeidhinishwa na baraza la kanisa na idara ya vijana ya field/conference?
2. Je changizo halipingani na kanuni na taratibu zilizowekwa ka serikali za mitaa?
3. Je changizo limejiepusha kuwa na sura inayofanana na kamari?
4. Kama kuna bidhaa za kuuza, Je, zitauzwa kwa kuzingatia ubora wake na bila kuhusianishwa na mahitaji ya chama/klabu au mwanachama?
5. Je wale wanaonunua bidhaa watafaidi thamani ya fedha yao?
6. Je kuna vyama/klabu zingine zinazofanya kazi katika eneo hilo hilo na kwa wakati huo huo mnapofanya changizo?
7. Je, mmehakikisha kwamba hakuna mtu yeyote anayehitaji kazi ambaye anaweza kuikosa kazi hiyo kutokanana na shughuli za changizo?
8. Je changizo litalinda sifa na heshima ya chama/klabu ya balozi na kanisa la waadvetista wasabato na halita sababisha madeni kwa conference/field.

**KUMBUKA**: Taarifa ya fedha lazima ipelekwe kwenye Baraza la kanisa angalau mara moja kila mienzi mitatu, na taarifa ya shughuli na matukio mbalimbali isomwe mbele ya kanisa na kutumwa na ofisi ya idara ya vijana ya conference au field kila baada ya miezi mitatu.

**MAHUSIANO YA KIJAMII**
**WAMBIE WANGINE SHUGHULI UNAZOZIFANYA!!!!**
Kama kanuni ya jumla, tunaonekana kuamini kwa nguvu usemi kwamba "Mkono wako wa kulia usijue kile mkono wako wa kushoto unachofanya" KOSA!!!!

Naam, kuna mahali pakutumia usemi huo, lakini siyo hapa. Kuwafahamisha wengine shughuli tunazozifanya ya paswa kuwa jambo/tendo endelevu na katika ngazi mbalimbali.

1. Wanachama – mara kwa mara hata wanachama wa klabu hawafahamishwi nini kinaendelea ndiyo maana kuungwa mkono kunakosekana.
2. Kanisa mahalia linategemea kusaidia na kujivunia vijana wake, sharti wafahamu mambo mazuri yanayofanywa na vijana.
3. Jamii- Taarifa za habari zimejaa mambo maovu yanayofanywa na vijana, tuna nafasi ya kubadili hali hii katika kutangaza mambo mazuri yanayofanywa na vijana, siyo kutaja tu misaada inayoongezeka toka vyanzo zisivyotegemewa katika jamii.
4. Ngazi mbali mbali za kanisa – Gazeti la kanisa mahalia, Union na Division, wavuti/tovuti vyote vinataka kufahamu kinachofanyika ili kuweza kuhimiza maendeleo katika maeneo mengine, mafanikio yanaweza kujirudia ikiwa kutakuwepo na fursa.

**MATUMIZI YA MADARAKA NA NISHANI ZA WATAFUTA NJIA NA A.Y**
Siku hizi madarasa na nishani kimsingi yanahusianishwa na chama cha watafuta njia, hata hivyo kwa asili jambo hili halikuwa hivyo. Madarasa hayo yalikuwa yakitumiwa kikamilifu na vijana wote kuanzia wenye miaka 10 hadi utu uzima kama dirisha la kuangalia na kuvumbua maajabu ya ulimwengu. Jambo hili ni vyema likabakia lilivyokuwa zamani. Pamoja na hayo, katika programu za klabu/chama cha balozi lengo na sababu yakutumia madarasa ni tofuati kidogo na chama cha watafuta njia, kwenye klabu ya balozi ushiriki ni zaidi wa kufungua tu madirisha ya udadisi na ugunduzi, ushiriki katika madarasa humaanisha pia kukuza uwezo wa kuongoza/uongozi wa uwezo wa kufundisha wale

walio kwenye madarasa ya chini. Kwa hiyo msisitizo mkuu utolewe kuhusiana na kukamilisha madarasa hadi kufikia darasa la juu kabisa; na nishani zote hadi ya juu kabisa. Ni mpango wa idara ya vijana makao makuu ya kanisa ulimwenguni kuziendeleza nishani zote hadi kufikia kiwango cha juu kabisa ndani ya miaka michache ijayo.

Madarasa mapya mengi ya juu yameongezwa hivi karibuni, orodha ya madarasa hayo mapya inaweza kupatikana kwenye tovuti: www.youth.gc.adventit.org ama kwa kuiandikia idara moja kwa moja. Kila mwanachama wa klabu ya balozi yampasa kuwa na faili maalumu kwa kila darasa na kila nishani alizo kamilisha kama zana ya kufundishia.

Faili hizo zijumlishe ushahidi wa kazi binafsi alizowahi kufanya:- michoro orodha ya vitabu vya kufundishia vinavyopatikana kwenye duka, majina ya wawezeshaji/walimu wanaofahamu kufundisha vizuri ndani ya kanisa na nje.

**KUDUMISHA BIDII/KUKUZA HAMASA**

1. Panga tarehe maalumu ya kukamilisha madarasa ama nishani:- tengeneza ratiba/chati muda wa mwaka mzima kwa darasa la jumla, madarasa ya juu, kiongozi mkuu, au uongozi wa AY, ili kwamba kila mwanachama apate nakala na kuitumia na kuhakikisha kwamba wanaenda sambamba na muda iliwaweze kuhitimu na kuvishwa pini/nishani. Nishani moja ikamilishwe ndani ya miezi mitatu.
2. Yafanye (mafunzo/masomo) kuwa ya thamani. Lazima yawe yenye kuburudisha, changamsha, umuhimu na kusaidia, usifundishe matakwa (mahitaji) kwa juu juu tu, utupunguza thamani ya mafunzo. Majaribio/mitihani inafaa sana katika kuhakikisha ubora wa kazi, mahitaji yote kwa ajili ya nishani husika sharti yakamilishwe.
3. Kubadilisha/kurekebisha mahitaji –katika matukio machafu, mahitaji fulani yanaweza kubadilishwa, mahitaji yenye uzito sawa yanaweza kubadilishana, hili lifanyike kwa kibali cha mkurugenzi wa vijana wa field au conference.
4. Kukamilisha mahitaji:- Kila kazi iliyotakiwa kufanywa sharti ifanywe. Maelezo matupu bila vitendo hayakamilishi hitaji. Kazi zote za mafunzo sharti zisainiwe na kiongozi mkuu, kiongozi wa AY au mwalimu aliyeidhinishwa na mkurugenzi wa vijana.
5. Tuzo za kiongozi:- Kuna tuzo 12 za kiongozi, kuwepo na msisitizo mkubwa wa kukamilisha/kufaulu tuzo zote, hili litadhihilisha kuwepo kwa nia kubwa na upendo kwa maeneo mbalimabli ya shughuli za vijana kanisani. Pia itampatia mhusika uwezo mkubwa wa mambo mbalimbali.
6. Huduma ya kuvisha pini/nishani- ni jukumu la uongozi wa chama kuwasilina na machungaji wa vijana wa field/conference na kupanga mkutano wa kuvisha pini/nishani ya wavumbuzi na watafuta njia ama unaweza kufanyika kwenye eneo maalumu litakalo chaguliwa ili kulifanya liwe la kuvutia zaidi.

**SHEREHE YA KUTOA MAELEKEZO KWA WANACHAMA WAPYA.**

Kutokana na mafunzo yasio na masharti mengi ya chama cha balozi ukilinganisha na chama cha watafuta njia, sherehe za kutoa maelekezo kwa wanachama wapya hazitakiwi, hata hivyo klabu zinazopenda kuwa na sherehe za namna hiyo zinaruhusiwa, wafanye sherehe rahisi yenye mguzo wa kiroho.

**KUMBU KUMBU ZA KAZI ZILIZOKAMILIKA**

Klabu mahalia inatakiwa kuwa na faili lenye kutunza kazi zote za darasani, nishani, na vyeti vya msalaba mwekundu na kazi nyingine ambazo zimekamilishwa na wanachama, hii itakuwa ni sehemu ya

uzoefu wao ndani ya chama/klabu ya Balozi, kutunza kumbu kumbu hizi kutasaidia pale mwanachama anapoteza cheti, pini au nishani.

**UONGOZI**

Viongozi wa klabu ya balozi watachaguliwa na baraza la kanisa husika (hizi ni klabu zinaoundwa na kufadhiliwa na kanisa mahalia) uongozi wa klabu za namna hii utakuwa angalau na kiongozi mmoja na mwanachama mmoja wa heshima mwenye umri unaozidi umri wa vijana. Viongozi hawa sharti wawe washiriki wa kanisa mahalia wenye msimamo thabiti (kiroho) na walio komaa kiimani (kiroho) kiasi cha kutumika kama washauri na waelekezaji wa mambo ya kiroho kwa wanachama.

Kuna wakati ambapo field/conference litapenda kuunda chama/klabu ya balozi ya mtaa, uongozi utachaguliwa na mchungaji kwa kushilikiana na wazee wa makanisa yaliyomo kwenye mtaa. Kwa klabu zinazo husisha eneo kubwa zaidi, mfano field/conference, viongozi watachaguliwa na mchungaji wa idara ya vijana wa field/conference kwa kushauriana na wachungaji wa mitaa ama makanisa. Sifa za viongozi hawa ni sawa na zile za kiongozi wa klabu kanisani, tofauti ni kwamba klabu ya field/conference itafanya kazi chini ya udhamini na ushauri wa mkurugenzi wa vijana wa field/conference.

Wote wanaochaguliwa kuwa viongozi wa klabu ya balozi waelezwe kuwa watashikilia nafasi hizo kwa muda usipungua miaka miwili, mabadiliko ya naweza kutokea ikiwa yataamuliwa na chombo kinacho fadhili klabu kutokana na kubadili mtindo wa maisha, uhamisho wa washiriki wa wanachama wetu viongozi wote pia yawapasa ama wawe wamemaliza mafunzo ya MASTER GUIDE au uongozi wa vijana au wakubali kufanya maandalizi ya kutuzwa vyeo hivyo kwa kipindi cha mwaka wa kwanza kazini. Mahitaji yao tofauti kwa nyakati tofuati kulingana na ukubwa wa vyama vyao. Waatalamu hawa lazima wahiari kufuata mtindo wamaisha ya kanisa la kiadventista nyakati zote. Kuna wakati itabidi kuwatumia wale wasio fuata mtindo wa maisha wa kanisa letu, kama wageni watoa mada katika baadhi ya mada, hali kama hizi zinatambulika kuwepo na zinaruhusiwa inapolazimu lakini hazipendekezwi kutumika mara kwa mara kwa muda mrefu.

**WAJIBU WA WANAKAMATI WA CHAMA**

Zifuatazo ni nafasi kumi za uongozi wa chama zilizooroshwa ambazo zaweza kuungishwa pamoja au kugawanywa zaidi kutegemea uhalisi wa kila chama. Yawezekana kukawa na aina nyingine zinazoweza kuongezwa na chama husika kulingana na mahitaji.

**Ufadhili:**

Kwa ujumla makanisa yanapenda kuchagua mtu wa makamo kama vile mmojawapo wa wazee wa kanisa kuwa kama mfadhili kwa kila chama na vyama vyote vya vijana kutoa ushauri wa busara, kuutia moyo uongozi na inapohitajika kuutetea muungano huo.

**Mkurugenzi:**

Mtu huyu huchaguliwa na baraza la kanisa, yeye anahusika na matendo yote ya chama na ndiye anaye wajibika katika baraza. Mtu huyu yapasa awe ameonyesha kiwango cha juu cha ukomavu na kuaminiwa na mwenye maarifa katika kusimamia mapato na fedha. Vile vile awe na upendo zaidi kwa vijana wa kanisa. Pia inapendekezwa zaidi mtu huyu awe mjumbe ya baraza la kanisa.

**Mkurugenzi msaidizi.**
Anaweza kuchaguliwa na baraza la kanisa, au kuteuliwa na mchungaji wa kanisa au mzee wa kwanza wa kanisa. Sifa zake ni sawa na sifa zote za mkurugenzi zilizotajwa hapo juu na atakuwa badala ya mkurugenzi wakati napale inapohitajika.

Mwenyekti wa kamati ndogo ya darasa.
- Master guide/Tuzo ya uongozi wa vijana
- Darasa la pamoja na mitaala mingineyo.

Mtazamo mmojawapo wa chama hiki ni kuandaa uongozi maarifa haya kuwa na maeneo mbali mbali ya kutazama. MASTER GUIDE imeandaliwa kwa ajili ya wale wanaohitaji kuwa viongozi wa watafuta njia na wagunduzi, tuzo ya uongozi wa vijana ni kwa wale wanaohitaji kuhusika na uongozi wa vijana wakubwa, semina nyingine za uongozi katika nyanja nyingine za uongozi wa shughuli za kanisa zaweza kufadhiliwa. Pale ambapo tayari kuna chama cha MASTER GUIDE au uongozi wa vijana, moja kwa moja vitakuwa sehemu hii ya Balozi, mkurugenzi wake aweza kuwa ndiye Mwenyekiti. Matukio yatakayo hitajika kukamilisha mahitaji ya kufikia MASTER GUIDE au uongozi wa vijana yatafanywa na kamati nyingine ndogo ndogo ili kuwa za manufaa zaidi kwa wale wote watakao kuwa wamehusishwa . Hapa chini pia kuna kipengele na mahitaji ya darasa la pamoja.” Baadhi ya Divisheni zimekwisha anzisha.

Mtaala maalumu kwa ajili ya vyama kutosheleza kundi la umri huu. Huduma hizi zaweza kujumuishwa pamoja katika chama hiki na kuwa chini ya uongozi wa kamati hii. Kwa vile wale watumiao mtaala huu wana vyanzo vyao, hawatahusishwa katika mpangilio wa mwongozo huu.

**Mwenyekiti wa kamati ndogo ya nishani**
- Mafunzo ya ufundi
- Kuibua hobi (Hobby)

Shughuli nyingine za mafunzo ya ufundi na hobi vyaweza kusisitizwa na kukuzwa kwa kutumia nishani zaidi ya 250 zilizopo. Hizi zitawapa moyo zaidi vijana wetu kukidhi nafasi za ajira katika maeneo yatakayo wavutia na kutosheleza wanapokuwa wakiyatazamia yale Mungu aliyowaandalia.

**Mwenyekiti wa kamati ndogo ya utembeleaji**
- Uinjilisti wa mahusiano
- Uinjilisti wenye matokeo

Lengo la mwanzo la ingizo lolote lidhaminiwalo na kanisa ni lile litakalo husishwa utimilifu wa jukumu la kazi injili. Hili linafanywa kupitia aina zote za unjilisiti, kuanzia aina zote za kawaida hata zile mbinu bora zaidi ambazo hazijafikiliwa. Ni jukumu la kundi hili gundua na kujizoeza njia zionekanazo kufaa kulignana na ujuzi wa wanachama wao na vyanzo vya utendaji sambamba na tamaduni za sehemu husika.

Kundi hili pia lifanya kazi kwa ukaribu zaidi na kundi la darasa na kikundi cha huduma kwa jamii kuhakikisha uwepo wa muungano wa shughuli na matukio maalumu.
- ***Mwenyekiti wa kamati ndogo ya huduma kwa jumuiya.***
- ***Mjumbe majeshini kwa ajili ya vyama vitoavyo huduma.***
- ***Mawasiliano –vyombo vya mawasiliano/kanisa***

- ***Mtazamo wa idara ya vijana wa kiadventista ni kutoa huduma na wokovu, kamati hii ndogo ina husika na ukamilifu wa sehemu ya pili ya mtazamo huo kuwa ushirika wake.***

Kila jumuiya ina mashirika yanayo hitaji msaada wa hiari kutoka kwa vijana wetu wa msalaba mwekundu kwa huduma za lishe, taasisi za afya na shule hizi zote zinafanya chaguzi kuwa nyingi kwa vile haya pia yako wazi zaidi kwa umma, kikundi hiki kitahitaji kuhusisha mzigo huu kutumia vyombo vya kidunia na vile vya kanisa.

**Mwenyekiti wa kamati ndogo ya mahusiano**

- **Matukio katika jamii / Mtindo wa maisha**
- **Semina kabla ya ndoa**

Hakuna kundi la vijana liliokamilika kusipokuwa na chombo imara katika jamii. Vijana wanahitaji kukusanywa pamoja kwa ajili ya wakati wa kiafya na kubadilishana mawazo. Hii ni njia pia kuwaleta vijana wengine katika elimu ya injili, kikundi hiki lazima kifanye kazi bega kwa bega na kikundi cha utembeleaji katika lengo hilo. Wengi wa vijana wakubwa huwa wamefikia umri ambapo mambo ya msingi ya mtindo wa maisha na maandalizi katika ndoa vinapewa umuhimu mkubwa. Chama kilicho kizuri kitaandaa mfululizo wa semina kabla ya ndoa na mtindo wa maisha kila mwaka hasa kwa wale wanachama wafikao hatua hii maishani mwao. Kijitabu kidogo kuhusu mtindo wa maisha kilichochapishwa na idara ya huduma kwa vijana chaweza kutumika pia.

Semina hizi zaweza kufanywa kama matukio makubwa kwa kuualika umma pia au zaweza kuwa mtukio madogo yaliyoandaliwa tu kwa ajili ya wanandoa wahitaji.

**Mwenyekiti wa kamati ndogo ya burudani**.

- Matukio ya ukambikaji
- Uvumbuzi mkuu
- Michezo

Aina ya shughuli hizi huchukua uzito zaidi, uhusishwapo na matukio katika jamii na yabidi kuwepo na uongozi kwa ajili ya shughuli hizi, uongozi huu utafanya kazi kwa ukaribu zaidi na kikundi tajwa (husika) hapo juu. Matukio yahusuyo safari ndefu, muda mrefu kambini, kundi hili litawajibika kutoa mfunzo maalum kwa ajili ya ushiriki bora kuna baadhi ya vyama vya vijana ambavyo tayari vimekwisha husika katika utafiti na uokaji, na shughuli nyingine za namna hii kama vile uvumbuzi na ushiriki wa michezo. Hivi vitakuwa ni sehemu ya uongozi wa kikundi hiki.

**Mwenyekiti wa kamati ndogo ya ubora wa viwango vya juu.**

- Tuzo ya fedha
- Tuzo ya dhahabu

Huduma hizi mbili zitahamasisha au kuratibiwa na klabu ya Balozi. Tuzo hizi zimeandaliwa mahususi kwa ajili ya kundi la umri huu. Pamoja na kuwa na mwingiliano mkubwa katika matumizi na kamati ndogo zilizo salia, ni zenye mambo mazito na timilifu kiasi cha kuhitaji kuwa chini ya kundi la viongozi. Ukamilisho wa tuzo hizi uko chini ya mwongozo makini zaidi, kwa kutoa orodha ya mahitaji kama ilivyo ainishwa katika nembo na sherehe ziwakilishazo tukio hili. Tuzo hizi si kwa ajili ya kukatisha tamaa wala kwa wale wanaohitaji kupata kitu kwa haraka. Zahitaji uvumilivu, utii, mafunzo mazito na shughuli – shughuli nyingi. Ukamilisho wa tuzo hizi za daraja la juu mtu hukaribia kuwa miongoni mwa daraja la washindi.

Miongozo kwa ajili ya tuzo hizi yaweza kunakiliwa katika tovyti ya General Conference (makao makuu ya kanisa la waadventista ulimwenguni).

Tovuti: youth.gv.adventist.org

# SEHEMU 4
***Mipango ya Ratiba za Chama***

**KUPANGILIA NA KURATIBISHA:**
**MAPENDEKEZO KATIKA KUPANGILIA**

1. Kukuza vipaji vya uongozi kupitia mtaala wa MASTER GUIDE na AY.
2. Kuitembelea jumuiya kwa njia ya utoaji wa huduma na mafunzo ya utayari katika dharura.
3. Kukua kiroho kupitia unjilisti wa kawaida na ule wa kisasa (ulioboreshwa zaida)
4. Mafunzo ya staadi za maisha/uwezeshaji katika kupitia mafunzo maalumu.
5. Mbinu za kukuza urafiki (uhusiano) kupitia mahusiano mahususi na semina kabla ya ndoa.
6. Kuboresha haiba na tabia/kujitambua kupitia mpango wa utembeleaji na uvumbuzi mkuu.
7. Kuboresha maisha kwa kupitia matumizi ya nishani kuu kama ilivyo ainishwa katika kijitabu cha nishani za A.Y.

Mikutano ya kila mara yatakiwa kufanyika angalau mara moja kwa mwezi, ikiwezekana mara mbili. Mikutano hii inatakiwa ilenge vifungu namba 1, 4 na 5 hapo juu, na ikilazimu itahusisha mafunzo yaliyo chini ya vifungu namba 2, 3 na 7.

Mpango yakinifu na ulioandaliwa kwa ufasaha wapaswa uanzishwe utakaoweka wazi shughuli za miezi kadhaa /au uliohusika hasa katika wiki, kadhaa kwa mwaka katika shughuli zihusuzo yaliyo chini ya vifungu namba 3, hapo juu.

Mbinu pamoja na mambo ya kuhusisha katika huduma mbali mbali vitabadilika kulingana na mahitaji, tamaduni, ujuzi uliopo na vyanzo vipatikanavyo. Pamoja na hayo uongozi lazima utambue kwamba matukio yote yatakwenda sambamba na utunzaji wa kanuni za kikristo na miongozo ya kanisa. Muda wa mikutano utatofautiana kuanzia saa moja hadi nusu siku na inatakiwa utangazwe angalau wiki moja kabla ya kila mkutano. Utunzaji wa huduma zilizoratibiwa na klabu ya vijana wakubwa (A.Y.S) uwe wa hakika ikiwa tatizo la mgongano wa ratiba waweza kuwepo hasa siku za Sabato mchana.

**RATIBA ZA MWAKA**

Zifuatazo ni baadhi ya ratiba zilizopendekezwa kwa ajili ya kamati ndogo za Balozi. Lazima itambulike kwamba haya ni mapendekezo tu ambayo lazima yafuatwe kutokana na uhalisi wa eneo husika. Uhalisi wa kila sehemu husika unatokana na sehemu ipi ya Dunia uliyopo. Miezi fulani yafaa sana upande mmoja kuliko mwingine, ratiba za shule za likizo zaweza kuathiri ratiba hii, kalenda ya matukio katika ngazi ya field yaweza kuathiri ratiba hizi pia, hivyo lazima kuwepo na mawasilinano wakati uandaapo mpango wako wa mwaka.

Tunaanza na huduma mbili kuu zaidi, zile za tuzo ya uongozi wa vijana wa MASTER GUIDE, shughuli nyingine zote zifuate ratiba hizi kama kikundi cha vijana ni kidogo na vijana hawa hawa ndio wahusika katika shughuli zote. Katika makundi makubwa yenye idadi kubwa ya vijana wa husikao kati ya moja ya makundi yaliyopo, si vyema kuziunganisha shughuli hizi pamoja. Mojawapo au zaidi kati ya hizi kamati ndogo miongoni mwa kikundi cha vijana hawa, yaweza kufanya shughuli kwa kujitetemea. Si lazima kuwepo na kikundi cha uongozi wa vijana au MASTER GUIDE (kiongozi mkuu) ndipo mafanikio ya utendaji wa shughuli za chama yafakiwe.

**RATIBA YA MASTER GUIDE (Kiongozi Mkuu)**

**Utangulizi:-**
- Awe na umri wa maika 16 au zaidi.
- Awe mshiriki wa kanisa

**JANUARI:**

Ibada & Jarida ( mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia )
Mipanga binafsi na malengo mahususi.
Mwanzo/mtaala wa mafunzo ya darasani
Mbinu za uongozi –e
Utangulizi katika msingi ya imani

**FEBUARI:**

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka Biblia
Mazoezi ya viungo vya mwili
Semina ya 1, masaa 2
Nishani ya simulizi za hadithi za kikristo
Mtaala wa darasani

**MACHI:**

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Mazoezi ya viongozi vya mwili
Semina ya II, masaa 2
Simulizi na hadithi za kikristo
Mtaala wa darasni.

**APRIL**

Ibada (mlolongono wa visa/mwaka wa Biblia
Mazoezi ya viungo vya mwili
Semina ya III, masaa 2
Mbinu za uongozi B
Mtaala wa darasani

**MEI**:

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Semina ya IV, masaa 2
(church heritage)

**JUNI:**

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Mbinu ukambikaji sehemu ya II
Nishani ya I

**JULAI:**

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Njia salama (kitabu)
Hadithi za watafuta njia
Nishani ya II

**AGOSTI:**

Ibada (mlolongo wa visa/mwaka Biblia)
kitabu kuhusu urithi wa kanisa.

**SEPTEMBA**

Ibada(mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Elimu
Matembezi msituni,
Mafunzo ya watumishi mwishoni wa wiki
Mbinu za uongozi ………………. C

**OKTOBA:**

Ibada(mlolongo wa visa/mwaka wa Biblia)
Kitabu cha uongozi
Huduma ya kwanza
Mbinu za uongozi …………………d

**NOVEMBA:**

Ibada (ESI/BY)
Kitabu cha maendeleo ya
Moto wa semina (mbinu)
Ujuzi wa Uongozi

**DESEMBA**

Ibada (ESI/BY)
Misingi ya mtihani
Urithi wa kanisa mtihani

Mbali na viongozi waliochaguliwa, kila chama kinahitaji kuhusisha huduma za wataalamu wengine zaidi kukidhi.

## RATIBA YA UTOAJI TUZO KWA UONGOZI WA VIJANA

Januari

Utangulizi
Wewe na Mungu (reg.2)

Februari:

Wewe na Mungu (Require 2 continue)

Machi
Wewe na Mungu (req.2 )
Wewe na vijana (req. 1 a)

April:
Wewe na Mungu (req. 2 cont.)

Mei:
Wewe na Mungu (req. 2 cont.
Wewe na Mungu (req. 4a)

Juni:
Wewe na Mungu (req. 2 cont.)
Wewe na kanisa (req.2 cont.)

Julai:
Wewe na kanisa (req. 2)
Wewe na jamii (req. 1)

Agosti:
Wewe na kanisa (req. 2 cont.)
Wewe na jamii (req.2 cont.)

Septemba
Wewe na Mungu (req.1)
Wewe na Kanisa (req 2)

Oktoba
Wewe na Mungu (req.3)

Novemba
Wewe na kanisa (req. 1)

Desemba
Wewe na Mungu (req. 3 tool)
Wew na kanisa (req. 1 tool)

## RATIBA YA NISHANI ZA SUBCOM KWA KWAMBA

**Januari:**
Nishani ya sanaa na ujuzi

**Februari:**
Nishani ya lishe (YLA)
Nishani ya masimulizi ya ukirsto

**Mach**
Nishani ya Afya na sayansi

**April**
Nishani ya Asili
Nishani ya sanaa na ujuzi

**Mei**
Nishani ya ubora wa mwili (YLA)
Nishani no. 1 ya ujuzi wa kambi

**Juni**
Nishania II ya ujuzi wa kambi
Nishani ya kuchaguliwa (MG)

**Julai**
Nishani II ya kuchaguliwa (MG)
Nishani ya mafunzo

**Agosti**
Nishani ya mahubiri ya Biblia

**Septemba**
Nishani ya utendaji wa nje

**Oktoba**
Nishani ya mafunzo
Nishani ya huduma ya kwanza

**Novemba**
Ukamilishaji wa nishani ambazo
Hazikukamilika

**Decemba**
Ukamilishaji wa nishani ambazo
hazikukamilika.

YLA = Youth Leadership Award
MC= Master Guide

## RATIBA YA USHUHUDIAJI WA SUBCOM KWA MWAKA

**Januari**
Mradi wa mahubiri ya kirafiki

**Februari**
Mpango wa mahubiri ya kirafiki yana endelea

**Machi**
Juma takatifu la mahubiri

**April**
Uandaaji wa semina

**Mei**
Semina za jamii

**Juni**
Semina za jamii

**Julai**
Uandaaji wa semina

**Agosti**
Mikutano ya kimahubiri (YLA)

**Septemba**
Ubatizo

**Oktoba**
Mradi wa mahubiri ya kirafiki

**Novemba**
Mipango ya Krismas

**Decemba**
Ushuhudiaji wakati wa chrismas

## RATIBA YA USHUHUDIAJI JAMII YA SUBCOM KWA MWAKA

**Januari:**
Mradi I wa mpango wa jamii

**Februari**
Mradi I wa jamii

**Machi**
Mradi wa lengo la maisha

**April**
Mradi wa maisha bora

**Mei**
Mradi wa maisha bora (YLA)

**Juni**
Mradi wa maisha bora (YLA)

**Julai**
Mradi II wa mkakati wa jamii

**Agosti**
Mradi wa jamii II

**Septemba**

**Oktoba**
Mradi wa mkakati wa jamii III

**Novemba**
Mradi III wa jamii

**Decemba**
Sherehe ya krismas kwa yatima

## RATIBA YA NISHANI ZA SUBCOM KWA MWAKA

**Januari:**
Nishani ya sanaa na ujuzi

**Feburari**
Nishani ya lishe
Nishani ya masimulizi ya ukristo (MG)

**Machi:**
Nishani ya afya na sayansi

**April**:
Nishani ya asili
Nishani ya sanaa na ujuzi

**Mei:**
Nishani ya ubora wa mwili (YLA)
Nishani ya mafundo

**Juni:**
Nishani II ya ujuzi wa kambi
Nishani I ya kuchaguliwa (MG)

**Julai:**
Nishani ya II ya kuchaguliwa
Nishani ya mafunzo

**Agosti**
Nishani ya mahubiri ya Biblia

**Septemba**
Nishani ya utendaji wa nje

**Oktoba**
Nishani ya mafunzo
Nishani ya huduma ya kwanza (MG)

**Novemba**

Ukamilishaji wa nishani
Ambazo hazikukamilika

**Desemba**

Ukamilishaji wa nishani ambazo
hazikukamilika

## RATIBA KWA MWAKA YA KUBORESHA TUZO YA FEDHA YA SUBCOM.

**Januari:**

- Ratiba ya mkutano wa vijana juu
Ya mipango ya mazoezi ya viungo

- Kuupatia uongozi majukumu katika
sehemu IV- A kwa miezi sita (6) ya mwanzo

**Febuari:**

Kuanza kipindi cha mazoezi
kwa kulingana na hali ya hewa ndani/nje

Kupanga safari ya uvumbuzi wa sehemu
ya III na ratiba juu ya hali ya hewa ya kawaida

**Machi:**

Kuchagua miradi wa jamii kwa sehemu
IV – B na ratiba ya kawaida ya mwaka

- Kuendelea kwa mazoezi ya viungo kwa
ukamilifu

**April**

- Kuendelea kwa mazoezi
ya viungo kwa ukamilifu

**Mei**

- Kuendelea kwa mazoea ya viungo ya
Ukamilifu

**Juni**

Jaribio la kwanza juu ya mazoezi
Kurekebisha utamaduni sehemu ya V

**Julai**

Nishani ya utumikaji katika jamii chini ya
Sehemu ya IV – C
Kuupatia uongozi majukumu sehemu ya
IV – A kwa kundi lijalo

**Agosti**

Nishani ya ujuzi chini ya sehemu ya II

Kuendelea kwa mazoezi ya vioungo ya
ukamilifu

**Septemba**

Kuendelea kwa awamu za maozezi
Kwa viungo kwa ukamilifu

**Oktoba**

Kuendelea awamu kwa mazoezi
ya viungo kwa ukamilifu

**Novemba**

Kukamilisha usomaji wa sehemu ya V

**Desemba**

Jaribio la pili mazoezi
Ukamilishaji wa sehemu ya II, III na IV

Hakikisha unaambanisha shughuli hizi nani ya kipindi cha miezi iliyopendekezwa na kuzijaza kabla ya desemba.

**Zingatia:** Kwa sababu ya ubora wa mafunzo ya mazoezi unaohitajika. Tuzo hii haikupangwa kukamilishwa na watu wote wa chama cha mabalozi.

## RATIBA YA MWAKA YA KUBORESHA TUZO YA FEDHA YA SUBCOM

**Januari:**

Ratiba ya mkutano wa vijana juu
Ya mazoezi ya viungo

Kuupatia uongozi majukumu kulingana na
Sehenu IV – ½ kwa miezi sita ya mwanzo

**Februari:**

- Kuanza kwa kipindi cha mazoezi kwa
kulingana mabadiliko ya hali ya hewa ndani/nje

Kupanga safari uvumbuzi na ratiba juu ya hali
ya hewa ya kipindi hicho.

March:

Kuchagua mradi wa kuonyesha Imani yako
Sehemu IV-3 na ratiba ya mwaka
-kuendelea na mazoezi kwa ukamilifu

April:

Kuendelea na mazoezi kwa ukamilifu wa
viungo

Mei:

Kuendelea kwa mazoezi ya ukamilifu ya
Nishani I ya utumikiaji jamii
Iliyochaguliwa sehemu ya IV-A

June:

-Jaribio kwanza juu ya ukamilifu wa shughuli
-Uboreshaji wa utamaduni V

Julai:

Nishani ya utumikiaji katika jamii
Sehemu ya IV-C
Kuanza kwa mazoezi ya ukamilifu awamu
Ya pili.
Kuupatia uongozi majukumu sehemu ya
IV –A kwa kundi lijalo.

Agosti

Nishani ya ujuzi sehemu ya II
Kuendelea kwa mazoezi ya kujiimarisha

September

-Kuendelea kwa awamu ya mazoezi
ya kujiimarisha
- Nishani ya ujuzi uliochaguliwa Agosti

Oktoba

-Kuendelea kwa awamu ya mazoezi ya
kujiimarisha

Novemba

-Kukamilisha shughuli ya sehemu ya V

Desemba

-Jaribio juu ya shughuli za kujiimarisha
-Kukamilisha sehemu ya II,III,IV.

Hakikisha unaambatanisha shughuli hizi ndani ya kipindi cha miezi iliyopendekezwa na kuzijaza kabla ya Desemba.

**Zingatia:**
Wakati ratiba hii inaeleza juu ya tuzo ya dhahabu ndani ya mwaka mmoja, miwili au zaidi inawezekana ikawa halisi mno. Kwa kuzingatia kiwango, cha juu, cha mazoezi ya vioungo kinachohitajika ili kukamilisha matukio, ifahamike kuwa tuzo hii haikuandaliwa kwa ajili ya kila mtu. Pia sio kila mtu wa chama cha mabalozi anaweza kukamilisha tuzo hizi, ila kwa wachache tu.

# BALOZI
(AMBASSADOR CLUB)

JINA: ____________________________________________ UMRI _____________________
KANISA/SHULE __________________________ Shule/Chama (club) ____________________

| MAHITAJI YA JUMLA | REKODI YA MKUFUNZI TAREHE | SAHIHI |
|---|---|---|
| 1. Uwe na umri wa miaia 16. | ______________ | ________ |
| 2. Uwe mwanachama hai wa chama cha Balozi au moja ya matawi yake | ______________ | ________ |
| 3. Uwe mshiriki aliyebatizwa au SS anayefuata taratibu za chama | ______________ | ________ |

**KUKUA BINAFSI**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Kariri na kueleza maana ya:- | | |
| - Ahadi za sheria ya watafuta njia | ______________ | ________ |
| - Kusudi na moto wa AY | ______________ | ________ |
| 2. Fahamu na eleza makundi ya nishani | ______________ | ________ |
| 3. Soma vitabu vifuatavyo:- | | |
| - The happy Path “njia ya furaha” | ______________ | ________ |
| - Steps to christ (njia salama) | ______________ | ________ |
| - kurasa 100 za uongozi au maendeleo ya vijana wadogo | ______________ | ________ |

**BALOZI**

II. **UVUMBUZI WA KIROHO**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Soma Biblia kwa mwaka | ______________ | ________ |
| 2. Soma injili nne katika tafsiri ya kisasa tafsiri iliyotumika | ______________ | ________ |
| 3. Jadili katika makundi (vikundi) vipengele vitatu kati ya vifuatavyo: | ______________ | ________ |

- Luka 4:19-26
- Luka 11:9-13
- Luka 21:25 - 28
- Yohana 13:12 – 17
- Yohana 14:1-3
- Yohana 15:5-8

4. Kwa kushirikiana na kiongozi wako, chagua moja ya habari zifuatazo za maandiko:
   - Yohana 3 – Nikodemo
   - Yohana 4 – Mwanamke msamaria
   - Luka 10 – Msamaria mwema
   - Luka 15 – Mwana mpotevu ______________ ________
   - Luka 19 – Zakayo

   **Na uonyeshe ni jinsi gani Yesu hutuokoa. Tumia moja ya njia zifuatazo**:
   - Njia ya majadiliano na kiongozi wako.
   - Mjadala wa Hadhara katika mkutano wa vijana (AY)
   - Mpangilio wa matukio katika mabango (Tangazo)
   - Katika shairi halisi au wimbo.

5. Soma kuhusu maisha ya J.N Andrews au mhubiri wa kujitolea (layman) katika nchi yako. Jadili umuhimu wa utume nje ya mipaka yako na kwa nini kristo alitoa agizo (utume) la injili katika Math. 28:18-20.

6. Kariri vitabu vya Biblia na awe tayari kuinua (kupanga) katika mpangilio(mafungu) wake kwa ujumla.

AGANO LA KALE
- Vitabu vitano vya kwanza vya agano la kale.
- Vitabu vya kihistoria
- Ushairi
- Manabii wakubwa
- Manabii wadogo ________________ __________

AGANO JIPYA
- Injili
- Historia
- Barua
- Unabii _______________ _________

7. Somo na uwasilishe (au uonyeshe) upendo wa Mungu kama ulivyo onyeshwa (hakikishwa) katika maisha ya Yusufu, Yona, Esta na Ruth. _______________ _________

8. Kwa kushirikiana (kujadiliana) na kiongozi/mwalimu wako chagua moja kazi ya mada zifuatazo:
- Mfano wa Yesu (fumbo)
- Muujiza wa Yesu
- Hubiri la mlimani
- Hubiri la kuja mara ya pili ______________ __________

Na uonyeshe uelewe wako juu ya mafundisho ya Yesu kwa kutumia moja kati ya njia zifuatazo:
- Kubadilishana mawazo na kiongozi/mwalimu wako
- Shughuli ambayo itahusisha kikundi (au kundi lako)
- Mpangilio wa maandishi (maeneo yasiyopungua kurasa 2) _____________ _________

9. Fahamu/elewa angalau msingi 15 ya kanisa la waadventista wasabato _____________ _________

10 Kamilisha jaribo (a) misingi ya Biblia na (b) urithi wa kanisa kwa kufaulu kwa kiwango kisichopungua alama 75%. (miongozo ya rejea inapatikana katika tovuti kitengo cha vijana makao makuu ya waadventista wasabato.

(a) ______________ __________

(b) ______________ __________

11. Hitimu (kamilisha) tuzo ya heshima ya cheti cha Biblia kwa kukariri fungu moja kwa kila vipengele vifuatavyo:-

**Insha kuu ya Biblia**
Zaburi 119:11 1 Wafalme 18:28, Wakolosai 3:16 Nyingine ____________ __________

**Wokovu**
Yohana 1:1-3,14 Mithali 28:13 Yohana 3:17 Nyingine _____________ __________

**Mafundisho makuu misingi (imani)**
Isaya 1:18 Mhubiri 12:13-14 Marko1:27-28 Nyingine ______________ __________

Maombi
Isaya 1:18 Zaburi 51:3 Ebrania 11:6 Nyingine ______________ __________

Mahusiano
Efeso 1:8-10 Mithali 19:19 1 Timotheo 4:12 Nyingine ___________ ___________

Tabia
Zaburi 34:3,4 Mithali 22:29 Gal. 6:7 Nyingine ____________ ___________

Ahadi na sifa
Zaburi 56; 35:7 Zaburi 91 Yakobo 1: 7 Nyingine ___________ ___________

III. **KUWAOKOA WENGINE**

1. Shiriki katika mjadala kuhusu kushuhudia vijana wengine na ufanye zoezi (weka katika zoezi) njia au maelekezo katika hali halisi _____________ ______.
2. Tumia angalau jumla ya masaa mawili katika kazi (mradi) zifuatazo
   - Kuleta angalau marafiki wawili kuhudhuria mikutano inayoendeshwa na kanisa _____________ __________

   - Saidia na shiriki katika huduma za kijamii za kanisa
   - Dhulu (tembelea) kwa kutoa (kuendesha) vipindi viwili Katika sehemu zifuatazo :- makazi wa watu wazima (wazee) Kwa maneno mengine kituo cha kutunza wazee, hospitali, Kituo cha yatima

   _____________ __________

3. Kwa msaada wa rafiki, tumia angalau siku moja (au masaa 8) katika kazi (mradi) kwa kanisa, shule au jamii.

IV. KUJIFANYA MARAFIKI

1. Taja sifa 10 muhimu za kuwa rafiki mwema. Jadili hali (mazingira) 4 tofauti unazoweza kutumia kanuni ya dhahabu (golden rule)
2. Shiriki mjadala (majadiliano) katika vipindi/kipindi redioni au katika luninga kuhusu shinikizo la rika (au ushawishi) na umuhimu wake au kazi yake katika kufanya maamuzi.
3. Kamilisha moja ya nishani zifuatazo:
   - Mwaonekano/usafi/unadhifu na tabia ya kikristo
   - Maisha ya familia. ____________ _________

4. Kwa wasomaji wa peke yako au majadilinao katika kundi, tambua mtazamo wako katika mada 4 kati ya zifuatazo:
   - Urafiki
   - Nguvu ya kujitolea (uhiari)
   - Kanuni au mawazo binafsi
   - Mahusiano kwa wazazi, familia na wengine
   - Shinikizo rika
   - Uchaguzi wa kazi
   - Upendo wa kazi
   - Upendo (mapenzi) na Ngono.
   - Kanuni za tabia njema. ____________ _________

V. **AFYA NA UKAKAMAVU/UKAMILIFU WA MWILI**

1. Elezea kanuni (au sheria) za afya kwa mwanafunzi wa shule ya msingi. _________ _________
2. Kamilisha moja ya kazi zifuatazo:
   - Andaa na ushiriki matukio au tukio la afya kama vile matembezi, mbio za masafa marefu, mwaliko wa kuendesha baiskeli au matukio kama haya ya kijamii.

- Soma kurasa 102-125 katika kitabu cha afya na kiasi mwandishi E.G White na ufaulu zoezi lililooneshwa ndani yake. ____________ _________
- Hitimu kozi lishe au fundisha afya ya kimwili (kama kozi kikundi/kundi)

3. Jadili kanuni za afya kimwili. Onyesha muhitsari wa programu yako ya mazoezi kisha weka sahihi mkataba wa programu ya mazoezi ya kila siku. __________ _________
4. Shiriki katika moja ya yafuatayo:-
   - Matembezi ya km 15 ya hiking
   - Kuendesha farasi kwa mwendo wa km 15
   - Safari kwa siku moja ndani ya mashua (boti) __________ _________
   - Endesha baiskeli umbali wa km. 80
   - Ongelea umbali wa km 1

5. Kamilisha moja ya shughuli zifuatazo, kisha andaa maelezo na uonyeshe ukubali kwa kutia sahihi kuhusu kuachana na maisha ya unywaji pombe.
   - Shiriki katika mjadala juu ya madhara ya pombe mwili. _________ _________
   - Tazama mkanda wa redio au luninga kuhusu mada ya pombe na madawa kulevya kisha jadili
   - Shiriki semina (warsha) inayohusu kuzuia uvutaji wa sigara, au tazama filamu 2 juu ya afya au tayarisha Bango juu ya uvutaji wa sigara na madawa ya kulevya au shiriki maonyesho ya afya.

6. Kariri na elezea 1 Koritho 9:24-27 ____________ _________
7. Hitimu nishani ya kuogelea hatua pili au nishani yoyote ya afya ya mwili ambayo ulikuwa haujaikamilisha hapo awali.

VI. **UONGOZI**

1. Chora na ujaze chati ya mfumo wa kanisa letu kwa kuzingatia divisheni yako. ________ ______
2. Fuatilia au jifunze kazi za mashemasi ndani ya course ya miezi miwili kasha toa taarifa ya kazi zao kama vile.
   - Ushiriki wao au jinsi wanavyoshirikishwa katika mahitaji ya washiriki na utunzaji wa mali za kanisa
   - Pasaka, ubatizo na matoleo.

3. Hudhuria angalau mara moja baraza la kanisa kisha toa taarifa kwa kikundi au kundi lako.
4. Kwa kushirikiana na viongozi wako andaa au panga huduma au shughuli za kijamii angalau mara moja kwa mwaka. __________ ________
5. Hitimu kozi zifuatazo
   - Kwata na Gwaride
   - Uongozi wa vijana wadogo
   - Uwakili ___________ _________

6. Saidia chama cha watafuta njia kuandaa na kukamilisha (kazi) mradi wakutoa huduma kwa jamii kama vile tukio au matukio kwa watoto wa mitaani au utunzaji wa mazingira (au uboreshaji) kwa jamii. __________ _________
7. Saidia chama cha watafuta njia kuandaa au kukamilisha shughuli maalumu kama vile siku ya wageni (inaweza kuwa shuleni, kanisani au chuoni) mapokezi maalumu, safari fupi (yaweza kuwa kupanda mlima) au kukambika kwa usiku moja. ___________ _________
8. Onyesha ujuzi (ustadi) wako wa uongozi na ukuaji kwa kutumia vigezo vifuatavyo:-
   - Andaa na uongoze mahubiri 3 katika kundi lako.
   - Fundisha angalau kozi 2 kwa watafuta njia au nishani 2 kwa vijana wadogo (wavumbuzi)

- Andaa na simamia kambi mwisho wa wiki (siku za mapumziko) kwa chama cha watafuta njia au vijana wadogo (wavumbuzi) ___________ _________

**VII. VIUMBE VYA ASILI**

1. Kukamilisha nishani moja kati ya makundi yaliyoorodheshwa hapa chini.
   (a) Jamii ya chura, ndege, mifugo(wanyama), jamii ya mijusi, miti, vichaka.
   (b) Nyota, calti, hali ya hewa , maua, njia iliyosababishwa na msongamano au kuandamana kwa wanyama. ____________ __________
   (c) Viumbe hai (utegemezi/ecology au jinsi vinavyotegemeana na mazingira) utunzaji wa mazingira.
   (d) Paka, mbwa, mamalia, mbegu, ufugaji ndege, ufugaji wa mamalia wadogo.
2. Tambua makundi haya ya nyota Alpha centaurus na Orion. Kisha fahamu umuhimu wa Orion kiroho kama ilivyoelezwa katika kitabu cha early writings ukurasa 41. _________ _________
3. Hitimu ushujaa au shujaa wa jangwa ___________ _________
4. Tambau angalau njia 6 zilizosababishwa na wanyama kisha weka alama angalau katika tatu kati ya 6. __________ ________
5. Tayarisha na ufafanei angalau shughuli (programu) 5 katika viumbe vya asili ambazo zitakuwa bora kufanyika Jumamosi (sabato) mchana.
6. Rejea histori ya gharika, soma au jifunze angalau aina tatu tofauti za maozea ya mimea au wanayama, kisha elezea uhalisi na uhusianao wake katika uasi wa sheria ya Mungu.
7. Tofautisha katika picha, mkusanyiko au kiumbe halisi moja kati ya makundi yafuatayo:-
   - Aina 25 za matawi ya miti – Aina 20 za miamba na madini –Aina 25 za maua ya kondeni --Aina 25 za vipepeo na wadudu wa wakao mwangani –Aina 25 za konokono. ________ ______

**VIII. MAISHA YA UKAMBIKAJI**

1. Fahamu jinsi ya kutengeneza kamba na jinsi ya kutumia.
   - Fahamu jinsi ya kutengeneza mafundo, kazi zake na tengeneza au chora mafundo 15 katika ubao.
2. Fahamu sheria au kanuni 10 za kufuata katika (hiking) kupanda mlima na namna gani au utafanya nini unapopotea.
3. Jifunze jinsi kutengeneza alama za kutembea, na uonyeshe ujuzi wako kwa kutambua na kufuata alama katika umbali wa km.2
4. Hitimu nishani yoyote ambayo ulikuwa hujahitimu (how to make trails) itakayo kuwa kigezo cha kutunukiwa nishani au pini ya kuogelea (au mimea na wanyama) ubunifu au michezo.
5. Tengeza aina tatu ya malazi katika jangwa na ujue jinsi ya kuyatumia, tumia moja kwa kukambuka mwishoni mwa juma.
6. Faulu mtihani/jaribio la kiwango cha daraja la juu kuhusu huduma ya kwanza (Advance First Aid).
7. Kamilisha nishani ya maelekezo (eleza) (orienteering).
8. Uwe na uwezo wa kuwasha mto kipindi cha mvua na ujue utapata wapi kuni na kuzifanya ziendelee kuwaka. Ujue kutengeneza na kukaza mpini wa shoka.
9. Tembeeni (Hike) kilometa 25 nyikani angalau kwa siku nzima mkiwa kundi la watu wanne(4) na kiongozi wenu akiwepo. Chukua kumbukumbu muhimu kwa ajili yakutathimini/kujadili kuhusu mipango, ushiriki na uchunguzi wa viumbe. (mimea na wanyama)
10. Buni miradi 5 ya ukambikaji kutumia kamba katika eneo la ukambikaji na club moja iwe na mlango wa kuingilia. Buni mikakati 5 ya ukambikaji na moja ya kufikia wakambikaji.
11. Andaa chakula cha safari cha siku 3 kwa watu 4, angalau aina tatu viwe vikavu na dehydrated 3.
12. Uweze kuwa na uwezo wa kutumia na kupokea ujumbe kwa kutumia semaphone au morse code ukitumia tochi au lugha ya ishara au ukiwa na msingi wa kutumia mateur radio.
13. Ujue kutafuta pande/pembe nane (8) za dunia bila kutmia kifaa (mashine) yaani (compass)

**IX. MFUMO WA MAISHA YENYE MAFANIKIO. Kamilisha nishani 2 kwa kila kundi hapa chini ambalo ulikuwa hujapata nishani yake.**

1. Andika sifa 2 katika kila kipengelea hapa chini ambacho hakijagusiwa/hakikutajwa
   (a) Jumba la sanaa au sanaa na ufundi.
      1. ……………………………
      2. …………………………..
   (b) Sayansi na afya au huduma kwa jamii.
      1. ………………………………
      2. ………………………………..
   (c) Utendaji kazi (huduma) njema. Elimu ya nje ya ujuzi wa viwanda vidogovidogo au sido

2. Kwa maelekezo ya kiongozi wako, jadili na kundi lako, moja ya mada zifuatazo:-
   - Mkristo na maisha ya kikristo
   - Burudani na vichekesho
   - Utunzaji wa Sabato

3. Kwa kujadiliana/au kwa kujisomea, tathimini mtazamo wako kwa mada mbili (2) kati ya zifuatazo
   - Utoaji mimba
   - Ukimwi (AIDS)
   - Utumiaji wa nguvu-mabavu (violence)
   - Madawa ya kulevya

X**. MAFUNZO YA UONGOZI (STAFF LEDAERSHIP TRAINING)**

**1.** Hudhuria semina ya masaa 2 ya watafuta njia (pathfinder) na wavumbuzi (adventurer) mafunzo ya uongozi.

**XI. MAFUNZO YA UTUMISHI.UONGOZI**

1. Hudumu kuwa mshauri mkuu au msaidizi wa mshauri aidha katika klabu ya watafuta njia (pathfinder) au wavumbuzi (adventurer) angalau mwaka mmoja.
2. Wasaidie kwa maelezo kundi la watoto katika moja ya madarasa ya AY angalau kwa miezi mitano (5) au mpaka watakapohitimu na kuvishwa tuzo.
3. Kamilisha nishani ya masimulizi ya kikristo.

**KUENDELEZA UWEZO MPYA**

1. Hudhuria angalau masaa ya mafunzo yaliyodhaminiwa na Idara ya vijana field kwa mada zifuatazo:-
   - Mshauri mkuu wa kitengo
   - Elimu ya mawasilinao
   - Ukambikaji na uongozi
   - Ubuni kwa vitu asili
   - Unjilisti katika vijana wadogo (Junior)

**REJEA NA MTIHANI**
**(REVIEW AND EXAMINATIION)**

Nathabitisha kwamba ______________________________________________________amekamilisha kozi/mafunzo Maalumu kwa darasa. mahali _________________tarehe _______/_______/__________
Mkurugenzi wa vijana Field ___________________________________________________
Kimetolewa na ______________________________________________________________
Mahali __________________________________________ tarehe _______/______/_______

# S E H E M U 5

***Shughuli za chama (matendo ya chama)***

## FALSAFA YA ELIMU YA JAMII

Vijana wadogo wa kristo wana kila sababu ya kuwa na furaha katika dunia hii. Yesu alisema "Nilikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele (Yohana 10:10) maisha yanakuwa marefu kwa kuwa na afya njema, lakini usumbufu kukinaiwa maisha sio uzima. Hata hivyo hatupaswi kuwa na furaha eti kwa sababu maisha ni mazuri ya kawaida au marefu. Hakuna mojawapo na hivyo kuwa na anastahili mtu (wakristo au wapagani) lakini Yakobo anasema tunaweza kufurahi, na tufurahi katika kila jambo. Paulo alilielewa vizuri hili ndio maana aliweza kuimba akiwa gerezani akipigwa. Haya yote yaweza kuwa utangulizi kwa sehemu hii, lakini kuna sababu. Jamii ya leo inaweka msisitizo hasa katika swala zima la kuburudisha starehe kwa gharama iwayo yote.

Maburudishao huleta furaha, soma/rejea vyombo vya mawasiliano Jeff Jacoby, mshairi wa gazeti, aliwahi kulifanyia kazi wazo hili na kuandika mtazamo wa maburudisho na furaha. "sio tu kwamba maigizo (maburudisho) ya televisheni (T.V) vinaonyesha vimetiwa (maelezo/vielelezo vya uongo ndani yake) lakini kwa kutiwa chumvi huko haviwezi kutusaidia.

Televisheni (TV) pamoja na semina (movies) ni vitu vinavyo bomoa/haribu maadili kwa sababu maandalizi/uzalishaji wake unapingana na malezi bora. Vinapingana na Judeo –Christian tradition. Jeff Jacob kuonyesha msingi ya migongano na anahitimisha anaendelea uchunguzi ufuatao:

Mgongano wa mwisho: TV na sinema vimejaa vimejawa na maburudisho na mzaha. Kwa wayahudi dini ya kuigiza" wanapofanywa vipofu kwa miali ya TV, wakati misisimko yao inapokoma, nini kinabaki?

Watu wachache sana …. Wanataka kuzikwa. "Hapa ndipo… anastarehe kedekede" Starehe sio maana halisi ya maisha yaliyo. Tena inapingana mno na vile jamii/tamaduni inavyotaka.

Tofauti kati ya starehe na furaha ni sawa na tofauti kati ya ngono na kupenda. Moja ni rahisi lakini hukoma nyingine inachukua muda lakini inadumu daima. Moja ni kwa ajili ya tamaa na jingine ni kwa kujenga (kuburudisha moyo)

Sio vigumu kuona tofuati ya starehe ya mkristo na maburudisho yaonekanayo kuwa ya kawaida kwa kusudi la kujifurahisha, yakionekane kufanyiwa kazi kupita kiasi, yakipinguza nguvu zetu/uwezo wetu kimwili, kiakili na kiroho. Shetani yuko pale pale kuhakikisha vijana hawatulii kwa kubuni mivuto mipya na yakukonga nyayo zao ambayo huharibu uthamani wa vijana na kuwatenga na Mungu. Kufurahia ambako kunaweza kusababisha kuweka pembeni misingi ya Imani, ni matatizo tele na kujiangamiza.

Ingawa furaha inayofulika yaweza kututoa nje kama mbio za panya, teknolojia ya kisasa inayotegemewa na viumbe (inayoongoza maisha ya mwanadamu) kamwe visifanye kuwa wakristo wasio na wajibu dini, haiwezi kuwa ndio kigezo cha maisha yetu ya kila siku.

Baada ya kusema hayo yote, tuna mtazamo/mwelekeo sahihi “Ni upendeleo wa pekee wa wajibu wa Wakristo kutafuta burudisho la roho zao na kuwa safina imara miili yao na uwezo wa akili kwa utukufu wa Mungu MYP 364.

**KUMBUKA**.
Ni wajibu kuwa na kushiriki furaha.

**MASHINDANO**
Kuna aina mbali mbali ya mashindano, mashindano mabaya katika hayo ni mashindano hatari yanayohamasisha kamali, upotevu na udanganyifu. Ile (michezo) ambayo husisimua / huchangamsha akili, kujifunza na sehemu zake kutoka ndani ya Biblia kwa mazingira (asili) na maarifa kwa ujumla hayo yanakubalika zaidi yale pia yakubalianayo na kufanya mazoezi na kutojitenga na jamii, pamoja na kujifunza yanayofaa.

**MICHEZO**.
Wakati tunaweza kuchagua wenyewe kuwa mashabiki kwa kiwango kikubwa au kidogo, michezo ambayo tunaihamasisha kama taasisi sharti iende sambamba na vitendo katika kushangilia, makofi upendapo, Adrenalin anamiminika kwa wingi na inakosa pa kwenda isipokuwa kupiga kelele na kuita majina. Kwa manufaa ya biashara (wafanyabiashara) humaliza wanapowapamba kwa kuwaita wachezaji “nyota” (mastaa), baadaye hufikia ulimwengu wa mashabiki, hiyo haimwesaidii chochote kijana mkristo (mshiriki) hujihusisha. Wakati michezo imetangazwa, na mashindano mengine ya aina hiyo yakiendelea katika vilabu mbali mbali yasiruhusiwe nafasi ya kushiriki mchezo kwa lengo la kujifurahisha isifanywe. Baada ya Ellen white kuwa amefurahi kwa kumwangalia mjukuu wake akicheza mpira wa kikapu (basketball) jioni moja. Mtu mmoja alimuuliza (kuhusu hilo). Jibu lake lilikuwa hivi:-

“Silaumu/sishutumu mazoezi rahisi ya kucheza mpira, lakini hata hili kwa urahisi wake, linaweza kufanywa zaidi” AH 499.

Kiasi ndio ufunguo wa shughuli za kijamii na binafsi (furaha) vijana wakati mwingine wamechanganyikiwa na semi za Ellen White kwamba anapinga kwendesha baiskeli na michezo ya tennis. Mara washawishika kupinga maandishi yake hasa hivi vinatumika isivyopasa kwa baadhi ya wakubwa wanaoelewa. Sababu inayopeleka semi hizi kutumika sana hata leo na zinapaswa zieleweke. Shughuli zote hizi zimeandikwa kwa sababu maalum.

Katika suala la kuendesha baiskeli, pesa nyingi zimetumika kugharamikia mashindano ya baiskeli kwa miezi kadhaa kipato cha familia kimetengwa kwa kusudi la kushiriki mbio za baiskeli na watu wa mjini mahitaji ya msingi ya familia chakula, nguo katika juhudi zao yamewekwa pembeni kwa ujumla mambo yanapelekwa ilimradi (yanakatisha tama) tu. Hali hiyo hiyo inaonekana kwa tennis. Wanafunzi walikuwa wakitoroka shule ili wakacheze “michezo zaidi” mashindano na jumuia yalipangwa na kuendeleza roho ya chuki ambayo ilihitajika kukukomeshwa.

Hizi ndizo sababu zinazofuta aina za shughuli / kazi sio baiskeli tu au tennis. Tozer ameliweka wazi zaidi “chochote kinitengacho/anitengaye na Biblia ni adui yangu hata kama kitakuwa hakidhuru” Best of Tozer PP 108.

**MUZIKI.**
Muziki ni moja ya masomo ambayo yanaonekana kutokuwa na watu ambao hawajui lolote sana kila mmoja anaonekana kuwa na mguso halisi ule unaokubalika na muziki usiokubalika . Karibu kila mmoja anaonekana kujisikia kwamba vyovyote aina ya muziki iwe, wanapendelea aina nzuri zaidi, kwamba kuna ya siku nyingi au zamani sana, kuna mawazo kwamba, kufundisha muziki huo-ukweli ni kawaida kote katika pambano kuu. Baada ya note zote za muziki kuwa tu – note za muziki hazisemi wala kufanya chochote / lolote kwa zenyewe ilivyo.

Huo ukiwa ndio ukweli, pia ni rahisi kudanganyika ni sawa na kusema herufi (alphabeti) kwenye kinanda – hazifanyi chochote / lolote kwa zenyewe, LAKINI, kwa namna alphabeti (herufi) zinvyotumika / zitumikavyo kutunga kuunda maneno hayo ni jambo jingine. Pia kwa namna noten (sofa) zitumikavyo kuunda muziki pia nalo ni jambo jingine. Shetani atatumia maneno kuandika kile kitakachowatenga watu na Mungu wao, ndivyo pia atatumia muziki kwa kusudi hili hilo kama tu kulivyo na namna nyingi za uandishi na uongeaji ndivyo pia kwa muziki. Kuna namna mbalimbali, vichekesho, kuigiza, utunzi bora, ugandamizaji, kushusha hadhi, kutukuza, ushairi, dhihaka yote haya na zaidi hutumika katika lugha ya maandishi, matamshi na kimuziki. Hata hivyo watunzi wengi hurejea juhudi zao kama lugha. Wanaweza kutumia muziki wa ujuzi kukumbukwa kila mistari wa wimbo wanaoutaka, kila pingamizi ya mtu wanayotaka kisaokolojia na mafunzo ya umbo kikemia huthibitisha hili. Muziki hubadilika katika pambano kuu umetumika sehemu mbili katika mapambano ya roho zetu, kila mmoja analo hili, lakini mkristo habanwi nafsi yake na muziki wa aina moja bila kumtukana Mungu.

Imekuwa kawaida kwa kile kinachotolewa kwake kama ibada tangu mwanzo wa historia ya mwanadamu ikithibitishwa katika kisa cha huzuni cha Kaini na Habili. Mungu ni chanzo na mwandishi wa aina zote za muziki, anapenda aina mbalimbali kama anavyoonyesha katika uumbaji wake. Lakini yeye siyo mwandishi na mwanzilishi wa kuharibika kwa usikivu ambapo ni miiba na magugu yaliyowekwa ndani ya shamba.

Katika vikosi na mikutano yetu tutataka kuelekeza muziki ambao utatuvuta kwa Mungu bila kupeleka ujumbe unaochanganya kwa kiwango kikubwa muziki unaopatikana kwetu utatutaka kuchagua upi uliokaribu, katikati ya barabara ambao utatoa pambano na mgawanyiko kati yetu ndani ya roho ya kila kijana.

**UANAFUNZI**
Kuna maneno mengi ambayo yanaonekana kuwa maneno yaongozayo katika idara ya vijana. Ufundishaji na uanafunzi pengine ni vitu viwili muhimu, Idara ya vijana haijihusishi kutenda zaidi na kila vijana wanachotenda na kufurahia. Ufundishaji huonyesha matendo ya viongozi, haijalishi wanafahamu aina ama umuhimu wa uongozi: Uanafunzi ni mwitikio wa uelekezaji, inagharimu kupitia njia nyembamba ya kristo sisi kama viongozi tuliteuliwa kwa ajili yao.

Idara ya vijana siyo tu burudani, michezo na mitindo ya maisha ingawa burudani na michezo huhusishwa mara kwa mara. Kama kijana hatatafuta mlango mwembamba na njia nyembamba anayoizungumzia kristo, mipango ya mikutano yetu, programu zetu, muda wetu, nguvu na mali hazina maana tena. Inafanana na ngoma tu kelele nyingi, msisimko, lakini hakuna utaratibu wa sauti, umoja na muziki udumuo.

**IBADA/MAOMBI.**
Kipengele kikuu cha maisha ya kila mkristo kinaonekana katika nadharia na matendo ya ibada kwa Mungu na muda wa maombi binafsi, kwa sababu uhusiano wa mwanadamu kwa Mungu ni wa muhimu kwa vipengele hivyo vya maisha, itakuwa ni vigumu kumtaja mtu kuwa ni mkristo asiyejihusisha yeye mwenyewe katika mpango na mpangilio unaokubalika.

**IBADA.**
Ibada inaonekana kama kitu Fulani ninachonufaika nacho au kitu kisichokuwa na thamani yoyote. Tunasahau kuwa ibada tunatoa kwa Mungu, siyo kwa ajili yetu wenyewe. Ni maelezo ya shukrani zetu kwa vile uhusiano wetu na Mungu uimarishwavyo kwetu. Hivyo hufanywa vizuri katika mtindo uangalifu wa kile kitokacho moyoni na kile Mungu atakacho kwetu.

Tuna maelezo wazi katika Biblia katika sura za mwanzo za kitabu cha mwanzo mahala ambapo Mungu huonyesha ibada anayoitegemea. Habili alimwabudu Mungu kama alivyoamini, Kaini alichagua kumwabudu Mungu kama hiari yake kwa kutumia njia hiyo alijisikia kuwa na faida. Leo hakuna tofauti kwa ibada nyingi, Ibada natolewa kama tunavyochagua na bila kufikiri Mungu anataka nini kwetu hivyo ibada yetu inaweza kuwa potofu kama ile ya Kaini. Kuna baadhi ya vipengele vya ibada na kila kimoja kifanywe kwa makini na kwa maombi ya kujipeleleza (kujichunguza) ndani ya mioyo yetu ili tuweze kutoa ibada ya kweli, muziki unaotumika, maombi yanayotolewa, maneno yanayosemwa, matendo yanayotendwa yote yamtukuze Mungu. Haitakiwi kuchanganywa utamaduni, wakati na mapenzi binafsi au udhuru wowote.

**MAOMBI BINAFSI.**
Huu ni muda awa kukidhi mahitaji kwa juhudi binafsi katika muda huu hutia nguvu zaidi hutosheleza mtima wa roho. Mpango wa muda si wa muhimu sana kama mtume asemavyo; ninakufa kila siku hiyo ndiyo rejea pekee tuliyonayo juu ya wakati. Maombi yanahitaji kuchukua nafasi kila siku, zaidi ya hayo yanaweza kudumu kwa dakika kadhaa au masaa kutegemeana na juhudi, maombi yaambatane na kusoma somo fupi siku moja na kuweka haja (shauku) siku nyingine. Wanaweza kuanza asubuhi na mapema kwa kuzungumza na Mungu kabla hatujatoka kwenye vitanda wanaweza kulindwa mchana kama tulalavyo katika tumaini lake. Muziki wowote, maneno yaliyosemwa, matendo yoyote, yote yanelekezwa katika hilo.

Mimi karibu na Mungu katika mambo yote yanayonihusu kama vile:- utamaduni wangu, mambo ninayothamini zaidi, Mungu ananilinda ananipa nguvu na moyo wa ujasiri wa kukabili kila changamoto za siku kwa ajili yake. Mtindo wa maisha ambapo mtu anakuwa na haraka muda hauwezi kuwa na sababu za kuziba ibada binafsi ya mtu. Ni Martin Luther ndiye alielewa hili vizuri; ananukuliwa akisema "Nina mambo mengi ya kufanya leo; ni lazima nitumie muda wa ziada katika sala ili kujiandaa kwa mambo hayo.

**UKAMBIKAJI NA VIUMBE VYA ASILI.**
Ukambikaji pamoja na shughuli zingine zinazofanyika nje ni muhimu katika kupanga makundi mbali mbali ya vijana kuna miongozo iko wazi inayofanywa na wote wanaoamua kuingia katika ulimwengu huu wa ugunduzi, hilo lapaswa kuwa ni sehemu ya mafundisho na tabia yetu. Mchungaji Robert Tyson mmoja wa viongozi wetu wa mwanzo wa vijana ambaye pia alikuwa mshauri wa kuaminika alifundisha kwamba alikuwa kiongozi wa vijana, ni lazima kwanza tuwe watu waliotayari kufanya shughuli za nje kama ukambikaji. Alimaanisha kwamba, hatuhitajiki tu kuwa na ujuzi katika shughuli za ukambikaji, na mambo ya hatari yanayoweza kutokea wakati wa shughuli za ukambikaji. Ni lazima pia tujenge tabia

ya kutambua na kuheshimu vitu (viumbe) vya asili. Hivyo visehemu vya viumbe hai vya porini vinabaki kwa ajili ya furaha yetu na ulinzi wetu, watu wanaoshughulika na shughuli za ukambikaji wa dhati, sio watu aina ya mcheza filamu aitwae "Rambo" ambae hutumia silaha kama kisu kuwadhuru viumbe pori na kuondoa uwepo wao katika mazingira.

Watu wanaoshughulika na shughuli za ukambikaji pamoja na mafunzo mengine yanayofanyika nje wanasifa zifuatazo;- Ni lazima wawe sehemu ya mazingira wanajifunza kutembea kwa uangalifu pasipo kuharibu uoto wa asili wakati wanapotembea. Wanatii kanuni zizilizopo kama vile; usiue kitu chochote isipokuwa muda, usiache kitu chochote isipokuwa alama za nyayo za miguu, usichukue kitu chochote mbali na kupiga picha. Hujenga mazoea na kila kiumbe hai kwa aina zake na kuheshimu kwa jinsi kilivyo kiwakilishi cha kazi ya Mungu ya uumbaji. Hiki pia ni kitu cha muhimu sana ambacho ni kugumu kueleweka kinachotoa picha ya pambano kuu, kila kimoja kikiwa na somo linalosubiri kueleweka/ kusomwa kadri mtu anvyozama zaidi katika uchunguzi na uelewe viumbe vya asili havipaswi kuogopa na kukimbia kwa woga wakati tunapovikaribia, vinapaswa vigundue uwepo wetu bila kueleweka au kugundua tuondokapo.

Moja ya malengo ya kila klabu (chama) katika shughuli zake zinaofanyika nje ka vile ukambikaji ni kuacha eneo lilitumika kwa shughuli zote za ukambikaji katika hali nzuri, safi na kiasili zaidi kuliko walivyoikuta wakati wanakambika.

Yeye pekee anayetembea kwa asili kazi za baba yake hujifunza kutokana na vitu vya asili kwa undani zaidi kwa kupokea huduma ya juu zaidi toka kwa vitu hivi vya asili. Ed 119 - 120

Tovuti iitwayo www.thru.hiker.com inatoa maelezo mengi kuhusu vitu vinavyotumia mionzi ya jua ambavyo mtu anaweza kutengeneza na kuokoa fedha kuanzia maturubai (tents) hadi mabegi madogo ya kubebea vitu mgongoni (mifukoni ya kubebea vitu na majiko rahisi ya mafuta) kila kitu mgunduzi anahitaji viwe ni vya bei rahisi/gharama nafuu na mwanga wa jua.

## VIFAA VYA HUDUMA YA KWANZA AJILI YA UKAMBIKAJI

Hii ni orodha ya vifaa vya huduma ya kwanza kwenye mfuko mdogo wa begi.

- Pea moja ya mikasi
- Bandeji ishirini (20) zenye vipimo vya 1"x3"
- Gundi ya solotep mbili zenye vipimo nchi vya 9"x18"
- Mzunguko mmoja (1) wa rip –top tape
- Kipande kimoja cha sabuni

**Ndani ya boksi la plastic**

- Chupa mdogo coricidiri
- Chupa ndogo ya asprin au advil
- Chupa ndogo ya Thlenol
- Chupa ndogo ya vidonge vya magnesium
- Chupa ndogo ya mafuta ya karafuu
- Nail Clippers moja (1)
- Mbanio mmoja (1)
- Pima joto moja
- Pima joto ya "hypotheimic moja
- Steristrips tatu (3)
- Wembe mmoja wenye makali upende mmoja

- Pini sita (6) salama
- Chupa ndogo ya oksaidi ya zinki (zno)
- Pakiti kumi (10) za diatrol
- Packet mast moja (1) kwa ajili ya CPr.
- Midsize airway moja (1)
- Stethoscope moja (1)

**Nanda ni begi la plastic.**

- Fomu sita za kutolea taarifa ya ajali
- Fomu sita za kutolea taarifa za dharura
- Chati sita za kutolea ishara muhimu
- Kijitabu kimoja (1) cha huduma ya kwanza
- Mouteineering medicine booklet moja (1)
- Tampons nne (4) Geuza pods 8 zenye vipimo cha 4” x 4”
- Mizunguko miwili ya kling
- Pakti mbili za spenco second skin
- Chupa moja ya beta dine (pharmidine) 40z.
- Kipande kimoja cha waya
- Oce bandage mbili
- Surgipads mbili
- Bendeji moja yenye umbo la statili
- Pea moja (1) ya miwani ya jua
- Hoseclamps 8
- Skni prep 8

## VIFAA VYA HUDUMA YA KWANZA KWA AJILI YA UKAMBIKAJI

Orodha hii hapo ni vifaa vya huduma ya kwanza.

**SANDUKU LA HUDUMA YA KWANZA**
**Ndani ya boksi la plastic**

- Pea mbili za mkasi
- Mibano miwili
- Ncul clippers mbili
- Pini salama 36
- Pima joto 3
- Pima joto za hypothermic tatu (3)
- Mafuta ya karafuu chupa mbili

**Ndani ya Bahasha**

- Vijitabu viwili vya huduma ya kwanza
- Fomu mbili za kutoa taarifa ya ajali
- Fomu kumi za kutolea taarifa ya dharura
- Fomu kumi za sahihi muhimu
- Telfa pads mia moja zenye vipimo vya 3” x 4
- Geuzoa pasa 100 zenue vipimo vya 4” x 4” (inchi  4 x inch 4)

- Gudni ya solotep mbili ya mizunguko 20
- Gundi (solotep) mbili ya mizunguko ishirini (20)
- Pea nne za miwani ya jua.
- Mzunguko mmoja mkubwa wa malestrin
- Asprini miatano (500) au Advil mia tano (500)
- Tylenol mia tano (500)
- Vidonge vya dawa baridi100
- Vidonge vya magnesium 100
- Chupa tatu (3) za betadine (pharmidine) 40z.
- Chupa mbili za benzoin
- Bendaji 4 za mstatili
- Vipimo vitatu (3) vya nyaya.
- Penseli 36
- Chupa ndogo tupu kumi na mbili (12)
- Pakiti hamsini (50) za 2siatrol
- Surgipase dressings 4 (nne)
- Hoseclemes 15 (kumi na tano)
- Mzunguko mmoja 1 wa rip stope tape.
- Steristrips tano
- Sperco second skin sita
- Mizunguko minane (8) yak ling
- Vipande kumi (10) vya sabuni
- Boksi mbili za nyembe zenye makali upande mmoja
- Boksi moja la tampors
- Skin preps hamsini

**Fomu ya uwanachama**

**KLABU YA MABALOZI**

Jina ____________________________________________________________

Anwani __________________________________________________________

_________________________________________________________________

Tareha ya kuzaliwa __________ Jinsia Me Mke Umebatizwa SDA Ndiyo Hapana

Namba ya simu_____________________________________________________

Ningependa kujiunga na balozi katika kanisa la waadvenstista wasaboto. Nitahudhuria na kushiriki kwa sharti katika kikundi (klabu) na nina kubali kuishi kulingna na miongozo na sheria zilizowekwa na (kikundi) (klabu) katika kuenenda na mfumo wa maisha inayofundishwa na kanisa la waadventista wa Sabato.

Nimekuwa ni mshiriki wa vyama vya vijana wa kanisa la waadvenista wasabato ndiyo hapana

Kama ndio kipi? ______ Wagunduzi_______ watafuta njia_____ vyama vya viongozi wakuu

_________vyama vya vijana (shirikisho)______ vyana vya vijana vinavyohusika nadharura

____________vyama vinavyohusika na kuokoa __________ jamii ya vijana wakiadventista

Vingine______________________________________________________________

Sahihi ___________________________________ Tarehe______________________________

**KWATA NA SHERIA ZAKE**

**UTANGULIZI**

**Kutembea** au gwaride, kama tunavyojua leo ni swala la wanajeshi,askari na vita. Matumizi ya kibiblia ya neno gwaride mara nyingi ni katika muktadha wa vita.

Pale bahari ya Shamu, " Hata Farao alipokaribia, wana wa Israeli wakainua macho yao, na tazama, Wamisri wanakuja [marching] nyuma yao." Kutoka 14:10

Wakati Daudi alipopigana dhidi ya Wafilisti, Mungu alimwambia awashambulie "hapo utakapoisikia sauti [marching] ya kwenda katika vilele vya miforsadi, uwapige jeshi la Wafilisti." 2Samweli 5:24

Wakati Joshua alipotembea kuzunguka Yeriko, "nanyi mtauzunguka mji huu watu wote wa vita [marching], mkiuzunguka mji mara moja. Fanya hivi siku sita." Yoshua 6:3,4,7,14,15. Neno lililo tumika hapa kwa kiingereza (NLT) NI MARCHING.

Neno la asili la Kiebrania lililotumika kwa aya hizi zote linaelekeza kutembea kama gwaride kwenye kundi tayari kwa vita, lakini si lazima kwa hatua. Wayunani waligundua njia mpya ya kupigana na kuona kuwa kundi la wanaume wakiwa pamoja pamoja na ngao zao na silaha lilikuwa jeshi imara kuliko kupigana mtu mmoja. Ili kukamilisha lengo lao hili na ili kuepuka kugongana miguu wao kwa wao, walianza kutembea kwa hatua, ndio msingi wa gwaride kama tujuavyo leo.

Njia ya kisasa ya gwaride ilitengenezwa kwa mara ya kwanza na Gustavus II Adolphus (1594-1632) mfalme wa Sweden na kuchukuliwa na mataifa mengine ya Kiulaya. Jean Martinet, afisa wa jeshi la Kifaransa miaka ya 1600 alianzisha urefu wa kutembea haraka kwa kuzunguka kwa nchi 30 ambako ndiko msingi uliochukuliwa na kutumiwa na Watafutanjia kwa Sm 50 (nchi 20)

Usisahau kuwa mbinguni tutainga kwa gwaride kubwa na Yesu Kristo akiwa kamanda wetu mkuu na tutapokelewa na Baba Mungu. Hapa inaonekana kwa macho ya kibinadamu sisi ndio tutakuwa wageni rasmi pamoja na Yesu kamanda wetu mkuu.

Sura hii ya nishani za vijana wa Kiadventista imekusudiwa kukusaidia kufundisha au kujifunza kwata na matembezi yake ili kukuwezesha kupata nishani ya kwata na mazoezi yake. Hili litakuwezesha kutumia muongozi wa kwata vizuri kama ulivyotolewa toka makao makuu ya kanisa ulimwenguni Idara ya huduma za vijana.

1. **Makusudi 7 ya kwata:-**
    (a) Amri = inasaidia kudumisha umoja wa taasisi
    (b) Motisha= inafundisha nidhamu na umoja wa kundi
    (c) Furaha= shughuli za furaha, inakuza matumizi ya ubunifu
    (d) Mahusiano= inamsaidia mtu kujifunza kupokea amri na kuzifuata

(e) Uongozi= inamsaidia mtu kutoa amri na kujenga kujiamini
(f) Kujitawala= kutoa usikivu kwa kiongozi

**2. FASILI YA HAYA YAFUATAYO:-**

(A) **UUMBAJI** = Uumbaji ni mpangilio wa vitu kwenye kwata ya watafutanjia kwatika hali inayoelezeka.

(B) **Mstari**. Mstari ni uumbaji ambao kwao vitu vinakaa upande kwa upande au sambamba ya kila kimoja. Katika chama mstari unawaweka watafutanjia katika kila kikosi sambamba na kingine kimoja kikiwa nyuma ya kingine.

(C) **Safu** (rank). Safu ni mstari ambao ni mmoja tu kwa kina.

(D) **Nafasi**(interval). Nafasi ni umbali kati ya watu waliosimama karibu na mwingine

(E) **Mlolongo**(column). Mlolongo unatengenezwa wakati watu wamesimama moja nyuma ya mwingine

(F) **sanjari** (file). Safu ni mlolongo mmoja.

(G) **Umbali**. Umbali ni nafasi kati ya watu katika mlolongo (mbele kwenda nyuma)

(H) **Jaza nafasi ( cover).** Amri ya kujaza nafasi inatumika kujirekebisha mwenyewe kati ya mtu wa mbele yako wakati huo ukidumisha umbali unaotakiwa.

(I) **Msafara**. Msafara ni upande wa kushoto au kulia wa uumbaji wo wote kutoka kwa mwonekano wa mtu ye yote katika muundo huo.

(J) **Kiimbo mpandoshuko**. Kiimbo mpandoshuko ni ile hali ya mwendo unaowiana ambao mwondoko unafanywa, au idadi ya hatua au hesabu kwa dakika ambao kwayo mwendo unafanywa.

3. **Maelezo ya matendo katika makundi haya yafuatayo:**-

**a. Legeza, legeza mwili, gwaride pumzika**

- Gwaride, pumzika ni kitendo kinachotolewa mara kwa mara kwa mkazo kwa amri hizi tatu. Inatolewa tu watu wakiwa wamekaza mwili. Yaani wakiwa wasikivu kupokea amri. Ni amri ya kuandaa mtu kwa kupokea amri, mkao wa gwaride kuwa kwenye mapumziko unapaswa kufikiriwa wakati watu wamelegeza mwili, au legeza, au pumzika. Watafutanjia wanafanya gwaride la kupumzika kwa kusogeza mguu wa kushoto pembeni nje( miguu inakuwa imeachana karibu inchi 8) na kuweka mikono yao nyuma, wakati mkono wa kulia uko juu ya dolegumba la kushoto vikiwa vimefungwa pamoja. Kichwa na macho bado vinatakiwa view vimetazama mbele, kwa sababu gwaride la kupumzika kwa urahisi tu ni kutokuwa katika hali ya usikivu mkubwa. Wakati wa mkao huu ndipo maelezo yanatolewa pamoja na kutoa maombi.
- Mguu pande . Hapa huruhusiwi kukaa. Kufanya amri hii, kufanya gwaride lipumzike kama hapo juu; pamoja na hayo macho daima yanatakiwa yawe kwa kamanda. Vyama vingine vinaweza kuruhusu mikono kupumzika lakini hili haliruhusiwi kulingana na muongozi wa kwata. Kupumzika kunaweza kuruhusiwa katika mkao wa hali hii. Mwili legeza na kupumzika kunaweza kuruhusiwa katika mkao huu sasa.

- Legeza mwili. Hapa kuna kupumzika zaidi. Mguu wa kulia utakuwa umekitwa bado ardhini katika sehemu yake. Watafutanjia sasa wanaruhusiwa kusogeasogea(isipokuwa mguu wa kulia umetulia) lakini unatakiwa uwe umetulia na kusimama. Kupumzika kunaweza kutolewa kwa mkao huu.
- Amri ya ziada ya kupumzika na wakati wa kuburudika zaidi. Mguu wa kulia lazima uwe bado umebakia kusimama ardhini, na watafutanjia bado wamesimama; sasa wanaruhusiwa kuzungumza katika mkao huu. Amri ya kulegeza yaweza kutolewa katika mkao huu sasa.

**b. Chapa mguu, chapa mguu kwa haraka, kutembea mbele.**

- Kuchapa mguu ni amri inayotolewa ikiwa na maana ya kuchapa mguu ukiwa umesimama hapo hapo. Wakati kikundi kikiwa kwenye kuchapa mguu, wanatakiwa wawe wanarekebisha nafasi zao toka mmoja hadi mwingine, kwa umbali na nafasi. Kuwa sahihi, amri hii inatolewa tu wakati wanatembea au wameanza kupunguza mwendo sio wakati wanatembea kwa haraka au wanasimama. Pamoja na hayo vikundi vingi vinapenda kutumia amri hii wakati watu wamesimama kwa faida ya kupata usikivu kwa makusudi ya kupokea maelekezo. Amri ya kutembea lazima itolewe kwa usahihi wakati miguu inapiga chini siyo ikiwa hewani. Wakati amri inatolewa chukua hatua moja baada ya nyingine ili kutembea kuwe kunafanywa kwa usahihi, usiweke mguu wako mbali sana na mwingine na tembea kwa nafasi. Kila mguu uinuliwe sawa kama inchi 2 juu wakati wa kutembea mbele. Ruhusu mikono yako itembee kwa asili bila kuilazimasha au kuikaza kama imefungiwa kamba na irekebishe kwa kadri inavyotakiwa.
- Kutembea mbele ni kutembea kwa mlolongo sasa wa hesabu ya 120 au hatua 120 kwa dakika kwa kadri ya hatua ya nchi 24. Mikono yako itembee vizuri nchi 9 ikiwa imenyoka mbele na nchi 6 kwenda nyuma kwenye makwapa yako. Mikono isijikunje kwenye kiwiko na vidole vyako view vimekunjwa kama wakati wa kuwa umesimama wima ukiwa sawa. Kunja gumi ya kike. Kichwa na macho vikiwa mbele. Watafutanjia wachanga wanawea kuona vigumu wakati wa kuanza, lakini kwa msaada wa waalimu wanapaswa kuweza na kuwa wepesi sana.
- Mwendo wa haraka sana sasa ni hesabu ya 180 au hatua 180 kwa dakika. Umbali wa hatua daima ni inchi 24. Amri lazima itolewe mwendo wa haraka mbele tembea. Ya kwanza ni mbele tembea, ya pili lazima ianze na mwendo wa haraka mbele tembea. Amri inatolewa wakati wamesimama au wanachapa mguu au wakiwa wanatembea mwendo wa kawaida. Kama itatolewa ukiwa umesimama lazima uanze kwa kasi mguu ukiwa umeinuliwa juu. Endelea kutembea kwa mwendo wa hatua 180 kwa dakika mpaka amri nyingine itakapotolewa. Amri nyingine itakayotolewa kwenye mwendo huu ni amri ya kusimama, macho kulia au kushoto, au nusu kulia au nusu kushoto.

**c. Kupiga saluti kwa mkono na kutoa mkono.**

- Kupiga saluti kwa mkono kunatumika mara nyingi kwa bendera, na inatolewa tu wakati mguu uko sawa. Ili kutoa amri hii, inua mkono wako wa kulia na uukunje kwenye kiwiko. Vidole vyako vya mkono wa kulia viguse kope za macho, au kama umevaa miwani kwenye mzunguko wa miwani yako, au kama umevaa kofia au kofia ya ngalawa, kwenye ukingo wa kofia( kama umevaa vyote yaani kofia na miwani gusa kwenye ukingo wa kofia. Sehemu ya juu ya mkono lazima iwe sambamba na ardhi, na mkono wa mbele, kiuno na mkono wa kulia/vidole lazima vitengeneze mstari ulionyooka(hakuna kukunja kiungo cho chote). Kiwingko kiende nyuma ili kisiwe mbele ya mwili, lakini kisiwe mbali sana nyuma ya mwili. Amri itolewe kwa usahihi. "toa saluti". Hapatakiwi kuwa na kelele zo zote wakati wa kutoa saluti hii, wala wakati wa kushusha saluti mikono isipige kwenye nguo au mwili na kutoa sauti yo yote.
- Saluti ya mkono ni sawa kabisa na ile ya kutoa kwa mkubwa wako, ila hii haina amri unaifanya unapokutana na mkubwa wako na kupindisha kichwa kuelekea mtu huyo na kumtaja wakati unapomtolea saluti. Akiitikia ndipo unashusha saluti hiyo, bila amri yo yote vile vile. Amri unajipa mwenyewe kimya kimya moyoni.

d. **Mwendo wa kugeuka upande wa kulia au kushoto na mlolongo wa kulia au kushoto**.


- Wakati watafutanjia wanatembea wanaweza wakapinga au kugueka upande wa kulia au kushoto. Nafasi kati ya maandalizi ya amri na amri kutimizwa ni hatua moja. Hii ina maana amri itatolewa kwa kuvuta pumzi. Kwa kutembea mbele kila mtafutanjia anachukua hatua moja zaidi na kugeuka upande alioamriwa. Wakati wa kufanya hivyo, mara tu baada ya hapo anatakiwa aibie kidogo ili kuhakikisha mstari umenyoka tena. Hii inafanywa kwa kuangalia kulia kwani mistari inanyoshwa kuelekea kulia.
- Mlolongo wa kulia au kushoto, kutembea mbele kulia au kushoto unaweza kutolewa wakati watafutanjia wamesimama wima au wakiwa wanatembea. Wakiwa wamesimama, amri inatolewa kuwa watafutanjia watatembea mbele kwa mlolongo wa kulia au kushoto na mtafutanjia anayekuwa mbele ya mlolongo karibu sana na amri kutolewa anageuka kwa nyuzi 90 kuelekea upande ulioamriwa na kutoa nje kwa mguu wake wa kushoto kwa upande mpya akichukua hatua moja ya inchi 24 na kuendelea mbele kwa nusu hatua (yaani inchi 12) mpaka milolongo mingine(mistari) imemfuata kwa usahihi. Viongozi wengine kwenye mistari mingine wanageuka kwa nyuzi 45 kwa upande ulioelekezwa na kutoa nje mguu wa kushoto kwa upande mpya wakichukua hatua moja yenye inchi 24 na kuendelea kwa kutengeneza kamduara (arc). Wanapamkaribia Yule kiongozi wa mstari wa kwanza wanachukua nusu hatua. Viongozi wote wnapokutana, wanatoka nje hatua moja yenye inchi 24 bila amri yo yote. Wengine wote wanawafuatisha viongozi hawa waliombele ya kila mstari kwa hatu zile zile. Kiongozi hapa lazima atolee amri kwenye mguu sahihi bila kuwakosesha wanachama. Amri iwe wazi kama ni kulia au kushoto, kupinda au kugeuka.

4. Kwa uhakika timiza miondoko hii ya msingi.
    a. Attention (mguu sawa). Kusimama mguu sawa kunahitaji miguu yako kuwa pamoja na vidole vyako vikiwa kwenye pembe ya nyuzi 45. Mikono yako ikiwa imebanwa kweny pindo la suruali yako au gauni au sketi kama vile umeshilia gombo lililoviringishwa na dole gumba likiwa juu ya kidole karibi nalo(index finger). Macho yako daima yatakuwa yametazama mbele. Huruhusiwi kuongea labda kama umeambiwa kufanya hivyo. Karibu amri zote za kusimama vile vile na amri za kutembea mbele zinatolewa katika mkao huu wa mguu sawa.
    b. Gwaride kupumzika. Kama wakati wa mguu sawa, macho yako daima yatakuwa yakitazama mbele. Wakati wa kuambiwa pumzika mguu wako wa kushoto unasogea mbali na mguu wa kulia na unakunjwa kidogo nyuma. Mikono yako sasa inakuwa nyuma mkono wa kushoto ukiwa nyuma ya mkono wa kulia. Grwaride pumzika ,amri hii inatolewa tu wakati mkiwa mguu sawa. Tumezoea kusema ‘heizi’ mwili legeza.
    c. Mguu pande. (stand at Ease). Mguu pande ni sawa kabisa na kupumzika isipokuwa tu kwa mambo mawili. La kwanza kila jicho na kichwa vinapaswa kumtazama daima anayetoa amri. La pili, mikono inakuwa imelegea zaidi kuliko la kwanza, japokuwa mikono inakuwa pale pale kama wakati wa kupumzisha gwaride.
    d. Mguu pande ni karibu sawa na kupumzisha gwaride. Japo unatakiwa uwe kimya na kuweka mguu wako wa kulia vizuri kwa kupokea amri wakati wo wote, japo hapa unaweza kusogea kama itakavyohitajika. Mikono yako inaruhusiwa kuwa chini zaidi kuliko inavyotakiwa kwa kupumzisha gwaride. Amri hii inaweza kutolewa ukiwa mguu sawa, kupumzisha gwaride(legeza mwili) au mguu pande.
    e. Usawa wa kulia.


**BAADHI YA MAUMBO YA KWENYE GWARIDE**

Kuitisha watafutanjia (FALL IN). kwanza wanasimama mstari mmoja toka mrefu hadi mfupi. Kisha wanahesabu namba toka kulia namba fupi fupi yaani 1 na 2; wanatengeneza mistari miwili kisha wanageuka kulia waliohesabu moja na waliohesabu mbili wanageuka kushoto. Aliye kulia anatulia kisha wanaanza kujipanga mistari mitatu.


UUMBAJI WA MISTARI.



MSTARI. KILA RANGI HAPA INAWAKILISHA KIKOSI CHA WATAFURANJIA



HAPA IDADI YA WATAFUTANJIA NI SAWA




HAPA IDADI SIYO SAWA


MSTARI UNAWEZA UKAWA WAKATI WATAFURANJIA WAMESIMAMA UPANDE KWA UPANDE




SAFU.




NAFASI




MSTARI MMOJA (SINGLE FILE)




UMBALI






RIGHT FLANK(upande wa kulia)



LEFT FLANK (upande wa kushoto)

Ukunjaji wa bendera za chama na za Taifa



**SHEREHE ZA UFUNGUZI**

Hii ni programu ambayo inafanywa kila siku Watafutanjia wanapokutana kwa ratiba zao za kawaida

Utaratibu wake.

1. Kuwaitisha watafutanjia (fall in)
2. Kupandisha bendera
3. Kuimba wimbo wa Watafutanjia
4. Kukariri ahadi na sheria
5. Taarifa ya mahudhurio ya vikosi mbalimbali vya Watafutanjia
6. Maombi na kutawanyika

**Programu inafuata kama ifuatavyo**

1. Kutambulisha wanachama wapya
2. Ibada- ikianza kwa nyimbo
3. Somo la maandiko Matakatifu
4. Kufundisha nishani mbalimbali
5. Kufundisha madarasa mbalimbali
6. Michezo mbalimbali
7. Mazoezi ya gwaride na kutembea

**Sherehe za kufunga**

1. Kuitisha Watafutanjia (fall in)
2. Kushusha bendera
3. Kuimba wimbo wa Watafutanjia
4. Matangazo ya mkurugenzi
5. Ombi la mwisho
6. Kutawanyika

Baada ya maelezo haya mafupi, hakikisha unakuwepo kwenye mazoezi ya mtaalamu wa gwaride ili kupata hali halisi ya kuwaongoza watafutanjia pamoja na Master Guides wote.

Hakikisha una mwongozo wa gwaride unaokubalika. Kwa sasa tunatumia Mwongozo wa Amerika ya Kaskazini ambao unapelekana na gwaride la Tanzania. Maelezo mengine yanatofautiana kidogo sana kulingana na hali yetu ya Kitanzania.

**SHERIA ZA MWANAKAMBI**

Niutaratibu kuwa kila palipo na wawili au watatu Mungu yupo na Mungu wetu ni wa Utaratibu. Hivyo basi katika mikutano ya kambi za vijana, vijana wanapo kusanyika lazima pawepo na utaratibu. Zifuatazo ni sheria za kambi.

1. Kila mwanakambi anapaswa kuwa kimya baada ya filimbi ya ujulisho wa watu wote kulala ikiwa imepulizwa.

2. Kila mwanakambi atatii ishara zote za filimbi na kuwepo mahali panapotakiwa awepo kwamujibu wa ishara ya filimbi

3. Kila mwanakambi anapaswa kuwaheshimu viongozi wote wa kambi.

4. Ugomvi wa aina yoyote hauruhusiwi kabisa kati ya mtu na mtu, wala matusi ya aina yoyote.

5. Kila mwanakambi anapaswa kushiriki vipindi vyote kambini kwa mujibu wa ratiba ya kambi.

6. Kila mwanakambi hataruhusiwa kutoka nje ya eneo la kambi bila kupata ruhusa kutoka kwa mkuu wa kambi.

7. Mahusiano yoyote ya kutatanisha na mtu wa jinsia tofauti hayaruhusiwi kabisa katika maisha ya mwanakambi awapo kambini.
   (Hii nipamoja na mwenendo wa maisha yako ya kila siku hata baada ya kambi)

8. Kila mwakambi anapaswa kuwa msafi mwili na nguo zake, hii ni pamoja na mazingira yake yote ya kambi.

9. Hairuhusiwi kujisaidia vichakani kwa haja zozote iwe kubwa au ndogo, kila watu katika chama chao wanapaswa kuchimba choo zao wenyewe kwa mujibu wa jinsia zao kama walivyo kuja.

10. Hairuhusiwi kuoga vichakani kwa mwanakambi yeyote, kila watu wajenge mabafu yao ya kuogea kumujibu wa jinsia zao.

Sheria hizi kumi zitakusaidia uishi kwa amani katika mikutano yetu ya makambi ya vijana. Ili kukua kiroho na kuwa mwanakambi aliyefanikiwa vifaa vifuatavyo unapaswa kuwa navyo:

i. Biblia
ii. Lesoni kama umebatizwa au kitabu cha Mafundisho kama hujabatizwa
iii. Kitabu cha wimbo
iv. Daftari na Kalamu

# *STADI ZA UKAMBIKAJI*

**Utangulizi**

Nawakaribisha katika mkusanyiko wa nishani nyingi ndani ya kozi moja. Tunapoongelea juu ya stadi za ukambikaji ni vigumu sana kuziweka pembeni nishani za ufungaji wa Mafundo, Mioto na upishi wa kambi, Ufundi kambi na Ukambikaji katika hatua zake zote. Maelezo yafuatayo yanategemewa kukidhi mahitaji ya nishani zote tajwa, aidha mengi katika nishani hizi ni ya kufanya kwa vitendo na si nadharia. Lengo kubwa ni kukuongezea wewe kiongozi maarifa zaidi katika yale maeneo ambayo kwayo ulikuwa hujabobea. Karibuni na Bwana azidi kuwabariki.

**A: KUCHAGUA ENEO LA KUFANYIA KAMBI**

Yapo mambo sita ya kuangalia unapochagua eneo la kufanyia kambi

- **I.** **Maji** – maji yawe mengi, safi na salama kwa afya ya wanakambi.
- **II.** **Kuni** – Kuni ziwe zimekauka, ziwe zinapatikana kirahisi kama ni za kununua ziwe za bei iliyo ndani ya uwezo wa wanakambi.

***Angalizo***

Hampo nyumbani, mpo porini au eneo ambalo mmebeba pesa Kiasi tu cha kuwawezesha kuishi kwa siku hizo.

Je maeneo hayo idara ya misitu inaruhusu uokotaji wa kuni kwa matumizi hayo?

- **III.** **Maeneo ya mifereji** – Je eneo hilo litakauka uepesi iwapo mvua itanyesha kwa ghafla na nyingi? Je eneo liko eneo la juu ambalo maji hayatuami?
- **IV.** Mandhari – Je eneo lipo kwenye madhari nzuri ambako vijana wanaweza kuwa na michezo?
- **V.** La faraja – Je eneo linafikiwa kirahisi linatia faraja? Je mbu hawapo, wadudu wabaya hawapo? Chungu chungu, siafu, nyuki nk.
- **VI.** Lina usalama – Li mbali na mawe au miti iliyooza inayoweza kuleta ajali? Ni eneo salama unapowasha moto?

***Yapo maelekezo sita unapotafakari hayo mahitaji ya mwanzo ya kuchagua eneo la kambi:-***

**UPEPO**

Je upepo utafanya kitu gani kwa kambi?

Upepo unaweza kufumua mahema na kuyabomoa au kuyapeperusha, unaweza kuangusha miti na kuleta maafa au uharibifu wa Vifaa. Upepo unaweza kubeba moto na ukateketeza hema.

**MAJI**

Eneo la ukambikaji linapaswa kuwa eneo ambalo lina maji ya kutosha. Kama upo maeneo ambayo maji hayana usalama na safi tumia dawa ya kusafishia maji yachemshwe vyema na kuyachuja vyema. Unapofanyia kambi karibu na ziwa, mto, au bahari, chemichemi ya maji siku zote ongeza vitu vya kuvutia. Maji yawepo mengi ya kutosha na salama. Kama usalama wake ni mdogo zitafutwe njia za kuyafanya yawe safi.

Maji salama na safi si salama kuja nayo toka nyumbani wakati wa ukambikaji, hivyo siku zote si rahisi kupata maji salama, maji safi yanaweza kupatikana tu kwenye chemichemi au ya mvua yaliyovunwa na kuletwa.

Hatari ya maji yasiyo salama siku zote ni kubwa kwa wanakambi yanayotokana na mimea mbalimbali. Na madhara yake yanaweza kuonekana baada ya siku saba baada ya kuyanywa. Matokeo ya kunywa maji yasiyo salama unaweza kuharisha, kutapika kusikia mwili unalegea, kupungukiwa uzito, kukosa hamu ya chakula na dalili zingine.

Mara nyingi maji yatokayo kwenye chemichemi ndiyo salama Kiasi fulani kutegemea zaidi na mazingira.

Namna ya kutatua tatizo hili ni kufuata taratibu za kusafisha maji:-
Yachote, yaache yatulie, chemsha, chuja weka kwenye chombo kilicho safi.
Kama yana rangi ya udongo tumia dawa kusafishia iodine.

**WANYAMA NA WADUDU WA PORINI**

Inzi, mchwa, mbu, ng'e, siafu, nyuki, mbung'o, viroboto nk. Hawa wanaweza kuvuruga kuishi kwako, wanaweza kuepukwa. Hii ndiyo sababu tunashauriwa kukambika eneo la juu, wadudu wengi wa aina hii wanapenda sehemu za mabonde karibu na maji. Unapofanya utafiti wa eneo hilo unapaswa kuyaangalia. Pia kuna vitu vingine vya porini vinavyoweza kuleta usumbufu, panya, tumbili, waweza kuleta usumbufu kwenye chakula na mahema. Tambua wanyama wanaopatikana katika maeneo au waliyo karibu. Angalia pia maua, ndege, pia miti inayozunguka eneo hilo.

**KUNI**

Unapokambika eneo ambalo kuni zinapatikana kwa wingi, kambi litakuwa na urahisi na la kupendeza kwa wanakambi. Eneo kama haliruhusiwi kukusanya kuni, majiko ya mafuta yaandaliwe au ya mkaa au andaa kuni zenu iwapo mna gari la kuzisafirishia badala ya kupata usumbufu.

**HALI YA HEWA**

Hali ya hewa ina maana gani kwa kambi?
Je ni wakati wa kiangazi Kiasi ambacho hutapata kivuli? Je ni wakati wa mvua, mahali ambapo mahema yataloa na chini ya hema kuwa na unyenyekevu unaweza kuleta madhara? Je kutakuwa na mafuriko yatakayo wasumbua? Eneo la ukambikaji liwe pale paliposawazika pasiwe mtelemko sana.
Usikambike mahali pa udongo wa mfinyazi mvua ikinyesha itawapa taabu, matope.

**SEHEMU ZA TAKATAKA NA MAJI MACHAFU**

Sehemu za kutupa takataka.
Hili mara nyingi si tatizo kama eneo lililochaguliwa ni la kutosha.
Hakikisha eneo mnaloweka kambi lina eneo la kutosha kuweka vyoo na mashimo ya uchafu kwa kila hema. Takataka zote, Karatasi, chupa za plastiki, mabaki ya vyakula vyote hivi vinapaswa kutupwa kwenye shimo, visizagae ovyo vitaleta madhara kwenye kambi.

Usafi wa kambi ni kitu muhimu sana kwa watu wanaoishi pamoja, uzingatiwe na kupewa kipaumbele.
Vyombo vya kupikia visafishwe na maji ya kuoshea vyombo na kuoga yapate mifereji ya kuyatiririsha na kuyapeleka kwenye shimo yasizagae ovyo.
Usitupe vitu ovyo ovyo. Angalia inzi watakufuata bila kujali wewe ni nani uko wapi.
Nguo chafu zifuliwe mara kwa mara usizirundike kwenye kona fulani ya hema.
Oga kila siku ni jambo la muhimu usafi wa kila jambo ni wa kuzingatia.


**DHARURA**
Siku zote vipo vitu vinavyojitokeza bila kujua ni muda gani, wapi na wakati gani havina taarifa. Kwa njia moja namna ya kuzuia dharura hizi ni kuhakikisha kuwa kila aliye kwenye eneo la kambi anachukua tahadhali zote za usalama. Ajue kanuni zote za usalama. Aina yoyote ya dalili ishughulikiwe mapema isije ikaleta madhara makubwa.

Kila kikundi kiwe na kisanduku cha huduma ya kwanza na kila kikundi kama kuna uwezekano kiwe na mtu mwenye elimu ya huduma ya kwanza.
Kabla ya kuondoka kila kanisa lihakikishe kuwa bima ya tahadhari kwa ajili mtu na mzigo inalipwa kwa mhazini wa Konferensi na majina yafike Ofisini wiki moja kabla ya kuanza safari.

**B: USAFI WA KAMBI**
**UCHAFU WA BINADAMU (MAVI)**
Kuacha kinyesi nje tu bila kukifukia ni dalili ya kuyanyanyasa mazingira kwa wale watakaofuata.
Siku zote unapokambika kitu cha kwanza ni kuchimba shimo la kuweka uchafu huo. Chimba shimo la kadiri ya kimo cha sm 90 na upana wa sm 30, unapojisaidia tumia mchanga kufukia, usitumie maji tumia mchanga unasaidia kufunika na kutokaribisha inzi kubeba uchafu na kuupeleka kwenye vyakula, shimo likijaa chimba lingine. Karatasi zote za kutawazia zifukiwe usiziache juu.
Mashimo ya choo yanapaswa kuwa mita 30 toka kwenye hema yenu, pia ziwe kinzani na upepo zisiwe mahali upepo unapoelekea kuepuka harufu. Pia zisiekelezwe mahali ambapo maji yapo.

Baadhi ya mifano ya vyoo vya kambi,

Choo cha nguzo – polelatrine Vyoo vya vichakani




Choo cha sanduku – kinaweza kuhamishika

**MASHIMO YA TAKATAKA**
Mashimo ya takataka na namna kambi itakavyokaa na mpangilio wake unahitajiwa kufanyika kabla ya kwenda hapo. Tunaweza kutumia mifuko kadhaa, kuepuka kuweka mashimo mengi kwenye uwanja, mifuko hii inapaswa iwe miepesi kubebeka kama uwezo wa kuyanunua haupo mashimo yachimbwe ya kina chenye sm 90 au mita moja na mashimo ya maji machafu ya bafuni na ya kuoshea vyombo, kila uchafu unaoingizwa au kutupwa umo ufukiwe na mchanga msiache wazi. Mahali popote uchafu unapokusanywa kunakuwa na wadudu wengi waharibufu wanaozaana.

**ENEO LIACHE LIKIWA SAFI**
Eneo tulilofanyia kambi linapaswa kuachwa likiwa safi, lisafishwe na kila aina ya uchafu uondolewe.

**MIMEA**
Tabaka la juu la mimea lililo kando ya ziwa au mito ni rahisi sana kuharibiwa na wakambikaji.
Mara tabaka hili la juu linapokuwa limeharibiwa wakati mwingine hayaoti tena, wanaopendezwa kuona vitu hivyo kando ya ziwa au mito wataona makovu ya uvunjifu wa vitu hivyo.
Kama kuna uwezekano, ukambikaji wetu usiwe mahali ambapo vitu hivi vinaweza kuharibiwa.
Tusiweke hema zetu mahali ambapo tutauwa mimea ambayo haitaota tena.
Usichume maua yaache ili wengine wayafurahie, kama unataka kuyakusanya yapige picha au yachore.
Utaona kuwa nishani nyingi za viumbe asilia zinaruhusu jambo hili, usitengeneze meza au viti kwa kutumia vitu vya asili. Epuka sana kukata na kuuwa baadhi ya mimea wakati wa ukambikaji. Epuka kuchimba mashimo mengi nunua mahema ambayo hayapitishi maji.

**MAJI**
Kudumisha usafi wa maji yetu ya kunywa porini matumizi ya sabuni yatumiwe kwa uangalifu sana, kuna kemikali ambazo si salama zinapowekwa ndani ya maji. Vyombo vyako zoea kuviosha na maji yaliyo chemshwa sana badala ya sabuni.

Oga, fua nguo na vyombo vyako vya chakula mita 300 toka kwenye chanzo cha maji. Tumia ndoo na mabeseni ya kubebea maji kwa kuogea na kufulia.

**NJIA ZA MKATO**
Wakati mwingine tunataka kutumia njia fupi kufika tunapokwenda au mahali palipo eneo la kambi, omba ruhusa kupitia hizo njia. Heshimu vitu vyote unavyovipita usikate au kuchuma vitu.

**RANGI ZINAZONG’ARA**
Kufanya mambo yaonekane vyema kwa namna Fulani nunua vitu vya kambini na nguo zenye kufaa, zile zinazofanana na ardhi, kahawia, blue, kijani zinazotaka kufanana na vitu vya asili. Rangi nyekundu ya mng’ao, rangi ya chungwa na njano zina haribu mandhari wakati mwingine zinaweza kuleta mwonekano usiyo mzuri sana. Hata umbali wa mita 300 rangi ya hema iko wazi na inaingilia mambo ya faragha ya watu inaonekana kwa haraka.

Kufanya kambi wakati wa uwindaji hili linaweza kuwa tatizo. Jizuie kupaza sauti wakati upo kwenye rangi hizo za kung’ara.

**C. MAHEMA NA SHERIA ZAKE**
Mara nyingi mahema yanapangwa kulinganana ukubwa wake na matumizi yake, umbo lake na urahisi wa kuyasimika; yanavyozuia upepo na uzito wake nk. Kuchagua aina sahihi kwa ukambikaji kama ni la kivuli au la kulala, chagua kulingana na matumizi yake. Kanuni ya uchaguzi wa hema inatokana na matumizi yake.

- Mahema mapesi yanatumika kwa kuweka kivuli cha kuwekea baiskeli za kufanyia ziara au mitumbwi.
- Yapo mahema pia yaliyotengenezwa kulingana na majira na maeneo ya hali ya hewa, mahema ya wakati wa kiangazi, kipupwe na majira ya mvua.
- Iwapo mahema yenu ni ya shughuli za kuvuta kasia chagua yaliyo mepesi yaliyo rahisi kusimika na kubomoa.
- Kwa misingi ya ukambikaji ni vyema kutumia hema aina ya kajumba kadogo, hasa mahali ambapo magari yanaingia. Utapaswa kufikiria nafasi ambapo magari yanaingia, utapaswa kufikiria nafasi

Unapofikiria hema la watu kadhaa kulala ndani mara nyingi hema la urefu wa mraba wa futi 12 kwa kila mmoja. Hema la watu wanne siyo kubwa kuliko la watu wawilli. Jambo la msingi katika ununuzi wa mahema unataka la watu wangapi? La matumizi ya aina gani? Linakupa picha ya kununua bila shida.

Tambua pia kuwa leo watengenezaji wa mahema wanaleta kila aina ya mtindo kukidhi haja yao ya biashara  na mahitaji ya watu.


Baadhi ya aina za hema ni kama ifuatavyo:-

**HEMA LISILO HAMA KWA UPESI – (Fixed –cam tent)**

Haya huwa ni mahema makubwa na mazito kwa vile yana vifaa vingi vya kulifanya lisimame. Matumizi yake yana mipaka – kulisafirisha utapaswa kutumia usafiri maalumu kama gari, mtumbwi nk. mengi yametengenezwa kwa nyuzi za Naironi, poplin wakati mwingine machanganyiko.

**Aina za hema zinazohamishika kirahisi**

a) Aina ya mwamvuli - umbrella
b) Kajumba kadogo – cabin
c) Kama tanuru – baker
d) Hema la ukuta – wallten




Aina ya mwamvuli – umbrella Kajumba kadogo – Cabintent

**Aina ya mwamvuli**


Hili hema lina miteremko pande nne na paa la aina ya pyramid. Ni rahisi kusimika na lilio imara. Kadiri lilivyo na mkeka mzuri chini wa kuzuia maji ndivyo pia linavyojitokeza chini zaidi kwenye mlango, lina nyavu nzuri za kuzuia mbu wasiingie, na pia madirisha mazuri yanaweza kufungwa kwa ndani na madirisha pia yanayopitisha hewa, kuta zake zimejengwa zile ambazo haziwezi kupitisha maji, juu pia limetengenezwa kwa kitambaa ambacho maji yanateleza na kwenda zake.

**Aina ya kabanda kadogo (cabin ten)**

Hema la aina hii ndilo hema la pekee lenye nyumba bora. Lina kuta za wima ambazo zinafanya utumie kitanda kidogo cha kulalia tofauti ya hema la kajumba na kibanda, lile la kajumba kadogo ni kubwa, kwa ndani lina vyumba kiasi kwamba unaweza kujikuta kuwa una vyumba viwili kama ilivyo wakati mwingine kwa hema la aina ya mwamvuli. Mahema haya yanakuja na kitu kama beseni kwenye kitako chake. Hema hii linakuja na nguzo ya kulisimamisha. Yanasimama

yenyewe baada ya kuingiza vyuma hivyo na pia inaweza kutumia kamba inapohitajika. Kuta zake hazipitishi maji.

**Hema**




Baker tent Wall tent

Mahema aina ya Tanuru (Baker) haya ni ya matindo wa zamani linatoa hisia kamili ya ukambikaji kwa sababu upande mmoja wa ukuta unaweza kuacha wazi, ukuta wa mbele unaweza kuinuliwa kwa ulalo na kutengeneza kitu Fulani au kushushwa na kulifunga hema.

Hema hili limeendelea kuboreshwa kwa kutengenezwa kwa Nailon na kuwekewa nyavu kwa tahadhari ya mbu.

**HEMA YA KUTA KAMA ZA NYUMBA**

Hii ni hema aina ya kizamani, leo mahema kama haya yanatumiwa na askari wa kulinda wanyama pori na wawindaji. Haya mahema ni makubwa kuyasimika ni rahisi, watu watatu tu waweza kulisimika.


**HEMA NYEPESI YA MAJIRA MAKAVU**

Haya mahema sasa ndiyo yanayoonekana kwa wingi. Yenye ukubwa wa kuanzia mtu mmoja hadi sita.

**Aina zake – aina ya (tube**)


Hili ni jepesi sana, lina usalama wa aina Fulani mahema ya aina hii mengi yanafunguliwa sehemu moja, laweza kuninginizwa kati ya miti miwili. Hema hizi hazipendekezwi sana kwa ukambikaji. Hema za namna hii zinaitwa “Dome”

Picha aina ya bomba




**Bivouac – sack -** Hema aina ya gunia ya kambi ya muda

Hema hili mara nyingi ni kubwa sana na kichwani kwake lina nyavu, jamvi lake ni la Nailoni na halipitishi maji na linafuliwa kirahisi. Hema hili linafaa wakati wa mvua.




**HEMA LA FREMU**

Hili hema laweza kuchukuliwa kirahisi kwa kubeba mgongoni. Linafaa kwa aina yoyote ile ya ukambikaji, yanetengenezwa kwa nyuzi za Nailoni na mazuri mengi yametengenezwa kwa kuta mbili ni rahisi kusimika, firemu zake zinajitegemea lakini zinapaswa kusaidiwa wakati wa upepo.






**Hema yenye umbo aina ya kuba - (DOME)**

Mahema ya aina hii kwa sasa yanatengenezwa kwa wingi na kwa aina zake. Haya mahema yanaweza kusimikwa mahali popote ni rahisi sana kusimikwa.

Hema kama reli – lenye vipenyo vingi – (Tunnel tent)

Hema hili kwa sababu ya sura ya umbo lake lina nyumbua upepo na lina wiano wa nafasi ya uzito umbo lake linatoa kichwa cha ndani na nyumba mahema haya yanaingiza hewa vizuri.




Dome tent Tunnel tent

**Mountaineering**

Hema hizi zinahimili hali ya hewa ya vilele vya milimani, yametengenezwa kiasi kwamba yanaweza kuingia kwenye mfuko mdogo. Hayana chumba kikubwa lakini jambo la muhimu maisha yako yanaweza kutegemea uimara wa hema hili.

**Matumizi ya mahema**

Baada ya kununua hema jipya, kuwa na uhakika wa kujua mikunjo ya kuzuia maji. Simika hema lako, ligeuze juu na jaribu kutazama maeneo yote, weka rangi za kuzuia mpenyo wa maji, ziba pia sehemu za jamvi kwenye kona zote, mali nguzo zinapopitia liache likauke usiku mzima.

Unaposimika hema yako chagua eneo zuri ambalo halina vitu vya kulichana au kulitoboa. Angalia vyema mahali ambapo panaanza kutoboka angalia pia upepo unatokea wapi, unaoweza kung'oa miti, usielekeze mlango mahali upepo unapotoka, utaling'oa kirahisi.

Angalia vifaa vyote vya kusimikia hema, vipo? Mahema mengine hayawezi kusimama kitu kimoja kinapopungua.

Sehemu unayoona hema yako imeanza kuonyesha uharibifu Fulani ikarabati mara moja ili isiendelee usiweke vitu vya kemikali juu ya hema lako.

Kabla hujalisimika hema lako andaa eneo.

**KUTAYARISHA ENEO LA KUWEKA HEMA LA KULALIA**

- Kila unaposimika hema hakikisha kuwa eneo unalosimika umelisawazisha vyema. Pasiwepo mashimo, visiki, vitu vyenye ncha kali n.k. shimo litajaza maji mvua inaponyesha kisiki kitatoboa hema
- Ni vyema hema lako lielekee kusini mashariki ili kukupatia mwanga fulani wa jua asubuhi. Sio vyema kulima kulizunguka hema maana kunaaribu mazingira na kuiacha ardhi ikiwa na makovu
- Chagua eneo ambalo halina mizizi ya miti, mawe visiki na vitu visivyofanya ardhi kuwe kweny usawazifu, mzuri – Toa vitu vyote vinavyoweza kuhatarisha hema kulitoboa au kulichana.
- Nyasi au mchanga ni vitu viziru vinavyopaswa kuwa chini ya hema yako mahali unapotaka kulala jaribu kulala hapo mahali kabla ya kusimika hema rasmi. Litandike lala usikie unavyokuwa.
- Unapochagua eneo la kambi – Angalia ardhi ile utakayosimika hema zako. Ardhi inahitaji iwe ile itakayostahimili kuvishikilia vigingi vyako ili lisichukuliwe na upepo, ardhi isiwe laini sana angalia mawe au visiki mahali utakapofunga kamba za hema.

## KUSIMIKA HEMA

Leo kuna mahema ya namna nyingi tofauti lakini njia ya kuyasimika hazitofautiana sana.

- Anza kulitandanza ili uone kona zake mahali unapotaka kulisimika kama ardhi inaulalo kidogo kichwa kitakuwa sehemu iliyoinuka
- Angalia upepo unatokea sehemu gani usilisimika mueleko ambapo hema litachukuliwa na upepo kirahisi
- Angalia pia kabla ya kusimika waliotangualia wameyapangaje, usijipangie tu
- Angalia njia za kupita wanakambi wengine zimepangwaje, kama wewe ndiye wa kwanza katika mstari huo simika vizuri wewe ndiye utakayekuwa alama ya kufuatisha
- Baada ya kuyaona yote sasa anza kuweka na kuinua nguzo za kuliinua mengine ya kisasa utaingiza zile nguzo na kulielekeza vema hakikisha hema limesimikwa vyema.
- Siku zote ziwepo hema za jinsia zote mbili, msilalae hema moja wavulana na wasichana au kuzisimika kwa kushikamana.

## KUFUMUA HEMA

Hakikisha hema limeakauka kabla ya kulifumua na kulikunja. Hakikisha linakunjwa kulingana na mikunjo yake ama sivyo utalisababisha kuchanika haraka. Unapolikunja ile sehemu ya kitako itakuwa juu mara nyingi ni mzito hakikisha vitu vyote vinavyohusu kulisimika hema vinachukuliwa na kufungwa na kuviweka katika mfuko wake.

## KUFUMUA HEMA BICHI LENYE UMANDE AU MAJIMAJI

Wakati mwingine utalazimika kufumua hema likiwa bichi kwa ajili ya ulazima wa kusafiri. Mara unapofika nyumbani ulianike mara moja usiliache muda mrefu limekunjwa litaoza na kuharibika.

## UTUNZAJI WA HEMA

1. Moto uwe mbali na hema zetu, moto ni tishio kwa hema, moto uwe kuanzia mita tatu
2. Tumia gundi ya hema linapokuwa na matundu
3. Tusipikie ndani ya hema mvuke unaharibu hema
4. Kabla hujasimika hema lako ili kulilinda tafuta kitu kingine cha kuliwekea chini liwe aina ya plasitiki isiyo ruhusu maji
5. Kabla ya kulitunza hema, hakikisha limekauka.

## MAHEMA HAYA YA NYLON

Mara nyingi yanaharibika kwa sababu hayakusimikwa vyema, usisimike hema mahali ambapo kuna vitu vya ncha kali, changarawe nyasi zilizofyekwa na kuacha visiki vya ncha kali mawe au ardhi isiyosawazishwa. Safisha eneo vizuri, ondoa mizizi na visiki kabla hujaweka hema lako. Vitu kama majiko ya kupikia stovu tafuta ubao uweke juu yake, mahali ambapo pana unyevunyevu weka mazuria mawili moja linaanza na la pili ndani kuzuia maji.

1) Vua viatu vyako kabla hujaingia ndani ya hema ukiingia na viatu utaleta uchafu ndani ya hema, weka kipande cha zuria mlangoni ili kuzuia uchafu.
2) Usisimike hema lako chini ya miti mikubwa haijalishi kuwa kuna hali gani mti waweza kuvunjika na kuharibu hema lako. Upo utomvu unaoweza kuangukia hema yako, jitahidi kuuondoa mapema, upo mwingine baada ya kukauka hautoki tena.
3) Hakikisha unapobomoa hema lako hakuna kitu ndani na umefagia vizuri kabisa hakuna takataka.
4) Kila mara lifanye hema lako kuwa safi na litunze mahali ambapo ni pakavu litadumu muda mrefu.
5) Ukiliezua likingali bichi lianike kikauke usitunze hema lako likiwa bichi.

**MAHEMA YA MATURUBAI**

Ukungu ni adui mkubwa wa maturubai, utakata nyuzi zote za pamba baada ya wiki chake, ukungu ni aina ya vimmea vidogo wakati mwingine twaweza kusema lakini Backeria pia wanaweza kuozesha nyuzi. Amira yaweza pia kuharibu. Hivyo kunahitajiwa uangalifu mkubwa sana katika kulisafisha ili usiruhusu wadudu kuozesha turubai lako, kausha hema lako vyema na kwa uzuri, chachu yoyote na ukungu visiruhusiwe kuota kwenye hema, kwa vile mara nyingi ni vigumu kuezua mahema yetu yakiwa yamekauka hivyo mara unapofika nyumbani likaushe.

Hakikisha hema lako halimwagiwi maji yenye kemikali ya kulifanya lioze.

**SHERIA ZA USALAMA WA MAHEMA YETU KWA MOTO**

**Moto ni hatari kwa mahema**

- Usipikie ndani ya hema
- Hema lisisimikwe mahali ambapo upepo unapeleka lisimikwe kinyume na upepo unapokwenda.
- Mioto yote iwe mita kuanzia 30 toka kwenye hema.
- Majiko ya mafuta pia hayapaswi kuwa sawa ndani ya mahema.
- Usitumie mshumaa ndani ya hema.
- Kitu kiitwacho moto kisiwe karibu na mahema ni hatari.

**D. MAFUNDO NA MATUMIZI YAKE.**

Yapo mafundo zaidi ya 150 ambayo hutumiwa katika maeneo, matukio, kazi na nyakati tofauti tofauti. Katika ukambikaji yapo mafundo yatumikayo sana kwa shughuli za kila siku kambini, baadhi ya mafundo hayo ni,


1. Square Knot(fundo Mraba) 2. Two half hitches 3. Timber Hitch
4. Clove Hitch 5. Sheepshank 6. Fishermen Knot 7. Bowline 8. Surgeon Knot
9. Sheet bend 10. Double bow 11. Slip Knot 12. Tautline Hitch 13. Timber Hitch.
14. Overhand Knot na 15. Lashes (Square, Diagonal, Shear na Trippod)

Yafuatayo ni maelezo ya mafundo machache,

**Hapa chini kuna mfundo manne ya msingi (Lashes)**

**DIAGONAL LASHING**


Diagonal lashing inatumika kufungia nguzo mbili pamoja zinazopishana lakini havigusani. Anza na fundo la kufunga magogo kuzunguka nguzo zote kuzikuza pamoja, fanya mizunguko angalau mitatu moja kwa upande mwingine.




Diagonal Lashing

**Fundo la mraba (Square lashing)**


Fundo la mraba linatumika pale ambapo miti miwili inapopishana na kugusana, unapofunga anza na fundo la clove hitch kwa nguzo moja. Zungusha kamba iliyo huru mwisho na ile iliyosimama ili kushikilia sehemu iliyolegea. Sasa zungusha kamba nyuma wima mbele ya pale zinapopishana, funga mara tatu.




Square Lashing

**SHEAR LASHING**


Fundo la shear lashing linatumika kuunganisha miguu ya nguzo. Fundo hili pia linafanya miti miwili iende sanjari wakati mwingine linatumika katika miti ya bendera.



Shear Lashing

**TRIPOD LASHING**

Hili linafanana na la hapo mwanzo shear lashing. Anza kwa kulaza miti mitatu pamoja kwenye ardhi kila moja likaelekea upande Fulani. Funga fundo la clove hitch au fundo la kufungia magogo katikati ya gogo. Funga mifundo minene kati ya hizo nguzo tatu kaza kabisa kila kati ya kila fundo. Malizia na fundo la clove katikati, inua kitu chako ulichotengeneza kwa kuzingeuza nguzo hizo



Tripod Lashing

**E. VIFAA KAMBINI**

Ifuatayo hapa ni mashauri ya Orodha ya vitu unavyopaswa kutayarisha kwa ajili ya kambi.

| Nguo | Vitu kwa ajili ya usafi | Vifaa vya kupikia |
|---|---|---|
| Suruali/sketi za kulalia | Sabuni | Sufuria ndogo kwa mboga |
| Nguo za ndani | Taulo | Kubwa la ugali nk. |
| Sokis | Mswaki | Kikombe |

| | | |
|---|---|---|
| Koti | Chanuo | Sahani |
| Kofia | Karatasi za kutawadhia nk. | Kijiko |
| Gloves | | Deli la kunawia |
| Sare za chama chako | | Vifaa vya kuwekea maji ya kutumia nk. |
| Mashka nk. | | |

**Vitu vingine kando ya hivyo**


- Panga
- Jembe
- Tochi
- Chandarua
- Kalamu
- Biblia
- Kisanduku cha huduma ya kwanza
- Kisu
- Wembe
- Kamba
- Kibiriti nk.

## SHOKA, PANGA NA KISU

### Jua vyema namna ya kunoa shoka, panga na kisu

Usinoe shoka au kisu kwenye jiwe la kunolea linalozugushwa na umeme. Ule mzunguko wa gurudumu hilo na joto linalotoka hapo laweza kuunguza sehemu ya kukatia ya shoka lako au kisu na kufanya kupoteza uimara wake. Jiwe la kuzungushwa kwa mkono ni zuri zaidi kuliko linalozungushwa na umeme.

Au tumia chuma cha kunolea (file) chenye ukubwa wa kati meno kati ya 10-12. utakuwa unanoa unavyotaka . kwenye kitovu kwenda eneo la makali funga shoka lako au kisu kwenye koleo (vise) itakayo kusaidia kuishika shoka yako vyema na kuanza kunoa bila tatizo. Noa shoka lako kwa kutumia meno ya tupa yako pekee. Weka mikono yako kiusahihi sukuma taratibu mgandamizo wa vidole gumba ukandamize mbele na nyuma, ili unoe vyema. Geuza upande na upande chunguza shoka lako vyema usijikute unanoa upande mmoja sana kuliko upande mwingine.



Endelea kufanya zoezi la kunoa taratibu hadi shoka limekuwa na makali ambayo waweza kukatia vitu bila wasiwasi. Baada ya kumaliza kunoa vyema kifaa chake weka mafuta kwenye makali kuzuia kutu.

Tahadhari unapotumia shoka au panga maeneo ya baridi ipashe joto kwanza, maana ukikata ikiwa baridi yaweza kukatika au kuvunjika.


**KISU**

Kitu kizuri cha kunolea kisu ni jiwe. Yapo mawe mazuri yanayotumika kunolea. Tupa (file) yaweza kutumiwa, si vyema sana kunoa kisu kwa kutumia jiwe la kuzungusha kwa umeme. Kisu kitapata joto sana na kupunguza ubora wake

**Yapo mapigo matatu ya msingi ya kunoa kisu.**

- Kufanya kama kunyoa – shaving
- Kuzungusha kama mduara – circular
- Tarakimu 8 – figure eight

Kila pigo jambo muhimu ni kuweka kisu katika ulalo Fulani kati ya makali ya kisu na jiwe au tupa unayotumia kunolea. Kwa muda wote na umbali wa kila pigo kwa kunoa vyema. Sehemu ya kukatia ulalo wake unapaswa kuwa nyuzi 10 toka uso wa jiwe la kunolea kwa namna hiyo makali ya kisu yatakuwa bora sana. Kwa visu vikubwa ulalo uwe $30^{0,}$ kwa namna hiyo makali yako ya kukatia yatakuwa mazuri sana. Kabla ya kuanza kunoa weka maji kidogo au mafuta kwenye kisu au jiwe hivi ni kupunguza msuguano mkali na joto kali linalotokana na kunoa.




Pigo la kunyoa – shaving Pigo la kuzungusha

Pigo hili linalojulikana na kunyoa ndilo rahisi sana na salama. Jiwe linakuwa ubapa katika usawa mzuri wa ardhi na makali ya kisu unayaelekeza kama kuja upande wako, kunyoa na kufanya kisu kufanana kama kinatoa ndevu kwenye jiwe lenyewe, fanya taratibu toka mwisho kwenda mbele ya kisu. Idadi ya mapigo ukuhakikishia ubora wa kuona kisu chako, waweza kuchanganya pigo la kunyoa nala kuzungusha.

Baada ya kunoa kijaribu kisu chako kama kinakata vizuri.





Figure-eight Stroke

Pigo – tarakimu nane – figure eight stoke)

Pigo la kuzungusha na kunyoa karibu yanataka kufanana, inaitwa tarakimu nane maana unazungusha kisu chako na kufanya umbo kama nane. Ingawa wakati mwingine linakuwa gumu kulitumia vyema. Uzuri wake tu unasaidia chuma kusichukuliwe kwa wingi na kuharibu kisu chako.

Visu vinavyonolewa kwa mashine masokoni mara nyingi havina ubora sana katika matumizi.

**Namna ya kupasua kuni**

Wakambikaji wengi wanajiumiza kutokana na kupasua au kukata kuni kwa kutumia panga, kisu au shoka. Matumizi mazuri ya vifaa hivi ni jambo muhimu sana, kwa sababu nguvu zinazotumika wakati wa kutumia vifaa hivi ni nyingi na hivyo swala la kujiumiza laweza kutokea sana kuliko kutumia vifaa vingine vya ukambikaji.

Vielelezo vya hapo chini vinaonyesha mfano wa namna ya kutumia shoka ki usahihi. Katika uzoefu wa ukambikaji, siku zote shoka yako iweke kwenye mkoba wa usalama.

- Unapokata kuni siku zote kata kwa ulalo fulani (mtindo wa V) kupunguza umbali wa kitu kuruka .
- Mkato wa kwanza uingie sana vya kutosha; ukuni ushike na mkono mwingine, na uchezeshe kuelekea chini katika pigo la kukata. Hii inakusaidia isiruke sana, kuja kwako au kwenda kwa watu wengine.
- Tumia mbinu ile ile kwa kupasua, kata mwisho wa kuni acha shoka likiwa ndani na lilete chini kwenye pigo la kukata.









**WINCHI ZA KIKAMBI**


Hapa chini kuna aina tofauti za winchi – ni rahis kuzitengeneza. Angalia mchoro hii hapa chini tengeneza zako.




Gin Pole Cranes




Cooking Crane and Notched Pothook



Swamp Fire



Chippewa Cooking Tepee



Adjustable Pot Prop

**F. MIOTO NA UPISHI KAMBINI**
**SHERIA NA TAHADHARI KWA MOTO**

1) Moto unapowashwa awepo angalau mtu mzima
2) Moto uwe mdogo wa kiasi
3) Usikaribie moto kabisa
4) Msijikusanye kuzunguka moto
5) Usiweke mafuta kama petroli karibu na moto
6) Angalia cheche zinazoruka zizime mara moja
7) Uwe na ndoo ya maji, magunia na mchanga tayari kwa kuzima moto unapojitokeza kuleta hatari.
8) Vaa vitu vinavyozuia moto unapopika
9) Nguo zinazoning'inia ovyo zisivyaliwe, nywele ndefu zifunikwe.
10) Vyombo vya kupikia vinavyotumia msukumo wa hewa visiwe karibu na moto.
11) Baada ya kupika hakikisha moto wote umezimika, usiache unawaka.

**VITU VINAVYOSHIKA MOTO KWA HARAKA NA MATAYARISHO YAKE – (Tinder and their preparation)**

Vitu vinavyoshika moto kwa upesi ni muhimu sana kwa kuwasha moto bila kutumia kiberiti. Kanuni inayohitajika kwa vitu hivi vya kuwaka upesi ni kwamba viwe vyepesi kushika moto na kwa haraka na viwe vya aina ya nyuzi nyuzi.

**Takataka za majani ya miti au nyasi**.

Takataka hizi za majani zinapaswa ziwe kavu, au majani au nyasi zilizopigwa pigwa na kutunzwa, zaweza kuwa manyoya, majani ya miti, nyasi nk. Ili kugundua kipi ni kizuri kutumia, fanya jaribio. Chukua vitu hivyo au takataka za majani/miti weka kaa la moto puliza kwenye hizo takataka. Moto toka kwenye mkaa ukishika mara moja na kuwaka kwenye takataka hizo tambua kuwa ni nzuri.

Hivi vitu vya asili vinaweza kuboreshwa zaidi kwa kuongeza vitu aina ya vumbi vumbi. Fanya zoezi la kuzikusanya na kuzifanyia majaribio utaona zinazowaka mapema, zitayarishe na kuzitunza ili uzitumie wakati utakapofika.

**Njia sita za kuwasha moto bila kutumia njiti ya kiberiti. Tengeneza/washa moto wa kambi kwa kutumia moja ya njia hizi**

a) Kwa kutumia jiwe gumu – flint
b) Msuguano – friction
c) Cheche – spark
d) Curved glass
e) Kiberiti cha chuma – metal march
f) Hewa ya kusukumwa – compressed air.

**MWALI WA MOTO WA MOJA KWA MOJA – (Direct flame)**

Njia hii inatumia sukari na dawa ya paramanganeti, chukua sukari kijiko kimoja cha chai nusu ya kijiko cha chai cha paramanganeti- vichanganye pamoja viweke kwenye shimo weka ubao mkavu. Shimo hili linapaswa kuwa kubwa la kutosha kuchukua mchanganyiko huu, zungusha kijiti chenye unene wa 3/8 nchi na chenye urefu wa futi moja na kina kifupi. Pata kifimbo kiweke katika unga huo na fikicha kijiti hicho kwa kukizungusha kati ya mikono yako. Mchanganyiko huo utaanza kutoa miali ya moto pole pole. Majaribio kadha yaweza kuwa ya lazima ili moto kamili utokee. Jaribio hili linaweza lisifanikiwe sana sehemu za baridi au penye maji.

**KUTUMIA MAWE MAGUMU – (Flint)**


Hii ni njia mojawapo ya kuwasha moto. Hii njia inaitwa "flint", kutumia mawe magumu kuyagonganisha kwenye takataka zinazowaka haraka, maana hivi ndivyo vitu viwili vinavyofanya moto uwake.

Kiberiti cha risasi ni mojawapo ya mfano wa njia hii.

Vipande vya jiwe la kiberiti litafanya kazi ya kutoa cheche linapogongwa kwenye chuma.Mahali pengi vitu hivi si rahisi kupatikana. Baadhi ya mito kando kando yake mawe ya jinsi hii yanapatikana. India yanapatikana kwa wingi. Haya mawe yanapogonganishwa pamoja mara moja hutoa cheche, mawe haya pia ni mepesi kuvunjika kama uonavyo kioo. Unapofanya msuguano huu vitu vinavyoshika moto kwa upesi vinapaswa kuwa karibu ili cheche inapotoka tu kwenye jiwe ikutane na takataka hizi.

Shikilia jiwe hili la kiberiti mkono mmoja na kipande cha chuma mkono mwingine. Weka vizuri jiwe lako na zile nyasi za kuunguza sugua kwa nguvu na mara moja.

Jiwe la kiberiti cha moto





**MSUGUANO – (friction)**

Njia hii ya kuwasha moto inaitwa upinde njia ya kuchonga ni rahisi kwa kutumia vitu ambavyo vyaweza kutoa moto haraka, lakini ni ngumu kama utatumia magogo au miti isiyoshika moto kwa haraka.

Kitu kinachotakiwa ni kiungo kizuri kilichopinda, mti wa kufikichia na ubao. Unaweza kushikilia unapofanya msuguano huo pamoja na takataka zinazowaka kwa urahisi. Zungusha kwa nguvu sana na haraka joto linapoongezeka utaona moshi.

Mchoro wa namna ya kufikichia

.




**CHECHE ZA MOTO**

Cheche za moto zinapatikana kwa njia ya kusugua jiwe la kiberiti na msuguano katika sehemu ya hitaji hili tutaelezea namna ya kupata moto kutokana na cheche za umeme. Njia hii yaweza kuwa ya hatari inahitajika tu itumike kama kunaonekana ni lazima. Kama imekulazimu kutumia ifanywe na mtu mzima akiwa na usimamizi.

Mtu ambaye amekwama mahali fulani na gari aweza kuwa na mafuta na cheche za umeme kama vyanzo vya moto. Funga kitambaa mwisho wa kijiti ili kufanya sehemu ya kupangusia kuwa kubwa, ichovye ndani ya mafuta, uliyonayo karibu yaliyoachwa na gari lisilofanya kazi. Kama injini bado inafanya kazi shikilia kile kitambaa ulichochovya kwenye mafuta kati ya nyaya zitakazotoa cheche za moto na nyaya zilizolengea wakati unapowasha kitu cha kuanza gari na kuanza kuwasha cheche zitakazoruka toka kwa waya uliyolegea ukigusa tu kitambaa hicho cha mafuta itashika moto mara moja.

Waya uliyofungwa kwenye betri utatoa cheche za moto wakati upande uliyolegea unapotingishwa. Tunapaswa kutambua kuwa njia hii ni hatari uwe mwangalifu unapoitumia. Tumia njia hii tu inapokuwa ni dharura.

**KIOO KILICHOPINDA – (Curved Glass)**

Kioo cha kukuzia vitu ni cha haraka kutumika kama kianzisha moto kama kuna mwanga wa jua wa kutosha. Nyanyua kioo hicho vizuri ukielekeza kwenye vitu vinavyowaka kwa upesi ili miali ya jua inapopenya kioo hicho inabadilishwa kuwa mwanga mkali kwenye vitu vinavyowaka upesi vitu vizuri vinavyoshika moto upesi vitaanza kuwa moto utaanza kutokea baada ya dakika kama mbili. Baada tu ya apo utaona miale ya moto, puliza ili kuongeza mwendo wa uwakaji moto.

Wasarifi wengi watakuwa na kitu cha kutumika kama kitu cha kuwashia moto, lensi ya kamera na vioo vinavyoweza kutumika katika kupata moto.


**KIBERITI CHA CHUMA**

Kiberiti cha chuma vinatengenezwa katika viwanda na kuuzwa kama shughuli za kibiashara. Inafanya kazi sawa na zile za njia za kupata moto kwa kusugua pande mbili. Kiberiti cha chuma kimetengenezwa kwa jiwe la kiberiti. Kama itasuguriwa kwa msuguo mzuri na sahihi itatoa moto au cheche zitakazounguza vile vitu ambavyo vinawaka kwa upesi, viberiti hivi vinauwezo wa kutumika muda mrefu, vinapatikana madukani.

**HEWA INAYOSUKUMWA AU KUGANDAMIZWA (compressed Air)**

Yapo maeneo ya ulimwengu huu wanawasha moto kwa kutumia mgandamizo wa hewa iliyo ndani ya chombo, ambayo mgandamizo huo unafanya kutoa joto na hiyo hewa inapoelekezwa kuliko na joto utoa moto. Hii jambo lilifanyika muda mrefu kabla ya mavumbuzi ya mafuta kuanza kutumika.

Compressed air




Hewa inayogandamizwa


## AINA ZA MOTO

### MOTO WA NYOTA – (Star fire)

Moto huu unatengenezwa au kuwashwa kama hauna kuni za kutosha au wakati ambapo hutaki kuwa na matumizi mengi ya kuni.

Baada ya moto mkuu umewaka vizuri mwisho wa ukuni mrefu unachomekwa kwenye moto, wakati ukuni unaungua unaendelea kuusukuma ndani zaidi uendelee kuungua.

**Angalia mchoro huu**




Star Fire

### MOTO WA MWINDAJI – (Hunter trapper fire)

Moto huu unatengenezwa kwa kupanga magogo mawili kila moja lenye urefu wa futi 3 na kipenyo kati ya gogo inchi 8 hadi 10 ili kuruhusu upepo uweze kuzunguka vyema kati ya magogo. Moto unawashwa kati ya magogo mawili – kuni za unene wa nchi 3 zaweza kuweka chini ya gogo moja toka mwisho kuruhusu hewa nyingi kupita kufikia moto.

Moto wa mwindaji




Hunter-Trapper Fire

### MOTO WA KUAKISI – (Reflector fire)

Moto mzuri wa kuokea ni moto unaoakisi ambao pia unatoa joto zuri wakati wa usiku wa baridi na pia ni moto uliyo na kinga dhidi ya upepo. Magogo yenye nchi kati ya 4 na 5 yanachimbiwa chini ya ardhi katika ulalo fulani. Vigingi vingine nyuma yake vinayashikilia au vinakuwa nguzo kati ya haya yanapangwa magogo yenye kipenyo cha nchi 6 hadi 8 moto unawashwa mbele ya

chombo hiki cha kuakisi, mkate unaweza kuokwa ndani ya chombo cha kuokea kilicho mbele ya moto huu wa kuakisi, bati kama litawekwa upande mwingine wa moto toka kwenye magogo haya





Moto wa kuakisi

**Moto wa aina ya mashauri (council fire)**

Wakati mwingine unajulikana kama moto wa mpasuko wa kuni (log cabin fire)

Huu moto unatumika kwa choto cha kambi ambapo wanakambi wanazunguka na kushauriana.





Mistari ya kwanza inapaswa kuinuka kadiri ya urefu wa futi tatu na kipenyo cha inchi 6 hadi 10. Wakati moto huu wa mduara umekuwa tayari miti miwili ya msingi inalazwa juu ya umbali wa futi tatu toka kila mmoja.

Mstari mwingine utakaofuata utakuwa mfupi kiasi na mwembamba. Mstari mdogo utapanda kwa juu kwenye hatari kama msalaba au zinakata upande mwingine na kufanya umbo la msalaba. Angalia michoro hapo chini kwa uangalifu. Fuatisha katika kutengeneza moto wako.

**CRISSCROSS FIRE**


Moto huu unaweza kujengwa kwa kiwango cha ukubwa wowote. Ni moto mzuri wa kupikia unafaa kama moto wa choto au zahama ya msalaba. Misingi yake moto zahama ya msalaba ni mfululizo wa miti mikubwa na midogo inayowekwa kila upande inawekwa upande. Unawaka mara moja kama hali ya kitanda cha kaa jekundu la moto ambao ni mzuri kwa kuokea. Angalia mchoro wake na fwatisha katika kutengeneza.




**Moto wa kupikia**

**Hunter Trapper Fire**

Moto unatengenezwa kwa kuwekwa mistari miwili ya magogo, kila mmoja kwa urefu wa futi tatu na upana wa upande wan chi nane na nafasi kati ya mti na inchi nane ili kwa upepo upate mzunguko sahihi. Kuni za unene wa inchi tatu zinaweza kuwekwa chini ya gogo moja umbali wan chi sita toka mwisho ili upepo upate kufikia moto




Moto wa kuakisi –Reflection fire Moto wa shimo (pit fire)

**Pit Fire -**Moto wa shimo unatumika zaidi nyakati za upepo au maeneo ya upepo. Chimba shimo weka mawe. Moto unaowekwa ndani ya shimo chini utaendelea kuwaka hata kama kuna upepo unaopuliza tu sehemu ya juu ya ardhi lakini siyo chini

**KUTAYARISHA CHAKULA CHA KAMBI KWA KUPIKA/KUCHEMSHA KUOKA NA KUKAANGA**

**KUCHEMSHA**

Njia rahisi ya kupika mlo wenye afya ni kukichemsha pole pole. Osha na kata vyakula vyako kama karoti, vitunguu na viazi; waweza kuongeza na mboga zingine ambazo utakuwa umechagua zaweza kuwemo kabeji maboga n.k. vile vitatu vilivyotajwa kwanza mara nying ni vya kupikwa kwa kuchemshwa. Vyakula vinavyoweza kulingana na mazingira ndivyo vinunuliwe kile kinachowatoshap kumbuka vihana mara nyingi wana kula sana.

Katika vyakula vya kuchemshwa nunueni kulingana na mazingira vitayarishwe nyema na kuweka ndani ya chombo cha kuchemsha na kichemshwe vema na muda wa kutosha kuendelea kutunza virutubisho vyake hakikisha unatumia angalau kuanzia dakika 20 na kuendela na uangalie kama vimeiva.

**VYAKULA KUKAANGA**

Vitu vya kukaanga vinavutia sana. Lakini mara nyingi havina lishe sahihi. Ingawa kambi lisilo na vitu vya kukaanga linageuka la huzuni. Vitu vya kukaanga vyaweza kuwa, viazi, ndizi, mayai n.k. utahitaji moto, mafuta na chombo cha kutumbukiza vitu hivi, moto wa kukaanga unapaswa kuwa wa kiasi. Kama unatumia mkaa ni bora zaidi maana joto ndilo litatumika zaidi kuliko mamiali yenyewe. Unapokaanga unapaswa kuwa mwangalifu, vaa vitu juu ya mikono kisichoshika moto kwa haraka (gloves za aina yake).

Unapokaanga vitu vyako uwe mwangalifu. Usitupe unachookikaanga ukiwa umbali mrefu mafuta yaweza kuruka au kusababisha moto Hakikisha unatumbukiza taratibu kwa umbali kidogo sana na mafuta. Moto usiwe mkali sana utaunguza. Ukifikiri vimeiva kumbe vimeungua tu juu ndani ni vibichi fanya zoezi la kukaanga.

Kama kuna uwezekano iteni mtaalam wa mambo ya kukaanga aje kuwapa zoezi.

**KUOKA**

Kutengeneza mikate juu ya fimbo, changanya maji na biskuti iliyokwisha tayarishwa. Hii inakusaidia usiongeze maji mengi- ili upate ndoge la unga ambalo halitang'ang'ania kwenye fimbo- fanya donge la unga wako kuwa nene kiasi na laini. Sikuzote ni busara kuchanganya na unga kidogo ili donge lililokandwa lisinate kwenye fimbo – usiongeze maji hadi wakati unapojisikia kuwa uko tayari kuanza kuoka.

Tayarisha unga wa kukanda pamoja na kijiti ambaco utaweka – kijiti kiwe kinene kiasi cha dole gumba la mkono wako – mti ukiwa mbali ni vyema zaidi. Hakikisha kuwa si mti wa sumu na unaoweza kushika mtoto kwa upesi. Baada ya kulitayarisha viringisha donge lako kuweye kijiti weka karibu na moto wako umbali wa inchi 8 au zaidi mahali ambapo doge lako litapata joto la kuivisha.

Kuoka mkate wako kwa kutumia vijiti kunahitaji moto mwingi unaotoa joto la kutosha na makaa unaowaka muda mrefu – usiozimika kwa haraka.

- Shikilia kijiti chako vyema chomeka mahali ambapo kitapata joto na bila kuungua – ukiinua karibu kuangalia jinsi mambo yanavyokweda.
- Mkate huu unaweza kuiva baada ya zaidia ya dakika 10 chagua njia nzuri ambayo itafanya uile vyema. Weza kuchomeka au tafuta gogo au jiwe agemeza kijiti chako chenye unga ukiweka karibu na mtoto
- Uangalie mkate wako vyema unapoanza kubadilika na kuwa na rangi kama ya dhababu geuza hivyo hadi uenee
- Epuka kutumia kijiti kinachotoa rangi nyeusi

**Kuoka kwa kutumia – chombo cha kuakisi (Reflector method)**

Jiko la kuakisi ukilitumia vyema litatoa vitu vizuri vitakavyookwa humo na kuwa kama tuko nyumbani.

Hili jiko la kuokea la kuakisi laweza kununuliwa madukani. Pia unaweza kutengeneza lako. Ingawa lisionekane zuri. Namna ya kutengenza nunua, bati la Aluminium au bati aina inayoakisi mwanga vizuri ya kiwango kimoja. Ukubwa wa mabati unategemea kuwa unataka jiko la ukubwa gani. Likiwa la ukubwa wa urefu wa 15x10 laweza unganishwe upate aina ya jiko unalotaka likiwa na mlango wa kufunga na kufungua. Pia weka matundu ya kuingizia hewa baada ya kumaliza kutengeneza washa moto ukiwa mbele ya jiko lako ambalo pia unaweza kuliegesha kwenye jiwe ili lipate joto kamili la kuivisha mkate wako

**KUOKA CHAKULA KWA KUTUMIA MKAA**

Hii ni njia rahisi kama unalobati zuri lenye kupitisha moto vyema, linahitaji kitako kizuri cha kukalisha kwenye mkaa wa moto. Tunaposema kitako kizuri tunamaana kile kinachotosha vyema kukaa kwenye mkaa na kutunza joto vyema la kuokea angalua kwa saa moja baada ya kuoka.

Tuchukuwe mfano unataka au kupika mlo wenye karoti viazi na vitunguu. Kata bati la Aluminium kubwa la kutosha la kufunika vitu hivyo na nafasi kidogo laza bati lako, zikate

katori zako kiurefurefu kata vitunguu vipange vizuri kwenye jiko – weka kwenye mkaa angalia joto liwe la kuivisha lisiwe la kuunguza fanya mazoezi kupata vitu bora sana.

**KUOKA VITU CHINI YA ARDHI**

Kuoka chini ya ardhi chagua ardhi kavu kwa ajili ya moto. Chimba shimo la kiasi unachotaka kulingana na vyakula unavyohitaji. Kama yapo mawe ni vizuri sana kuyalaza maana mawe yanatunza joto vizuri ndani ya shimo ukitumia kuni nyingi zilizokauka. Fanya moto uwake angalau kwa saa moja au zaidi. Kifungua kinywa chaweza kupikiwa juu ya moto huu.

Baada ya moto kuwaka na shimo kupata moto pamoja na kuta zake sasa usafishe huo mkaa unaowaka weka chakula chako, kumbuka kuondoa mkaa mwingine na kuuweka kando ya shimo. Sawazisha mkaa huo ili iwe na kima kimoja pande zote- kile unachotaka kupika kifunge kwenye majani au chombo fulani tumbukiza ndani humo kwa muda Fulani. Baada ya kufunga chakula chako vizuri kwenye majani au karatasi fulani tumbukiza ndani ya shimo funika juu vizuri kwa mchanga kisha weka mkaa wako juu ule uliyoundwa kwenye shimo. Kama utafuata hatua hizi kwa utaratibu kabisa baada ya muda fulani utakuta chakula chako kimeiva kabisa tayari kwa kuliwa.

## G. UTUNZAJI WA VYAKULA

**Njia sahihi ya kutunza na kuangalia chakula kambini, na namna ya kujenga mahali pa kufichia vyakula mbali na wanyama/ndege.**

Kama ulivyo utaratibu mkambikaji anayetunza kambi yake na kuitumia vyakula vichache atakuwa na matatizo machache ya wanyama na wadudu wasiyotakiwa kumsumbua kambini. Vyakula vilivyoachwa mezani au katika sanduku wazi au kwenye chombo wazi kinakaribisha wadudu na wanyama. Hapo chini kuna taratibu za kufuata.

a) Chakula kisitunzwe juu ya vichaka au masufuria yaliyo wazi.
b) Vyakula vya ziada vifunikwe katika chombo safi au kwenye chombo kisichopitisha hewa.
c) Chakula chako kipowe kadiri inavyowezekana, vyakula vinavyopaswa kuwa baridi vifanywe kuwa baridi ili visiwe sumu.
d) Mabaki yote yazikwe.
e) Wakambikaji wa porini mara nyingi wanaacha au kuninginiza mabaki juu ya miti ili wanyama wasiyafikie kirahisi, wenye magari wanapaswa kutunzia kwenye magari yao.


***MAHALI PA KUFICHIA VYAKULA (CASHES)***

**Kipooza joto cha chemichemi**


Chimba shimo kwenye chemichemi na panga mawe. Hakikisha kuwa ni shimo la kutosha kubeba chombo chako na ufunge lisipitishe hewa. Maji haya ya chemichemi yatapaswa yapenye katika mashimo yaliyotayarishwa na kutakuwa na kipooza kizuri.

**Kipooza joto cha ardhini**

Siku zote ni baridi kuanzia futi moja au mbili, chimba na weka chombo chako humo, weka chakula chako kwenye chombo na mwaga maji kwenye mchanga wa pembeni. Funika mahali pote pa kupoozea na karatasi zilizolowana. Funika shimo lote.




Spring Water Cooler




Ground Cooler

**Kipooza cha kuyeyuka**


Kabati la kufichia laweza kutengenezwa ndani ya kipooza, kama vile sanduku kwa kulifunika na nguo au magunia mazito. Sehemu ya juu iliyofunikwa inaninginizwa kwenye maji yaliyowekwa kwenye kabati hilo. Maji yatafyonzwa kwenye nguo hizo kwa muda kidogo tu. Haya maji yatapooza hewa yanapopita kwenye nguo hizi ndani ya sanduku.




Evaporating cooler

**Kipooza rahisi cha ndoo**

Hii inafanyika kama  hapo juu, ndoo ya maji inaninginizwa juu ya ndoo iliyo na vyakula. Nguo inatumika kufunika kitu cha kupoozea chote na nguo za juu zikizamishwa kwenye ndoo ya juu.




**Kabati ya kufichia**

Aina yoyote ya chombo iliyoning'inizwa isifikiwe na wanyama, mahali pa kuficha chakula hiki panapaswa pasiwe pa kuhamahama na ambapo paweza kuteremshwa au kupandishwa.

## H. KANUNI/SHERIA ZA KAMBI

Shughuli chache za nje za wakati wa kambi ni salama kuliko ukambikaji wenyewe. Chache ni za kufurahisha iwapo kila mwana kambi anashiriki kuliko ile iliyo nyumbani. Ingawa kutokuwa waangalifu kunaweza kusababisha ajali katika kambi au kukuletea matatizo madogo madogo katika mwili ambayo yanaweza kuepukwa.

Wanakambi wote wanapaswa wawe na ufahamu wa vitu vinavyoweza kuleta shida wakati wa ukambikaji na kujifunza kuviepuka. Pia inagharimu kujua upaswacho kufanya wakati dharura ndogo inapojitokeza, mkambikaji ambaye anatumia akili ni mkambikaji aliye salama, anafanya kazi zote za kambi kwa tahadhari zote' busara yote kuliko mjinga na anayefanya kazi yake mahali palipodhahiri.

Hii haimaanishi kuwa sasa ni mwoga na wasiwasi asiye na imani kwa Mungu. Hii ina maana kuwa anachukua tahadhari kabla ya kutenda jambo lolote.

Waweza kuwa mtu wa aina hii kwa kuchagua kuwa salama, mwenye afya kambini mwenye nidhamu unayesimika kambi lako kwa usahihi na mpangilio, unaytumia Vifaa vyote vya kambi kwa uangalifu.

**Hapa zipo baadhi ya sheria za kambi unazopaswa kuzitafakari na kuzifuata.**

i. Usikambike peke yako au kutembea peke yako (kundi la watu watatu au zaidi ni nzuri)
ii. Pata ruhusa ya mwenye ardhi unayotaka kukambika kwake.
iii. Usitoke kambini bila ruhusa toka kwa viongozi na kuwajulisha pale uendako na uendacho kukifanya.
iv. Pata ruhusa ya kuwasha moto pale inapohitajika.
v. Ziwepo saa za kula, kutembea, kulala, kuamuka nk. Kunahitajika kufuata ratiba iliyowekwa. Kundi linapokuwa kubwa utaratibu unahitajiwa ufuatwe kwa uhakika na makini.
vi. Kambi za mchanganyiko wa wanaume na wanawake jinsi zinazohitaji ziheshimiwe kwa hali ya juu hasa kwa matumizi ya vyoo na mabafu, kulala mwingiliano uepukwe pawepo mahema ya wavulana na wasichana kwa upande wa kulala. Ni marufuku wanakambi wa kiume na kike kulala kambi moja, isipokuwa la mme na mke.
vii. Usiende kuongea au kupiga kasia peke yako.
viii. Usiende kuongelea mbali na ufukwe bila mtumbwi au ubao ukiwa na wengine karibu.
ix. Usizamie ndani ya maji usiyoyajua kina chake au usalama wake.
x. Usiuwe wadudu au wanyama ovyo ovyo isiyo lazima.
xi. Epuka manung'uniko lawama kwa wenzako.
xii. Hakikisha eneo lako ni safi.
xiii. Usibabaike kunapojitokeza jambo la dharura usilolitegemea, ugonjwa nk.

**KANUNI ZA UKAMBIKAJI ZA WATAFUTA NJIA**

1. Nitakambika tu pale panaporuhusiwa
2. Nitaweka mazingira ya eneo la ukambikaji safi wakati wote na kuliacha likiwa safi ninapoondoka.
3. Sitaacha sehemu nilizotumia kupika bila kuzikagua, kuhakikisha moto umezimika.
4. Sitatumia kisu au shoka kutoa miti au matawi.
5. Sitachuma maua ya aina yoyote bila ruhusa
6. Sitakata kitu chochote ninapotembea
7. Sitachafua ziwa, mto au chemichemi za maji.
8. Nitaheshimu mambo ya binafsi ya wakambikaji wenzangu.
9. Nitakuwa mpole na makini
10. Nitaheshimu mabango yoyote, mamlaka na sheria zote na mali binafsi za watoto wengine.
11. Siku zote nitaishi kama mwanachama wa Watafuta Njia na mkristo.
12. Siku zote nitaacha eneo la kambi katika hali ambayo nitakaribishwa tena.

Usiache nyayo na endelea kupatengeneza vizuri ni usemi ambao utaendelea kuboreshwa.

## I. <u>UKIPOTEA</u>

**Elewa kanuni nane za kufanya unapopotea**

Tambua swala la kupoteza mwelekeo siku zote linatokea hasa pale unapokwenda kwenye mazingira usiyo yazoea.

Siri ya kutopotea siku zote ipo kwenye ukweli kuwa unapaswa kujua pale ulipo na pale ulipotokea; na maarifa haya siku zote tambua pale ulipo. Kama hutazitegemea kumbukumbu zako, unapaswa kuwa na ramani inayokuonyesha vitu muhimu, waweza kutumia saa yako kukuelezea ni umbali gani umesafiri kuelekea upande gani.

**Pale unapogundua kuwa umepotea na hujui mahali pa kuelekea fuata kanuni nane zakufuata.**

**1.** Kaa chini tulia na fikiri
Omba kupata mawazo yaliyo tulia kukumbuka vyema na mbingu ziingilie kati. Ondoa wasiwasi jilazimishe kukaa chini hadi pale utakapoona umepata mawazo yaliyotulia, usijaribu kukumbuka kila kitu, bali vitu maalumu. Ulikuwa wapi pale ulipoanza kutambua kuwa sasa umepotea.

**2.** Weka alama mahali ulipo
Usiondoke mahali hapo hadi pale utakapoweka alama, peperusha kitambaa au kofia iweke mahali fulani. Fanya kitu fulani mahali hapo kupakumbuka.

**3.** Kwenye Mti
Jaribu kuweka alama kwenye miti itakayokukumbusha usiharakishe. Angalia kila maeneo yanayozunguka angalia kama kuna moshi dalili ya kuonyesha kuwa kuna watu eneo hilo.

**4.** Chukua ujasiri kufanya jambo
Toka pale ulipo ulipoweka alama jipe ujasiri wa kutembea kama hatua 50, 70, 84, 100 toka hapo. Itategemea uko mazingira yapi. Siku zote hiyo alama iweke maanani uone kama utapata sehemu nyingine.

**5.** Je likiwa giza?
Kama ni wakati wa jua kwenda kuzama uwe tayari kulala mahali hapo kwa raha tu usiogope.

**6.** Tengeneza moto
Tengeneza moto wa usalama, pata kuni za kutosha kama kuna uwezekano ili ziweze kuwaka na kukupa mwanga usiku wote.

**7.** Ishara ya kuomba msaada
Ikiwa ni asubuhi kama unauhakika na mwelekeo wa kwenda, washa matawi ya Majani mabichi ili yategeneze moshi, lakini usizimishe moto. Tengeneza mioto mitatu ambayo inatoa ishara ya kuomba msaada.

**8.** Subiri msaada
Subiri msaada kuja, sikiliza sauti ya wanaokufuata kwa makini.

***"BWANA NA AWABARIKI"***

# MASIMULIZI YA KIKRISTO

(Christian Story – Telling – (OM – 8)

## UTANGULIZI:

Wale wanaochukua kozi ya Kiongozi Mkuu (Master Guide) wanatakiwa kuhitimu nishani ya masimulizi ya Kikristo. Nishani hii ni muhimi kwao kwani itawaptatia elimu inayowafanya wawe walimu bora wa watoto na watu wazima.

Watu wote wanapenda masimulizi, lakini watoto wanapenda zaidi. Master Guide lazima ajue kusimulia vyema ili wawasaidie watoto na vijana wanaopenda masimulizi zaidi.

Kusimulia hadithi ni mfumo wa zamani uliotumiwa kufundishia watu. Mfumo huu uliachwa yapata miaka 500 iliyopita baada ya uchapishaji machapisho kuibuka. Hadithi zikawa zinachapishwa badala ya kusimuliwa. Siku hizi, usimuliaji hadithi umepata umaarufu tena baada ya kubainika kuwa hadithi zilizochapwa hazieleweki vizuri kama zile zinazosimuliwa. Mtu anayesikiliza hadithi, anasikia maneno kwa masikio yake na kumwona msimuliaji na ishara anazozifanya kwa macho yaye. Kuona na kusikia hufanya mtu aelewe zaidi kuliko kusoma. Televisheni inafanya mtu aelewe zaidi kuliko Radio

Mafundisho yaliyo kwenye hadithi hueleweka vizuri na kwa urahisi na kukumbukwa zaidi wasimuliaji wanatakiwa kujisikia kuwa wana nafasi nzuri zaidi ya kupandikiza ukweli kwenye akili za wasikilizaji wao na kubadili akili zai zifae kwa wokovu. Hadithi na visa kufanya kazi kama vielelezo vya ukweli. Mwalimu mkuu Yesu, alifundisha ukweli kwa mafundisho yake kwa njia ya visa au hadithi, hupendwa sana na vijana anaowaongoza na klabu au darasa lake huwa hai.

### I. THAMANI NA MAKUNDI YA HADITHI

Akieleza thamani ya hadithi E.B Hare anasema: "Thamani ya hadithi haijaweza kupimika". Hata hivyo, A.W Spalding anajaribu kueleza thamani ya hadithi, anasema: "Hii ni thamani ya usimuliaji hadithi, hadithi zinafurahisha, zinafundisha ukweli na zinavuta watu wafuate ukweli" Yafuatayo hapa chini ni maelezo machache juu ya thamani hadithi:-

1. Hadithi ni moja ya misaada ya kufundishia.
2. Hadithi inaanzisha urafiki kati ya msimuliaji na wasikilizaji.
3. Hadithi hukuza usikivu.
4. Watu wote wanapenda kusikiliza hadithi.
5. Akili ya mtu huelewa yasiyoeleweka yanapofananishwa na yanayoeleweka kwa njia ya hadithi.
6. Hadithi hulifanya somo likumbukwe kwa urahisi. Mtu anaposikiliza hadithi huwa msikivu hivyo hukumbuka somo kwa urahisi.
7. Hadithi ni "uchawi" wa mwalimu kwani:-

a. Inaanzisha upenda na heshima kati ya msimuliaji na msikilizaji.
b. Inasahihisha tabia mbyaya bila kumkwaza mhusika.
c. Inaamsha hisia ya kupenda kitu
d. Inarahisisha somo.
e. Inakuza tabia ya kutoa shukrani.

## II. MAKUNDI MAKUU MAWILI YA HADITHI

(Yako makundi mawili makuu ya hadithi)

1. Hadithi zinazoburudisha

Hadithi hizi husimuliwa ili kubadili hali (mood) za wasikilizaji, mfano, wasikilizaji wenye huzuni au wenye mawazo mazito hawako yayari kupokea ukweli, maana wataendelea kuwaza mambo yako wakati ukweli unaelezwa. Hivyo hadithi ya kuburudisha inapoelezwa, inabadilisha hali ya huzuni na kuwafanya wawe yayari kusikiliza ukweli.

2. Hadithi zenye mafundisho

Msimuliaji huhadidhia hadithi zenye mafundisho anapoona kuwa wasililizaji wake wako yayari kupokea mafundisho.

## III. MAMBO MUHIMU KATIKA USIMULIAJI HADITHI

Yapo mambo saba ambayo ni muhimu katika usimuliaji hadithi. Mambo hayo ni kuwa na kusudia na kilele, uchaguzi bora wa hadithi, urekebishaji (modify) hadithi kadri inavyohitajika uandaaji dondoo (outline) za hadithi, kuijua vizuri hadithi, kuguswa na hadithi wewe mwenyewe kwanza na kuieleza hadithi kwa wazi bila kupindapinda.

1. Kuwa na kusudi na kilele

Kusudi ni nini?

Kusudi ni kile anachotaka msimuliaji wajifunze wale anaowasimulia hadithi. Kwa maneno mengine, kusidi ni somo au wazo ambalo kwalo hadithi inalenga. Hivyo:-

a. Kusudi au somo ni roho ya hadithi, hadithi isiyo na somo imekufa.
b. Kusudi humsaidia mtu kuchagua hadithi, huwezi kuchagua hadithi vila kuwa na kusudi.
c. Hadithi inaweza kuwa na makusudi au masomo mengi. Msimuliaji mzuri huwa na kusudi moja tu kwenye hadithi kwani makusudi mengi hutatanisha.
d. Kusudi linatakiwa liwe dhahiri au wazi kwa wasikilizaji.
e. Hadithi yenye makusudi mengi, inaweza kusimuliwa tena na tena na kila inaposimuliwa, msimuliaji hulenga kusudi tofauti na kwanza, hivyo kufanya hadithi ionekane mpya kila mara.

2. Ni kwa namna gani msimuliaji hupata kusudi la kusisitiza kwenye hadithi?

a. Msimuliaji lazima aamue jinsi anavyotaka wasikilizaji wake wawe maishani mwao. Namna anavyotaka wawe humfanya apate kusudi.
b. Mahitaji muhimu ya wasikilizaji huwa chanzo cha kuwa na kusudi. Na ikumbukwe kwamba usimuliaji wa kikristo hufanya kazi ya kujenga tabia njema polepole, kila hadithi ni sawa na tofali kwenye jengo.

3. Kilele ni nini?
   Kile ni hitimisho la kusidi au pale kusudi linapowekwa wazi. Kilele ni sehemu ya juu zaidi ya uelezaji hadithi kwa kuweka wazi zaidi kusudi lililokusudiwa. Kilele au kusudi linapokuwa wazi, hitimisha usimuliaji wako.

4. Namna ya kufika kilele vizuri
   Vipengele vifuatavyo vitakusaidia kujua namna ya kufikia kilele vizuri
   a. Panga vipengele vya hadithi kwa mfuatano.
   b. Eleza matukio kwa furaha na msisimko.
   c. Eleza kwa sauti inayosikika vizuri.
   d. Weka mazingira yatakayowafanya wasikilizaji wasikie yatakayotokea.
   e. Usitoe vielelezo virefu vya mambo ya kiroho katikakati ya hadithi kiasi kwmba vielelezo hivyo inageuka kuwa hubiri au hadithi ndani ya hadithi.
   f. Kilele kizuri ni kile ambacho mhusika mkuu katika hadithi anafanya uamuzi mzuri katika maisha yake au anashinda tatizo. (mfano, "Tokea hapo, Masanja hakuiba maembe tena".
   g. Kilele lazima kijibu maswali yanayojitokeza mwanzoni mwa hadithi.
   h. Usimuliaji wa kikristo, hauwaachi wasikilizaji na huzuni. Mhusika mkuu katika hadithi (Principal Character) lazima ashinde tatizo. Mfano, usimalizie hadithi ya Yona katika tumbo la Nyangumi, au Daniel kwenye tundu la Simba au Paulo na Sila gerezani. Kufanya hivyo kunawafanya wasikilizaji wawe na huzuni wasione faida ya uadilifu.

5. Uchaguzi bora wa Hadithi
   Unapochagua hadithi, zingatia yafuatayo:-
   a. Aina ya wasikilizaji – Hadithi inaweza ikawafaa aina moja ya wasikilizaji na siyo aina nyingine. Makundi ya wasikilizaji yanaweza kutengwa kulingana na umri wao.
      i. Kundi la watoto wachanga miaka 3 – 5
      ii. Kundi la watoto wadogo miaka 6 – 8
      iii. Kundi la vijana wadogo miaka 9 – 12
      iv. Kundi la vijana wa kati miaka 13 – 17
      v. Kundi la vijana wakubwa na watu wazima miaka 18 na kuendelea.

   Hata hivyo, mtu anaweza kusimulia hadithi kwa kundi la watu mchanganyiko, lakini, ahakikishe kuwa maelezo yake yanatosheleza kila kundi.
   b. Tukio lililotokea hivi karibuni linaloendelea kutokea au litakalotokea karibuni kunaweza kumfanya mtu achague hadithi itakayoeleweka zaidi.
      Mfano: Mkutano wa makambi unaoendelea, watu wanapooanisha maelezo ya hadithi na tukio ambalo bado linakumbukwa, wanaelewa zaidi.
   c. Hali ya wasikilizaji inaathiri uchaguzi wa hadithi. Jiulize, je, wasikilizaji wanataka kuburudishwa au kufundishwa? Ukigundua wanachohitaji kutendewa, chagua hadithi.

d. Hadithi kama imesimuliwa haifai kusimuliwa tena hasa kwa watoto wanaopenda vitu vipya. Inaweza kusimuliwa tu kama msimuliaji ana kusudi tofauti na lile lililotumika awali.
e. Unapochagua hadithi, zingatia linachopendelea kundi lako:
    i. Watoto wachanga hupenda kusikia juu ya watoto wachanga wenzao na wanyama wa nyumbani, mfano: paka na mbwa.
    ii. Watoto wadogo hupenda kusikia juu ya watoto wenzao, wanyama wa nyumbani, wanyama wengine na shughuli za nyumbani.
    iii. Vijana wadogo wanapenda kusikia juu ya vijana wa jinsia zao.
    iv. Vijana wa kati na wakubwa wanapenda hadithi za mafumbo, mifano, watu waliofanya vitu vya maana maishani, hadithi za uchumba na mengineyo.
    v. Watu wazima wanapenda kusikia juu ya fedha, maisha ya kila siku, watoto, vitu visivyo vya kawaida na kadhalika.

6. Urekebishaji hadithi, (Modifying the Story)
    a. Kwa nini tusieleze hadithi bila kuirekebisha?
        i. Hadithi lazima irekebishwe kufuatana na wasikilizaji watakaoisikiliza. Wasikilizaji wanatofautiana watoto wadogo hawawezi kuelewa, lugha, mazingira, shauku, kazi na mengineyo sawa sawa na vijana na watu wazima.
        ii. Kusudi la msimuliaji hadithi hubadilika mara kwa mara. Hivyo, vielelezo hubadilika pia.
        iii. Muda aliopewa msimuliaji hadithi unaweza kubadilika badilika. Anaweza kupewa muda mfupi au mrefu, hadithi lazima irekebishwe kulingana na muda aliopewa msimuliaji.
        iv. Hadithi ya nchi za mbali au ya zama za kale lazima irekebishwe ieleweke kwa msimuliaji.

    NB: Kurekebisha hadithi si kuibadilisha bali ni kuieleza kwa maneno yanayoeleweka kwa msikilizaji, kuifafanua kwa vielelezo vinavyoeleweka kwa wanaosimuliwa au kuifupisha ipatane na muda uliopewa kueleza.

    b. Njia mbalimbali za kurekebisha hadithi.
        i. Kurekebisha muundo (style) – Hii inajumuisha urekebishaji wa maneno na sentenso.
            a. Msamiati unaotumika lazima uwe unaoeleweka kwa msikilizaji.
            b. Msimuliaji lazima awaze kama wasililizaji wake wanavyowaza. Kama wasikilizaji ni watoto, msimuliaji lazima aelewe mambo wanayoyapenda kama wasililizaji ni wageni, lazima aelewe mila zao asije akawakwaza.
            c. Ni makosa kutumia misemo inayoeleweka kwa watu usiowajua, wanaweza wakawa hawajui misemo hiyo.

d. Hadithi za Biblia lazima zielezwe kwa maneno ya siku hizi ili wasililizaji wasioelewa misamiati kama, suria, viunga, mabarasi, shekeli n.k haitumiki sasa hivyo, haieleweki kwa wengi. Tumia misamiati inayoeleweka.

ii. Kwa upande wa ufupishaji hadithi, hadithi hufupishwa kama maelezo baadhi hayatawanufaisha wasikilizaji au maelezo ni marefu sana.

a. Uamuzi wa sehemu za kufupishwa utatokana na kusudi la msimuliaji. Kama sehemu ya maelezo ya hadithi haya, kusudi sehemu hiyo inaweza kuachwa.
b. Hata hivyo, hadithi iliyofupishwa lazima iwe "kamili", wahusika wa hadithi na matumio yapendezayo lazima yaelezwe. Kinachoachwa ni maelezo ambayo hayabadilishi maana ya hadithi. Mfano: ukiacha kueleza jinsi Daudi alivyoshindwa kutumia silaha za Sauli alipotaka kupigana na Goliathi, hakutabadili hadithi ya tukio la Daudi kumwua Goliathi.

iii. <u>Kuirefusha hadithi</u>

Hadithi hurefushwa wakati maelezo yake hayatoshi au hayaeleweki, unaweza kurefusha hadithi kwa kutoa maelezo ya mambo unayofikiria yalifanyika. Mfano: Japo haielezwe kuwa familia ya Daniel ilihuzunika wakati alipotupiwa kwenye tundi la Simba, na kwamba familia za washitaki zilifurahi, kueleza kuwa, "Nadhani familia ya Daniel ilihuzunika sana wakati familia za washitaki wake zilifurahi" ni salama kwani ni ukweli ambao kwa vyovyote ulitokea, kwenye maelezo yako eleza wazi kuwa maelezo haya ni yako tumia neon "nathali, naamini, inawezekana". Kufanya hivyo hurefusha hadithi bila kusema uongo.

iv. <u>Kufanya hadithi iwe wazi zaidi</u>

Ifanye hadithi iwe wazi zaidi kwa kusoma vitabu vinavyoeleza:-

a. Nchi ambayo kisa kilitokea.
b. Watu waliokuwa wakiishi katika nchi hiyo au wanaoishi sasa na mila zao. Ukitoa maelezo ya nchi, watu na desturi za watu ambao kwao kisa kilitoka, unaiweka wazi hadithi na kuirefusha.

v. <u>Tengeneza dondoo za hadithi yako</u>

Ni muhimu kutengeneza dondoo (Outline) ya hadithi yako. Kwa kawaida hadithi huwa na:

1. Kusudi
2. Utangulizi
3. Hadithi yenyewe
4. Kilele
5. Hitimisho.

Namna ya kutengeneza dondoo:

a. Andika kusudi la hadithi
b. Andika kichwa cha hadithi
c. Andika utangulizi kwa kifupi
d. Andika hadithi yenyewe – Andika maelezo kwa mfuatano
e. Andika kilele cha hadithi
f. Andika hitimisho

Ufuatao hapa chini ni mfano wa dondoo (outline) za hadithi:

KUSUDI: Kuwafundisha wasikilizaji faida ya kuwa mwaminifu

KICHWA: Mtumwa achanguliwa kuwa Waziri Mkuu

UTANGULIZI: Je, umeshawahi kusikia habari za mtumwa aliyechaguliwa na bwana zake kuwa Waziri Mkuu wao? Hili limewahi kutokea na leo tutaona kile kilichofanya litokee na ni wapi na kwa mtumwa gani.

HABARI KAMILI:
i. Daniel apelekwa utumwani Babeli
ii. Daniel anakuwa mwanafunzi wa Shule ya Ikulu
iii. Daniel apewa kazi Ikulu
iv. Daniel atafsiri ndoto ya Mfalme.
v. Daniel apandishwa cheo

HITIMISHO: Tumeona jinsi uaminifu wa Daniel ulivyomfanya apandishwe cheo na kuwa waziri mkuu wakati akiwa utumwani. Sisi nasi tukiwa waaminifu, Mungu atatutoa katika utumwa wa dhambi na kutufanya watawala pamoja na Kristo milele.

(N.B). Ingawaje unakuwa na dondoo usisome dondoo hizo mbele ya watoto. Karatasi ya dondoo unaweza ukawa nayo ukawa unatazama kipengele kinachofuata kama umesahau, ni vyema ukihadithia bila kuwa na karatasi ya dondoo.

Mambo yafuatayo yanatakiwa kukumbukwa unapoeleza hadithi:

i. Eleza hadithi wazi usitumie mafumbo.
ii. Mhusika mkuu wa hadithi lazima ashinde ili wasikilizaji waone jinsi wema unavyoshinda na utakavyoshinda daima.
iii. Hadithi inapoelezwa kwa watoto wadogo lazima iwe wazi zaidi na iwe na mfuatano mzuri zaidi.
iv. Vitendo wakati unapoeleza hadithi vinakuza usikivu.

HADITHI ZISIZOFAA KUSIMULIWA

Zifuatazo ni hadithi zisizofaa kusimuliwa:

i. Hadithi za kubuni zinazohusu maisha ya viumbe wasiopo duniani, Mfano: zimwi, ndege anayeongea n.k.
ii. Hadithi za watu walio na uwezo usio wa kawaida, mfano "Super man"
iii. Hadithi za kweli zinazoinua uovu, mfano sulemani alivyooa wanawake 700.
iv. Hadithi za watu wabaya walioinukia na kuwa watu mashuhuri bila kuacha uovu wao.
v. Hadithi za kikristo zinazohuzunisha zielezwe mara chache kwa watoto wasije wakafikiria kuwa ukristo ni kuteseka.

7. <u>KUJUA VIZURI HADITHI YAKO</u>

Sababu zinazofanya wengi wasisimulie hadithi ni kutojua hadithi vizuri. Jitahidi kuielewa hadithi yako. Hata kama wewe ni msimuliaji mwenye uzoefu, jiandae kabla ya kuhadithia kwa kujikumbusha hadithi yenyewe. Kama wewe ni mwanafunzi wa usimuliaji, jitahidi kuwa na mudia mrefu zaidi wa kujikumbusha hadithi. Chunguza kusudi na vipengele vyake kwa makini usikariri hadithi bali ielewe, uwezekano wa kusahau vipengele Fulani Fulani ni mkubwa ukiikariri hadithi.

8. <u>KUGUSWA NA HADITHI WEWE MWENYEWE</u>

Kuguswa na hadithi ni zaidi ya kuelewa hadithi kiakili, bali ni msimuliaji kuona matukio ya hadithi kimawazo, kusikia kupanda na kuteremka kwa sauti za wahusika wa hadithi katika mawazo yake na kujisikia kana kwamba matukio yanatokea mahali alipo.

9. <u>KUELEZA HADITHI KWA WAZI BILA KUPINDAPINDA</u>

"Uhai" wa hadithi unatokana na jinsi inavyoelezwa. Unapoeleza hadithi kumbuka

1. Kuzungumza wazi
2. Eleza vitu vya maana
3. Wafanye watu waelewe maelezo yako.

Unapoeleza, tumia misamiati na muundo rahisi wa uelezaji. Ikumbukwe kuwa kilicho rahisi kwa mtu mzima kinaweza kisiwe rahisi kwa watoto. Yapasa uwatazame wasikilizaji wako, usitazame wasikilizaji wa upande mmoja bali wa pande zote.

Unapoeleza hadithi, usipindishepindishe maelezo yako, toa maelezo moja kwa moja. Unapoeleza watoto wadogo, inapendeza sana kuwataka warudie rudie baadhi ya maneno unayoyatamuka. Kufanya


hivyo kunakuza usikivu na kuwafanya watoto waikumbuke hadithi kwa urahisi.

## KUFANYA TATHIMINI

Baada ya kueleza hadithi ni muhimu kufanya tathmini kama hadithi yako imeeleweka kwa wasikilizaji. Unaweza kupima kama hadithi yako imeeleweka kwa kuangalia kama:

i. Watoto wanafaya michezo ya hadithi hiyo
ii. Kama watu wazima wanaieleza hadithi hiyo kwa watu wengine.
iii. Kama wale uliowahadithia wanataka uwasimulie hadithi nyingine
iv. Kama wasikilizaji watapiga makofi baada ya kumaliza kuhadithia.

**MICHEZO YA BIBLIA (Bible games)**



**Michezo ya Biblia nini?**

Huu ni ubunifu unaofanywa na kiongozi wa vijana au Watoto kwa kutumia visa, hadithi, mafungu, Majina, nk vilivyomo ndani ya Biblia kwa namna ya mchezo hivyo kuwafanya watoto kushika kwa uharaka na iwepesi simulizi zinazopatikana katika Biblia.

**Ubunifu unahitajika sana**

Kutokana na kujifunza nishani ya Masimulizi, jinsi unavyoweza kuvuta usikivu wa watoto, ndivyo unavyopaswa kutumia namna hiyo hiyo kubuni michezo ya Biblia itakayo wavuta Watoto kufurahia Hadithi na Visa mbali mbali vilivyomo katika Biblia.

**Michezo ya Biblia imegawanyika kama ifuatavyo:**

1. Kukuza uwezo wa kielimu
2. Ni maburudisho
3. Hukuza mambo ya kiroho

**Kufundisha masomo ya Biblia (Teaching Bible Lessons)**

Fikiria jisi ambavyo ni vigumu sana kufundisha masomo ya Biblia kwa Watoto, kwa Vijana na hata watu wazima. Nivigumu sana kuchanganua, lakini kwa kutumia michezo ni njia rahisi sana kwa motto au mtu mzima kushika fundisho au somo hilo kwa urahisi na kulifurahia.

**Michezo ya Biblia na zawadi kwa watoto, vijana na watu wazima**

Michezo iliyojengwa katika msingi wa Biblia ni zawadi kubwa kwa watoto, vijana na watu wa wazima. Huamsha ari ya kuipenda Biblia na kuleta hamasa ya kuisoma mara kwa mara.

**Hisia za kiroho (Spiritual Feeling)**
Wakati watoto wanashiriki michezo mbali mbali ya Biblia, hasa wakiwa katika makundi yao, wanapata ule mguso wa kiroho, siyo tu wasisimuliwa na kufurahia tu kutokana na hiyo michezo. Kupitia hapo, wengine hushika nguvu ya imani katika umri huo wa ujana, kumbe wanalikosa hiyo nafasi huenda wasingalipata kufurahia neon la Mungu hadi kufikia umri wao wa uzee.

**Michezo inawafaa rika zote**
Je unachukulia michezo ya Biblia kuwa ni ya muhimu kwaajili ya kupata elimu ya Biblia? Njia moja nzuri ya kuweza kufanya ni kutafuta michezo mbali mbali ya Biblia. Jambo la kushangaza ni kwamba michezo hii inao uwezo wa kuchukua mvuto au usikivu wa watu wa rika zote na inaweza kuchezwa pia katika ngazi ya kifamilia.

**Michezo ya Biblia inachezwa kwa malengo**
Inaweza kuonekana kuwa watoto wanafanyaaina ya kelele, lakini hiyo ndiyo njia ya kujifunza. Baada ya muda watoto watakuwa wamepata hazina kubwa ya kiroho katika maisha yao. Hata hivyo kila mchezo wa Biblia unapomalizika, liwepo fundisho la kiroho ambalo watoto watajifunza. Aidha watoto wenyewe wawezakuulizwa kutoa maelezo kuwa wanajifunza nini kutokana na Mchezo huo wa Biblia au wewe mwalimu wa hao watoto waweza kutoa mafundisho mawili au matatu ya huo mchezo.

**Faida za Michezo ya Biblia**
1. Watoto, Vijana na Watu wazima watalipenda kanisa
2. Wataipenda Biblia (kitakuwa kitabu chao cha muhimu) na kuyajua maandiko
3. Wataandaliwa kuwa wahubiri
4. Watamtetea Yesu wakati wa mateso
5. Watamshudia Yesu kwa wale wasio mjua Yesu
6. Neno la Mungu litawachangamsha (watakuwa na furaha katika Bwana)

**Aina mbali mnali za michezo ya Biblia**
*Michezo ya kubahatisha watu/vitu ndani ya Biblia*
Tafuta neon fulani katika Biblia (Guess the Bible word)
Tafuta Muhusika/Wahusika Fulani katika Biblia (Guess the Bible character)
Tafuta maeneo Fulani katika Biblia (Guess the Bible place)
Tafuta kitabu Fulani katika Biblia (Guess the book of the Bible)

*Kushindana kwa kutafuta*
Kushindana kutafuta maneno na kifungu cha maneno.
Kushindana kutafuta Vitabu vya Agano la Kale
Kushindana kutafuta vitabu vya Agano Jipya


*Kutafuta Maneno, Wafalme wa Israel na Manabii*

Kutafuta maneno katika Biblia (Search for biblical words)

Kutafuta Wafalme wa  Israel (Search for Kings of Israel)

Kutafuta Manabii katika Biblia (Search of biblical prophets)

Mfano wa mchezo wa Biblia (Jaza katika namba hi kwa wima na kwa ulalo)




***Wima***

1 Kitabu cha nne cha injili kimeandikwa na …

2 Mototo wa Yese aliitwa …

3 Kitabu cha tatu cha Injili kimeandikwa na …

4 Waraka wa Paulo wenye sura tatu tu ni …

8 Kitabu cha mwisho cha Biblia kinaitwa …

9 Mfalme ambaye Mungu alimkataa Israel wakamtaka ni …

10 Nabii mwanake katika (Lk2:26) aliitwa …

***Ulalo***

3 Mke wake … aligeuka akawa nguzo ya chumvi


6 Atakapokuja huyo Roho wa kweli mtapokea …

7 Sulemani katika fahari yake hakuvikwa uzuri kama … (Lk12:27)

10 Katika Biblia mji wenye herufi mbili ni …

12 Mtu mfupi katika Biblia aliitwa … (Lk19:2)

Tengeneza maswali ya jedwali hili kama sehemu zoeli lako la ubunifu
(Mshazari kwenda juu na Mshazari kwenda chini)




***Mshazari kwenda chini***

1 …………………………………………………………………………………………………

3 …………………………………………………………………………………………………

5 …………………………………………………………………………………………………

6 …………………………………………………………………………………………………

7 …………………………………………………………………………………………………

8 …………………………………………………………………………………………………

***Mshazari kwenda juu***

2 …………………………………………………………………………………………………

3 …………………………………………………………………………………………………

4 …………………………………………………………………………………………………

9 …………………………………………………………………………………………………

10 ………………………………………………………………………………………………

11 ………………………………………………………………………………………………

12 ………………………………………………………………………………………………

# Utangulizi.

Vita kuu kati ya Kristo na shetani mabayo ilianzia mbinguni na hatimaye kuhamia hapa duniani hatimaye itafikia mwisho wake. kitabu cha Danieli na kitabu cha Ufunuo vinaelezea jinsi mambo yatakavyokuwa. Lakini kabla ya mambo hayo, hebu nikuonjeshe kwa ufupi tu sura chache za Danieli na Ufunuo, kisha anza kuvisomo vitabu hivi kwa makini kwa muda hautoshi kueleza yote.

# ZAIDI YA MATEKA

Kitabu cha unabii cha Danieli kiliandikwa kwa ajili ya wakati wetu. Unabii wake unaongea kwa uongezeko zaidi kwa kizazi hiki.
Malaika Gabrieli alimwambia kwa maalumu hasa Danieli "yafunge maneno haya ukatie muhuri kitabu hata wakati wa mwisho". Danieli 12:4. Danieli nabii wa Biblia anaorodhesha kwa undani matukio ya Dunia ambayo yanafunuliwa sasa mbele ya macho yetu. Utabiri wake unafunika miaka 2500 ya historia, kwa uwazi na undani anaorodhesha matukio ya Dunia toka kipindi alichoishi nabii [2600 BC] mpaka wakati wetu hata kuja kwa Mwana wa Adamu. Kama tulivyo karibu na kufungwa kwa historia ya Ulimwengu; maunabii haya ya kushangaza yanakuwa ya wazi mno. Yanatoa taarifa za ndani juu ya mipango ya adui. Yanafunua udanganyifu anaotumia shetani kuwadanganya wakazi wa Dunia hii. Vile vile yanaorodhesha mikakati ya Mungu kwa wakati wa mwisho.

Nzuri kuliko zote, nabii anafunua namna ya kufanikiwa kwa nyakati ngumu zilizo mbele yetu. Siku zijazo za mbele zitakuwa ngumu sana. Hatari isiyofikirika itaipata dunia yetu hii. Rafiki unaweza ukafanya zaidi ya kuokoka, unaweza ukafanikiwa, unaweza ukaneemeka. Danieli anaelezea namna ya kuteka na kuingia kwenye raslmali ya nguvu za kiroho. Kama mateka kwenye nchi ya kigeni, akiwa anawajibika kwa msongo wa namna ya kutumia mawazo yake, Danieli alishinda. Alishinda kwa kishindo kisichoelezeka. Nawe waweza kuwa Danieli wa leo.

Kama tutakavyojifunza masomo haya, utaweza:-

1. Kugundua siri za maisha ya maombi.
2. Utapata uzoefu mpya juu ya nguvu za Mungu katika maisha yako binafsi.
3. Utajenga nguvu ya kiroho ya kupinga majaribu
4. Utajifunza matukio yatakayoutingisha ulimwengu mara juu ya dunia hii kama uvamizi wa kutisha wa ghafla.
5. Utapata funguo za kufahamu ukweli kwa wakati wetu.

Kila somo litakuongoza katika safari ya kugundua ndani ya Maandiko Matakatifu. Unavyoendelea kuangalia majibu ndani ya Biblia yako mwenyewe utaona kuwa kujifunza Biblia ni zawadi ya uzoefu. Utagundua njia ya kupata furaha na maisha ya raha ya milele.

Sura ya kwanza ya Danieli inatoa utangulizi wa kusudi zima la kitabu cha Danieli. Pambano kubwa mno kati ya mema na mabaya. Inafunua nguvu ya Mungu ya uungu katika hali isiyo ya kawaida. Mipango yake inashinda katikati ya yasiyoshindikana.

# Ukweli kwa ajili ya wakati wa mwisho.

Unabii wa Danieli uliandikwa kwa nyakati maalumu katika historia ya dunia hii. Danieli 12:6,8,9,13. Mungu anatoa ahadi kwa watu wake kuhusu wakati ujao. Amosi 3:7.

Roho Mtakatifu anafunua ukweli kupitia manabii wa Biblia. Wakati ujao ulifunuliwa wazi. Kwa nini tujifunze unabii wa Danieli? Yohana 14:29.

Unabii uliotimia unaongeza matumaini yetu juu ya ukweli wa Biblia. Vile vile unatuandaa kushinda kabisa kwa matukio yaliyo mbele.

Yesu alitoa ushauri katika hubiri lake juu ya matukio ya wakati wa mwisho kuhusiana na maunabii ya Danieli. Mathayo 24:15. Kitabu cha Danieli lazima kiwe cha muhimu sana. Ndicho kitabu pekee ambacho Yesu alisema maalumu kwa watu wake wa mwisho kujifunza. Kina ukweli wa wakati wetu. Unabii wa Danieli unafunua mipango ya Mungu na kufunua mipango ya adui. Kitabu cha Danieli kinaweza kugawanywa katika sehemu mbili. Hadithi na unabii. Hadithi zinafunua namna ya kuwa tayari kwa siku za mwisho za ulimwengu. Maunabii yanafunua ni wakati gani matukio ya siku za mwisho yatatokea.

Katika somo hili tumegundua asili ya matumaini ya Danieli. Hili ni hitaji langu na lako pia. Dunia hii imeathiriwa na dhambi na kuchafuliwa vile vile na dhambi.

Kitabu cha Danieli kinaanza na pambano zito sana Mashariki ya kati. Mataifa mawili yalihusika Yuda na Babeli. Danieli 1:1 wafalme wawili walihusika:-

- Nebukadneza wa Babeli
- Yehoyakimu wa Yuda

Mwaka wa 605 BC Nebukadneza mfalme wa Babeli aliuhusuru Yerusalemu. Miji hii miwili inawakilisha njia mbili za maisha--------- mawazo mawili--------- falsafa mbili. Babeli ilikuwa kitovu cha uasi dhidi ya Mungu wa kweli. Ilisimama kwa uasi au mfumo wa dini ulio kinyume na sheria ya Mungu.

Yerusalemu mji wa Danieli unasimama juu ya utii, uaminifu, na haki. Inawakilisha ibada kwa Mungu wa kweli na utii wa sheria ya Mungu. Katika fungu la kwanza,la kitabu cha Danieli pambano hili kati ya nguvu za wema na nguvu za uovu linaelezewa kwetu. Vita kuu kati ya mema na mabaya ambayo ilianza mbinguni. Ufunuo 12:7-9 inaendelea hapa Duniani.

# Mateka wakamatwa

Sifa za vijana wa Kiebrania ambao Nebukadneza aliwachukua mateka. Danieli 1:4

- Wasio na mawaa
- Wazuri wa uso
- Wajuzi wa hekima
- Werevu kwa ajili ya maarifa yao
- Wenye kufahamu elimu
- Watakaoweza kusimama ikulu
- Wanaofundishika.

Mfalme alifanya nini ili kubadili utambulisho wa mateka hawa wa Kiebrania? Danieli 1:6,7. Aliwapa majina mengine kulingana na miungu ya Babeli.

- Danieli akaitwa Belteshaza= bel ina maana ya bwana "lord" means protect the king's life.
- Hanania akaitwa SHADRAKA = Corruption of Marduk ,mungu wao mkuu japo jina si la kibabiloni ni jina la Kielamu.
- Mishaeli akaitwa Meshaki= siyo kibabeli vile vile.
- Azaria akaitwa Abednego = Ebednego ikiwa na maana ya mtumishi wa mungu [servant of the god].

Nebukadneza alianza kuosha akili zao kwa kubadilisha majina ya vijana hawa wa Kiebrania ili kuwakilisha miungu ya kipagana ya Babeli. Kwa njia hii alitumainia kuharibu utambulisho wao. Tafakari juu ya adui shetani amekupa jina gani kuwakilisha tabia yake bila wewe kujua au unajua na wewe umeridhika hivyo. Saa imefika ya kupata akili kama akina Danieli na wenzake.

Danieli akaazimu moyoni mwake. The word purpose means to determine or decide. The governing power within our mind is our will. Wakati tunapochagua kufanya vema, Mungu anatoa nguvu ya maadili kuongoza mauchaguzi yetu[to carry out]. Roho wake Mtakatifu anatuongoza kufanya uchaguzi--- na tunapofanya anatupa nguvu ya kufanya tulicho chagua. Kesi sasa iko hapa umechagua nini? Unataka uwe nani katika maisha yako ya kiroho na kimwili.

Danieli anamwomba mtumishi wa mfalme. Danieli 1:12. Imani ya Danieli ilimwongoza kwamba Mungu ataheshimu uchaguzi wake. Alijua kwamba kamwe Mungu hatamkatisha tamaa. Elewa rafiki Mungu hatakukatisha tamaa mradi tu umemwelewa anavyofanya kazi na umejitoa kwake kikamilifu kwa maisha yako yote.

## Matokeo ya miujiza

Danieli na wenzake walipata faida kwa uchaguzi wao wa kuwa watiifu kwa Mungu.

- Matokeo ya kimwili= Danieli 1:15
- Matokeo ya kiakili= Danieli 1:17
- Matokeo ya kisiasa= Danieli 1:19,20.

Uaminifu wa Danieli kwa Mungu ulimfikisha kwa mibaraka ya Mungu. Tunapofanya maamuzi ambayo kwa hakika ni maadili mema, tukifanya vema kwa sababu ni vizuri kufanya hivyo, nasi vile vile tunategemea kupata mibaraka ya upendo toka kwa Baba wa Mbinguni. Tunaweza tukakata tamaa. Ilikuwa hivyo kwa Danieli. Lakini uhakika ni kuwa mwishowe ni ushindi. **Mungu anageuza kushindwa kwetu kuwa kushinda**. Anageuza makovu kuwa nyota zing'aazo kwa utukufu wake milele. Katika majaribu ya maisha tunaweza kumwamini na kumtegemea Mungu hakika.

# WAKATI UJAO UNAFUNULIWA NA NENO LA MUNGU

Ulimwengu una shauku ya kujua nini kitatokea kesho. Watu wengi wanakwenda kwa watazama nyota ili wawaambie na kutafuta kuwa wakati ujao una nini.

**Wakati ujao ni swali kubwa sana kwa watu wengi**. Wengi wanahangaika kama wakati ujao kutakuwa na vita, na tayari kuna vita katika kona zote za dunia leo. Je, kutakuwa na vita kuu ya tatu ya dunia na ya mwisho ambayo itaharibu kila kitu alichofanya mwanadumu? Je, kutakuwa na

machafuko kama tetemeko au gharika au vitu vya kuharibu sehemu kubwa ya makazi ya watu? Au kutakuwa na mbingu mara moja? Je, Mungu ataweka ufalme mpya? Na Yesu atakuja na kuturudisha nyumbani, mahali ambapo hakutakuwa na maombolezo tena au masumbufu au kifo?

Au je dunia itaharibiwa na silaha za nyuklia au moto? Je, familia zetu zitegemee nini? Kwa karne zote kama tulivyokwisha sema, wakati ujao daima umekuwa fumbo kwa watu. Tuna hamu ya kujua nini kipo mbele yetu. Tunawezaje kuikabili kesho kwa ujasiri mkubwa? Watoto wetu wataishi kwa ulimwengu uliofananaje?

Leo tunapaswa kumshukuru Mungu kwa sababu Biblia inavuta pazia nyuma na tunaweza tukafahamu nini kitatokea wakati ujao. Danieli sura ya pili, Mungu anawapa wenye hekima changamoto, na anajifunua mwenyewe kama wa pekee tu ambaye kwa kweli anajua wakati ujao. Katika sura hii, Mungu anaeleza kwa ufupi miaka 2500 ya historia kabla ya kutokea, kwa uhakika anaeleza kupanda na kushuka kwa himaya mbalimbali. Unapojifunza sura hii utashangaa kwa uwezo wa Mungu wa kuongoza miisho ya mataifa. Kama ana hekima ya kutosha kutabiri wakati ujao na mwenye nguvu vya kutosha kuruhusu kupanda na kushuka kwa mataifa, kwa hakika anaweza kuongoza maisha yetu binafsi. Somo letu la leo linafunua wazi kwamba ni salama kumtumainia Mungu.

# NDOTO YA MFALME WA ZAMANI

Nani pekee anaweza kusema habari za wakati ujao? Isaya 46:9,10.
Kama miaka 2600 iliyopita kulikuwa na mfalme mkuu sana aliyetawala himaya kubwa. Jina lake alikuwa Nebukadneza na himaya yake ilikuwa Babeli.

Mfalme huyu alifikiria nini kitaitokea Babeli baadaye. Usiku mmoja aliota ndoto. Ndoto hii ilimvutia sana. Asubuhi hakuikumbuka ndoto yake. Alikusanya wenye hekima wote wa Babeli. Aliwataka wamwambie ndoto na kisha tafsiri yake. Hii ilikuwa changamoto kwa wenye hekima wote wa Babeli maana ni vigumu sana kusema kilicho ndani ya kichwa cha mtu mwingine na mtu huyu amesahau kilicho ndani yake. Danieli 2:1

**Mfalme alifanya nini? Danieli 2:2.**
Amri ya mfalme ilikuwa kali sana na adhabu yake ilikuwa ni kifo. Wenye hekima wa Babeli walishindwa kabisa. Kwa hali ya kimiujiza Mungu alificha ndoto kwa Nebukadneza. Kama mfalme angekumbuka, wenye hekima wangeliweza kujaribu kutoa tafsiri yake.
Kwa hekima ya mfalme, kwa akili yake aliita:-

- waganga
- wachawi
- wasihiri
- wakaldayo
- wanajimu

**Wanajimu**= watazama nyota wenye elimu ya anga.
**Wasihiri**= wenye elimu ya umizimu, wanaoongea na wafu juu ya wakati ujao.
**Wakaldayo**= waelimishaji wajinga ambao wanajaribu kusema wakati ujao kwa akili za mwanadamu, mahesabu na falsafa.

**Waganga** = wanatumia viini macho, uchawi, na ujanja.

Mfalme mwenye hasira aliwalaumu wenye hekima wote wa Babeli na kuwahukumia kifo kama watashindwa kumwambia alichoota na tafsiri yake.

**Danieli alienda kwa njia tofauti.**
Danieli alikuwa miongoni mwa wenye hekima. Aliomba muda kidogo. Danieli 2:13-15. Kwa maombi usiku ule Danieli akaota ndoto ile ile na kupewa tafsiri yake. Danieli 2:19-23.

Mungu ana ubora wa aina mbili. Danieli 2:20
- Hekima
- Uwezo

Mungu pekee ndiye awezaye kufunua ndoto. Danieli 2:28.

Kitabu cha Danieli maalum kabisa kinafunua matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu. Ndoto ya mfalme inasonda wakati wa mwisho. Inasema matukio ambayo yatatokea wakati wa kufunga historia ya ulimwengu.
Siku iliyofuata Danieli alisimama mbele ya mfalme kwa ujasiri mkuu. Mfalme aliona ndoto. Danieli 2:31.

Kichwa = dhahabu= Babeli
Kifua na mikono= fedha= Umedi /Uajemi.
Tumbo= shaba= Uyunani.
Miguu= chuma = Rumi.
Nyayo= chuma na udongo
Jiwe= ufalme wa Mbinguni wa Yesu Kristo wa milele.
Danieli 2:32-35
Babeli = 605- 539 BC Hapa ndipo ilipo Iraq ya leo; maili 60 Kusini mwa Baghdad mungu wake mkuu aliitwa Bel- Marduk alitengenezwa kwa dhahabu. Isaya 14:4. Babeli haitadumu milele.

Umedi/Uajemi= 539- 331BC Isaya 44:28; 45:1

Kisha Uyunani. 331- 168 BC. Kwa kuongozwa na ALEXANDER MKUU.
Baada ya Uyunani Rumi 168BC - 476 AD Baada ya hapa hakuna ufalme mwingine wa dunia nzima

Nyayo zinatupa historia ya ajabu sana. Hakuna ufalme wa dunia yote baada ya Rumi ila Rumi kugawanyika.
Kwa maneno mengine tunaishi kwenye nyayo za ile sanamu kubwa; chini kabisa mwa mwisho wa historia ya mwanadamu. Falme za sasa hazitaweza kuungana. Historia inaonyesha kwamba mataifa yalijaribu yakashindwa, ukomonisti ulishindwa, ulaya haitaungana.

Ufalme wa ulimwengu unaofuata ni ufalme wa jiwe lilianguka na kuharibu ile sanamu. Danieli 2:44,45.

Kuna mambo muhimu katika kisa hiki:-

- ♦ Ufalme wa mwisho mkuu unafuata baada ya Ulaya kugawanyika.
- ♦ Ufalme unaofuata utawekwa na Mungu na utakuwa tofauti na wengine wote.

Mungu aliahidi na atatimiza ahadi yake. Ufalme huu utakuwaje? Ufunuo 21:4; Hauna makaburi, hakuna kifo, hakuna kutengana, amani tele. Twapaswa kujiandaa kuwa raia wa ufalme wa jiwe.

# KUTOTII AMRI YA KIFO

Kwa kila ukweli wa Biblia kuna bandia. Mwovu ameamua kuwadanganya watu wa Mungu. Toka mwanzo kazi yake ni udanganyifu tu. Yeye ni baba wa uongo. [Yohana 8:44]. Alidanganya alipomdanganya Hawa pale Edeni [Mwanzo 3:4], na amekuwa mdanganyifu tokea mwanzo. Kwa namna nyingine Yesu ni njia na kweli na uzima [Yohana 14:6]. Ukweli wa Yesu unafunua uongo wa shetani. Ukweli ni wa thamani kuishi kwao na ni wa thamani hata kufa kwa ajili ya ukweli. Uaminifu wetu kwa Kristo na kwa ukweli wake utaamua umilele wetu.

Somo letu la leo linafunua gharama waliyoamua kulipa vijana watatu wa Kiebrania kwa ajili ya ukweli. Kuliko kukubali bandia, kutomtii Mungu na kuangukia kwa uongo wa shetani waliweka maisha yao hatarini. Imani yao iliwaongoza kwenye tanuru la moto na kuwaletea ushindi mkubwa. Katika somo la leo tutagundua namna sisi wenyewe tunavyoweza kukabiliana na amri hii ya kifo wakati wa kufungwa kwa historia ya ulimwengu. Lakini kumbuka hii haiji mara moja tu, imepaliliwa kwa muda mrefu kuwa na uzoefu na mambo matakatifu na Mungu mwenyewe.

## Kupewa changamoto ya bandia.

Mfalme Nebukadneza alitengeneza kitu kilicho kinyume na tafsiri ya ndoto aliyoota na kupewa maana yake. Kwa kutengeneza hiyo sanamu aliiweka kwenye uwanda wa Dura nchini Babeli. Danieli 3:1. Unakumbuka Danieli sura ya pili Mungu alimpa Nebukadneza ndoto ya wakati ujao. Katika sura ya tatu mfalme anatengeneza sanamu yake kinyume na ile aliyoonyeshwa. Hii ni kinyume kabisa na Mungu alivyoonyesha juu ya wakati ujao. Mfalme Nebukadneza aliamua kujichukulia wakati ujao mikononi mwake mwenyewe.. Mungu alifunua kuwa wakati ujao siyo wa Babeli yenyewe kuna falme zingine lakini Nebukadneza hakutaka. Alisahau kuwa kuna fedha, shaba, chuma na kisha chuma na udongo na mwisho Jiwe. Alitamani Babeli iendelee milele. Na wengi wetu leo tunataka dunia hii iendelee milele lakini siyo mpango wa Mungu tena baada ya dhambi kuingia duniani humu.

Mfalme aliwaita wawakilishi kutoka pande zote za utawala wake. Amri ilikuwa ya dunia yote. Swala la kiini katika jambo hili ni juu ya ibada. Ibada ya kweli iligongana na ibada bandia. Katika tukio hili kwenye uwanda wa Dura utii kwa mfalme kuligongana na utii kwa Mungu wa kweli. Danieli 3:3-5. Mfalme alitoa na adhabu kwa ye yote ambaye hatatii amri hii. Danieli 3:6.

Tafadhali ona kuwa ukweli huu ulikuwa wazi sana. Mfalme mwenye nguvu sana duniani alitoa amri ya kifo kwa dunia yote. Swala la kiini hapa linahusu ibada. Adhabu kwa asiyetii amri hii ya mfalme mwenye nguvu ni kifo na mfalme amechanganya maswala ya serikali na kanisa na adhabu ni kifo.

Ni amri gani mahususi kama vijana hawa wa Kiebrania wangeamua kutii amri hii wangelivunja? Kutoka 20:3-6. Kitabu cha Ufunuo kinaelezea amri inayofanana kabisa na hii ambayo nayo itatangazwa wakati wa mwisho. Ufunuo 13:15-17 na ona kufanana kwa amri hizi:-

- ♦ Kwa kila sehemu mfalme mwenye nguvu wa dunia anatumia nguvu ya serikali kulazimisha
- Kwa kila sehemu, kiini cha tatizo kinahusiana na ibada.
- Kwa kila sehemu, adhabu ya mwisho ni kifo

Ni maelekezo gani ya hakika ambayo mtume Petro anatupa katika Matendo 5:29. "imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu." Kulingana na Warumi 13:1, wakristo wana wajibu kutii mamlaka yaliyopo. Tunapaswa kutii sheria za nchi. Lakini pamoja na hayo hakuna mamlaka ya duniani yaliyo na mamlaka ya kuingilia kati ya mtu na Mungu wake. Sheria za Mungu ziko juu ya sheria za serikali. Kama nchi yo yote itatoa sheria za kuwataka raia zake kuvunja sheria ya Mungu, watu wanawajibika kwa sheria ya juu ya Mungu.

Vijana hawa watatu wa Kiebrania waliwekwa sehemu ya kujaribiwa. Kushikilia utii wao kwa Mungu kulikuwa na maana ya kuwa kinyume na Nebkadneza.

**GHARAMA YA KUJITOA**

Vijana hawa wa Kiebrania walifanya uchaguzi gani? Danieli 3:16-18. Mwitikio wa Shadraki, Meshaki na Abednego ulikuwa mara moja. Biblia ya King James inasema, "We are not careful to answer thee in this matter, O King" (fungu la 18). Maana ya neno hili kwa kiingereza cha zamani ina maana ya hesitant. Hii ina maana hawakuksita au kuchelewa kujibu, maana kwa kufanya hivyo wangelimpa shetani nafasi kwa majaribu. Usalama wetu wakati wa majaribu ni kuchukua uamuzi kusimama kwa ajili ya ukweli.

**Nini matokeo ya uamuzi wao?** Danieli 3:19-21. Walitupwa kwenye tanuru la moto wakiwa wamefungwa sawasawa peke yao., walikabiliana na kifo.

# MATUKIO YA MWISHO YA KUFUNGA HISTORIA YA DUNIA

Yapo matukio muhimu 31 ya kufungia historia ya dunia hii na kila msafiri wa Mbinguni anapaswa kuyafahamu na kuyaelewa vizuri bila kuchanganyikiwa; nayo ni kama yafuatayo:-

1. Kanisa la masalio
2. Hukumu ya upelelezi
3. Ujumbe wa malaika watatu
4. Malaika wa nne
5. Mapigo saba ya mwisho
6. Amri ya Jumapili ya Taifa,
7. Amri ya Jumapili kwa mataifa yote
8. Mateso makali
9. Kilio kikuu
10. Mvua ya vuli na masika
11. Ukweli wa Sabato unaendelea
12. Kupepetwa na kutingishwa
13. Hukumu ya wenye haki
14. Wakati wa kuwekwa mhuri, mhuri wa mwisho
15. Alama ya Mnyama
16. UASI WA TAIFA UNAKAMILIKA
17. Uangamivu wa Taifa unafuata
18. Amri ya kuuwawa inatolewa
19. Amri ya kuuwawa inatekelezwa usiku wa manane
20. Wakati wa taabu
21. Arusi ya Mwanakondoo
22. Uamsho bandia
23. Shetani anamwiga Kristo
24. Sanamu ya Mnyama
25. Muunganiko wa watatu wakamilika
26. Kuanguka kwa Babeli kwa kamilika
27. Kufutwa kwa dhambi
28. Kufungwa kupimwa
29. Kuokolewa kwa watu wa Mungu
30. Kuja kwa Yesu mara ya pili
31. Dunia kufanywa ukiwa, miaka elfu kuanza

Matukio ya kufunga historia ya Dunia yameonyeshwa wazi wazi.

- matukio yanayounganisha na kufungwa kwa kupimwa na kazi ya maandalizi kwa wakati wa taabu yameonyeshwa wazi [GC 594].
- Katika unabii nyakati zijazo zimefunuliwa mbele yetu kwa uwazi kama ilivyofunuliwa kwa wanafunzi kwa maneno ya Kristo. [GC 594].
- Tunapaswa kujifunza alama kuu za njia zile ambazo zinaonyesha nyakati ambazo tunaishi

sasa. [OHC 340].

- Wale wote wanaojiweka wenyewe chini ya utawala wa Mungu... watakamata matukio yaliyoelezwa[yaliyowekwa wakfu] na Yeye ili kutukia. [7T14].
- Mungu ana watu katika ulimwengu ambao kwa imani na utakatifu, na matumaini wanafwatisha mzunguko wa unabii unaotimia haraka. [4T307].
- Ujumbe mzito ambao umetolewa kwa amri yao katika ufunuo, unapaswa uchukue nafasi ya kwanza kwenye akili za watu wa Mungu. Cho chote hakipaswi kuruhusiwa kuteka usikivu wetu. [8T302].
- Hatari kubwa inakaribia haraka, picha kubwa inaonyesha kwamba muda wa kutembelewa na Mungu umefika, wale wote wanaotembea nuruni wataona dalili za uangamivu zikikaribia.

**MATUKIO YA KUFUNGA HISTORIA YANAKUJA KWA UTARATIBU.**

- Nimeona kwamba nguvu za dunia sasa zinatikiswa na kwamba matukio yanakuja kwa utaratibu. [EW 41].
- Tutaona katika historia utimizo wa unabii ili kuelewa maendeleo ya matukio katika mapambano ya mataifa kwa pambano la mwisho la pambano kuu. [MH442].
- Katika Neno Lake, Mnyororo wa unabii unatuambia mahali tulipo sasa katika maendelezo ya vizazi na kile kinachotazamiwa. [Ed.178].
- Kwa kadri tunavyokaribia kufungwa kwa historia ya dunia, unabii unaohusiana na siku za mwisho, maalumu kabisa unadai kujifunza kwetu. [COL.133; EV. 151, PK 547].
- Sura ya 13 ya Ufunuo na mafungu matano ya kwanza ya sura ya 14 ni mnyororo unaounganisha wakati uliopita, uliopo na matukio yajayo mpaka ukombozi wa wale 144 elfu, na sasa fungu la 6 linatoa mnyororo mwingine wa matukio ambao unatuchukua mpaka kupita historia ya watu wa Mungu katika hali hii ya kufa.
- Tunapaswa kuishi na kutenda kwa utakatifu wote kwa kulingana na kuja kwa mwana wa Adamu [EW 58].

**Mkristo ana chati inayoonyesha kila alama ya njia ya safari ya mbinguni na hapaswi kubuni kitu cho chote [GC 598].**

1. Mwanzo wa hukumu ya upelelezi; Danieli 8:14 hii huenda mpaka mwaka 1844. Mwisho wa siku 2300.
2. Amri ya Jumapili ya Taifa
   (A) Alama ya Mnyama
   (B) sanamu ya Mnyama
   © Babeli umeanguka Ufunuo 13:11-17; 14:8- 12
3. Kufungwa kwa kupimwa. Danieli 12:1; Ufunuo 22:11
4. Kuja kwa Kristo mara ya pili Tito 2:13;Mathayo 24:14.

Kwa kila hatari kubwa ya Dunia, Mungu alituma ujumbe maalum ili kukabiliana na hatari hiyo. Ujumbe huu maalum ulikuwa “ukweli wa leo” kwa wakati huo ulitimiza haja maalum ya saa hiyo. 2 Petro 1:12

5. Miaka 120 kabla ya gharika Nuhu alitumwa na ujmbe [ukweli wa leo]. Wakati wa uasi

mkuu katika Israeli [Eliya alitumwa]. Ukweli wa leo. Kabla ya kuja kwa Yesu mara ya kwanza [Yohana Mbatizaji alitumwa]

6. Leo kabla tu ya mwisho wa dunia na kuja kwa Yesu mara ya pili- giza kuu la dunia yote, kuasi amri ya Mungu, kuthamini vitu [materialism] - kuabudu kiumbe badala ya Muumbaji [Kanisa la masalio] limetumwa na ukweli wa leo . Ufunuo 14:6-12; 18:1-4.

SDA ni mafundi wakiwa na mashine za kushonea, ujumbe kwa ulimwengu uliofilisika kwa maadili. Ujumbe huu maalumu wa mwisho wa onyo ni ujumbe wa malaika watatu wa Ufunuo 14:6-12 na 18:1-4. Huu ni ukweli wa leo. Huu ndio ujumbe husika; unaohusika sana, unaohitajika zaidi kuliko ujumbe wa kusisimua kwa ulimwengu wote.

Hili ni onyo la mwisho kwa ulimwengu. GC 603-612 linauandaa ulimwengu kwa mwisho wake na kuja kwa Kristo. Tukio linalofuatia ujumbe huu kutolewa ulimwenguni ni kuja kwa Yesu mara ya pili. Ufunuo 14:14 kanisa pekee katika dunia hii la kutoa ujumbe huu kwa ulimwengu ni kanisa la Maslio. Kanisa la Waadventista wa Sabato. Na tunato kwa zaidi ya lugha 11,000 na kabila.

# UJUMBE WA MALAIKA WATATU.UFUNUO 14:6-12;18:1-4

- Ulianza mwaka 1844 Yesu alipoingia patakatifu pa patakatifu EW 254.
- Unajumuisha ujumbe wa malaika wa kwanza na wa pili Ufunuo 14_6-8 ; 8T197.
- Unagawanya ngano na magugu na kuweka mhuri. EW 118; GC 379.
- Unakoma wakati wa kupimwa unapoisha GC 613.
- Ujumbe wa kuogofya sana kuliko yote unaobana ambao haujawahi kutolewa kwa watu wenye kufa unaoonekana kwa ujumbe wa malaika wa tatu. GC 449.
- Ujumbe wa malaika wa tatu unahusisha onyo la mwisho kutolewa kwa wote wakaao juu ya nchi. GC 604.
- Ujumbe huu ni wa mwisho ambao umewahi kutolewa kwa ulimwengu na utamaliza kazi yake GC 390. Ujumbe huu utakapokwishatolewa Yesu atakuja. Ufunuo 14:6-14; 5T 206,207.
- Ujumbe wa malaika watatu utatingisha dunia hii kwa misingi yake hasa, ulimwengu wote utaangazwa kwa utukufu wa ujumbe wa malaika watatu. Dunia yote itajua kuwa kanisa la Waadventista wa Sabato ni kanisa la kweli na siku ya Saba ndiyo Sabato ya kweli. Ufunuo 18:1-4.
- Ujumbe wa malaika watatu utaiangaza dunia kwa utukufu wake, lakini wale tu waliosimama na kushinda majaribu kwa uwezo wa aliye Mkuu wataruhusiwa kuchukua nafasi katika kuutangaza wakati utakapofikia kiwango cha kilio kikuu. RH. NOV. 19,1908.

# MAANDALIZI KWA HATARI YA MWISHO

Leo ulimwengu unajikuta wenyewe ukiwa karibu na mwisho wa matukio marefu ya historia. Mungu amewapendelea watu wake na mafunuo ya ajabu ya kiunabii ya saa tunayoishi kwayo, akionyesha maendeleo ya mipango ya mbingu na kuonyesha matukio makubwa ya wakati ujao. Baadhi ya maujumbe haya aliyatoa kupitia kwa kalamu iliyovuviwa ya Ellen G. White. Yamekuza unabii wa Biblia, yanafungua mbele yetu mfululizo wa matukio yanayokuja na kututak kupata maandalizi tunayotakiwa kwa hatari kubwa inayokaribia.

**TUKIUJUA WAKATI**

Paulo alisema kwa hakika: "naam tukiujua wakati, kwamba saa ya kuamka katika usingizi imekwisha kuwadia; kwa maana wokovu wetu u karibu nasi kuliko tulipoanza kuamini(Warumi 13:11). Maneno haya yanatumika kwa nguvu ya pekee kwa watu wa marejeo.

Wakati ulimwengu unapotetemeka kwa hofu kwa kile kitakachoupata kesho, tunapaswa kuujua wakati. Kila msafiri wa kimataifa anabeba ratiba na ramani. Anajua ni sehemu gani ya safari

ameshamaliza tayari na vituo gani vimebaki kumalia safari nzima. Anajua kabla ya siku inayofuata na saa ya kufika uwanja wa ndege.

Kwa uangalifu wake na usikivu kwa maelezo, ratiba yake inafanya kazi kwa usahihi. Wana wa Mung kwa safari yao ya kushangaza kwa goli la mwisho, vile vile ina ramani nzuri kuliko zote, Biblia na ratiba yenye usahihi uvuvio wa unabii.

**HATUA ZILIZOKAMILIKA TAYARI**

Kwa kuangalia nyuma, wanaminifu wanapata ujasiri wakati wanapotazama namna mautabiri yalitofanywa maelfu ya miaka iliyopita yalivtotimia kwa usahihi bila kukosea. Himaya nne za zamani zilivyoinuka na kupotea kama ilivyotangulia kusemwa katika unabii wa Danieli 2 na 7. Himaya ya chuma ya Rumi iligawanyika kufanya mataifa ya Ulaya ya leo (UK), ambayo leo yamebakia mgawanyiko licha ya majaribio yote ya kuyaunganisha- kama mfano wa chuma na udongo katika nyayo na vidole katika sanamu.

Miaka 1260 ya utawala wa upapa, sasa ni historia, inasimama kama ushahidi mwingine wa uhakika wa karama ya unabii wa milele. Moja ya kichwa cha mnyama wa kwanza wa Ufunuo 13 kilipata jeraha la mauti, lakini vile vile lilipona- yote kama unabii wa mbingu ulivyosema. Leo tunashuhudia utimizo wa sehemu ya mwisho ya unabii ule kama tunavyoona ulimwengu wote ukimstajabia mnyama huyu. Kutokea utabiri wa muda mrefu na wa kugusa sana wa Biblia , siku 2300 za Daniel 8:14, pamoja na majuma yake 70 yanayokuwepo pamoja kwa sura ya 9, yamekuwa kweli kwa usahihi tena kwa mshangao. Kurudi kwa Wayahudi toka Uajemi kwenda Yerusalemu kujengwa upya kwa mji na kuta zake, ubatizo wa Yesu na kifo cha Mwokozi juu ya msalaba wa Kalvari, vilitokea kwa utaratibu sahihi wa mahesabu kama uvuvio ulivyokwisha sema.

Na wakati wa mwisho wa kufungwa kipindi hiki ulipowadia, moja ya tukio kubwa kuliko yote la unabii lilichukua nafasi. Kwa utimizo wa unabii wa Danieli 8 na 9 na 14, miondoko ya Uadventista uliinuka kwa wakati halisi kuhubiri ujumbe wa hukumu na Injili ya milele katika hali yake ya

kisasa. "ukwel iwa leo".

Ishara katika mbingu zilizotabiriwa na Bwana Yesu katika hubiri lake la kiunabii miaka elfu mbili iliyopita- jua kutiwa giza na mwezi kutotoa mwanga wake na nyota kuanguka vilikuja kutokea na kupita zaidi ya karne iliyopita. Hali ya jamii leo, siasa, na ulimwengu wa kidini vinatimiza unabii wa Biblia kwa maonyesho ya uhakika. Maongezeko ya uzinzi na uasherati pamoja na uhalifu, woga ambao unakausha mioyo ya wanadamu, vita na tetesi za vita, maongezeko ya matetemeko ya ardhi ya mara kwa mara, manabii wa uongo na dini za kujifanya, ishara na maajabu vikikamilishwa kwa nguvu za adui; yote haya yanatangaza kwamba tunaishi saa ya mwisho, wakati ambako kanisa na dunia vitashuhudia matukio makubwa katika historia.

Kukua kwa maajabu katika ufahamu wa kisayansi kwa kasi kwamba mauvumbuzi yasiyo ya kawaida au magunduzi haya mshangazi ye yote sasa. Miondoko ya mwendo kasi ya safari, vikiendeshwa na mtu wa kisasa na kuteka nafasi vnnatimiza utabiri wa nabii Daniel kwamba maarifa yataongezeka na watu watakimbia huku na huko. Daniel 12:4

Mtazamo wa nyuma kwa maneno mengine unatushawishi kwamba unabii wa Biblia umetimia kwa utaratibu wa kushangaza; kwamba unabii wake wa muda mrefu ukiishia mwaka 1844 na kwamba sasa ni matukio tu ya siku za mwisho yakifika kileleni kwa kurudi kwa Yesu kwa utukufu katika mawingu ya mbingu kunakotungojea. Lakini kabla ya waliokombolewa wa Mungu kufikia lengo lao la kutamanika, Neno la Mungu na ushuhuda wa unabii unaelekeza kwamba matukio mchanganyiko yakikuzwa sana yatakuja haraka sana na kupita kwa haraka yakifuatana; matukio ambayo yatalirusha kanisa lifike katikati ya hatari kubwa (catapult).

**Catapult = chombo cha kurushia ndege katika manowari au ndege nyingine. Kwa sababu ya hili kila muumini binafsi anahitaji maandalizi maalumu.**

Wakati uliopita unatupa uhakika na ujasiri wa wakati ujao. Usahihi wa kila tukio katika unabii umetimia wakati wetu, unatuhakikishia kuwa wakati ujao nao utakuja na kupita kama ulivyotabiriwa. Njia ya ajabu ambayo Mungu aliwaongoza na kuwalinda watu wake kupitia vizazi, akitawala mipango ya nguvu za mwovu inaonysha kwamba kanisa sasa katika pambano litaendelea kulindwa mpaka litakapokuwa kanisa katika ushindi. (Hatuna haja ya kuogopa cho chote kwa wakati ujao labda tu kama tumesahau njia ambayo Bwana alituongoza kwayo, na mafundisho yake ya historia yetu iliyopita." LS 196.

**PICHA YA WAKATI UJAO**

Kwa matumaini haya, kwa uhakika huu, hebu sasa tupekue kwa haraka wakati ujao, tupanue ugo wetu mbali mpaka kuja kwa Kristo. Hebu tutazame kwa picha maono, tuchukue matukio ambayo yatatukabili kama watu mpaka siku ya mwisho ya ukombozi wetu wa mwisho. Katika sura zifuatazo tutaona matukio haya kwa undani kama yalivyoelezwa kwa maneno yaliyovuviwa. Lakini kwanza ufupisho- mtazamo kwa ujumla wa yote. Hili litatusaidia tujenge uhusiano sahihi kati ya moja na jingine.

Kabla ya muda wa kupimwa kukoma, wakati watu bado wanaweza wakakubali nafasi iliyotolewa ya Injili, matukio yafuatayo yatatokea:-

- Kutiwa muhuri
- Mvua ya masika
- Kilio kikuu
- Kumalizika kwa kazi
- Wakati wa kutingishwa

Kuorodhesha matukio haya kwa mpango hakuna maana kwamba yatatokea kwa mfuatano huo. Baadhi au yote yanaweza yakatokea kwa wakati mmoja. Tunajua kwamba wakati wa amri ya Ufunuo 22:11 ikitamkwa, na muda wa kupimwa kufungwa, matukio haya yatakuwa nayo yamekwisha. Kwa hali hiyo njia itakuwa imesafishwa kwa kuanza wakati wa taabu kuu.

Lakini kwa kuunga mkono matukio haya katika hali ya maandalizi ya njia yake, kutatokea ndani ya kania la Mungu miondoko ya kweili ya matengenezo. Kwa sehemu kubwa yatakuja kama matokeo ya ujumbe wa Shahidi wa kweli kwa Laodikia na kwa ufahamu wa kanisa na mapokezi ya somo kuu la haki kwa imani. Hili litasababisha mwamko wa kiroho na kufanywa upya kwa maisha. Litaharakisha kumwangwa kwa mvua ya masika na kutangazwa kwa ujumbe wa kuandaa watu kwa wakati wa taabu na kutokea kwa utkufu wa Kristo.

**KUWEKWA MUHURI**

Ili kwamba aweze kuandaa watoto wake kwa ajili ya wakati wa taabu, Mungu anatamani kuwaweka alama, mhuri wa amri yake, wa tabia yake na ukamilifu wake. Tukio linalofanyika sasa karibuni litamalizika. Kwa ukweli ni kuwa kuwekwa mhuri kunahusiana na mtu binafsi na linaweza kuelezwa kwamba linamalizika pamoja na kipindi cha kupimwa; kwamba ni wakati wa kifo cha muumini au mwisho wa hukumu ya upelelezi. Ni wale tu wanaojiandaa ndio watawekwa mhuri, na ni wale tu waliowekwa mhuri watapita kwa ushindi wakati wa taabu na kuingia mbele za Bwana wakati wa kuja kwake mara ya pili. Maanadalizi yanahusisha kutakaswa kutoka dhambini na ushindi juu ya kila udhaifu na kila kasoro.

Mvua ya Masika, Kilio kikuu na kumalizika kazi, kuharakisha kwa kukamilisha kwa utume wa Injili, Mungu anatamani kuwamwagia watu wake mvua ya masika ya Roho Mtakatifu. Kama vile mvua ya vuli ilivyoliandaa kanisa la mitume kutangaza habari njema ya wokovu kwa mafanikio na ufanisi kwa sehemu zote za ulimwengu wao, hivyo huku kumwagwa kwa nguvu ya mbingu kutawezesha watu wa Mungu leo kumaliza kazi iliyobakia na kufikia kila taifa, kabila, lugha na watu kwa ujumbe wa mwisho wa Injili. Ahadi ya mvua ya masika ni leo si kwa kesho au wakati fulani baadaye.

Lakini sharti la masharti kabla ya utimizo ni kwamba sehemu kubwa sana ya washiriki wa kanisa wajitoe wakfu wenyewe kamili kwa Mungu, wajikane nafsi, wakatae dhambi kwa kila hali, na kumtafuta Bwana kwa unyenyekeve. Kwa muda mfupi kilio kikuu cccha ujumbe wa mwisho lazima kitolewe. Kikiongozana na maonyesho ya nguvu za mbingu, dunia itaangazwa kwa utukufu wa Bwana na kazi itamalizika kulingana na mpango wa ahadi ya Mungu. Ufunuo 18:1-4

Tukio maalumu la matengenezo na utakaso vitahitajika miongoni mwa ngazi za kanisa, ambako kutaathiri sehemu kubwa ya washiriki kwa maandalizi ya mvua ya masika, kilio kikuu na kumaliza kazi ya Injili.

**KUTINGISHWA**

Kutingishwa ni tukio linguine kubwa ambalo litaleta athari kwa kanisa wakati wa kipindi cha rehema. Msamiati huu unasema kuwa baadhi ya wale ambao wamehesabiwa miongoni mwa watu wa Mungu wataasi. Wengi Waadventista wataachia ngazi kwa sababu hawakukubali kwa mioyo yao yote wito wa mbingu kuongoka na kujiweka wakfu kamili, na kwa sababu walikataa ujumbe wa Kristo kwa kanisa la Laodikia, ujumbe wa kutubu na matengenezo ya maisha, walidumisha tu mtindo wa uzoefu wa juu juu tu. (kujifanya).

Wakati wa hatari kubwa kwa kanisa ukifika na mateso kuanza na kusukumwa na amri ya jumla ya Jumapili, wengi watatoka, na baadhi yao watakuwa maadui zetu wabaya sana. Ni kujitoa kamili kwa maisha tu kwa Mungu na uzoefu wa kuendelea wa kukua katika neema kutakuwa usalama wetu kwa hatari hii kubwa na itatufanya tudumu kuwa na umoja na jeshi la waliojiweka wakfu wanaume na wanawake ambao watashinda kwa utukufu Kristo atakapotokea.

**WAKATI WA TAABU WA MWANZO**

Saa za mwisho za kipindi cha kupimwa zitakuwa za tufani sana na ngumu kwa ulimwengu kwa ujumla; na vile vile kwa watoto wa Mungu. Katika ulimwengu, hata wakati bado malaika 4 wanashikilia pepo, vita, machafuko, matatizo ya kisiasa, uchumi na huzuni za jamii, kutengana na mfarakano wa familia, hofu na woga vitaongezeka. Serikali japo zitajitahidi sana hazitaweza kupelekana na matatizo yenye kuchanganya yakiwakabili. Wakati huu wa mwanzo wa taabu ambao Yesu aliuelezea kwa Luka 21:25 unakuja kabla ya wakati wa taabu kuu ambao utaanza mara tu baada ya kufungwa kipindi cha kupimwa.

Kwa watu wa Mungu kipindi cha mwanzo cha taabu kitakuwa na mateso makali ambako watapambana na nguvu za uasi. Pamoja nahayo, Mungu atakuwa pamoja nao kuwaimarisha na kuwasaidia kuishi kwa ushindi na kuteseka kwa furaha kwa ajili yake. “Kwa kuwa umelishika neno la subira yangu, mimi name nitakulinda utoke katika saa ya kujaribiwa iliyo tayari kuujia ulimwengu wote kuwajaribu wakaao juu ya nchi, naja upesi shika sana ulicho nacho, asije mtu akaitwaa taji yako.” Ufunuo 3:10, 11.

**MATESO**

Ufunuo 13:11-17 inatoa maelezo ya kiunabii juu ya mateso; ambako Roho ya Unabii imeelezea kwa uwazi. Mateso haya yataanza kabla ya kufungwa kwa kipindi cha kupimwa na yatakuwa makali zaidi baadaye, maalumu kabisa wakati wa taabu ya Yakobo. Lakini saa ya kukombolewa itafika.

Mnyama wa pili wa Ufunuo 13 yeye aliye na pembe kama mwanakondoo, anawakilisha Marekani (USA), taifa change, linaloundwa na watu wanaopenda uhuru, chi ya kidemokrasia ikiongozwa na katiba mfano, usalama unaovutia wa haki za binadamu na uhuru, maalumu uhuru wa nia na mawazo ya watu. Nchi hii imetimiza na inaendelea kutimiza ukweli wa utume wa kihistoria. Kwa kupata mafanikio ya juu sana ya uhuru wa dini kwa marekebisho ya kwanza kwa katiba yake ambayo inakataza utungaji sheria kwa kogress juu ya maswala ya dini, imeunda mtengano kamili na unaoheshimiwa kati ya dini na serikali na imekuwa kinga ya uhuru wa nia ya mawazo. Kwa sababu ya pwani zake nzuri, wanaume na wanawake wanaoteswa wamepokelewa toka sehemu zote za ulimwengu wakitafuta makimbilio chini ya mfumo wenye uhakika wa kisiasa.

Kwa sababu ya uongozi wa Mungu, alichagua USA ambako ameunda makao makuu ya ulimwengu kwa kanisa la Waadventista wa Sabato. Bila kusukumwa wamisionari wamekuwa wakitoka kwenda duniani kote miaka baada ya maiaka na kuchukua ujumbe wa malaika watatu. Pamoja na hayo, unabii unathibitisha kuwa nchi hii inawakilishwa na mnyama kama kondoo itabadilisha hali yake kabisa na kwa matokeo yake itafanya haya yafuatayo

1. Itanena kama Joka: fungu la 11 na Joka wa Ufunuo 12 ni nguvu inayotesa.
2. Itawalazimisha wote wakaao juu ya nchi kumsujudu mnyama wa kwanza, hii ni kusema Rumi. Itawalazimisha wanadamu wote kutii nguvu ya dini na tabia ya kidini. Hii itafuta uhuru wote wa dini uliotunzwa mpaka sasa na kufungua mateso na msuguano
3. Itafanya maajabu makubwa ya kudanganya hata kufanya moto kushuka toka mbinguni. Fungu la 13,14. Hili litawezekana kwa sababu ya nguvu ya ziada isiyo ya kawaida ya umizimu na kwa sababu ya kuungana na Uprotestant na Ukatoliki
4. Itawaamuru wote wakaao juu ya nchi kufanya sanamu kwa mnyama wa kwanza wa Ufunuo 13, hii ina maana kwa nguvu ya Rumi. Fungu la 4. Kwa vile mnyama huyu anawatesa watakatifu, sanamu kwa mnyama itakuwa ni nguvu nyingine inayofanya jambo hilo. Sanamu hii kwa mnyama kama tutakavyoona kwa sura zifuatazo ni shirikisho la makanisa ya Uprotestanti ambayo mwishoni yataasi na kuungana kwa kudai kutoka kwa nguvu ya serikali kulazimisha sheria ya dini
5. Itasababisha wote kupokea alama ya mnyama kwa kumkataza ye yote asiuze au kununua mpaka awe nayo. Fungu la 16,17. Japokuwa si wote kuhusiana na swala hili wanalielewa bado, hata hivyo halitaeleweka mpaka gombo litakapozungushwa. "Alama ya mnyama ni sawa kabisa kama lilivyotangazwa kuwa litakuwa." 6T17. "Alama ya mnyama ni… kutunza siku ya kwanza ya juma. 8T117."

   Kwa kuwa alama au mhuri wa Mungu ni sheria ya mbingu, na maalumu kabisa Sabato, siku ya kweli ya kupumzika, alama ya mnyama lazima iwe siku ya uongo ya kupumzika. Tunajua kwamba kutunza Sabato kwa kupatana na amri ya nne inashuhudia utii wetu kwa Mungu kama Muumba na Mkombozi wetu na kwa serikali yake. Kwa hali hiyo hiyo ulazimishaji wa kutunza Jumapili (siku ya jua) ambao utakuwa wa dunia yote ukilazimishwa na sanamu ya mnyama na nguvu zingine za uasi, kwa upana fulani ni alama ya mnyama au alama ya utii kwa nguvu ya uongo ambayo ni adui wa Mungu na ukweli.

Mwishoni kabisa kiini cha vita kuu nay a muda mrefu kati ya ukweli na uongo, kati ya Kristo na Shetani itakuwa utunzaji au uasi wa siku ya kweli ya kupumzika. Wale wote watakaokataa kukubali alama ya mnyama, wote watakaokataa kutunza Jumapili au kushiriki katika matendo ya kuabudu sabato hiyo ya uasi watateswa, watakanwa na ulinzi wa kiserikali. Ulinzi wa kikatiba utaondolewa kwao na wataondolewa haki zote muhimu hata zile za haki za msingi za maisha kama vile kuuza na kununua.

Kabla ya wakati wa kupimwa kukoma, Marekani (USA) itapitisha amri ya Jumapili. Kwa sababu hii kitaanza kipindi cha majaribu makuu kwa kanisa, hatari kubwa sana katika historia yake. Leo amri za kufanya pumziko la Jumapili liwe halali linaonekana kuwa la kijamii na tabia ya kiafya na kuruhusiwa kufanya vinginevyo. Watu wanaofanya hivyo wanasisitiza kwamba wamebadilisha matakwa yote ya kidini. Sheria za namna hii zimeenea pote katika muungano, lakini punde sheria hizi zitalazimishwa kwa taifa lote na shirikisho la utungaji sheria. Agizo hili

litaonekana la kidini, likihusisha kwa namna fulani kama tendo la ibada ambalo litaasi siku ya kweli ya pumziko. Kupitishwa kwake kutadaiwa na sanamu ya mnyama (muunganiko wa Uprotestanti ulioasi na serikali), ukiungwa kamili na Ukatoliki na umizimu. Hili litaanzisha mateso makubwa.

Miondoko hii itaenea punde kwa nchi zingine za ulimwengu ambapo amri za namna hiyo zitatekelezwa, hivyo kufanya mgandamizo wa watunza Sabato wachache kuwa wa dunia yote. Hii itakuwa ni ishara kwa watoto wa Mungu ambao bado wanaishi kwenye miji mikubwa kuondoka na wale walio kwenye miji midogo kuandaa kuondoka mara. Wakati mapigo saba yatakapoanza kumwagwa, hii ina maana baada ya kipindi cha kupimwa kufungwa, au wakati wa taabu kubwa, tukio linalofuata kwenye mfuatano.

6. Sanamu ya mnyama itajaribu kuwaua wote ambao hawaabudu mnyama na sanamu yake. Fungu la 15. Amri ya kuuwawa itatolewa dhidi ya wote wanaotunza Sabato. Wataonekana kama maadui wa sheria na amri na chanzo cha matatizo yote yanayotokea duniani yaani mapigo. Tarehe maalumu ya kutekelezwa amri itawekwa. Wakati hili litakapotangazwa, watoto wa Mungu watakimbia toka kwa vituo vyote vilivyo na watu, hii ni pamoja na miji midogo, na watatafuta makimbilio misituni, majangwa na sehemu za miamba, mahali ambapo watafurahia ulinzi maalumu wa Mungu. Malaika wa mbingu watawahudumia kwa chakula. Wakati huu utakuwa wa taabu kubwa ambayo waaminifu watamlilia Mungu bila kukoma ili wakombolewe.

Nguvu zitajiunga kwenye vita dhidi ya Mungu, ukweli wake na watu wake, nguvu hizo zitakuwa Joka, mnyama na nabii wa uongo. Ufunuo 16:13. Joka anamwakilisha shetani, katika hali hii atafanya kazi kwa njia ya umizimu kwa hali zake zote za kipagani. (Kwa kuabudiwa na miujiza). Ukristo, hii ikimaanisha muunganiko wa Uprotestanti na Ukatoliki wakiabudu kwa njia ya miujiza na katika msingi wa kawaida wa kukubali fundisho la hali ya roho kuishi baada ya kufa, nk. Mnyama anasimama badala ya upapa au kanisa la Kiroma la Kikatoliki; na nabii wa uongo ni uprotestanti ulioasi na kwa vile uprotestanti pamoja naupapa utafany kazi kwa karibu na mapatano na serikali utalazimisha sheria za tabia za dini. Na muunganiko huu wa kanisa na serikali utaenea duniani kote.

**ARMAKEDONIA:** Tendo litakalofuatia katika mfululizo wa matukio litakuwa ni vita ya Harmakedonia. Vita ya mwisho kati ya wema na uovu kama ilivyoelezewa kwenye pigo la sita. Nabii aliona ikitoka katika mdomo wa Joka (umizimu), mnyama (upapa) na nabii wa uongo (uprotestanti ulioasi), roho tatu za uchafu ambazo ni za mashetani, ambazo zitafanya ishara kubwa kudanganya na zitaenda kwa wafalme wa dunia kuwafanya wapigane vita hii ya mwisho dhidi ya Mungu, watu wake na ukweli wake. Ufunuo 16:12-14. Wakati mateso yatakoma, waaminifu watakuwa katika ulinzi maalumu wa Bwana na malaika zake watakatifu. Katika kukimbia kwao kwa mwisho kwa dharura toka mijini watashambuliwa na majeshi yaliyojipanga, lakini maupanga yalitoinuka kwa ajili yao yataanguka bila nguvu yo yote kama majani makavu. Malaika watawatetea kama wapiganaji hodari. Kwa njia ya miujiza, maji na mkate vitatolewa kwa ajili yao jangwani.

Siku hiyo hiyo iliyopangwa ya kutekeleza amri ya kifo; Bwana atawakomboa waaminifu. Atawadhoofisha waovu kwa mwondoko mkuu sana mawinginu na duniani na kwa maonyesho yasiyo ya kawaida kabisa kwa vitu vya asili. Katikati ya kuchanganyikiwa na ghadhabu, wapiganaji hawa wataanza kupigana miongoni mwao wenyewe wakiharibiana wenyewe. Wakati huu sauti ya Mungu inasikika, ufufuo wa pekee unatokea, na muda kitambo baada ya hili kuonekana kwa Mwana wa Mungu katika utukufu unatokea mawinguni.

**WAKATI WA TAABU.**

Wakati huu unaelezewa kwenye kitabu cha Danieli 12:1. "Wakati huo Mikaeli atasimama, Jemedari mkuu asimamaye upande wa wana wa watu wako; na kutakuwapo na wakati wa taabu, mfano wake haukuwapo tangu lilipoanza kuwapo taifa hata wakati uo huo; na wakati huo watu wako wataokolewa; kila mmoja atakayeonekana ameandikwa katika kitabu kile."

Hili linaanza wakati wa kupimwa. Kutingishwa kumesitishwa. Kuburudishwa toka kwa kuwako Mungu wakati wa mvua ya masika kumeshuka. Kuhubiriwa kwa Injili kumekamilika. Ndipo sasa Mikaeli, yaani Kristo, Jemadari mkuu ambaye anafanya upatanisho kwa ajili yetu kwenye hekalu la mbinguni "atasimama" (stand up) na kuacha kazi yake ya upatanisho. Atavua vazi lake la ukuhani na kuvaa joho la kifalme. Hekalu la mbinguni litajaa moshi, na hakuna awezaye kuingia ndani yake.

Malaika wane wa Ufunuo 7, ambao walikuwa wanashikilia pepo zisivume sasa wataziachilia. Watu waovu wasioweza kuzuiliwa watakuwa na hasira asiyoweza kuzuia mtu, wana uchu. Na mapigo saba ya mwisho yatamwagwa juu ya wasio haki. Huu utakuwa muda wa maumivu makali sana kwa ulimwengu. Mapigo ambayo mwanadamu hajawahi kuyaona yataijaza nchi. Lakini kwa ukweli kwamba mapigo haya hayatakuwa ya dunia yote, ulimwengu wote utaangamizwa.

Japokuwa wana wa Mungu watakuwa wakilindwa kutoka kwa mapigo, lakini vile vile kwao kutakuwa na wakati wa taabu isiyoelezeka; kwa njia mbili. Moja, itakuwa ni wakati wa taabu ya vifaa kwa sababu ya kukimbizwa kwa mateso. Wengine watapoteza uhuru wao na kupitia siku kadhaa jela. Hesabu kubwa ya wao watakuwa wakitembea kwa kuchoka kwenda sehemu kadhaa za maficho. Japo wakikingwa na kutetewa na malaika watakatifu ambao kuwepo kwao kutabadilisha jela ziwe makao ya nuru, lakini watapitia kipindi kigumu cha kimwili.

Lakini vile vile watateseka kiakili na mistuko. Wakati huu hawatakuwa na mwombezi. Kama watakuwa na dhambi yo yote ambayo haikuungamwa au kusamehewa uovu wo wote katika maisha yao, watashindwa kabisa. Watapitia saa isiyoeleweka na mateso. Kwa kitambo kidogo wataona kana kwamba hawana uhakika kwamba dhambi zao zote zimefutwa. Kama Yakobo usiku ule kwenye kivuko cha Yaboki; watanyenyekesha mioyo yao mbele za Mungu.

Japokuwa imani zao zinapimwa vikali sana, wanaimarishwa na uzoefu usio wa kawaida. Hatimaye maombi yao yanajibiwa na wanapata amani. Hawakumbuki dhambi yo yote ambayo haikuungamwa na kutubiwa. Kabla ya kufungwa kipindi cha kupimwa, kwa nguvu ya mbingu walipata ushindi juu ya uovu na wametiwa mhuri. Wokovu wao umehakikishwa.

**KATI YA KUWEKWA HURU NA KUJA KWA KRISTO MARA YA PILI**

Wakati wa kuingilia kati kwa utukufu kwa Mungu ambako kutawalemaza waovu kwa majaribu yao ya kutaka kuwaangamiza waaminifu, jua litachomoza usiku wa manane na woga

(hofu kuu) inaonekana isiyo ya kawaida itatokea. Bahari itachemka na kuvimba na tetemeko kuu la kutisha likisababisha majumba makubwa kusambaratika na kuangamia. Hapa ndipo sehemu ya ufufuo itatokea. Makaburi yatafunguka na watakatifu wengi watafufuka kushuhudia kuja kwa Kristo, lakini maalumu kabisa wale waliokufa katika imani ya ujumbe wa malaika watatu. Danieli 12:2; Ufunuo 1:7. Vile vile wale waliomchoma Bwana Yesu watatoka makaburini mwao na vile vile wale maadui wakubwa wa ukweli. Ufunuo 1:7

Wakati waovu wana hofu kamili, watakatifu watashangilia; "Tazama huyu ndiye Mungu wetu ndiye tuliye mngoje, na tushangilie na kuufurahia wokovu wake." Isaya 25:9.

Wanaopotea watakapogundua kuwa wamedanganywa, wataanza kulaumiana kila mmoja na mwenzake. Maalumu kabisa watawalaumu wachungaji wa uongo wa kundi. Na maupanga waliyokusudia kutumia dhidi ya watakatifu watayatumia dhidi yao wenyewe. Mara mashambulizi haya yanageuka dhidi ya kanisa kuu, dhidi ya Babeli. Ufunuo 17:16, ambalo litaharibiwa na kukatwa vipande vipande. Kwa kuunganisha na matukio haya sauti ya Mungu inatangaza siku na saa ya kuja kwa Kristo.

**KUONEKANA KWA KRISTO KWA UTUKUFU**

Hatua ya mwisho ya vizazi vyote imefika, wakati ambao kwa muda mrefu umetanguliwa na manabii. Wingu dogo jeusi linaonekana mawinguni, na kwa kadri linavyokaribia linakuwa angavu zaidi na kung'aa zaidi, hatimaaye linaonekana kuwa ni kundi la malaika ambao wamemsindikiza Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana katika msafara wa ushindi kuja duniani. Kristo anakuja akiwa amezungukwa na miale ya moto. Mbingu zitakujnwa nyuma kama kurasa. Nchi inatetemeka. Milima inaondolewa.

Wakati msafara huu mkuu wa mbingu unavyozidi kukaribia, tetemeko la ardhi lenye nguvu sana linaitetemesha dunia, na sauti ya Kristo inaamsha watakatifu waliolala kuishi bila kufa tena. Watakatifu walio hai wanabadilishwa. Wale waovu wanaoishi bado wanaangamizwa na utukufu mkuu wa mbingu.

Muda mrefu wa kungojea umekoma. Usiku wa mateso umegeuka mwishoni kuwa wa utukufu. Na sasa familia yote ya Mungu duniani, waliokombolewa na damu ya thamani ya Mwana kondoo wanaungana na mpendwa wao na Bwana wao na Baba yao wa mbinguni. Maelfu ya miaka ya matumaini yametimizwa kwa asubuhi moja ya milele ya ushindi halisi. **<u>Wewe na mimi lazima tuwe pale.</u>**

**Sasa ndio siku ya utakaso, kesho itakuwa ile ya utukufu.**

**REJEA:**

1. White G. Ellen, Pambano kuu

___________, Early Writings

# SEMINA YA WAHUBIRI MASTER GUIDES
# KANUNI ZA MAHUBIRI NA PR. JOHN KIMBUTE

# UTANGULIZI

**A: Hatari kubwa kuliko zote katika Uadventista.**

1. Kiini cha ibada cha Waadventista Wa Sabato: sherehe au kutangaza?
2. Mashauri ya hivi karibuni toka kwa washiriki.
3. Je, shetani ameingilia kuhubiri kwa Waadventista Wa Sabato? Kiini cha ujumbe dhidi ya matatizo ya pembeni.

B: **Safari yangu pekee katika kuhubiri**.

1. Semina hii ni akisi yangu mwenyewe katika kuhubiri. Nimefikiria namna ninavyofanya.
2. Hatuzaliwi wahubiri. Mungu anatuita na kutufanya wahubiri. Wanafunzi wa Yesu walikuwa wanyenyekevu, wasio wasomi, na watu wa kawaida, lakini wakawa wahubiri wenye nguvu sana.
3. Njia iliyo nzuri kuliko zote ya kujifunza kuhubiri ni kuhubiri. Huwezi kujifunza kuogelea mpaka uwe umejitupa ndani ya maji.

C: **Umuhimu wa kuhubiri**.

1. Kanisa ni kama hoteli:

1. Mungu ndiye mpishi mkuu [chef]
2. Biblia ndiyo chakula [food]
3. Washiriki ndio wateja [client]
4. Mhubiri ni mhudumu [waiter]

2. **Watu wanaangalia nini hotelini?**

a. Hali ya hewa ya kupendeza
b. Mhudumu mzuri
c. Bei nzuri na yenye thamani
d. Wepesi wa kuhudumiwa
e. Zaidi ya yote ni chakula kizuri
f. Nyumba iliyo nzuri

Chakula kinapokuwa kizuri watu hawampi sifa mhudumu ila mpishi. Chote wanachofanya wahubiri ni kutoa chakula cha Mungu na utukufu ni kwa Mungu [mpishi]. Tunatakiwa kutoa chakula cha Mungu siyo kukifanya! Ukweli ni kuwa tunatakiwa tuwe waangalifu sana siyo kubadilisha chakula chetu badala ya chakula cha Mungu-hatuwezi kukifanya kiwe kitamu kuliko alivyokifanya! Kuwa mwangalifu sana juu ya kuwalisha watu wa Mungu takataka za chakula cha kiroho

Mhubiri ni kama taa. Lazima apate mafuta ya dhahabu ili kwamba aweze kutoa mwanga. Mhubiri ni mfereji tu.

Mfereji hautengenezi mafuta, unahakikisha unayapata kutoka kwa chanzo na kuyapeleka kunakotakiwa. Ole wa mhubiri anayeziba bomba kwa mawazo yake mwenyewe na kanuni zake na kwa hali hiyo kuwaacha watu gizani.!

**BIBLIA NA KUHUBIRI.**

a. 2 Timotheo 4:1-5- Lihubiri Neno, kwa nini?
2. 1 Korintho 1:19-27. Upumbavu wa kuhubiri
3. 2 Timotheo 2:15. Ligawe Neno kwa halali
4. 1Korintho 9:16. Ole wetu kama hatukuhubiri Injili.
5. Yeremia 20:7-9. Moyoni kuna moto unaowaka.
6. Ezekiel 3:14. Mkono wa Bwana u hodari kwa mhubiri.
7. Matendo 4:20. Hatuwezi kunyamaza; Mdo. 4:13,29,31.
8. Hesabu 22:18-38. Hatuwezi kwenda zaidi ya Neno la Bwana.
9. 2 Nyakati 18:13. Cho chote anachosema Bwana chapaswa kusemwa.

Kabla ya kuhubiri hubiri lo lote. Jiulize mwenyewe: "Je nitafurahia kusikiliza hubiri hili? Kama halitakuvuvia wewe usilihubiri! Lazima uone kuwa utakufa kama hutahubiri hubiri hili!

Kuhubiri ni kutangaza Neno la Mungu kunakofanywa na Mtu wa Mungu ambaye amevuviwa na Roho wa Mungu kwa watu wa Mungu. Kwa hivyo basi kuna mambo makubwa manne katika kuhubiri: Neno, Roho Mtakatifu, Mhubiri na watu.

**MHUBIRI:**

**A: Maisha ya maombi ya mhubiri.**

1. Kamwe usifungue Biblia bila maombi
2. Pata fundisho la Martin Luther kwenye maombi.

**B: Kiasi na mhubiri.**

1. Sheria nane za afya ni za muhimu kwa mhubiri.
2. Usafi wa mwili na akili utaongoza kwenye ujumbe ulio wazi.

**C: Mwonekano binafsi wa mhubiri.**

1. Mavazi yanaongea kuliko maneno

**D: Tabia ya kujifunza ya mhubiri.**

1. 2Timotheo 2:15. Jitahidi kujionyesha umekubalika
2. 2Timotheo 3:14-16 lazima kujifunza Maandiko Matakatifu

**E: Maisha/tunda la mhubiri.**

**TUHUBIRI NINI?**

A: Kile watu wanachotaka ni ukweli wa leo [2Petro 1:12; EW63]

1. **Ukweli wa leo wakati wa:**

- Nuhu
- Abrahamu
- Musa
- Elia
- Yohana Mbatizaji
- Petro wakati wa Pentekoste
- Paulo
- Martin Luther
- Wesley
- William Miller

2. Kurudia ujumbe wa Paulo wakati wa Yakobo utawafanya watu wathibitike tu katika uasi wao [Galatia 3:6 na Yakobo 2:21,24].
3. Kuhubiri ujumbe wa Luther wakati wa Eliya hautakuwa na maana.
4. Ukweli wa leo leo.

a. Counsels on Writers and Editors, p. 30-31

2. Ujumbe wa malaika watatu ni ukweli wa leo wa Mungu [Ufunuo 14:6-12] na utaendelea mpaka mwisho wa wakati kwa sababu huu ndio ujumbe wa Mungu wa mwisho!

1. Mcheni Mungu = sheria [Mwanzo 22:12]
2. Mpeni utukufu= hekalu na afya

[1Kor. 3:16,17 ; 6:19,20; 2 Kor. 6:14-18]. Ujengaji wa tabia wakati shakaina inatawala Mbinguni na ndani ya moyo.

3. Saa ya hukumu = hali ya wafu [ Waebr. 9:28]
4. Msujudieni yeye = Sabato, mhuri wa Mungu
5. Wito kutoka Babeli [ Ufunuo 14:8]
6. Onyo la mwisho dhidi ya alama ya mnyama [Ufunuo 14:9-11]
7. Maujumbe haya yalionwa na E .G. White kama nanga dhidi ya udanganyifu wote wa mwisho wa shetani-ulimwengu unahitaji haya maujumbe sasa.
8. Mfano wake ni wakati wa Nuhu.

**B:Hatari ya elimu jamii kutawala ujumbe wa theolojia.**

1. Mahubiri lazima yatoe changamoto kwa jamii, siyo kupatana na jamii. Mahubiri lazima yabadilishe jamii siyo kubadilishwa na jamii.
2. Ukweli wa leo daima unakwenda kinyume na msimama uliopo, unaelea kwa changamoto za jamii zilizopo. Siyo ya kawaida mfano; wakati wa William Miller, Nuhu, Elia, Paulo, Petro, Yohana Mbatizaji, Martin Luther nk.
3. Kama jamii inatawala ujumbe wa mahubiri, basi watu watasikia kile wanachotaka kusikia na siyo kile Mungu anachotaka wasikie.
4. Mahitaji ya kujisikia dhidi ya mahitaji halisi: Lazima tuwafikie watu mahali walipo na kuwaongoza pale Mungu anapotaka wawe. Ikiwa tutakaa tu kwa mahitaji ya kujisikia, watu watasikia tu kile wanachotaka wasikie. Lakini wakati mwingi watu hawajui kile ambacho hasa ni hitaji lao. Angalia Yesu alivyofanya na yule kijana tajiri, Nikodemasi, mwanamke pale kisimani, Mathayo wa Lawi, wanafunzi waliokuwa wavuvi.
5. Hatujaitwa kuhubiri falsafa, elimu jamii, saikolojia lakini elimu juu ya Mungu, Elimu ya Mungu ya Biblia [1Kor. 2:4,5 na muktadha wake wa kihistoria katika Matendo 17:16 na sura ya 18].
6. Neno letu halina nguvu- ni Neno la Mungu ambalo lina nguvu.

- Kuna nguvu ya ajabu katika Neno la Mungu kwa sababu kwalo ulimwengu uliumbwa. Zaburi 33:6
- mjumbe wa Mungu alisema. “nguvu ya uumbaji iliyoita ulimwengu huu kuwepo ipo kwa Neno la Mungu. Neno hili linatia nguvu, linatoa uhai. Kila amri ni ahadi; linakubaliwa na mapenzi, linapokelewa moyoni, linaleta na uhai wa Yeye wa milele. Linabadilisha asili, na kuumba upya nafsi katika sura ya Mungu. **Ed. 126.**
- Waebrania 4:12,13 linasema juu ya nguvu hii ya Neno. Lina nguvu ya ajabu ya kutambua na kujua na kugawanya na kukatilia mbali dhambi.
- Biblia ni kama mbegu [Luka 8:11; 1Petro 1:23-25] na lina nguvu ya ajabu ya kuota. Linapandwa katika udongo wa moyo litaota na kutoa mazao na matunda ya ajabu.

Kanuni na ahadi za Neno la Mungu zina nguvu ya kutenda kile lililosema. Neno halitufundishi tu namna ya kuishi bali hakika lina nguvu ya kutusaidia kuishi kama linavyofundisha.

7. Usafi wa utume unategemea usafi wa ujumbe. Kazi iliyomalizika inategemea hili.

**KUTAFUTA NA KUANDAA HUBIRI LENYE KULETA TOFAUTI.**

A: Misingi miwili ya aina ya mahubiri.

1. **Ufafanuzi.** Hubiri linahusiana na kichwa fulani kilichochaguliwa kufafanuliwa; kwa mfano, zaka,ubinadamu, miaka elfu, hali ya wafu, sabato nk.
2. **Fungu.** Hubiri linahusiana na fungu au aya fulani iliyochaguliwa kwa mfano; Isaya 4:1; Luka 10:25-37; kitabu cha Filemoni; Yohana 15:1-10; nk.

**B: Zana zinazotumika katika kuandaa hubiri.**

1. Kwanza chagua kusudi, aya au fungu
2. Tumia itifaki ya Biblia iliyo nzuri. Tumia Biblia yenye mafungu pembeni na maelezo ya ziada ndani ya Biblia yenyewe
3. Pata tafsiri nyingi za Biblia kwa kadri inavyowezekana. Lakini uwe mwangalifu sana.
4. Angalia masomo ya Roho ya unabii kwa kusoma vitabu vya Roho ya unabii. Kama unaweza kupata CD ya E G. White itakuwa vizuri.
5. Tumia kamusi ya Biblia ili kujua asili ya mafungu hayo. Lakini uende kwa kamusi hizi tu mara baada ya wewe mwenyewe kusoma Biblia yenyewe kwanza na kuielewa hivi viwe ni vya ziada siyo msingi. Omba sana msaada wa Mungu kuliko mawazo ya watu; na mawazo ya Mungu yapo ndani ya Biblia yenyewe.

6. Uzoefu wako wa asili kwa somo hilo unaloandaa utakusaidia sana. Toa vielelezo vinavyoeleweka kwa wakati uliopo kwa uzoefu wako wa kujua asili; mfano mzuri ni Bwana Yesu kwa mifano yake au mfalme Sulemani kwenye mithali na mhubiri.
7. Usikivu wa makini kwa wahubiri wenzako utakupatia mawazo ya ziada kwa somo lako. Chagua wahubiri wanaolichunguza Neno kwa undani.
8. Unapoendelea kujifunza akisi, fikiria na tafakari namna utakavyolitoa, na aina ya mtindo utakaotumia. Amka usiku ufikirie sasa unahubiri kwa watu somo hilo. Lipangilie vizuri, ukipata la ziada amka na uandike maana kesho hutakumbuka sawasawa.

C. Mambo ya kufanya wakati ukijifunza
1. Omba, omba, omba kwa uongozi wa Roho Mtakatifu
2. Jifunze kwa uangalifu maneno muhimu ya aya hiyo au fungu hilo. Kwa hili itifaki ya Biblia itakusaidia sana na maneno ya pembeni mwa Biblia yako na tafsiri mbali mbali za Biblia.
Mfano: Isaya 4:1; Danieli 2- udongo; 2 Thesalonike 2:4; Mwanzo 5:24.
3. Jifunze sarufi[grammar] na sintaksi[ tawi la isimu linaloshughulikia kupanga na kuhusisha vipashio na maneno kisarufi.] za aya hiyo, kwa mfano mwizi pale msalabani.
4. Jifunze muktadha wa aya hiyo.
a. Warumi 6:14,15
2. Warumi 5:20
3. Warumi 3:28
5. Fikiria lugha iliyotumika kwa fungu au aya unayoshughulika nayo. Je, ni shairi? Angalia mlandano. Je, ni mfano? [Lazaro na Tajiri]. Nathari. Lugha ya mjazo? [Ayubu] je, ni mambo yajayo? [Daniel, Ufunuo, Ezekieli]. Je, ni historia au unabii [Mwanzo].
6. Jifunze jiografia ya aya hiyo.
a. Tundu la sindano
2. Mfalme wa kusini na wa Kaskazini
3. Mlima wa utukufu
4. Harmakedonia
7. Jifunze historia ya mahali fungu lilipoandikiwa. Mwandishi ni nani? Wakati gani na lini aliandika? Alikuwa anawaandikia akina nani na kwa nini? [mfano : Zaburi 51; Ayubu; Mhubiri; Hagai; Zaburi 52; 1Timotheo 4.
8. Jifunze mila na desturi za wakati huo
9. Jifunze muundo wa sentensi wa kitabu hicho, sura, aya au fungu. Je aya unayojifunza inaingia wapi katika kiini cha majadiliano ya kitabu hicho?
a. Mihuri
2. Ufunuo 22:10-12
3. Mathayo 24:37-39

10. **Jifunze kuuliza fungu hilo maswali na tafuta majibu yake**.

**KUWEKA HUBIRI PAMOJA**

A. Hubiri ni kama safari- una mwanzo, mwisho na miji yote utakayopitia hapo katikati. Unajua ramani ya safari yako kabla ya kuanza na kujua hakika kule unakokwenda.
B. SEHEMU ZA HUBIRI.

Kwa kawaida ziko sehemu saba za hubiri ambazo mhubiri ye yote anatakiwa kuzifahamu na kuzipitia katika kuhubiri.

1. Maombi kwa ajili ya uongozi wa Roho Mtakatifu
2. **Utangulizi**
a. Lazima uamshe shauku lakini usiwe mtamu kuliko hubiri lenyewe
2. Unapaswa uongoze kwenye somo lenyewe
3. uwe karibu sana na somo lenyewe na vihusiane
4. Usiuchafue na matangazo, kuomba msamaha au mambo yasiyohusiana na somo.
5. **Aina za utangulizi:**

1) Soma aya na toa msingi wake (mfano, somo la mlima wa utukufu)

2)uliza swali au mfululizo wa maswali (mfano miaka elfu.

3)toa kisa au mfano (mfano; ubatizo; Naamani).

4)waambie kuwa unakwenda kuwapa nini na namna utakavyofika hapo. (Mfano, hali ya wafu).

5)elezea tatizo na sasa tumia hubiri kutatua tatizo hilo. (Mfano, kanisa la kweli, alama ya Mnyama).

**MWILI WA HUBIRI.**

i. Chagua pointi chache tu za msingi- hakikisha unahubiri hubiri moja tu!
ii. Lazima kuwa na sehemu ya kiini cha mvutano ambapo kila pointi itaingia hapo. Mwishoni mchungaji anapouliza: "Nilihubiri juu ya nini?" Watu waweze kuelezea somo.
iii. Kuwe na mwendelezo ulio wazi toka pointi moja kwenda nyingine.
iv. Hubiri lililo hai linasogeza watu mahali fulani. Hubiri lazima liwe linatiririka kama mto.
v. Usitoe maelezo ya undani sana kiasi kwamba watu watapoteza pointi ya msingi. Usipoteze msitu kwa sababu ya miti. Usiwe wa undani sana kupita kiasi.
vi. Piga kwenye kiini mara kwa mara kwa njia mbalimbali.
vii. Jifunze kutoa maelezo mafupi ya hubiri lako katika njia ya mantiki na kwa njia rahisi.

## HITIMISHO

**6. Usihitimishe mara kumi**

1. Inaleta usikivu kutoka kwa mhubiri na wasikilizaji. Panga hitimisho mapema!
2. Katika kuuza vitabu unaweza ukawa umetoa hotuba nzuri sana lakini kama hutoi hitimisho zuri lenye nguvu na wito hutauza cho chote.

7. Njia za kutoa hitimisho la hubiri:-

i. Muhstasari
ii. Swali linalowawajibisha
iii. Mfano unaotoa maamuzi mazito
iv. Kusoma aya ya kufungia yenye nguvu (mfano, Isaya 33:12-16)
v. Nukuru au shairi au wimbo.

**WITO**

1. Kama hutafanya wito watu wataachwa na hisia: "hili ni sawa na safi sana lakini anataka nifanye nini?" daima uwe unataka kufanya maamuzi mwisho wa hubiri.
2. Fuata kanuni nzuri za kufanya wito. Kumbuka sasa unasimama kati ya uzima na mauti. Kumbuka wengine huu ndio wito wao wa mwisho hawatapewa mwingine tena maisha yao yatakoma milele.
3. Ombi la mwisho kumuuliza Mungu kubariki maamuzi yaliyofanywa. Usihubiri hubiri hilo hilo mara kwa mara. Badilisha ili lilete ladha tofauti.
4. Sasa fanya matembezi kuwaona waliofanya maamuzi baada ya hubiri. Mahubiri mazuri hayaishii mimbarani au kwenye kibweta. Tofauti kubwa itaonekana wakati mhubiri anapowatembelea watu wake majumbani mwao au maofisini mwao.

**KUHUBIRI BILA MAANDISHI**

- Lazima tujenge akili iliyopangiliwa na yenye kuleta maana kabla ya kuandaa hubiri.
- Panga hubiri lako akilini mwako na kariri mawazo muhimu.
- Nunua Biblia yenye maelezo ya ziada ambayo yatakusaidia wakati unahubiri bila kwenda kwa maelezo mengine.
- Rudia rudia hubiri lako mara kwa mara mpaka uwe umejua mawazo ya kiini kwa moyo. Tunajifunza kwa kurudia rudia

**KUHUBIRI HUBIRI**

A. Kuna mambo matatu yanayohusika katika kutoa hubiri.
   1. Taarifa ( mhubiri)
   2. Kusadikisha (Roho Mtakatifu)
   3. Tendo (msikilizaji).

**B: Nukuru za Roho ya Unabii.**

1. Juu ya wanafunzi: " walitakiwa kutupa mshale, na Roho wa Mungu alitakiwa kuongoza mpini [wano]

(shaft) moyoni." Ev. 69.

2. " Kazi ya upandaji wa mbegu ni wako, na kazi ya kueneza mbegu ni kazi ya Bwana wa mbingu." Ev. 178.
3. Katika kuwalisha wale 5000. Yesu alitengeneza mkate, wanafunzi waliugawa na watu waliula

**C: Mashauri halisi:**

1. Hali ya mimbari
   a. Dumisha vitendo sahihi, ukaaji na usimamaji.
   b. Zungumza waziwazi, taratibu na kwa nguvu
   c. Tumia maneno sahihi, matamshi na taja kwa usahihi.
   d. Usianze kwa kuomba msamaha
   e. Usiringe ringe mimbarani. (Show off).
   f. Jifunze namna ya kupumzika. Punguza sauti yako. Jifunze kutumia ukimya kama zana yenye nguvu.
2. Mhubiri Yesu katika muktadha wa ukweli wa leo na pambano kuu. Kupitiliza kwa aina mbili unakotakiwa kuepuka:
   a. Kumhubiri Kristo bila mafundisho
   b. Kuhubiri mafundisho bila Kristo
   c. Kila fundisho linakuwepo kwa kusudi maalumu la kulinda mahusiano yetu na Kristo - fundisho ni kama gome la mti (bark) na Kristo ni maji ya mti ,majani. (Sap).
   d. soma EV. 185-87, 272.
3. Hakikisha mazungumzo yote ya hubiri ni ya uhakika na yamehakikishwa ( soma 5T708, aya ya 1) usitumie sauti isiyo na mantiki.
4. Hubiri lapaswa kuwa linatekelezeka kwako.
   a. Halipaswi kujibu tu swali "niamini nini?" lakini vile vile napaswa kufanya nini?
   b. Watu watauliza: " kutakuwa na tofauti gani katika maisha yangu ikiwa nitaamini na kutenda hili?"
   c. Mfano: Matendo 2:38 na Matendo 16 (katika gereza kule Ufilipi).

5. Hubiri lapaswa kutoa wito toka akilini siyo kwa msisimko tu.

a. Hubiri linapaswa lifikie moyo kupitia kichwani. Lazima tulinde sana dhidi ya misisimko inayopitiliza na kutumia akili.
b. Misisimko yenyewe kamwe haiongozi kwa badiliko linalodumu- misisimko inaweza ikatoa machozi machoni na kutoa dola mifukoni lakini haitakuwa na matokeo ya kudumu kwa muda mrefu.
c. Neno na Roho vinaenda pamoja (Soma Yohana 4:24; 14:14,15; 16:13; Matendo 5:32; Efeso 6:17; 5:25-27; 1Yohana 4:13; 2:3-6; 5:7; 1Petro 1:2).

6. "Tunapaswa sisi wenyewe tuwe tunazoea kuzungumza kwa tuni yenye kufurahisha, kutumia lugha sahihi na safi na maneno ambayo ni ya upole na kutia moyo. Matamu, maneno ya upole ni kama umande mwororo unaomiminika kwa roho." COL 336.
7. Ujumbe unapaswa utolewe kwa shauku kubwa, nguvu na wenye kusadikisha. Kuna hatari mbili:
   a. Kusema mambo mazuri yasiyokuwa na shauku
   b. Kuwa na shauku kubwa lakini hakuna la kusema
   c. Ni lazima kusema kwa maneno ya huruma yaliyotakaswa.
8. Neno lazima lizungumzwe kwa nini ni muhimu kutekelezwa sasa. Toa kila ujumbe kama swala la uzima au mauti.
   i. Sisi ni kama watu ambao wako kwenye hatari ya kutoa ujumbe wa malaika watatu kana kwamba tuko kwenye hali isiyoelezeka kiasi kwamba haiwastui watu. Ujumbe wetu ni wa uzima au mauti na ni lazima tuuache ujumbe huu utoke kama ulivyo- nguvu kuu ya Mungu. Sasa Bwana ataufanya uwe na athari. Tunapaswa tuutoe kwa nguvu zote kama wenyewe ulivyo na nguvu." EV. 230.

"Katika wakati huu wa kuogofya kabla tu ya Kristo kuja mara ya pili, wahubiri waaminifu wa Mungu watapaswa kuchukua bado ushuhuda ulio mkali kuliko uliochukuliwa na Yohana Mbatizaji." 1T321. " Lazima kusiwe na kupunguza sauti kwa ukweli, hatupaswi kufunika ujumbe wa wakati huu. Ujumbe wa malaika watatu lazima uimarishwe na kuthibitishwa .Sura ya 18 ya Ufunuo inafunua umuhimu wa kutoa ukweli kwa kiwango kikubwa lakini kwa uthibiti na nguvu... kumekuwa na kuzunguka kwingi katika kutangaza ujumbe wa malaika watatu. Ujumbe haujatolewa kwa uwazi na uzito kama inavyotakiwa." EV. 230

ii. Rudia mara kwa mara kwamba kuna vita ya uzima na mauti ya kupiganwa kwa kila roho duniani.
iii. Hubiri kana kwamba hili ndilo hubiri la mwisho ambalo watu wanakwenda kusikiliza. Utapaswa uhubiri nini kama utajua hili?
iv. Mfano: Kuhubiri ujumbe wa Sabato.

9. Hubiri lapaswa kufanywa kuwa rahisi.
a. Mpumbavu wa zamani atafanya mambo marahisi kuwa magumu. Mtu mwenye akili ya hali ya juu sana anachukua mambo magumu na kuyafanya kuwa rahisi.
b. Kuhusiana na Yesu mama White anathibitisha: "Aliwazungumzia kwa lugha rahisi kiasi kwamba hawakushindwa kumwelewa... maneno ya uzima yalitolewa kwa urahisi kiasi kwamba hata mtoto angeweza kuyaelewa." Ev. 54,56

10. Uwe mwangalifu juu ya urefu wa hubiri. (Katika hali ya kawaida lisiwe zaidi ya saa moja).
11. Jifunze kutumia nguvu ya vielelezo.
    a. Moja ya maelezo aliyoyapendelea sana Yesu: 'Ufalme wa mbinguni ni kama...." Marko 4:33-34
    b. Soma kitabu cha vielelezo hai. (COL.)

    c. Neno kielelezo linatokana na neno la Kiyunani ***LUX*** ambalo lina maana ya nuru.vielelezo lazima vitoe nuru kwa somo, siyo kulifunika somo.
    d. Neno *Parabole* lina maana ya kuweka kitu fulani kando ya - hii ina maana ya kitu ambacho ni cha kawaida katika ulimwengu huu ambacho kitaonyesha uhusiano halisi.
    e. Sababu za kutumia vielelezo
    f. Vyanzo vya vielelezo

i. Biblia
ii. Uzoefu wa maisha yako- fundisha macho yako na masikio kuona vielelezo vya hubiri
iii. Kusoma hadithi, sayansi, fasihi, maisha ya watu, mashairi nk.
iv. Vitabu juu ya vielelezo

    g. Kanuni za kukumbuka:-

- kielelezo lazima kilingane na somo lako kama vile glove inavyolingana na kiganja. Wasikilizaji lazima waone uhusiano
- kusudi la kielelezo siyo maburudisho au kuwafanya watu wacheke
- kuwa mwangalifu kutumia kielelezo ambacho kutahafifisha ujumbe (TM 318; GW 155).
- Usichague kisa kisha ukajenga hubiri lako hapo. Chagua aya kisha jenga kutoka kwa aya hiyo ya Biblia
- jua kwa nini Yesu alitumia mifano (CT 178,179).

12. Katika uinjilisti, onyesha namna ujumbe unaotoa unavyohusiana na ujumbe wa Waadventista Wa Sabato.
    a. Ujumbe wa Kiadventista ni mnyororo wa ukweli; ni fumbo lenye sehemu nyingi. Tuna ukweli wenye mwili, mfumo wa ukweli.
        i. Hekalu kama sumaku kubwa ya Theolojia ya Waadventista Wa Sabato.
        ii. Uhusiano wa Sabato, sheria, hali ya wafu, na hukumu.
        iii. Uthibitisho wa Mungu katika hatua tatu za hukumu.
        iv. Ikiwa utafundisha kosa moja katika fundisho la wokovu, itagusa mafundisho yote. Haki kwa imani, kufanywa upya, utakaso na tendo la utukufu katika hali moja ya kuyajenga.

**MIITO NA MAITIKIO AMBAYO YATAONGOZA KWA MAAMUZI YA KUDUMU KWA KRISTO.**

Daima fanya wito wa maamuzi mwishoni mwa kila hubiri. ( unaweza ukalifanya rahisi kwa kuuliza maswali kama somo lilivyofunuliwa). Uamuzi unawezakuwa wa kuzungumza au wa kuandika. Fanya hili kwa hotuba yako ya kwanza ili kwamba watu wawe wamezoea kupewa wito wa kufanya maamuzi. Angalia mashauri haya yafuatayo:" Kuna roho kwa kila mkutano ambazo zinasita kujitoa kamili kwa Mungu. Uamuzi unatolewa kwa muda na kwa milele; lakini mara kwa mara swala ni kwamba mhudumu hana roho na nguvu ya ujumbe wa ukweli ndani ya moyo wake mwenyewe, hivyo hakuna mwito wa moja kwa moja unaofanywa kwa roho hizo ambazo zinatetemeka kwa mizani... wanaamua kungojea kwa fursa iliyo nzuri zaidi, lakini kamwe haijafika." 6T 447

“Mwisho wa kila mkutano, maamuzi lazima yatolewe kwa wito. Washikilie wale wote walio na shauku mpaka wawe wamethibitika katika imani.” 6T 65.

“Wakati wale watu wanaosadikishwa hawakuletwa kwenye maamuzi katika kipindi cha mwanzo kabisa inavyowezekana, kuna hatari kwamba usadikisho utaondoka taratibu...” EV. 229.

Sababu ya msingi inayotufanya tuogope kuita mwito ni kuwa huenda wito utakataliwa. Lakini kumbuka. Ni Mungu anayeita kupitia kwetu. Kukataliwa kunaweza kukatusikitisha lakini kunamsikitisha Mungu zaidi yetu. Yesu na Paulo wote walikuwa na miito iliyokataliwa (Kijana tajiri, Yerusalemu, Agripa; Felex) lakini waliendelea kuita wadhambi kutubu.

**B:USHAURI HALISI WA NAMNA YA KUFANYA WITO**

1. Ikiwa tunawataka watu wafanye maamuzi sahihi lazima tuhakikishe kuwa tunawapatia maelezo sahihi ya kushikilia kwa uamuzi wao.
2. Ni jambo la muhimu sana kufahamu namna watu wanavyofanya maamuzi
3. Ni muhimu vile vile kufahamu namna ya kuwafanya wahamasike kufanya uamuzi Mungu anaotaka kwao kufanya siyo wewe au kanisa.
4. Utambuzi wenye msisitizo na utambuzi wa sauti za kelele zilizokosa mwafaka. Umuhimu wa kumotisha watu kufanya uamuzi umejengwa juu ya mamlaka iliyo kuu (Matendo 5:39).
5. Miito ya maamuzi lazima iwe halisi na wazi, siyo isiyo wazi na kuleta wingu.
6. Wito uwe kwa mtu binafsi- mwangalie mtu machoni kana kwamba ndiye tu; usitoe wito wa maamuzi mazito kwa kundi zima. Mkumbuke malaika kwa Lutu, mke wa Lutu pamoja na binti zao; jiponye nafsi yako.
7. Wito wapaswa usisitize matokeo chanya ambayo yataelekeza kwenye maamuzi.
8. Waongeze watu kutoka kwa nadharia kwenda kwa vitendo, toka kwa wazo kwenda kwa tendo.
9. Wito wapaswa uwe wa asili na hiari kuliko wa kuigiza na kulazimisha.
10. Daima kumbuka kunukuru Biblia kama msingi wa maamuzi. Kama unatumia mfano binafsi au kisa daima tumia Biblia kuunga mkono kisa hicho. Toa nukuru za Biblia zilizo rahisi kumsaidia mfanya maamuzi.
11. Kazia kuwa ni jambo muhimu sana kufanya maamuzi mara moja. Kwa kadri mtu anavyochelewa kufanya uamuzi ndivyo itakavyokuwa vigumu kufanya baadaye. (Waebrania 3:8,9; Yoshua 24:15; Matendo 26:15).
12. Fanya wito endelevu: ni wazi? Je, ni ajabu? Kumbuka kwamba Yesu anasema katika Neno lake.......

**WASIKILIZAJI: KATIKA KUHUBIRI.**

A: Jifunze kusoma lugha ya mwili na nyuso za wasikilizaji wako (DA 254-256).

B: Watembelee wasikilizaji wako

C: Mama White ana maanisha nini kuhusu kuhubiri? Chukua kibweta na hubiri lakini usipowatembelea watu maneno yote hayatakuwa na matendo

**WOGA KATIKA KUHUBIRI**

A: Kwa nini tunapata woga?

- Utambuzi binafsi kuhusu namna tutakavyoonekana mbele za wengine
- Tunaweza tukasahau la kusema
- Tunaweza tukasema jambo fulani la kipumbavu.
- Tunaweza tukaishiwa ya kusema

B: Tunawezaje kushinda woga?

- Omba kuwa mtulivu
- Jiandae vizuri. Jifunze vizuri, jifunze namna ya kutoa hubiri
- Pumua kwa nguvu. Usipumulie kipaza sauti watu watajua umeogopa.
- Kumbuka: uko kwa utume wa Mungu siyo utume wako mwenyewe.

**ZAWADI YA MWISHO YA KUHUBIRI**

A: Kuhubiri kunapaswa kutoe taarifa, kubadilishe na kuleta matengenezo

B: “Wapamdao kwa machozi, watavuna kwa kelele za furaha. Ingawa mtu anakwenda zake akilia, azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake.” Zaburi 126:5,6.

C: “Mbegu njema inayopandwa inaweza wakati mwingine kuwa katika ubaridi, ulimwenguni, moyo wenye ubinafsi bila kuwa na uhakika kwamba imekuwa na mizizi; lakini mara kwa mara Roho wa Mungu anafanya kazi kwa moyo, na kutilia maji kwa umande wa mbinguni, na mbegu iliyojificha kwa muda mrefu inaota na mwisho inatoa matunda kwa utukufu wa Mungu. Hatujui katika kazi yetu ya maisha kwamba ni ipi itaota na kunawiri hii au ile. Haya siyo maswali yetu sisi maskini tunaokufa kuyajibu. Tunapaswa kufanya kazi yetu na kuacha matokeo kwa Mungu.” EV. 64,300.

**NUKURU ZA ROHO YA UNABII JUU YA WAHUBIRI NA KUHUBIRI**

1. WACHUNGAJI, WAINJILISTI,WAALIMU
    A. “Agizo lililotolewa kwa wanafunzi linatolewa kwetu vile vile leo kama lilivyotolewa, mwokozi aliyesulubiwa, aliyefufuka anapaswa ainuliwe mbele ya wale ambao hawana Mungu na bila tumaini katika ulimwengu. Bwana anaita wachungaji, waalimu na wainjilisti.” GW 29.
    B. “Mungu ameweka mitume, wachungaji, wainjilisti na waalimu kwa ajili ya kuwakamilisha watakatifu, kwa ajili ya kazi ya huduma, kwa ajili ya kuukamilisha mwili wa Kristo.... Wale wote watakaofanya kazi kwa ajili ya Mungu lazima wafanye kwa akili kujaza tena mapungufu yaliyo upande wao na kumtukuza Bwana Mungu wa Israeli kwa kusimama katika nuru, kufanya kazi katika nuru ya jua la haki.” TM 406.
    C. “Mungu anaita wainjilisti. Mwinjilisti wa kweli ni mpenzi wa roho. Anawinda na kuvua watu. Wachungaji wanahitajika- wachungaji waaminifu- ambao hawatawadanganya watu wa Mungu au kuwatendea kwa ukatili, lakini watakao walisha kwa mkate wa uzima. Kazi ya kila mtendakazi aliyemwaminifu imelala karibu sana na moyo wa Yeye aliyejitoa mwenyewe kwa ukombozi wa kizazi.” Letter 21, 1903.
    D. “.... Kazi kubwa inatakiwa kufanywa , na kwa wakati huu wapo wachache walio tayari kuifanya. Mtu mmoja kwa kawaida anafanya kazi ambayo ingefanywa na wawili; kwa sababu kazi ya mwinjilisti ni muhimu ikiunganishwa na ile ya mchungaji, kuleta mzigo mara mbili kwa mtendakazi aliye shambani.” 4T 261.

**KUHUBIRI KAMA NENO LA BWANA**

A. “Wengi hawaangalii kuhubiri kama njia ya Kristo ya kuelekeza watu wake, na kwa hivyo, daima inapaswa kuwekwa kwa thamani kubwa. Hawasikii kuwa hubiri ni Neno la Bwana kwao, na kulipima katika kiwango cha ukweli unaozungumzwa; lakini wanalipima kama anavyozungumza mwanasheria mahakamani- kwa ujuzi wa kutoa hoja, na nguvu na usafi wa lugha. Mchungaji siyo asiyeweza kukosea, lakini Mungu amempa heshima kwa kumfanya awe mjumbe wake. Mungu hajaanzisha njia mpya ya kuwafikia watoto wa watu... kamwe hatupaswi kusahau kuwa Kristo anafundisha kupitia kwa watumishi wake. Kuna uwezekano wa kuongoka bila njia ya hubiri. Pale watu ambapo wanaweza wakaelewa kuwa wanavutwa kwa njia ya neema, wanaletwa kwa uongozi wa Roho Mtakatifu wa Mungu na kusadikishwa juu ya ukweli kupitia kwa kusoma Neno; lakini njia Mungu aliyochagua ya kuokoa roho ni kupitia “upumbavu wa kuhubiri.” 5T298-300.

B. “Kupitia kwa mtunga Zaburi Mungu alisema, ‘yeye anayetoa sadaka ya kusifu ananitukuza mimi’. Kilicho kwa wingi katika ibada ya Mungu ya hadhara imejengwa kwa kusifu na kuomba, na kila mfuasi wa Kristo anapaswa kuhusika katika ibada hii. Kuna huduma ya kuhubiri vile vile, inayoendeshwa na wale wote ambao kazi yao ni kuelekeza mkutano katika Neno la Mungu. Japokuwa wote hawakuitwa kuwa wachungaji wa Neno na mafundisho, wasikilizaji hawahitajiki kupoa na kutohusika. Wakati Neno la Mungu lilipokuwa likizungumzwa kwa Waebrania wa zamani, Bwana alisema kwa Musa, Hebu watu wote na waseme amina’. Mwitikio huu kulingana na nafsi zao ulihitajika kama ushahidi kuwa wameelewa Neno lililozungumzwa na wamelitamani.” ST June24, 1886.

**MHUBIRI KAMA BALOZI, MZUNGUMZAJI KWA AJILI YA KRISTO**

A. “Mabalozi wa Kristo, wana kazi nzito na muhimu, ambayo kwa wengine wameiona kuwa nyepesi sana. Wakati Kristo akiwa mhudumu kwenye hekalu mbinguni juu, vile vile kupitia kwa wajumbe

wake mhudumu kwa kanisa lake duniani. Anaongea kwa watu wake kupitia kwa watu aliowachagua na kuendeleza kazi yake kupitia kwao kama ilivyokuwa siku za kujidhili kwake, anatembea akiwa anaonekana juu ya dunia." 4T 393

B. **"Watu hawapaswi kuwachukulia wachungaji wao kama wazungumzaji wa hadhara tu na wahutubu, lakini kama mabalozi wa Kristo, wakipokea hekima yao na nguvu kutoka kwa kichwa kikuu cha kanisa. Kudharau na kutojali Neno lililozungumzwa na mwakilishi wa Kristo, siyo kuonyesha kutojali kwa mwanadamu tu bali vile vile kwa Bwana aliyemtuma. Yeye ni badala ya Kristo; na sauti ya Mwokozi yapaswa kusikiwa kwa mwakilishi wake." 4T393.**

**MCHUNGAJI KAMA MFAFANUZI**

"Tunaishi katika kipindi cha makini sana. Wote wana kazi ya kufanya kuhusiana na uaminifu. Maalumu sana katika ukweli huu wa mchungaji, yeye aliye mwangalizi na mlishaji wa kundi la Mungu. Yeye ambaye kazi yake maalumu ni kuongoza watu katika njia ya ukweli, anapaswa awe anaweza kufafanua Neno, anayeweza kuingiza mafundisho yake kwa mahitaji ya watu. Anapaswa awe karibu sana na muunganiko na mbingu ili awe mfereji ulio hai wa nuru, mdomo wa Mungu."4T260.

**MAHUBIRI YA KIBIBLIA**

A. "Wajibu wa mhudumu wa Kristo umeonyeshwa wazi katika maelekezo na maneno yenye nguvu (2Timotheo 4:1,2). Anawajibishwa kuhubiri Neno, siyo mawazo ya watu na tamaduni za watu, siyo hadithi zenye kupendeza ili kuleta mvuto kwa watu na msisimko. Hakupaswa kujiinua mwenyewe kwa kuona utekelezaji wake wenye mafanikio au kuonyesha hekima aliyo nayo; lakini kama aliye mbele za Mungu na Kristo, ambaye atahukumu walio hai na wafu, anapaswa kusimama mbele za ulimwengu unaopotea na kuhubiri ukweli wa Mungu wa muhimu sana. Hakuna purukushani, upumbavu, hakuna tafsiri za ubunifu, lakini kwa ukweli wote na uaminifu wa kina, **mhudumu lazima awe sauti kutoka kwa Mungu akielezea Maandiko Matakatifu...**

Wale wote wanaohubiri Neno lazima wawe na ufahamu juu ya mafundisho na kanuni. Lazima wajifunze kujionyesha wenyewe kuwa wanakubalika na Mungu. Kama mtumishi wa Mungu lifungue Neno kwa unyenyekevu utatafuta kujua maana yake, maana yake itakua wazi kwa ufahamu wake. Lakini lazima awe mwanafunzi mwaminifu na mwenye kujua maumivu ya kujifunza. Lazima asiwe anayetegemea mauchunguzi ya watu wengine tu au mawazo ya watu wengine tu. Lazima afanye uchunguzi yeye mwenyewe. Mawazo yaliyo imara yanahitaji mazoezi. Uwezo wa kujua Neno la Mungu unategemea kwa kazi inayotumika kwa muda wa kujifunza Neno-inategemea mtazamo wa roho kumwelekea Mungu. Njia za akili lazima ziwe imara na uwezo wa kushughulikia maswali makubwa ya ukweli na wajibu. Kujifunza lazima kuwe kwa ndani na kwa uhakika na kufanywe kwa unyenyekevu na kwa uaminifu wa makusudi ya kuujua ukweli kama ulivyo katika Yesu." RH, April 24, 1888

B. "Lihubiri Neno". Ni Neno linalohitaji usikivu wako. Hakuna hitaji zaidi la ufahamu wa watunzi kama uelewa wa Kitabu cha vitabu. Kufikiri kwa undani na kazi ya maumivu inawekwa ndani ya akili wakati Maandiko Matakatifu yanapotafutwa kwa uaminifu. Mazoezi ya ukweli katika maisha yako ya kila siku ni kulihubri Neno na vile vile ufafanuzi wa Maandiko mimbarani. Elimu unayopata uikabidhi kwa watu waaminifu ambao watawafundisha wengine. Watu maelfu zaidi wangeliokolewa ikiwa watu wangelilihubiri Neno, badala ya mawazo ya watu, falsafa na mafundisho ya watu. Kama kutoka kwa kila mimbari kungesikika ukweli wa Mungu, watu wangeliachwa na ufahamu wa kweli wa Biblia, na usadikishwaji wa kina wa ukweli na kanuni zake na uhalisi wa ahadi zake; na watu wangeliufahamu ukweli na kuwa na uelewa wake na kujua ukweli ni nini. Dunia imejawa na vitu visivyo mafundisho ya kweli, desturi na mawazo ya watu kanuni za roho chafu; hebu kila aliye na ufahamu wa ukweli wa leo, ajifunze kujionyesha mwenyewe kuwa amekubalika na Mungu; na kwa neno na tendo hebu atangaze Neno la Mungu kwamba linaishi na kutawala milele." RH, April 24,1888.

C. "Wapo watu wanaosimama mimbarani kama wachungaji, wakiwa na taaluma ya kulisha kundi wakati kondoo wana njaa kwa kukosa mkate wa uzima. ... hisia za wengine zinaguswa, wanaweza wakatoa machozi kidogo lakini mioyo yao haijavunjika. Bwana Yesu amekuwepo wakati walipotoa kile walichokiita hubiri, lakini maneno yao yalikosa umande na mvua kutoka mbinguni. Wameshuhudia kuwa mtiwa mafuta aliyeelezwa na Zakaria (soma sura ya 4) hakuwahudumia ili kwamba wawahudumie wengine. Wakati mtiwa mafuta anapojimwaga kwao kupitia kwa bomba za dhahabu, mafuta ya dhahabu yanatiririka kwao kwenda kwa mabakuli ya dhahabu, kwenda kwa taa, makanisa. Hii ni kazi ya kila mtenda kazi wa kweli aliyejiweka wakfu

wa Mungu aliye hai. Bwana Mungu wa mbinguni hawezi kudhibitisha kile kinacholetwa mimbarani na wale wanaokuwa na taaluma ya kuzungumza neno la Bwana. Hawawezi kutoa mawazo ambayo yatakuwa mibaraka kwa wasikilizaji. Kuna kurahisishwa kwingi, kurahisishwa sana kunakowekwa mbele za watu." TM 33,337.

D. "Hebu mahubiri na yawe mafupi, kiroho kiinuliwe. Hebu mhubiri ajawe na Neno la Bwana. Hebu kila mtu anayefika mimbarani ajue kwamba anao malaika kutoka mbinguni kwa wasikilizaji wake. Na wakati hawa malaika wanapomwaga kutoka kwao mafuta ya dhahabu ya ukweli katika moyo wa yeye anayefundisha Neno, sasa matumizi ya ukweli yatakuwa ya maana na jambo muhimu sana." TM 338.

E. "Mtu anaweza akatoa kwa ukarimu hazina yake yote ya elimu yake, anaweza akatumia nguvu zake zote za kimwili za asili na bado asitimize lo lote, kwa sababu yeye mwenyewe hajapokea mafuta ya dhahabu kutoka kwa wajumbe wa mbinguni; kwa hiyo haiwezi kumiminika kutoka kwake na kutoa maisha ya uzima wa kiroho kwa hitaji.. Ikiwa mchungaji wa kikristo anapokea mafuta ya dhahabu, ana uzima; na pale palipo na uhai hakuna kuganda hakuna mazoea ya kudumaa." TM 338.

F. "Ni Roho Mtakatifu anayefanya ukweli uwe na mvuto. Weka ukweli kwa matendo mbele za watu." GW 405.

**UMUHIMU WA KUHUBIRI.**

A. "Mhudumu anapaswa kuwa mwaminifu sana yeye mwenyewe, akijisikia kutoka moyoni maneno anayotamka, na ashindwe kuzuia hisia zake kuhusiana na roho za wanaume na wanawake ambazo Kristo alizifia. Kwa Bwana alisema, ' juhudi ya nyumba yako imenila na kunimaliza.' hali ya namna hiyo hiyo yapaswa iwe kwa mwawakilishi wake." 4T396.

**MUUNDO WA SOMO**

- (Kwa ndugu A. July 6, 1870) "katika kuhubiri kwako kwa ujumla uko mkavu sana na kwa mtindo tu. Hutembei na uhalisi wa fundisho. Unaongea kwa muda mrefu na kuwachosha watu. Badala ya kuzama kwa sehemu tu ya somo ili kwamba uweze kulifanya liwe wazi kwa wote unakwenda mbali kutoa mambo ya ndai ambayo hayasaidii somo na yanapita tu. Wakati mambo mengi yanapoletwa yasiyo na ulazima wasikilizaji wanapoteza ule mnyororo wa mazungumzo na hawawezi kulikumbuka somo akilini. Wakati mhudumu anapowasikiliza wasikilizaji wake anapaswa kwenda hatua kwa hatua kwa umbali kiasi kwamba mawazo yake yanazibwa na maneno mengi na undani mwingi. Anapaswa kulainisha mawazo yake mbele za watu kama vibao vya alama. ..." 2T54.
- "Lakini pamoja na kuwa mwalimu wa ukweli anapaswa kuwa mwaminifu wakati wa kutoa injili, hebu kamwe na asitoe mafundisho mengi ambayo watu hawawezi kupokea kwa sababu ni mapya kwao na magumu kuelewa. Chukua hatua moja kwa wakati na ifanye hiyo ieleweke wazi, ukiongea taratibu na sauti ya mkazo. Ongea kiasi kwamba watu wanaweza kuona ni nini uhusiano uliopo kati ya hatua moja na nyingine kwenda kwa ukweli mwingine wa muhimu." EV. 202.
- "Hebu hubiri lako liwe fupi. Kuna sababu mbili kwa nini tufanye hivi. Moja ni kuwa utapata kuwa mzungumzaji mwenye usikivu sana kwa watu. Nyingine ni kuwa utatunza afya yako." EV. 177,178.
- 

**KUHUBIRI/ MUUNGANO WA WITO WA KICHUNGAJI**

A. "Roho ya mchungaji wa kweli ni moja ya ile isiyosahau. Kwa kulihubiri Neno na kwa huduma binafsi katika nyumba za watu, anajifunza mahitaji yao, huzuni zao, majaribu yao na kushirikiana na mbeba mizigo mkuu anashiriki maumivu yao, anawafariji kwa maumivu yao, anawajaza njaa yao ya kiroho, na kupata mioyo yao kwa Mungu." GW 184.

B. "Mhudumu ni yule anayehudumu. Kama unamalizia kazi yako kwa kuhubiri kundi la Mungu litateseka kwa kuwa wanahitaji juhudi binafsi. Hebu hubiri lako liwe fupi. Mahubiri marefu yanakuchosha wewe na watu. Kama wahudumu wangelifanya mahubiri yao nusu tu wangelifanya vizuri zaidi na wangelibakiwa na nguvu za kufanya kazi zaidi. Tembelea familia, omba pamoja nao, jadiliana nao, tafuta Maandiko pamoja nao, na utawafanyia vema. Wape ushuhuda kuwa unawatakia mafanikio na unataka wawe wakristo wenye afya."

C. "Ikiwa utamalizia kazi yako kwa kuhubiri, kundi la Mungu litateseka kwa kuwa wanahitaji juhudi binafsi." EV. 348.

D. "Kuna hitaji la kuwa karibu na watu kwa juhudi ya binafsi. Kama muda pungufu ungetolewa kwa kuhubiri na muda wa ziada ungetumiwa kwa huduma binafsi, matokeo makubwa yangelionekana." Ev. 459

E. "Katika kazi ya wahudumu wengi kuna kuhubiri kwingi na muda kidogo sana wa kazi ya moyo kwa moyo." GW 185

F. “Dawa nzuri unayoweza kutoa kwa kanisa siyo kuhubiri au kuwahubiria lakini kupanga kazi kwa ajili yao.” Ev. 356.

G. “Kama nusu ya kuhubiri kungelifanywa na mara mbili ya muda huo kwa kazi ya binafsi kutolewa kwa roho majumbani mwao na katika makutano, matokeo yangeonekana ya kushangaza.” Ev. 430

H. “Mhudumu anaweza akafurahia kuhubiri, kwa vile ni sehemu ya furaha ya kazi, na kwa kweli ni rahisi ukilinganisha na zingine; lakini mhudumu ye yote asipimwe kwa ajili ya uwezo wake wa kuzungumza kama mzungumzaji. Kazi ngumu zaidi inakuja baada ya kuacha dawati, kumwagilia maji mbegu zilizopandwa.” Ev. 437,438

I. “Wahudumu wengi hawana habari juu ya umuhimu wa kuchukuliana na mazingira, na kuwafikia watu mahali walipo. Hawajitambulishi wenyewe kwa wale wote wanaotamani kuwasaidia na kuwainua kwa kiwango cha kweli cha Biblia cha ukristo.” 4T 261.

J. “Mchungaji anapaswa kutembea nyumba kwa nyumba miongoni mwa kundi lake, akifundisha, akizungumza nao, na kuomba na kila familia, na kuangalia mafanikio ya roho zao.” 4T 266

K. “Ni umuhimu wa hali ya juu sana kuwa mchungaji ajichanganye zaidi na watu wake ili kwamba aweze kuelewa aina tofauti za hali ya ubinadamu, awe tayari kufahamu namna akili zinavyofanya kazi, aingize mafundisho yake kulingana na akili za watu wake na kujifunza kuwa sadaka kubwa inakuwa tu kwa wale wanaojifunza kwa karibu hali ya watu na mahitaji yao. Wale wote wanaojitenda wenyewe na watu wako katika hali ya kutowasaidia watu.” 4T 266,267.

L. “Kama vile mganga anavyojihusisha na magonjwa ya kimwili, hivyo hivyo mchungaji mhudumu kwa ugonjwa wa dhambi wa roho. Na kazi yake ni ya muhimu zaidi kuliko mganga wa kimwili kwa vile uzima wa milele ni wa thamani zaidi kuliko uwepo wa muda tu. Mchungaji anakutana na mambo mbalimbali yasiyokoma; sasa ni wajibu wake kuwaelewa washiriki wake katika familia ambao wanasikiliza mafundisho yake ili kwamba aweze kuazimia njia gani zinaweza kuwavutia kwa mwelekeo sahihi. Kwa mtazamo huu wa wajibu wa kaburini, swali litazuka, ‘nani anayestahili mambo haya?’ moyo wa mtendakazi utakaribia kuzimia anapofikiria kazi mbalimbali zinazomkabili; lakini maneno ya Kristo yanamtia nguvu kwa uhakika wenye matumaini, ‘ lo! Tazama Nipo pamoja nawe hata ukamilifu wa dahari.” 4T267

M. “Lakini kuna pointi nyingine ambayo karibu ningeisahau. Ni mvuto ambao mhubiri anaopaswa kuonyesha katika huduma yake. Kazi yake siyo ya kusimama katika dawati tu. Inaanzia pale tu. Anachukua mahubiri yake tokea pale anayachukua nje kwenye matendo yake na maneno yake. Anapokuwa akitembelea familia, anapaswa kuwaulizia hali zao. Je, yeye ni mchungaji wa kundi? Kazi ya mchungaji wa kundi haiishii kwenye dawati. Anapaswa kuongea na washiriki wote wa kundi; pamoja na wazazi kujua msimamao wao na pamoja na watoto kujifunza msimamo wao. Mhudumu anapaswa kulilisha kundi Mungu aliloliweka juu yake na akamfanya kuwa mwangalizi wake.” 4T618

**MJADALA - SIYO MAHUBIRI PEKEE.**

A. “Imeonyeshwa mara kwa mara kwangu kuwa inapaswa kuwa na kuhubiri kudogo kwa wahudumu wanaoonekana kama wachungaji wa makanisa mahalia tu, na kwamba juhudi kubwa ya binafsi inapaswa kutiwa nguvu. Watu wetu hawapaswi kufanywa wafikirie kuwa wanahitaji kusikiliza hubiri kila Sabato. Wengi wanaosikiliza hubiri mara kwa mara hata kama ukweli umewekwa wazi mstari kwa mstari, lakini wanajifunza kidogo tu. Mara kwa mara itakuwa ya faida zaidi ikiwa mkutano wa Sabato ungekuwa wa hali ya darasa la Biblia. Ukweli wa Biblia unapaswa kutolewa katika hali rahisi, inayovutia ambayo wote inakuwa rahisi kuelewa na kupata kanuni za wokovu.” Letter 192,1906.

**KUWAANGALIA WAUMINI WAPYA**

A. “Wakati wanaume na wanawake wanapokubali ukweli, hatupaswi kuondoka na kuwaacha na kutokuwa na mzigo nao tena. Wanapaswa kuangaliwa na kutunzwa. Wanapaswa kuchukuliwa kama mzigo wa roho, na lazima tuwaangalie kama mawakili ambao watatoa hesabu. Sasa unapoongea kwa watu, mpe kila mtu sehemu yake chakula kwa wakati, lakini lazima uwe kwenye sehemu yao unapotoa chakula hiki.” Ms 13, 1888.

**TABIA YA MHUDUMU NA NGUVU YA KIBWETA**

A. “Na tutatazamiaje nguvu zaidi na kwamba Mungu atajifunua mwenyewe kwa watu wakati Neno lake

limechukuliwa bila kujali, na wakati mioyo haikutakaswa kupitia kwa ukweli? Watu ambao wameongoka nusu, ambao wanajiamini binafsi na wamejitosheleza binafsi kwa tabia, wanawahubiria wengine. Lakini Mungu hafanyi kazi pamoja nao kwa sababu si watakatifu katika moyo na maisha. Hawatembei kwa unyenyekevu pamoja na Mungu. Lazima tuwe na huduma iliyoongoka na hapo tutaona mwanga wa Mungu, na nguvu yake ikisaidia juhudi zetu." 4T402

**KUJIENDELEZA BINAFSI KWA MHUDUMU**

A. "Baadhi ya sababu ambazo Bwana atafanya kupitia kwa Roho wake kumkamilisha mtu kuongea kama ambavyo angemtaka; lakini Bwana hapendekezi kufanya kazi ambayo amekwisha mpa mtu kufanya. Amekwisha tupa nguvu ya kufikiria, fursa kuelimisha akili na hali. Na sasa baada ya kufanya yote tunayoweza kufanya wenyewe, tukitumia vizuri fursa zilizo katika uwezo wetu, sasa tunaweza kuangalia Kwa Mungu kwa maombi ya dhati kufanya kupitia kwa Roho Wake kile ambacho hatuwezi kufanya wenyewe , na daima tutaona kupitia kwa mwokozi wetu nguvu na ufanisi." 4T405.

**ELIMU ENDELEVU KWA WAHUDUMU**

A. "Anaweza akawa mhubiri lakini lazima awe anafaa kufanya kama mchungaji. Kujifunza kamwe kusikome. Lazima kuendelee kipindi chote cha kazi yake bila kujali amehitimu kazini mwake kiasi gani anavyojifikiria mwenyewe. Muda tulio nao unadai kutumia akili sana, huduma iliyoelimika, siyo mwanafunzi(novices) wa utawa. Mafundisho ya uongo yanaongezeka. Ulimwengu unaelimika kwa kiwango cha juu sana; na dhambi, wasioamini na udanganyifu unakuwa na nguvu sana, kwa hiyo ufahamu wa akili kali sana unahitajika. Hali ya vitu hivi inaita utumiaji wa kila nguvu ya akili; kwa kuwa ni akili yenye umakini, chini ya utawala wa shetani ambavyo mhudumu atakutana nayo." 5T528.

B. "Wahudumu wetu ambao wamefikisha umri wa miaka arobaini au hamsini hawapaswi kujisikia kuwa haipaswi kuwa na mafanikio kama awali. Watu wa umri mkubwa na uzoefu ndio wanaotakiwa kufanywa imara na kuongozwa kwa juhudi. Wanahitajika maalumu kabisa kwa wakati huu; kanisa haliwezi kusonga mbele bila wao. Mtu wa namna hii hapaswi kuzungumzia juu ya mwili na akili kuchoka. Au kufikiria kuwa siku za utumishi wao hauna faida tena... Wahudumu wa umri mkubwa na uzoefu wanapaswa kujisikia kuwa ni wajibu wao, kama watendakazi wa Mungu kuendelea mbele, kuendelea kila siku, kuendelea kuwa na ufanisi zaidi katika kazi yao, na kwa kuendelea kutafuta na kukusanya mambo mapya kuyaweka mbele za watu." 4T269,270.

**MAMBO MUHIMU YA KUKUMBUKA:**

Usihubiri hubiri la aina moja kila wakati maana kuna hali tofauti kila wakati na mahali na aina ya watu unaowahubiria. Kwa kawaida yapo mahubiri ya aina sita:-

1. Mahubiri ya kufafanua Maandiko matakatifu
2. Mahubiri ya kuelezea kanuni za Biblia na mawazo ya kibiblia.
3. Mahubiri ya kuwaleta wasikilizaji karibu na Mungu na kumpa utukufu
4. Mahubiri ya kiuinjilisti; kutoa kweli za Biblia
5. Mahubiri ya kiunabii
6. Mahubiri ya kuomba msamaha

Mhubiri mzuri atatumia yote kwa nyakati mbali mbali na wakati mwingine atatumia zaidi ya aina moja kutokana na hali na mahali.

Usisahau kuwa Mungu anataka kukutumia kama chombo chake. Mungu anatumia mahubiri kubadilisha maisha, kufundisha na kuwalisha waaminifu, kuwafariji , kuwatia moyo na kuwaimarisha watakatifu. Usisahau kuwa hukuitwa kwa vile unafaa ila umeitwa ili utengenezwe ufae. Hata hivyo ni upendeleo. Kwa kadri unavyoelezea Neno la Mungu kwa wengine ndivyo linavyozidi kuwa wazi kwako.

**Pointi mbili za kukumbuka:**

1. Ujumbe wa mhubiri wa kweli unatoka kwa Mungu
2. Ujumbe huu unakuja kupitia kwa mwanamume au mwanamke ambaye kweli amejitoa kwa Mungu.

Kumbuka kuwa kuhubiri ni kama kupanda mbegu shambani. Sasa ili shamba liweze kuleta matokeo mazuri hatua hizi ni za muhimu:-

- Mkulima lazima atifue ardhi Hosea 10:11-12
- Lazima apige haru. Ayubu 39:10; Isaya 28:24
- Baada ya kuandaa ardhi kuna kupanda mbegu. Mwanzo 47:23
- Epuka kuchanganya mbegu. Yeremia 23:28; Lawi 19:19
- Epuka kupoteza mbegu kwenye udongo mgumu au miiba. Mathayo 13:19-22; Yeremia 4:3
- Mbegu njema itakuhakikishia mavuno ikiwa imetanguliwa na maandalizi mema ya shamba. Mathayo 13:23,24
- Kwa mazoezi mkulima anatarajia kuvuna matunda ya kazi yake. Yakobo 5:7

Kwa hali hiyo mhubiri lazima aandae mdongo wake ambao ni akili yake na roho yake. Tumia muda wako na talanta na karama zako vizuri; jifunze Neno la Mungu kwa bidii, acha kwenda mimbrani bila maandalizi, soma vitabu vya Roho ya Unabii. Wajue wasikilizaji wako wakati wote. Kubali mapungufu uliyo nayo, hakuna aliyemkamilifu asilimia mia.

**Kumbuka:**

1. Usiombe msamaha unapoanza somo hata kama hukujiandaa. Jua wewe na Mungu wako.
2. Unapotumia kielelezo cha uzoefu wa maisha kisiwe kirefu kikachukua somo.
3. Usizunguke zunguke somo bila lengo
4. Usitoe swali ambalo somo lako halitalijibu
5. Usiache swali ambalo halikujibiwa na ulilitaja

# KANUNI ZA KUPAMBA KIBWETA

Kanuni tano za mafanikio ya mhubiri:-

Siyo kile unachosema tu ambacho kitaamua namna watu wanavyopokea hubiri lako. Lugha yako ya mwili, ulivyojipamba na uchaguzi wa nguo, na usahihi wa maisha yako haya yote yataathiri mapokezi ya hubiri lako. Kosa moja litakugharimu mpendwa. Kwa hali hiyo haya yafuatayo ni ya muhimu kwa mhubiri anayetaka kufanikiwa.

1. Mwonekano
2. Kijipamba
3. Uaminifu
4. Mwenendo
5. Mtindo

wale wote walioaminiwa kuongoza mambo ya kiroho ya kanisa wanapaswa kuwa waangalifu sana wanapoonyesha mifano ambayo wanatazamia wengine waige kutoka kwao. Wasitoe nafasi ya kiburi, wivu na majivuno. Acha kuiga vitu kwenye runinga vya mavazi ya wanamuziki au wasanii, wewe siyo msanii ni mhubiri wa injili.

**MWONEKANO.**

Mwonekano wako mimbarani ni wa muhimu sana. Unaweza ukawasiliana kwa mambo mengi sana juu yako mwenyewe kabla ya kufungua mdomo wako kuhubiri. Nguo zako zinapaswa ziwe kwenye mwonekano mzuri, zisikwaze watu, ziwe safi, na mwonekano mzuri. Epuka nguo zinazoleta usikivu zenyewe, labda kwa kuwa za kisasa zaidi au za zamani sana. Usivae nguo kama za wasanii na zenye maandishi. Vaa tai iliyo nzuri na iliyofungwa vizuri isiwe ndefu sana au fupi sana. Epuka makoti yenye rangi na suti zenye kung'aa sana na zilizo na mchanganyiko wa rangi. Kiwango cha kawaida kwa waadventista wanaohubiri ni suti ya kawaida yenye rangi ya kawaida, mara nyingi nyeusi , tai nzuri iliyofungwa vizuri siyo ndefu sana wala fupi sana, shati zuri la rangi moja. Kwa nyakati chache kama kuna joto sana waombe wasikilizaji wako kama watajisikia vibaya ukivua koti.

Wahubiri wanawake wawe wanavaa vizuri inavyokubalika kwa jamii ya kikristo. Kumbuka kuwa uvaaji ni kitu dhaifu sana kati ya kuvaa kunakovutia na kusiko vutia hasa kwa wanawake. Kuwa mwangalifu sana kwa sketi fupi na ilivyoshonwa. Kuwa mwangalifu kwa shingo yako, usionyeshe matiti au cho chote kitakacholeta maswali kwa wasikilizaji wako. Vaa kama mwanamke mchaji wa Mungu na mjumbe wake. Sehemu zingine utalazimika kufunika kichwa ili usiwakwaze wasikilizaji wako. Epuka mitindo, rangi zenye kung'aa sana kama mhubiri wa injili. Usiwafanye watu kupata nafasi ya kukujadili badala ya kujadili ujumbe.
Usivae nguo ambayo itakufanya uwe na mashaka ya kuiangalia kila saa na kupoteza usikivu wako mwenyewe.

**KIJIPAMBA.**

Mwonekano wako siyo ulivyovaa tu, lakini namna unavyojipamba mwenyewe. Kwa mbali na kwa karibu unaonekanaje? Nywele ziwe safi fupi na zilizochanwa. Usiache ndevu. Kama umeamua kuweka ndevu, mimbari siyo mahali pake, subiri mpaka utakapoamua kunyoa ndevu. Meno yawe yamesafishwa vizuri na hewa iwe safi. Hakikisha huli vitunguu saumu unapokwenda mimbarani au kuhubiri, kama ni dawa tumia mapema kabla ya wakati au saa za usiku. Kuwe na muda wa saa 24 toka kutumia vitunguu saumu hadi kwenda mimbarani. Kucha zako ziwe safi na zilizowekwa sawa. Hakikisha umejiweka sawa kabla ya kwenda mimbarani watu wanatazama sana mikono ya mhubiri anapohubiri. Viatu vyako viwe vimewekwa rangi vizuri na viwe safi, suruali iwe nadhifu, shati liwe safi angalia ukosi wako uwe safi saa zote. Usiache kucha kuwa ndefu wakati wo wote au kutunza ukucha mmoja hii si sahihi kwa mhubiri wa injili.. Vito vya thamani siyo mahali pake, habari ya pete na aina zake, hivi hata kanisani havikubaliki. Kumbuka kujipamba rasmi kwa waadventista ni kujipamba kwa ndani siyo kwa nje.

**UAMINIFU**

Imeandikwa kwa Yesu kuwa watu walipomsikia walimwona akiwa anaongea kwa mamlaka siyo kama waandishi. Mamlaka yake yalitokana na Uwana wake na Mungu, kutokana na uelewa wake wa Maandiko, kutokana na mazungumzo yake yaliyo wazi, kutokana na tuni yake yenye huruma. Lakini juu ya yote kile alichofundisha aliishi kwacho. Kile alichofundisha ndivyo alivyokuwa. Maneno yake yalikuwa maelezo ya tabia yake na uzoefu wa maisha yake. Hakuhubiri ukweli tu, alikuwa ukweli. Hili ndilo lililoyapa mafundisho yake nguvu. Lazima tuwe kama tunavyofundisha ndipo mafundisho yetu yatatufanya tuwe na mamlaka. Tunaweza tusiwe kabisa kama Bwana wetu alivyokuwa lakini lazima iwe wazi kuwa yeye ni Bwana wetu na tunaishi maisha ya ukristo. Matendo yetu nje ya mimbari yatazungumza zaidi kuliko maneno tuliyozungumza

**MWENENDO.**

Tunasema mengi kwa namna tunavyosimama. Tusimame wima mimbarani hata kama maumbo yetu siyo marefu. Inua kichwa chako uwatazame watu. Toa sauti yako kana kwamba hakuna kipaza sauti na unaongea na wale walio mwisho wa mkutano wako. Usizunguke zunguke ukirekebisha kipaza sauti kihakikishe wakati kwaya inaimba. Hakikisha umepata mtu wa vyombo anayeelewa kuviweka sawasawa. Hakikisha una maiki yako mwenyewe kama mhubiri usitumie pamoja na za kwaya. Usirekebishe nguo zako wakati umeanza mkutano ziangalie mapema kabla ya kusimama. Vitabu vyako visikuchanganye mwenyewe, panga notes zako mapema na kwa utaratibu. Soma vizuri Biblia na mafungu yake.

**MTINDO.**

Hakikisha umejiandaa vizuri. Mimbarani ni mahali pa juu sana kuliko sehemu zingine zote hapa duniani maana unasimama kati ya uzima na mauti.tunapaswa kujiandaa vema ili watu wajue kweli tunajua tunachofanya. Kuna mambo mawili ambayo daima tunapaswa kuyafanya:-

Hakikisha umejua unakwenda kusema nini. Juu muktadha wako na kusudi lake. Fanya uchunguzi wa somo lako usije ukaleta uasi kwenye mahubiri yako itakuwa vigumu sana kusahihisha maana watu wanakuamini kwamba umefanya uchunguzi wa kutosha. Ili kuwalisha kondoo na wana kondoo, mhubiri anapaswa kujifunza kutumia maneno rahisi sana na lugha rahisi. Kumbuka Yesu aliwakuta watu mahali walipokuwa na lazima tufanye hivyo

hivyo. Ni vigumu sana kutumia maneno rahisi, mafupi kuliko marefu. Acha maneno na misamiati ya kitheolojia. Hakuna anayeyafahamu, hata wanatheolojia wakati mwingi hawayafahamu. Wanayatumia tu mara nyingi wakiwa vyuoni siyo kwenye mahubiri , mara nyingi hayahitajiki ili kumwongoa mtu. Watu wanaongolewa na mambo rahisi yaliyoelezewa kirahisi.
Tumia maneno rahisi hata kuelezea mambo magumu na ukweli mgumu. Toa maelekezo sahihi katika mafundisho yako. Toa muhstasari unaoeleweka, fanya ufupisho na fanya tena ili kuondoa yasiyohitajika. Watu wanachohitaji kutoka mimbarani ni hewa safi, siyo hewa ya joto.

Kumbuka kuna kondoo wengi kwenye kila kundi kuliko twiga. Kumbuka twiga wanaweza kuchukua chakula kutoka chini lakini kondoo hawawezi kuchukua chakula toka juu. Kumbuka ni muhimu kuwalisha wote kwa wakati mmoja au ulishe kondoo kwanza kisha twiga au twiga kwanza kisha kondoo kwa malisho maalumu siyo yote.

**Makosa ya kawaida kuepuka:**

1. Usiombe msamaha wakati unaanza kuhubiri kwa sababu zilizotokea. Hili ninalikazia tena na tena. Linaharibu usikivu wa watu.
2. Usiibe. Kama umeazima hubiri au wazo toka kwa mhubiri mwingine, usijifanye ni lako mwenyewe. Unaweza ukalifanyia kazi tena na sasa ukalifanya lako. Wewe mwenyewe ulicheue liwe lako usilichukue kama lilivyo labda tu kama ni nukuru za Roho ya Unabii hupaswi kuzigeuza hizi au mafungu ya Biblia.
3. Usirudie somo. Kwa kawaida haturudii somo kwa watu wale wale labda kuwa na sababu maalumu ya kukazia vipengele fulani. Hatari ni kuwa wewe mwenyewe utadharau maandalizi binafsi na hili litakufilisi kiroho. Kama utalihubiri tena tumia muda kulisoma tena na upogoe baadhi ya vitu ili liwe tamu hata kwako mwenyewe, kumbuka usihubiri kitu ambacho wewe mwenyewe huwezi kukaa na kukisikiliza.
4. Usiige. Usiige wahubiri wengine hata kama umewatamanisana. Hatuwi nakala ya mtu fulani hapa duniani kila mmoja ana mtindo wake wa kuhubiri, hakikisha wewe ni wewe. Usiige sauti tumia yako watu wanataka wakusikie wewe siyo fulani. Ukiwaiga wengine utaacha karama Mungu alizoweka kwako zisitumike na mwisho zitafifia.

Bwana akuongoze uwe na mafanikio makubwa katika kuhubiri kwako.

**Ni mimi mhubiri mwenzako.**

**Mch. John Kimbute.**